# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 6 Mei, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Waziri Mkuu. Hakuna Mbunge aliyekuwa amejiandikisha kwa ajili ya kumuuliza maswali Waziri Mkuu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali ya kawaida, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa mfungo huu wa Ramadhan wenzetu wote wametuheshimisha kwamba mko tayari kuheshimu huu mwezi wa Ramadhan tukawa kitu kimoja. Na ukawa unavaa mpaka ile lesa yako, na ukapendeza sana. Nakushukuru na nakupongeza sana na wanapongeza nyote. Kwa hiyo naomba sasa swali langu namba 101 lipatiwe majibu.

**NAIBU SPIKA:** Swali ni namba 200. Hebu rudia tena Mheshimiwa ili Taarifa Rasmi za Bunge zikae vizuri, rudia namba ya swali lako. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji.

Na. 200

**Watu Wenye Ulemavu Kupatiwa Mafunzo ya Ujasiriamali**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa mafunzo ya ujasiriliamali kwa Watu Wenye Ulemavu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo : -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia bajeti ya kila mwaka wa fedha imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuwezesha mafunzo ya ujasiriamali kwa watu wenye ulemavu waliopo katika ngazi mbalimbali, zikiwemo halmashauri zote nchini. Tumekuwa tukifanya hivi ili kusudi watu wenye ulemavu wanaopewa fedha hizi waweze kuzifanyia kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imekuwa ikiendelea kushirikiana na wadau, na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa watu wenye ulemavu kwneye fani mbalimbali lengo la kuwawezesha kujiajiri na kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kuwaingizia kipato. Kwa mfano, katika mkoa wa Dar es Salaam pekee, kwa mwaka 2019/2020, zaidi ya wajasiriamali wenye ulemavu wapatao 160 walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa fedha na uanzishaji wa miradi endelevu. Mafunzo haya yalihusisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Benki Kuu ya Tanzania, mifuko yetu ya hifadhi ya jamii *NSSF*, Benki ya *Exim*, Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), na Vyama vya Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, uwezeshaji wa Watu Wenye Ulemavu katika mafunzo ya ujasiriamali umekuwa ukiendelea kufanyika kupitia vyama vyao wakati wa matukio mbalimbali kama maadhimisho ya siku ya watu wenye ulemavu lakini vile vile tumekuwa tukiendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika maeneo mbalimbali kwa mfano kule Mbeya – Kyela tunashirikiana na wenzetu wa *trade craft exchange* na mashirika mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kutoa maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jamii iliyo kuwa inawaona watu wenye ulemavu hawawezi kufanya kazi ikiwemo ujasiriamali. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha watu wenye ulemavu nao wajaikwamue kimaisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kwenda Zanzibar kwenda kuwaona watu wenye ulemavu jinsi wanavyojikita kuhusu suala la ujasiriamali? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Amekuwa akifuatilia kwa ukaribu sana masuala yetu ya watu wenye ulemavu.

Niseme kwamba suala hili la watu kuwaona watu wenye ulemavu kama wanabaguliwa na hawawezi kufanya shughuli, nataka nimwambie tutaendelea kutoa elimu lakini kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tutaendelea kuwasaka wale wote wanaowanyanyapaa na kuwatumikisha watu wenye ulemavu ili kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tutaendelea kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu wao wenyewe waweze kujiamini na waone wana mchango katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari tuambatane naye baada ya kukamilika kwa bajeti hii na twende Zanzibar tukafanye kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaenelea na Ofisi ya Rais. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 201

**Hitaji la Watumishi – Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya upungufu wa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe hasa kwenye Idara za Afya, Elimu na Kilimo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ikama ya mwaka 2020/2021, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe inapaswa kuwa na watumishi 2,630. Hadi Machi 2021 Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ilikuwa na watumishi 2,294 hivyo ina upungufu wa watumishi 336 sawa na asilimia 12.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ikama Idara ya Afya katika Halmashauri ya Wlaya ya Korogwe inapaswa kuwa na watumishi 392, na hadi Machi 2021 Idara ya Afya ilikuwa na watumishi 263 hivyo ina upungufu wa watumishi 129 sawa na asilimia 32.9. Idara za Elimu msingi na sekondari zinapaswa kuwa na watumishi 1891 lakini zina watumishi 1604 hivyo zina upungufu wa watumishi 287 sawa na asilimia 15.2. Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika inapaswa kuwa na watumishi 55 na ina watumishi 45 hivyo ina upungufu wa watumishi 10 sawa na asilimia 18.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuajiri na kuwapnaga watumishi wa kada

mbalimbali katika halmashauri nchini ambapo katika mwaka wa fedha 2020/21 watumishi 81 wapya waliajiriwa na kupangwa katika Halamshauri ya Wilaya ya Korogwe. Kati ya hao, watumishi 22 ni walimu wa sekondari, 35 shule za msingi, 6 watumishi wa kada za afya na Afisa Ugani 1 pamoja na 17 wa kada mbalimbali. Pamoja na jitihada hizo, katika Ikama ya mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya imetenga nafasi za ajira mpya 150 ambao watapangwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu haya ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna haja ya kukaa nae baadaye tuangalie hizi takwimu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na majibu hayo ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, moja ya sababu kubwa ya upungufu wa watumishi kwenye Halmashauri za Vijijini kama ilivyo Halmashauri ya Korogwe au kama ilivyo kwenye Jimbo la Mlalo kule kwa ndugu yangu Shangazi, sababu kubwa ni kwamba watumishi wanaenda kule, wakipata ajira wanahama. TAMISEMI mmekuwa mkipitisha uhamisho wa watumishi wakati mwingine bila kuzingatia maoni ya wakurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua ni lini sasa TAMISEMI mtakubali kuzingatia maoni ya Wakurugenzi kutoa watumishi mbadala kabla ya kuwahamisha waliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wakati mwingine tunaweza kupunguza shida ya upungufu wa walimu kwa kusawazisha Ikama ndani ya halmashauri yenyewe. Kwa mfano Halmashauri ya Korogwe zaidi ya miaka mitatu kifungu cha *moving allowance* hakijawahi kupat afedha. Inasababisha ugumu katika kusawazisha Ikama ya watumishi ndani ya halmashauri yetu. Ni lini Serikali itakuwa tayari sasa kutoa fedha ya kutosha kwenye vifungu hivi vya uhamisho ili

kuweza kusababisha Ikama ndani ya Halmashauri yenyewe? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tumekuwa na changamoto ya upungufu wa watumishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwemo Halmashauri ya Korogwe. Lakini kama ambavyo nimetangulia kutoa m ajibu ya msingi kwamba Serikali imeendelea kuweka jitihada za kutosha kuhakikisha kwamba tunaendelea kuongeza watumishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kweli tumekuwa na changamoto kubwa sana ya watumishi hasa wanaokuwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa maeneo ya vijijini kuomba uhamisho wengi wao wakiomba kuhamia mijini. Ofisi ya Rais TAMISEMI na Serikali kwa ujumla imeendelea kuhakikisha inazingatia Ikama katika maeneo ya vijijini na imeendelea kuhakikisha inasimamia kwa karibu uhamisho wa watumishi hasa kutoka vijijini kwenda mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba si kweli kwamba TAMISEMI imekuwa kila siku inapitisha maombi ya uhamisho kwa watumishi wote wanaoomba. Mara kwa mara tumekuwa tunachuja sababu za msingi ambazo zinasababisha baadhi ya watumishi kukubali lakini watumishi walio wengi kutokukubaliwa kupata uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili Serikali imeweka utaratibu sasa. Ofisi ya Rais TAMISEMI tutaenda kuzindua mfumo wa kielektroniki ambao sasa maombi ya uhamisho yatapitishwa kwa njia ya kielektroniki na yatawezesha sasa kuchuja kwa uhakika zaidi hamisho zote ambazo zinaombwa na itawezesha sana watumishi wetu katika maeneo ya vijijini kubakia kufanya kazi katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili tutakwenda kuwa na mikataba ya watumishi wanaoajiriwa. Watumishi wengi wamekuwa wakiajiriwa maeneo ya vijijini, wakifika na kupata *cheque number* wanaanza kufanya jitihada za kuhama. Sasa kabla ya kuajiriwa tutahakikisha tunakuwa na mikataba kwamba baada ya kupangiwa kwenye vituo hivyo ni lazima wakae angalau miaka mitatu au mitano kabla ya kuanza kuomba vibali vya uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itatuwezesha sana kuhakikisha watumishi wetu katika maeneo ya vijijini wanabaki na kutoa huduma ambazo zinakusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ugumu wa kusawazisha watumishi kwa maana ya ikama katika maeneo yetu, ni kweli na Serikali imeendelea kutenga fedha za matumizi mengineyo kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha kuhakikisha yale maeneo ambayo yana watumishi wengi lakini maeneo mengine yana watumishi wachache tuweze kufanya usambazaji wa ndani ya halmashauri. Hili pia tumeendelea kusisitiza Wakurugenzi katika Serikali za Mitaa kutenga bajeti za uhamisho wa ndani katika halmashauri zao ili waweze kuhakikisha mgawanyo wa watumishi ndani ya halmashauri unazingatia ikama na angalau unakuwa *reasonable.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha msambao huu pia unakuwa wenye tija zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa changamoto ya upungufu wa watumishi iliyoko Wilaya ya Korogwe ni sawa sawa kabisa na iliyoko Jimbo la Babati Vijijini hasa Sekta za Afya na Elimu. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hili la watumishi hawa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu kwa swali hilo kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tuna upungufu wa watumishi lakini kama ambavyo nimetangulia kusema kwenye jibu la msingi, Serikali imeendelea kutenga ikama kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kuandaa na kuomba vibali vya ajira kila Mwaka wa Fedha ili kuendelea kuongeza idadi ya watumishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa hivyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Baran kwamba katika Wilaya ya Babati pia tutahakikisha tunaipa kipaumbele katika ajira za Mwaka wa Fedha ujao ili angalau tuendelee kuboresha idadi ya watumishi katika halmashauri hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi. Wilaya ya Misenyi ni Wilaya yenye Kata 20. Inavyo vituo vya afya viwili ambavyo havina watumishi kabisa pamoja na Idara za Elimu na Kilimo. Je, ni lini Serikali itaweza kutupatia watumishi wa kutosha ili watoe huduma nzuri kwa wananchi wa Wilaya ya Misenyi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha ujao 2021/2022 Serikali na Ofisi ya Rais – TAMISEMI tumeomba vibali vya ajira takribani 12,000 kwa ajili ya watumishi wa kada mbalimbali katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na hivyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Kyombo kwamba katika mgawanyo wa watumishi katika Mwaka ujao wa fedha tutahakikisha tunaitazama Halmashauri ya Misenyi kwa jicho la karibu ili tuendelee

kuboresha huduma za afya katika vituo hivi ambavyo havina watumishi lakini pia katika kada nyingine katika halmashauri hiyo na kote nchini kwa ujumla wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba niulize hivi, Je, Wizara ya TAMISEMI haioni umuhimu wa kuweka maafisa masoko kwenye halmashauri zetu. Tunajua kwamba tatizo kubwa kwenye halmashauri ni ukosefu wa masoko. Watu hawajaunganishwa na masoko, sasa tungekuwa na maafisa hawa wangetusaidia sana. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika uendeshaji wa shughuli za masoko katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Serikali imeweka utaratibu ambao pamoja na wakuu wa idara wengine, wakuu wa idara ya fedha na biashara kuna maafisa biashara katika halmashauri zetu ambao kimsingi wanafanya kazi kwa karibu ambazo zinafanana sana na Maafisa Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tunaendelea kuhakikisha kwamba tunaboresha mfumo huo kuhakikisha kwamba wale maafisa biashara ambao wanasimamia masoko na shughuli nyingine zote za biashara katika halmashauri wanafanya kazi zao kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wazo lake pia la kuwa na Maafisa Masoko tunalichukua, tutalifanyia tathmini na kuona kama tunaweza tukaongeza nguvu katika eneo hilo kuwa na maafisa biashara na pia kuwa na maafisa masoko. Kwasababu lengo la Serikali ni kuhakikisha kuna ufanisi mkubwa wa biashara na ustawi wa mapato ya ndani lakini pia ya wananchi katika masoko yetu.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 202

**Kufufua Viwanda – Jiji la Arusha**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Viwanda vya *General Tires* na *Pharmaceutical Industries Ltd.* ili kuongeza ajira na upatikanaji wa dawa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Bisahara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na viwanda mbalimbali nchini vikiwemo viwanda vya matairi na dawa ili kuchochea uchumi wa nchi kwa kuzalisha bidhaa na ajira. Kiwanda cha matairi kinachojulikana kama *General Tire* kilichopo katika Jiji la Arusha ni moja ya kiwanda kikubwa cha matairi katika ukanda wa Afrika Mashariki. Uzalishaji katika kiwanda hicho ulisimama mwezi Agosti, 2007 baada ya kukosa fedha za kujiendesha, husasan fedha za kununua malighafi. Hivyo, Wizara imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukifufua kiwanda hicho ili kufikia malengo ya Serikali kujitosheleza kwa mahitaji ya matairi nchini, kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza matairi kutoka nje na kuzalisha ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* iliunda Timu ya Wataalam ili kufanya tathmini juu ya njia bora ya kuendesha kiwanda hicho. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa mitambo na teknolojia iliyopo imepitwa na wakati na hivyo ikashauriwa kuwa mashine na mitambo ya kisasa ifungwe ili kuleta tija na ufanisi katika uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali kupitia *NDC* inaendelea kutafuta mwekezaji mwenye uwezo wa kuwekeza teknolojia mpya katika kiwanda hiki hususan ya kisasa kuendana na mahitaji ya bidhaa za matairi zilizopo sokoni. Tayari utaratibu wa kutangaza zabuni umefanyika ili kumpata mbia wa kufufua Kiwanda cha Matairi Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo na Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda na Mkakati wake, viwanda vya dawa ni moja ya viwanda vya kipaumbele ikizingatiwa kuwa kiasi kikubwa cha fedha kinachotumika kuagiza dawa kutoka nje ya nchi kwa mwaka, ajira zinazopotea pamoja na umuhimu wa kuzalisha dawa kwa ajili ya usalama wa wananchi wake. Hivyo, Wizara inaona kuna umuhimu mkubwa wa kuharakisha kufikiwa kwa maamuzi ya kesi inayoikabili Kiwanda cha *TPI* na pia kwa kuzingatia kuwa Serikali inamiliki hisa asilimia 30 katika Kiwanda hicho ili kuruhusu mara moja kuanza kwa uzalishaji wa dawa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sijaridhika kabisa na majibu yaliyotolewa na Serikali kwa sababu wakati anaongea maneno haya Kiwanda cha *TPI* tayari mwekezaji aliyeko pale ameshauza ekari tano kwa *1.3 billion* kwa mtu mwingine na ukizingatia Serikali ina *share* ya asilimia 30 kwenye kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, tunafahamu kwamba Serikali ilipeleka kiasi cha dola milioni 10 kwenye Kiwanda cha *General Tire.* Ningeomba nipate majibu leo hapa fedha hizo zimefanya kazi gani na zimeendeleza nini katika kiwanda hicho ili kiweze kutoa ajira na fursa kwa watu wa Arusha na Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, Serikali ina mpango gani pia wa kufufua kiwanda chetu cha *TPI* ili tuweze kuongeza dawa, lakini pia na kuongeza ajira kwa watu wetu wa Arusha na nchi nzima ya Tanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Gambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu Kiwanda cha *TPI,* asilimia 30 ya kiwanda hicho Serikali ina *own share.* Kwa hiyo, Serikali iko katika hatua za kutafuta mwekezaji ambaye atawekeza kwa ubia na Serikali, ili kiweze kufufuliwa. Kama Mheshimiwa Mbunge ana mwekezaji yeyote na Bunge hili na Watanzania wote, Kiwanda cha *TPI* kiko *open* kwa kumpa mwekezaji kwa kiwango cha asilimia 70 ili kiweze kufunguliwa. Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba kiwanda hicho kinafunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha *General Tire,* ni kweli Serikali iliweka fedha na ni kweli kwamba mwekezaji aliyekuwa amewekeza eneo lile na aliyekuwa amepewa *ownership* ya kuki-*run* kiwanda kile alikabidhiwa fedha na tathmini ya awali ilionesha kwamba fedha zile hazikuweza kufikia malengo yaliyokuwa yametarajiwa. Kwa hiyo, Serikali hatua iliyochukua ni kuhakikisha kwamba kwanza inakirudisha mkononi mwake na kukikabidhi Shirika la *NDC* kukitafutia mwekezaji mwingine. Yule bwana aliyekuwa amepewa *majority shareholder share* zake zilirudishwa

Serikalini. Kwa hiyo, ni dhamira ya Serikali kuona kwamba Kiwanda cha *General Tyre* kinafanya kazi ili kufikia lengo la Serikali kwa ajili ya kuwekeza katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa swali hili linalohusiana na Kiwanda cha *General Tyre* limeulizwa kwa muda mrefu sana na sisi tumekuwa tukifuatilia muda mrefu sana tangu Mheshimiwa Gambo akiwa Mkuu wa Wilaya, amekuwa Mkuu wa Mkoa, hadi leo hii yupo ndani ya Bunge, lakini Serikali imekuwa ikitoa majibu yaleyale. Wananchi wa Arusha wanataka kufahamu ni lini Kiwanda cha *General Tyre* kitaanza kufanya kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa Niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali dhamira tunaelewa na *frustration* iliyoko kwa wananchi wa Mkoa wa Arusha na umuhimu wa Kiwanda cha *General Tyre.* Hili jambo ni la wazi, ni dhamira ya Serikali kuona kwamba Kiwanda cha *General Tyre* kinafanya kazi. Ndiyo maana Serikali mara zote imekuwa ikitangaza nia ya kumtafuta mwekezaji yeyote mwenye uwezo wa kuwekeza na kuwapa fursa wananchi wa Mkoa wa Arusha na Tanzania kwa ujumla waweze kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni muhimu vilevile Waheshimiwa Wabunge wakaelewa, unapowekeza katika kiwanda kuna dhana ya *comparative advantage.* Hii ina maana kwamba tunapotengeneza tairi Tanzania, tairi hilohilo linazalishwa na nchi nyingine, tunapoenda sokoni litanunuliwa

kwa bei gani? Kwa hiyo, suala la teknolojia ni muhimu sana. Nitumie nafasi hii kuwahamasisha Watanzania kwamba Serikali iko *open* kumruhusu Mtanzania yeyote mwenye uwezo ama mwekezaji kutoka nje kuja kuendesha kiwanda hiki. Mkoa wa Arusha unakaribishwa kama kuna uwezekano tunaweza kukutana nao kama Serikali tujadiliane ni namna gani tunaweza ku-*revive* Kiwanda cha *General Tyre.* Pia siyo lazima kizalishe matairi tu, kinaweza kuzalisha jambo lingine lolote ambalo litaweza kuleta manufaa katika nchi na uchumi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwa kuwa, uwepo wa viwanda visivyofanya kazi katika Mkoa wa Arusha inafanana kabisa na Mkoa wa Mtwara ambako kuna viwanda vya korosho ambavyo havifanyi kazi. Naomba kujua ni lini Serikali itahakikisha Viwanda vya Kubangua Korosho vilivyopo katika Mkoa wa Mtwara, Wilaya ya Masasi, Newala na Mtwara vinaanza kufanya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa Niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hokororo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa muda mrefu Viwanda vya Kubangua Korosho katika Mkoa wa Mtwara na maeneo ya Pwani vilisimama kufanya uzalishaji. Sababu ya msingi ilikuwa ni kwamba mfumo wa uuzaji wa korosho wa minada ulikuwa unawaweka kwenye *disadvantage processors* wa viwanda ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatua ya kwanza ambayo Serikali imechukua na marekebisho haya tumeyafanya mwaka jana ni kwamba, tumeruhusu mfumo

wa *primary market* kwamba wenye viwanda vya kuzalisha korosho wanaainisha mahitaji yao ya awali na tunawaruhusu kwenda kununua moja kwa moja katika vyama vya msingi badala ya kusubiri kwenye mnada kwa sababu, kwenye mnada wanakuwa *not competitive* na matokeo yake gharama ya wao kuchakata korosho inakuwa kubwa. Mwaka huu vipo viwanda viwili ambavyo vimeanza kufanya hiyo *process* na tumevifanyia majaribio na tumeona manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini changamoto ya pili inayowakabili wenye viwanda vya kuchakata korosho ni thamani ya mtaji unaotakiwa kununua sokoni ili aweze kuhifadhi kwa msimu mrefu kwa maana ya mwaka mzima.

Kwa hiyo, sasa hivi tunafanya mazungumzo na *Tanzania Agricultural Development Bank* ili tuanzishe mfumo wa *Collateral Management System* kwamba wenye viwanda wanapata *raw material* zinahifadhiwa katika maghala, wanakuwa wanachukua kidogokidogo kutokana na mahitaji yao ili waweze ku-*sustain* katika kipindi cha mwaka mzima. Msimu huu wa korosho utakaoanza mfumo wa *primary market* kwa viwanda kununua moja kwa moja katika vyama vya msingi tutawaruhusu ili viwanda vya Mkoa wa Mtwara na Lindi viweze kufanya kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 203

**Kupeleka Maji Vijiji vya Tabora Kaskazini**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia maji wananchi walio katika Vijiji ambavyo havifikiwi na Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria katika Jimbo la Tabora Kaskazini?

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Maji, Mheshimiwa Juma Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tabora Kaskazini lina kata 19 na vijiji 82. Katika utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Nzega, Igunga na Tabora jumla ya vijiji 20 vya Jimbo la Tabora Kaskazini ambavyo ni Ibushi, Igoko, Isikizya, Ikonola, Ikonola, Mswa, Itobela, Ibelamilundi, Isenegezya, Mtakuja, Majengo, Kalemela, *Saw Mill*, Imalampaka, Magiri, Kinyamwe, Lunguya, Upuge, Kasenga na Mhogwe vimenufaika na mradi. Aidha, Serikali imekamilisha utekelezaji wa miradi mitatu ya mtandao wa bomba inayonufaisha vijiji vinne vya Kilungu, Milumba, Migungumalo na Ishihimulwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali iko kwenye hatua za awali za utekelezaji wa miradi sita itakayonufaisha vijiji kumi na mbili vya Makazi, Ugowola, Ndono, Mbiti, Kalola, Ufuluma, Nzubuka, Izugawima, Ibiri, Mayombo, Nsimbo na Kagera. Katika Mpango wa bajeti ya fedha 2021/2022, Serikali imepanga kutekeleza miradi mitano itakayonufaisha vijiji vinane vya Ikongolo, Kanyenye, Kiwembe, Kongo na miji 28 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 500 kutoka Benki ya Exim India ambao utanufaisha vijiji 14 na hivyo kufanya jumla ya vijiji 58 vya Jimbo la Tabora Kaskazini kupata huduma ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Athuman Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sijapata majibu mazuri namna hii katika Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, namshukuru sana. Nawapongeza sana Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nina maswali madogo tu mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile vijiji vitano alivyovitaja Ikongolo, Kanyenye, Kiwembe, Kongo na Hurumbiti ni bakaa ya mradi wa Ziwa Viktoria na hela zake zipo shilingi bilioni 25. Je, lini mradi huu wa kumalizia vijiji hivyo vitano utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa vile wananchi wangu wa Jimbo la Tabora Kaskazini wanahitaji mafunzo na elimu kuhusu matumizi ya maji hayo, lakini vilevile kuhusu utunzaji wa miundombinu ya maji, je, lini elimu hiyo kwa wananchi itaanza kutolewa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Maji, Mheshimiwa Juma Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Mzee wangu Almas Maige kwa kazi kubwa na nzuri hasa ya kuwapigania wananchi wake wa Tabora kuhakikisha maji tunayatoa Ziwa Viktoria na kuyapeleka Tabora, Igunga, Nzega. Historia itakukumbuka mzee wangu, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake kwamba lini tutatekeleza mradi katika vijiji vitano, nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, sisi Wizara ya Maji si Wizara ya Ukame, vijiji vile vitano vilivyobaki tunakwenda kuvikamilisha mara moja ili wananchi waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa kuhusu suala zima la elimu katika eneo lile la Tabora, Wizara ya Maji tumetekeleza mradi mkubwa sana wa zaidi ya bilioni 600 katika Mji wa Tabora, Igunga, Nzega. Pasipo elimu kwa wananchi inawezekana wakahujumu miundombinu ya maji. Hii ni kazi yetu sote Mheshimiwa Mbunge, mimi Waziri wa Maji na Waheshimiwa Wabunge wote kuhakikisha kwamba tunatoa elimu ya kulinda na kutunza vyanzo na miundombinu ya maji ili kuhakikisha wananchi hawa wanaenda kuvilinda

na kuvitunza, ili miradi hiyo iwe na manufaa kwa vizazi vya sasa na vya baadaye. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kuuliza swali langu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara ya Maji kusambaza maji zinaweza kuwa bure kama gharama za kuunganisha maji hazitashushwa. Swali langu ni hili, kwa nini Serikali isishushe gharama za kuunganisha maji, ikiwa ni pamoja na kuzuia wananchi kulazimishwa kununua vifaa vya kuunganisha maji kwenye Mamlaka za Maji na gharama zake zikawa kama umeme wa *REA* shilingi 27,000? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Maji, Mheshimiwa Juma Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Sisi kama Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji, si maji tu, lakini kwa gharama nafuu. Kwa hiyo, nikiwa Waziri wa Maji tumepokea ushauri, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mji wa Munze katika Wilaya ya Kishapu ni mji ambao umepata maji ya Ziwa Viktoria. Kumekuwepo na tatizo kubwa sana la maji kukatika katika Mji wetu wa Kishapu, wa Munze. Je, ni tatizo gani linalosababisha maji haya kukatika huku tukitambua kwamba maji ya Ziwa Viktoria yamekuwepo kwa wingi sana na halipo tatizo la maji, lakini changamoto kubwa ni kukatika kwa haya maji? Naomba majibu.

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana. Waziri wa Maji, Mheshimiwa Juma Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Kishapu kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna mradi ambao tumepeleka maji ya Ziwa Viktoria katika Jimbo lake la Kishapu. Kukatika kwa haya maji changamoto kubwa ilikuwa ni deni la umeme. Sisi kama Wizara ya Maji tumeshatoa milioni 600 kuwapa wenzetu wa *KASHWASA* kuhakikisha wanalipa deni lile *TANESCO* ili wananchi waendelee kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Wizara ya Maji ina dhamira njema na wananchi wa Jimbo langu la Manyoni Magharibi. Kuna visima ambavyo vimeahidiwa na Wizara katika Vijiji vya Jeje, Njirii, Kamenyanga, Itagata, Ukimbu, Chabutwa, Makale na Kalangali na Itagata, je, ni lini wataenda kuchimba visima hivi?

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Maji, Mheshimiwa Juma Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Kubwa nimuombe Mheshimiwa Mbunge baada ya dakika chache nakuja kuwasilisha bajeti yangu ya Wizara ya Maji na bajeti yetu imesikiliza ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tumezingatia maelekezo yako katika kuhakikisha wananchi wako tunawachimbia visima. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na utoaji na usambazwaji wa maji mijini na vijijini bado kuna malalamiko makubwa sana ya ankara za maji kutokuwa na uhalisia. Je, Serikali ina nini la kusema au kuna tamko gani la Serikali ili kuondoa mkanganyiko huu ambapo wananchi wanabambikwa ankara ambazo hazina uhalisia? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Aweso, Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Mbunge lakini niseme tu wazi ni haki ya mwananchi kupatiwa huduma ya maji na mwananchi ana wajibu wa kulipia bili za maji, lakini wajibu huo wa kulipia bili za maji zisiwe bambikizi. Kwa hiyo, maelekezo ya Wizara yetu ya Maji kwa Mamlaka zote za Maji nchini watoe bili halisia ambazo zimeidhinishwa na *EWURA.* Ikiwa kuna Mkurugenzi au msoma mita kwa makusudi anambakizia mwananchi bili ya maji tutashughulika naye.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa juhudi zinazoendelea za kuwapatia maji wananchi wa Jimbo la Kyerwa kwenye Mradi wa Vijiji 57.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ziko kata ambazo haziko kwenye Mradi wa Vijiji 57, kama Kata ya Bugara, Kibale, Businde pamoja na Mlongo. Nini juhudi za Serikali kuwapatia wananchi hawa maji?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana sana kaka yangu Mheshimiwa Bilakwate kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Jimbo lake la Kyerwa. Kubwa ambalo nataka kusema, sisi kama Wizara ya Maji, tumejipanga na zaidi ya miradi 1,527 tunakwenda

kuitekeleza katika maeneo ya vijijini katika kuhakikisha wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishe maeneo ambayo hayana maji, sisi kama Wizara tumejipanga kuhakikisha tunawafikishia hii huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi.

Na. 204

**Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Vijiji vya Singida Magharibi**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa kujenga miundombinu ya maji katika vijiji vya Kipunda, Minyughe, Ighombwe, Makungu, Mpetu, Magungumka na Mnang'ana?

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jimbo la Singida Magharibi. Ili kuendelea kutatua changamoto hiyo, Serikali imekamilisha upatikanaji wa vyanzo vya maji kwa kuchimba visima virefu katika Vijiji vya Kipunda, Minyughe, Ighombwe, Makungu, Mpetu, Magungumka na Mnang'ana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa visima hivyo kwa kujenga miundombinu ya usambazaji utaanza mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja ununuzi na ufungaji wa pampu saba, ujenzi wa nyumba za mashine saba, matanki ya kuhifadhi maji saba yenye ukubwa lita 90,000 na 100,000 na ununuzi na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilometa 85.9 na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 79. Pia, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kutekeleza miradi minne ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika vijiji vya Irisya, Iglansoni, Ihanja na Kaugeri vilivyopo katika Jimbo Singida Magharibi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana, sana, sana, ambayo kimsingi yatawatia moyo sana wapiga kura wangu pamoja na wananchi wa Jimbo la Singida Magharibi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mradi wa Maji wa Kata ya Mtunduru umechukua muda mrefu sana katika kukamilika.

Nilikuwa nataka nijue; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutoa agizo kwa Serikali ku-*release* fedha haraka ili mradi wa maji wa Mtunduru pamoja na vijiji vya Igombwe uweze kukamilika haraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kama yangu Mheshimiwa Kingu. Kiukweli wewe ni Mbunge unayetosha mpaka chenji inabaki. Kubwa ambalo ninataka niseme, sisi Wizara ya Maji tunapokea fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji kupitia Mfuko wa Maji kila mwezi. Ndani ya mwezi huu tutatoa fedha kwa ajili ya mradi wako kuhakikisha tunaukamilisha. Ahsante sana *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna kero kubwa ya maji katika Kata za Ruaha, Mikumi, Ulaya, Tindiga na Malolo; na Serikali inatambua hilo:-

Je, ni lini Serikali itakwenda kutatua shida ya maji katika Kata hizo? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, lakini sisi kama Wizara ya maji kwa dhati kabisa tunataka kumaliza tatizo la maji Mikumi pamoja na Morogoro. Hakuna sababu hata moja ya wananchi wa Morogoro na Mikumi kulalamikia suala la maji ilhali wana vyanzo vya maji vya kutosha. Kwa hiyo, sisi kama Wizara ya Maji tumejipanga sasa kujenga miundombinu ili wananchi wako wa Mikumi waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upendeleo mkubwa baada ya bajeti nitafika katika Jimbo la Mikumi ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kufanya kitu pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Changamoto za maji zilizopo katika Jimbo la Kalenga kwa Kata za Lumuli, Masaka, Kiwele, Luhota, Kalenga yenyewe na Magulilwa zimekuwa ni kubwa sana:-

Je, Serikali mna mkakati gani sasa wa kuhakikisha wananchi hawa wanapata huduma za maji safi na salama? *(Mkofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kilio hiki cha wananchi wake, lakini kubwa sisi kama Wizara ya maji, tumepewa maelekezo mahususi kabisa na Mheshimiwa Rais wetu kipenzi Mama Samia Suluhu Hassan; na akaenda mbali kabisa, kwamba tukizingua atatuzingua. Sisi hatupo tayari kuzinguliwa, tutakwenda kuhakikisha kwamba wananchi wako wanapata huduma ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri kuhusiana na mradi wa maji wa Hanga, Mawa na Msindo ambapo upembuzi yakinifu ulishafanyika na uko Wizarani:-

Je, Serikali inaweza kutueleza ni lini mradi huo au inaweza ikaweka katika bajeti hii mradi huo ukaanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeze kaka yangu Mheshimiwa Kawawa kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Jimbo lake la Namtumbo. Wizara yetu ya maji jukumu letu mahsusi ni kuhakikisha wananchi wa Tanzania na Namtumbo wanapata huduma ya maji. Namwomba sana kaka yangu, eneo kama mradi unahitaji kibali na sisi kama Wizara ya Maji tupo tayari kutoa kibali na mradi ule uanze na wananchi wako waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Nami naomba kuuliza swali

dogo la nyongeza kuhusiana na ahadi ya Serikali ya kupeleka matawi ya maji katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa bomba kubwa la maji safi na salama yaliyotoka katika mto simba Mlimani Kilimanjaro kwenda Longido na vijiji hivyo ni Eliarai hasa Kitongoji cha Himotong, Tingatinga, Ngareiyani na Sinya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge. Kiukweli historia kubwa ambayo umeiacha Longido ni juu ya ule mradi wa shilingi bilioni 16 ambao tumeutekeleza katika Jimbo lako.

Kwa hiyo, eneo lile ambalo limepitwa na bomba kuu vijiji upande wa kulia wa bomba kuu na kushoto, zaidi ya kilometa 12 navyo tutavipatia huduma za maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Liwale ina Kata 20 na vijiji 76, lakini bado upatikanaji wa maji ni wa shida sana hasa hasa kwenye vijiji vya Kihangara, Makata, Kikulyungu, Nahoro, Lilombe, Ngorongopa, Mkutano, Mtawatawa, Kimambi na Nanjegeja.

Mheshimiwa Waziri, ni lini vijiji hivi vinaweza kupatiwa maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Mheshimiwa Mbunge wa Liwale amekuwa akilia sana juu ya suala zima la maji katika Jimbo lake. Sisi kama Wizara ya Maji tumewapatia fedha wakala wa Uchimbaji visima *DDCA* waende katika Jimbo lako la Liwale waende wakachimbe visima ili wananchi

wako waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Danielson Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nami kuniona. Changamoto zilizopo katika Jimbo la Singida Magharibi hasa kwenye miundombinu ya maji zinafanana sana na zile zilizoko Arumeru Mashariki, hususani Kata ya Keri ambayo ina taasisi nyingi za Serikali:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuja kukarabati ile miundombinu na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama kwenye kata hiyo pamoja na Embaseni, Maji ya Chai, Kikatiti, Maroroni na Majengo? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru. Nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwani amekuwa mfuatiliaji mkubwa hususan wananchi wake wa Arumeru. Tunachotaka ni kujenga *commitment* katika Wizara yetu ya Maji kupitia bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni makubwa ya Waheshimiwa Wabunge tumeyazingatia, nataka nikuhakikishie maeneo ambayo ameyaeleza tutayafanyia kazi kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali iliahidi kupeleka visima 23 kwenye Halmashauri ya Mji wa Tarime kuweza kupeleka visima hivyo pembezoni mwa kata ambazo zipo nje ya mji tangu mwaka 2018.

Ni lini sasa Serikali itakwenda kuchimba visima hivyo wakati tukisubiria mradi wa Ziwa Victoria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Matiko. Maji hayana mbadala. Maji ni uhai, nasi hatupo tayari kupoteza uhai wa wana Tarime. Kabla ya mwaka huu wa bajeti kwisha tutafanya shughuli hiyo kuhakikisha wananchi wake tunawachimbia visima vya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa pamekuwa na malalamiko ya mara kwa mara kwa watumiaji wa maji kubambikizwa bili:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha mfumo wa kufunga mita ambao zitakuwa za malipo kwanza kama Luku ya umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, Mzee wangu, Mzee Hussein. Kiukweli kongwe huvusha, tunakushukuru sana. Kubwa ambalo nataka kusema, kizuri huigwa. Tumeona wenzetu wa *TANESCO* za kuwa na mita hizi za Luku, nasi kama Wizara ya Maji tuna *pre-paid meter* ambapo tumeshaanza na tumefunga katika baadhi ya taasisi. Mkakati wetu na maelekezo kwa mamlaka zetu zote za maji ni kuhakikisha tunajielekeza huko katika *pre-paid meter* ili kuhakikisha kwamba wananchi wanalipa bili halisia bila ya usumbufu wowote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tumalizie na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu kwa Mheshimiwa Waziri: Ni lini miradi mikubwa ya kutatua changamoto ya maji kwa hatua ya awali iliyopo Jimbo la Ndanda itatekelezwa, zaidi kwenye Kata za Namajani, Mpanyani, Msikisi pamoja na Chiwale? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nampongeza Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Cecil Mwambe, kwa kweli amekuwa mfuatiliaji mkubwa hasa katika Jimbo lake la Ndanda. Ahadi ambayo nampa katika maeneo ya kipaumbele nitakayokwenda mimi mwenyewe baada ya Bajeti, ni katika eneo lake katika Jimbo la Ndanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ni kwamba katika Bajeti hii pia tumezingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Ni imani yangu maeneo ambayo ameyataja yatakuwemo ili kuhakikisha tunakwenda kutatua tatizo la maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Mnaweza kuona, Mheshimiwa Aweso ameulizwa maswali mengi sana, lakini katika muda mfupi. Naamini wale wanaokuja kujibu maswali hapa, wamejifunza kujibu maswali kwa kifupi ili kutoa fursa kwa Wabunge wengi zaidi kuuliza maswali. Mnaweza kuona sasa kwa nini yeye ni Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waziri amekuja hapa na ametoa funzo zuri sana kwa wote wanaojibu maswali hapa mbele, wajitahidi kutumia muda mfupi na kwa sababu yeye anatoa majibu mafupi na Wabunge wameuliza mawali mafupi. Kwa hiyo, tujitahidi. Tukianza kwenda namna hiyo, itaturahisishia sana, kila Mbunge anaweza kuwa anapata fursa ya kuwasemea wananchi wake kwenye hoja anazotaka kuzipa kipaumbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali siku ya leo. Tutaanza na wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika na hawa ni wageni 10 wa Mheshimiwa Spika kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika *(Tanganyika Law Society - TLS)* wakiongozwa na Rais wa Chama hicho Dkt. Edward Hosea. Karibuni sana sana. Huyu ni Rais wangu mimi pia, kwa sababu na mimi ni Wakili. Kwa hiyo, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 86 wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaye ni Waziri ya Maji ambao ni viongozi wakuu wa Wizara ya Maji wakiongozwa na *Engineer* Antony Sanga ambaye ni Katibu Mkuu. Halafu ameongozana na *Engineer* Nadhifa Kemikimba ambaye ni Naibu Katibu Mkuu. Pia ameongozana na Ndugu Lucas Kwezi ambaye ni Mwakilishi wa *DFID.* Pia ameongozana na Ndugu Lilian Mkama ambaye naye ni Mwakilishi wa *DFID.* Karibuni sana. *(Makofi)*

Hebu simameni tena watu wa maji. Eeh, Waheshimiwa Wabunge, humu ndani mlikuwa mnapiga makofi mengi sana wakati Mheshimiwa Waziri akija kuweka Hati hapa Mezani, ilikuwa inaashiria mambo mazuri kutoka Wizara hii; na hao ndio watendaji wake, kwa hiyo, nadhani mtambue uwepo wao hata kama hatukupata fursa ya kuwataja majina wote. Tunawashukuru kwa kazi nzuri. Wabunge bado wana changamoto, lakini wanatambua kazi nzuri mnayoifanya mpaka sasa. Mnaweza kukaa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vile vile ipo familia ya Mheshimiwa Jumaa Aweso na hapa kuna Ndugu Fatuma Massanga ambaye ni mama yake mzazi, karibu sana. Siyo mara yake ya kwanza kumleta mama mzazi hapa, huwa anapenda kuzungumza habari zake. *(Makofi)*

Tunakushukuru mama kwa kuleta mtoto mwenye adabu na mchapakazi. Pia amekuja na mama yake mdogo, ambaye Ndugu Khadija Omar, Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* wakiongozwa na Ndugu Jully Lyimo. Karibuni sana, sana, sana, wageni wetu kutoka *TANAPA. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni hawa watakuwepo katika viwanja vya Bunge wakifanya maonesho kuhusu vivutio vya utalii katika hifadhi za Taifa kuanzia tarehe 6 -14 Mei, 2021. Lengo lao hasa ni kuhamasisha utalii wa ndani ambao unawahusisha pia Waheshimiwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge mtembelee banda lao na huwa wanaweka utaratibu mzuri ambao katika kipindi hiki cha Bunge pengine mwishoni mwa wiki mojawapo wanatengeneza utaratibu mzuri ambao Wabunge mnaweza kwenda katika vivutio vilivyo karibu na maeneo haya. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mwende. Wale mnaowaona pale, kuna wanamama; hebu wanamama mikono juu. Hao wote ni akina mama. Haya, jamani twende kwenye hilo banda wapo akina mama wamejaa hapo. *(Makofi/Vigelegele)*

Wapo pia wageni 15 wa Mhehimiwa Ummy Nderiananga ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu, ambao ni familia yake, wafanyakazi wenzake na wawakilishi wa Mradi wa Uwezeshaji wa Kiuchumi na Elimu ya Ujasiriamali *kupitia* mradi wa *Cofee, Cocoa and Palm Oil Value Chain (CCP)* wakiongozwa na mume wake Ndugu Rashid Tembeleni. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri. Ndugu Rashid Tembeleni ndio yupi kati yenu? Hebu wengine mkae mumwache, haya sawa. *(Makofi)*

Nadhani Waheshimiwa Wabunge mmemwona Ndugu Rashid Tembeleni ambaye ndiye mume wa Mheshimiwa Ummy Nderiananga. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma kutoka *TAWASANET* ambao ni *Engineer* Herbert Kashililah na *Engineer* Gerald Msanja, karibuni sana. Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Yustina Rahhi ambao ni wanafunzi wa *Internship* kutoka *RUWASA* Dodoma wakiongozwa na Ndugu Neema Ndumbaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Florent Kyombo kutoka Misenyi Mkoa wa Kagera ambao ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ndugu Projestus Tegamaisho na Ndugu Judith Projestus na Ndugu Angel Tegamaisho. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka *DSTV* Tanzania wakiongozwa na Ndugu Jackline Oiso, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Edward Olelekaita ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Kiteto na hao ni Ndugu Honest Kamota, ndugu Ibrahim Sindo na Ndugu Hamza Mngia, karibuni sana. Kati yenu Ndugu Honest Kamota ndio yupi?

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Edward Olelekaita anasema huyu alikuwa ni mgombea wa ACT Wazalendo, Jimbo la Kiteto na yeye sasa anafanya kazi kwa karibu sana na Mheshimiwa Mbunge na ametambua kwamba kwa kuwa amemtangulia, basi si mbaya na yeye anafuata nyayo za kufanya kazi naye, kwa sababu wameamua kuliletea Jimbo la Kiteto Maendeleo na siyo kelele za siasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Cecil Mwambe kutoka Shirika la *Relief Partners International* la Kimarekani, wakiongozwa na Ndugu Charles Walter, karibuni sana na kwa namna mama alivyovalia hapo naamini Kiswahili kiko vizuri, kwa hiyo hatuna haja ya kuzungumza Kiingereza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni 37 kutoka Chuo cha Magereza kilichopo Morogoro ambao ni Maafisa Teule daraja la kwanza na Wakufunzi wao saba ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake wakiongozwa na Mkuu wa Chuo hicho *ACP* Lazaro Nyanga, karibuni sana maafisa wetu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 90 kutoka Shule ya Theresia inayomilikiwa na Masista wa Shirika la Moyo Safi wa Maria wa Morogoro ambao ni wanafunzi 75 na Walimu 15 nao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi ama linavyoendesha shughuli zake. Karibuni sana naona na Walimu wao wako pale na wanafunzi karibuni sana. Naona wanafunzi wengine wanazidi kuingia sijajua wao ndiyo wengi au wepi ni wachache, lakini karibuni kwa umoja wenu wote mjifunze. Tunaamini hapo baadaye baadhi ya hao watoto watakuja kuchukua hizi nafasi, lakini siyo sasa hivi maana Wabunge wanakuwa na hofu kidogo. Kwa hiyo watoto watakapokuwa baadaye Wabunge hawa wakiwa wameshamaliza kazi yao.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu, Katibu.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mwongozo wa Spika,

**NDG. EMMANUEL MPANDE – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Katibu subiri kidogo, Mheshimiwa Gambo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 76, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Endelea unataka Mwongozo kwenye hoja gani.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 76 inasema Mbunge anaweza kusimama...

**NAIBU SPIKA:** Usiisome, naifahamu usiwe na wasiwasi, wewe elezea hoja yako.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kuhusiana na tukio ambalo limetokea leo hapa Bungeni kwenye kipindi cha maswali na majibu ambako mimi binafsi kama Mbunge sikuridhika na majibu ambayo yamekuwa yametolewa, hasa ukizingatia kwamba kuna fedha kiasi cha dola milioni 10 kutoka *NSSF* ambazo ni fedha zinatokana na makato ambayo wanakatwa wafanyakazi. Zilipelekwa kwa ajili ya kuendeleza Kiwanda cha *General Tyre.*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha kwenye kiwanda hakuna kilichoendelezwa, fedha hizi za wafanyakazi, hamna ambacho zimefanya. Kwa hiyo, nahitaji kupata maelezo ya Serikali ili kufahamu kwamba je, hizi fedha ziko wapi? Maana kiwanda hakuna, sasa hivi ni miaka kumi na nne toka kile kiwanda kimeacha kufanya kazi, ukizingatia kwamba wafanyakazi wengi sasa hivi wana matatizo makubwa ya kutokulipwa mafao yao na kumbe fedha zimechukuliwa kupelekwa kwenye eneo ambalo hakuna matokeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mwongozo kwamba wakati Serikali inasema kwamba ipo kwenye michakato ya kuendeleza Kiwanda kile cha *TPI,* bado pale kuna eneo limeuzwa la ekari tano kwa kiasi cha fedha kisichopungua bilioni 1.3. Serikali inakuja kuleta maelezo hapa, kilichoko *field* ni kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mwongozo wako kwa sababu haya ni *serious,* tunahitaji ajira za wananchi wetu, tunahitaji pia fedha zetu ziweze kupatikana vizuri. Hivyo, Serikali hapa ilete majibu yanayoeleweka ili tufahamu hizi fedha za wafanyakazi ziko wapi, lakini pia na hatma ya

viwanda hivi ni nini? Maana ni miaka 14 sasa toka 2007. Naomba muongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Gambo hapa kuomba Mwongozo kuhusu jambo ambalo kanuni yetu ya 76 inataka aulize kama hilo jambo linaruhusiwa au haliruhusiwi, ndiyo lengo la Kanuni ya 76. Kwa maana ya kwamba huenda kuna kanuni imevunjwa lakini Mbunge hana uhakika kama kuna kanuni imevunja au hapana, ndiyo Kanuni ya 76.

Kwa hiyo, unakuwa unasema je inaruhusiwa kufanya hivi au hapana, ndiyo lengo. Sasa yeye ameeleza kuhusu kutoridhishwa kwake na majibu ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye kanuni zetu ambazo mnazo kwenye vishikwambi vyenu, mkienda kusoma kanuni ya 51, 52 na 53 zinaeleza kuhusu maswali. Ukizisoma hizo kanuni mtasoma kwa muda wenu Mbunge ambaye anakuwa ameuliza swali la nyongeza halafu kama hakuridhika na majibu yaliyotolewa anaruhusiwa kupeleka hilo swali lake la nyongeza likawe la msingi ili Serikali ilete majibu mahususi kuhusu swali lake.

Sasa kwa namna swali la msingi lilivyokuwa limeulizwa na majibu yaliyotolewa na Serikali yale majibu yako kamili, maswali ya nyongeza yaliyoulizwa yaliyohitaji majibu ya ziada kama Mheshimiwa Mbunge hujaridhika, unapeleka linakuwa swali la msingi ili Serikali ilete majibu mahususi kuhusu swali hilo.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, swali lilijibiwa kikamilifu na yale ya nyongeza kama kuna mahali ambapo taarifa hazijakamilika, basi Mheshimiwa Gambo unaruhusiwa kupeleka swali la msingi ili uletewe majibu mahususi.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - WIZARA YA MAJI

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimwite Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso ili aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Kabla sijasoma hotuba yangu nilikuwa naomba hotuba yote hii iingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Killimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Dkt Christine Ishengoma, ambayo ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha mpango na makadirio ya mapato ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge Mifugo na Maji wakati wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Mpango wa Makadirio wa Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mwaka wa Fedha 2021/2022, yamezingatiwa wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Wizara yangu. Natumia fursa hii kumshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee na kwa masikitiko makubwa ninaomba kwanza kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mama Janeth Magufuli na familia ya Hayati Dkt. John Joseph pombe Magufuli, wewe, Bunge lako Tukufu na wananchi wote kwa ujumla kwa kifo cha aliyekuwa

Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kifo kilichotokea tarehe 17 Machi 2021 Jijini Dar es Salaam. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kutoa pole kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi kwa kifo cha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad. Natoa pole pia kwa familia ya marehemu, ndugu, jamaa, pamoja na watanzania wote kwa msiba wa kuondokewa na aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa Balozi Mhandisi John Kijazi. Aidha, napenda kutoa pole kwako wewe Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa na marafiki wote kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, Mheshimiwa Martha Umbula na aliyekuwa Mbunge wa Muhambwe, Mheshimiwa Atashasta Nditiye. Naomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na moyo wa uvumilivu wafiwa na azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa kilioupata katika Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge na Madiwani uliofanyika mwezi Oktoba, 2020. Aidha, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kwake kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Pia nampongeza kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Dkt Philipo Isidori Mpango kwa kuteuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge kwa kishindo kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaondoe hofu watanzania kwamba hatujaachwa yatima kwa kuondokewa na baba bali tuna mama anayesaidiwa na Makamu wa Rais

ambao ni walezi na viongozi madhubuti wapenda haki, wapenda maendeleo na wapenda wananchi wao na hasa akinamama wanaoguswa moja kwa moja na Wizara yangu. Nina imani kubwa kuwa chini ya uongozi wa sekta ya maji ambayo ni mojawapo wa sekta muhimu kwa maendeleo ya Taifa itasimamiwa kikamilifu na kufikia malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, kwa kuteuliwa tena kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa tena na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mbunge kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa ridhaa kuwa Waziri wa Maji, Wizara inayomgusa kila mwananchi. Nakishukuru Chama changu Chama cha Mapinduzi kwa ushirikiano, maelekezo, maoni na ushauri kinaonipatia wakati wa upangaji na utekelezaji wa mipango katika sekta ya maji. Njia pekee ya kurudisha imani hiyo kubwa ni kuwatumikia wananchi wa Tanzania kwa uadilifu, haki na bila upendeleo. Naahidi kufanya hivyo kwa uwezo wangu wote kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia na naahidi kuwa sitakuwa kikwazo kwa Serikali, chama changu na kwa wananchi wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge kupata huduma ya maji safi salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa hotuba yake nzuri na yenye matumaini aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 22 Aprili, 2021 ambayo pamoja na mambo mengine imebainisha mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya Awamu

ya Sita katika sekta ya maji kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maji; Mhandisi Anthony Damian Sanga; kuwa Katibu Mkuu; na Mhandisi Nadhifa Sadiki Kemikimba; kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo ni dhahiri kuwa wameonekana kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yao ili kufikia malengo ya Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo inatoa dira ya utekelezaji wa kazi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hiyo, imeonesha mwelekeo wa uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 - 2025. Nawapongeza pia, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na Wabunge waliochangia hoja hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa napenda kuchukua fursa hii kutoa maelezo ya hotuba ya bajeti ya Wizara ambayo imejikita katika maeneo yafuatayo:- Hali ya Sekta ya Maji Nchini; Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021; Mafanikio yaliyopatikana; changamoto na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo; mpango na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Sekta ya Maji Nchini; napenda kutoa maelezo kuhusu hali ya Sekta hiyo kwa kuzingatia hali ya rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; na upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya rasilimali za maji; tafiti zilizofanywa na Wizara mwaka 2019 zimeonesha kuwa rasilimali za maji zinazoweza kupatikana kwa mwaka kwa matumizi mbalimbali nchini ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126. Kati ya hizo, mita za ujazo bilioni 105 ni maji juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 ni maji chini ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu milioni 55.9 katika mwaka 2019, kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takriban wastani wa mita za ujazo 2,250. Kiasi hicho ni zaidi ya wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ubora wa maji katika vyanzo vya maji kwa maeneo mengi nchini inaonesha kuimarika. Hiki ni kiashiria kwamba afya ya ikolojia katika vyanzo hivi inaendelea kuimarika na maji yake yanaweza kutumika baada ya kuchakatwa kulingana na matumizi yaliyokusudiwa. Aidha, mifumo yetu ya usambazaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani imeendelea kusambaza maji yanayokidhi viwango vya ubora wa maji vya kitaifa licha ya kuwepo kwa changamoto chache kwenye baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini na Mijini; Serikali imeendelea kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini na mijini hadi mwezi Machi, 2021, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imefikia wastani wa asilimia 72.3 kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwezi Machi, 2020. Kwa upande wa mijini hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi imeongezeka kutoka asilimia 84 mwezi Machi, 2020 hadi asilimia 86 mwezi Machi, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; Hali ya Upatikanaji wa Fedha katika mwaka 2020/21; Fungu 49 – Wizara ya Maji liliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Shilingi 733.284, kati ya fedha hizo Shilingi

28.275 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 705.009 zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili, 2021, Wizara imepokea jumla ya Shilingi 396.771 sawa na asilimia 54.1 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 376.422 ni fedha za maendeleo, sawa na asilimia 53.4 ya bajeti ya maendeleo. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida, kiasi kilichopatikana ni Shilingi 20.349, sawa na asilimia 72.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi na Programu Mbalimbali zilizotekelezwa katika mwaka 2020/2021; Wizara imeendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maji nchini kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inayolenga kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Hali ya utekelezaji wa miradi na programu hizo katika mwaka 2020/2021 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; rasilimali za maji nchini zinasimamiwa na kuendelezwa kupitia Bodi za Maji za Mabonde tisa ambazo zina majukumu ya kutathmini na kufuatilia rasilimali hizo; Kuhifadhi na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji; Kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo; na Kuendeleza rasilimali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu hayo. Wizara imejenga na kukarabati vituo 159 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji; Imeweka mipaka katika vyanzo vya maji 25; Imetoa vibali vya matumizi ya maji 1096; na Imefanya usanifu kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa mawili na malambo sita ya maji. Maelezo ya kina kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji yanapatikana ukurasa wa 12 hadi 28 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Ubora wa Maji; Usimamizi wa Ubora wa Maji; Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuhakiki kufuatilia ubora na usalama wa maji katika vyanzo na mitandao ya kusambaza maji kwa lengo la kulinda afya ya jamii na ikolojia. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara iliendelea kuhakiki ubora

wa maji nchini katika vyanzo kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, umwagiliaji, ujenzi na utafiti pamoja na ubora wa maji taka yanayorudishwa katika mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Wizara iliendelea na utekelezaji wa mkakati wa uondoaji wa madini ya *fluoride* kwenye maji ya kunywa na kupikia katika mikoa iliyoathirika zaidi na madini hayo ya *fluoride.* Ubora wa madawa ya kutibu na kusafisha maji na kuimarisha maabara za maji ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi. Maelezo ya kina kuhusu huduma za ubora wa maji yanapatikana katika ukurasa 28 hadi 34 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini, kwa Mwaka 2020/2021, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 1,169. hadi kufikia mwezi Machi, 2021 miradi 355 yenye vituo 6,687 vya kuchotea maji umekamilika na wananchi 1,984,575. Wahishio vijijini Utekelezaji wa miradi hiyo umegarimu kiasi cha shilingi bilioni 154,659. Aidha, utekelezaji wa miradi 814 iliyobaki unaendelea na upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Miradi yenye Changamoto za Muda Mrefu, katika kuhakikisha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini inakuwa bora na endelevu, Serikali imekuwa ikifanya maboresho ya kimuundo na kisheria. Hapo awali, hali ya utoaji huduma ya majina usafi wa mazingira hususan vijijini na kwenye Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo haikuwa ya kuridhishakutokana na changamoto za usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji. Hali hiyo kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na mfumo uliokuwepo, ambapo usimamizi na utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Maji ulikuwa kwenye Wizara mbili tofauti ambazo ni Wizara ya Maji na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo husababisha mlolongo mrefu katika kuchukua hatua kunapotokea ukiukwaji wa taratibu za kiutumishi au kiutendaji. Kufuatia

changamoto hizo za kimfumo, tarehe 10 Mei, 2018 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya maamuzi ya kisera na kuelekeza kuhamishwa kwa majukumu ya utoaji wa huduma za maji kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI kwenda Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maamuzi hayo, Serikali ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) unaohusika katika ujenzi wa miradi na usimamizi wa huduma ya maji vijijini. Kuanzishwa kwa Wakala huo kumeenda sambamba na kurithi miradi yote ya maji ikiwemo ile miradi ya *program* ya vijiji 10 iliyokuwa inatekelezwa chini ya Halmashauri za Wilaya. Baadhi ya miradi hiyo iliyorithiwa imekuwa na changamoto ya kutokukamilika kwa wakati na mingine kukamilika bila kutoa maji. Jumla ya miradi 177 ilibainika kuwa na changamoto hizo ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2021, jumla ya miradi 85 imepatiwa ufumbuzi na kugharimu jumla ya Shilingi 66,923 miradi hiyo tayari imeanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na miradi ya maji ya Ntomoko – Dodoma, Nyamtukuza – Geita, Mibono – Tabora, Rugeye – Mwanza, Malinyi – Morogoro, Muze group – Rukwa, Kinesi – Mara na Imalabupina-Ichwankima – Geita, na Mtomoko Shinyanga. Ukwamuaji wa Miradi hiyo unaendelea kwa kutumia Timu Maalam za Wataalam na tumezipa jina maarufu kama "*Water Rescue Team*" maelezo ya kina kuhusu huduma za usambazi maji safi na usafi wa mazingira vijijini inapatikana katika ukurasa wa 34 hadi 40 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji inayolenga kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji hadi mwezi Machi 2021 miradi 177 ya maji imeendelea kutekelezwa katika Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji midogo na Miradi ya Kitaifa. miradi miradi 67

imekamilika kwa gharama ya shilingi 759,211na utekelezaji wa miradi 110 upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika jiji la Arusha, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Jiji la Arusha unaogharimu takribani Shilingi bilioni 520 hadi mwezi Machi 2020/2021 utekelezi wa mradi umefikia wastani wa asilimia 62 na unatarajia kukamilika mwezi Oktoba 2021 kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 hadi mita milioni 200 kwa siku muda wa upatikanaji wa huduma majisafi kutoka saa kumi na mbili za sasa hadi saa 24 kwa siku pamoja na kuongeza huduma ya uondoshaji majitaka kutoka asilimia 7.6 za sasa hadi asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dodoma, baada ya Serikali kuhamia Dodoma ni bayana kwamba mahitaji ya maji yameongezeka na kwa sasa yanakadiriwa kuwa zaidi mita za ujazo laki moja na tatu kwa siku ambapo uzalishaji wa sasa ni mita za ujazo 66,600 kwa siku. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma kwa kutekeleza miradi wa kutoa maji katika visima vya Ihumwa kwenda Tanki la Njedengwa ambao unagharimu Shilingi bilioni 2.4. ambao utekelezi wake umefikia wastani wa asilimia 70 na Ujenzi wa tanki la maji lenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 2.5 katika eneo la Chamwino ambao umefikia wastani wa asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha uchimbaji wa visima nane na ukarabati wa na visima vitatu umekamilika, vile vile, Serikali imeanza kuchukuwa hatua za muda mrefu zinazolenga kuondoa adha ya upatikanaji kwa kuanza maandalizi ya mradi ya kutoa maji ziwa Vitoria kuleta jijini Dodoma hadi mwezi Machi 2020/2021 upembuzi wa awali umekamilika na taratibu za kumpata mtaalam ushauri

atakayefanya upembuzi yakinifu yaani *Feasibility Studies* na usanifu wa kina yaani *Detailed Design* zinaendelea. Aidha, taarifa za wa awali imeonesha maeneo yatakayonufaika mradi huo ni pamoja na baadhi ya maeneo ya mikoa ya Singida na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa maji Tabora Igunga Nzega, kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya *Exim*-India imetekeleza mradi wa upanuzi wa mtandao wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na vijiji 102 vilivyopo umbali wa kilometa 12 pembezoni mwa bomba kuu kwa gharama ya takriban Shilingi bilioni 617. Mradi huounauwezo wa kuzalisha kiasi cha mita za ujazo 54,145 kwa siku na kuhudumia zaidi ya wakazi milioni 1.2 wa maeneo mbalimbali yanayopitiwa na mradi, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mradi huo unatoa huduma kwa wanufaika na ulizinduliwa rasmi tarehe 30 Januari, 2021 na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, pia tumepewa maelekezo mahususi na Rais sasa Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan maji haya kuyapeleka Kaliua, Urambo mpaka Sikonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria Kwenda Miji ya Tinde na Shelui Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya *Exim* inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji ya Tinde na Shelui. Mradi huounatekelezwa kwa gharama ya takriban Shilingi bilioni 24.752. Usanifu wa mradi huo umekamilika na utiaji saini wa Mkataba wa ujenzi ulifanyika tarehe 25 Februari 2021. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe unatekelezwa katika miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 38 vilivyomo kandokando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*, *OFID*, *SAUDI Fund* na Kuwait Fund. Mradi utakapokamilika utazalisha

maji lita milioni103.7 kwa siku na utawanufaisha wananchi wapatao 438,930.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 25 Desemba, 2020 Wizara ilisitisha mikataba kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huo baada ya kuonekana wakisuasua katika ukamilishaji wa mradi. Wizara imeamua kwamba sehemu ya utekelezaji wa mradi inayohusu miundombinu ya usambazaji itafanyika kwa utaratibu wa *Force Account* kutumia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ili kukamilisha kwa haraka kazi hizo. Aidha, kwa kazi nyingine taratibu za manunuzi ya kumpata mkandarasi atakayekamilisha mradi unaendelea. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021 na utaondoa kero ya maji ya muda mrefu kwa wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Isimani – Kilolo, Serikali inatekeleza mradi wa maji wa Isimani – Kilolo kwa gharama ya shilingi bilioni 9.2 na unahusisha kupeleka maji katika vijiji 29 vya Wilaya za Kilolo vijiji 5 na Wilaya ya Iringa vijiji 24. Mradi huo umesanifiwa kuhudumia wananchi wapatao 80,000 ifikapo mwaka 2038. kufikia Machi 2021, wastani wa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 37 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28, itakumbukwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na mji mmoja visiwani Zanziba unaogharimu dola za marekani milioni 500 kufikia mwezi Machi 2021, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi zimekamilikana wakandarasi watakuwa maeneo ya miradi mwishoni mwezi Mei 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niyataje maeneo ambayo yatatekelezwa miradi katika miji hiyo 28 ikiwemo Geita, Chato, Mgumu, Roriya, Tarime, Kayanga, Kasulu, Chamwino Chemba, Manyoni, Singida, Kiomboi, Urambo na

Kaliua, Sikonge, Mpanda, Nanyumbu, Makonde, Mafinga, Wanging'ombe, Makambako, Njombe, Lujewa, Chunya, Songea, Ifakara, Kilwa Masoko, Pangani, Muheza, Handeni, Korongwe, *rrunk main*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa, Serikali imeanza kutekeleza miradi ya kutoa maji kwenye Maziwa Makuu ya Victoria Tanganyika na Nyasa kupeleka kwenye vijiji vilivyomo kando kando ya maziwa hayo hadi mwezi machi, 2021 usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni miradi ya kutoa maji ya Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika umekamilika, mradi wa Ziwa Victoria unatarajia kuhudumia wananchi milioni 2,854,292 kwenye vijiji 300 na mradi wa Ziwa Tanganyika utawahudumia wananchi 616,000 wa vijiji 73 utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwenye baadhi ya vijiji kwa upande wa Ziwa Nyasa usanifu wa kina wa mradi unaendelea na unatarajia kukamilika mwezi Juni 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine inayotekelezwa miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi katika Mkoa wa Simiyu, miradi ya kuboresha huduma ya maji safi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani ya Kibaha, Kisarawe, Mkulanga, Chalinze na Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Mugango-Kiabakari Butiama pamoja na mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Mji wa Hokasment maelezo ya kina kuhusu huduma ya usambazaji wa majisafi na usafi wa mazingira mijini yanapatikana ukurasa wa 40 hadi 60 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya maji ni pamoja Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kutoka asilimia

70.1 vijijini na 84 mijini mwaka 2019/2020 hadi asilimia 72.3 vijijini na 86 mijijni; Kuzinduliwa kwa miradi mikubwa ya maji ya Tabora – Igunga - Nzega pamoja na Isaka – Kagongwa baadaya kazi kubwa ya utekelezaji wake kukamilika; Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 422 ya maji ambapo kati ya miradi hiyo ya vijijini ni miradi 355 na mijini miradi 67; Kuanza kutoa huduma ya maji kwa miradi 85 iliyokuwa na changamoto baada ya kupata ufumbuzi. Kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji na kupungua kwa gharama za ujenzi kutokana na kutumia *force account* ambapo zaidi ya miradi 150 imetekelezwa na kuongezeka kwa idadi ya maabara za ubora wa maji zenye sibati kutoka moja ya Mwanza hadi kufikia saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojitokeza na hatua zinazochukuliwa, pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021 Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa vyanzo vya maji, uhitaji mkubwa wa fedha za kutekeleza miradi ya maji, utendaji usioridhisha wa wakandarasi na watendaji, mwamko mdogo wa wananchi kulipia huduma ya maji kwa imani kubwa kwamba maji yanatoka kwa Mungu mabomba tu ndiyo yanatoka kwa mzungu na upungufu wa Wataalam wa Sekta ya Maji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wizara inaendelea kuchukua hatua kukabiliana na changamoto hizo ikiwa pamoja na kuchukua hatua kali kwa wakandarasi na watendaji wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao kuimarisha vyombo vya utoaji huduma na kutoa elimu kwa wananchi maelezo ya kina kuhusu changamoto na hatua zinachukuliwa yameonyeshwa katika ukurasa 75 hadi 79 ya hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa utekelezaji kwa Mwaka 2021/2022 napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mpango wa Utekezaji wa miradi ya maji kwa mwaka 2021/2022 umeshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge katika kuibua miradi ya

kipaumbele. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na Ofisi ya Rais TAMISEMI katika kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi ya maji katika Halmashauri za Wilaya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimatumaini yangu kwamba utaratibu huu utawezesha kufikia malengo ya sekta ya maji kwa haraka na uhalisia. Mpango na Bajeti umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2016 – 2030, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Sera mbalimbali za Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2020 – 2025) na Maagizo na ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais na Viongozi wengine wa Kitaifa; pamoja na maoni ya waheshimiwa Wabunge kama nilivyotangulia kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali imepanga kuendelea kuweka msisitizo katika usimamizi wa watendaji, uvunaji wa maji ya mvua hususan kwenye maeneo kame, usimamizi wa Vyombo vya Utoaji Huduma za Maji Vijijini (*CBWOs*), kutumia Chuo cha Maji kikamilifu na kuimarisha kitengo cha uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za maji Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa takwimu za hali ya rasilimali za maji, kusimamia utoaji wa vibali vya matumizi ya maji, usimamizi wa huduma za ubora wa maji na miradi ya majisafi na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali imepanga kutekeleza jumla ya miradi 1,527 ya maji katika maeneo ya vijijini na miradi 114 ya mijini ikihusisha miradi mipya, miradi ya upanuzi na ukarabati wa miundombinu. Vile vile, Serikali imepanga kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya maji vya Maziwa Makuu pamoja na mito ya Rufiji, Ruvuma na Kiwira mwaka wa fedha 2021/2022, Mto Rufiji na Mto Ruvuma, Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miundombinu ya kupeleka maji katika miji iliyo karibu na mito hiyo. Aidha, Serikali itaanza mradi wa maji kutoka maji ya mto Kiwila kupeleka katika jiji la Mbeya,

maelezo ya kina kuhusu mpango wa utekelezaji unapatikana katika hotuba yangu ukurasa wa 80 hadi 84.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, ninapenda kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa njia moja ama nyingine kufanikisha majukumu ya sekta ya maji katika kipindi cha mwaka 2020/2021. Shukrani hizo ziwaendee nchi marafiki, Uingereza, Ujerumani, Korea Kusini, Marekani, India, Uholanzi, Hispania, Ubelgiji, Ufaransa, Kuwait, Misri, Morocco na Saudi Arabia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kuyashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kitaasisi za Kimataifa za maendeleo ya Kimataifa, mifuko ya maendeleo idara mbalimbali za maendeleo ya kimataifa mashirika ya nchi wahisani na mashirika ya kimataifa napenda kuwashukuru mashirika na Taasisi za Kidini pamoja na taasisi zisizo za kiserikali kwa michango yao katika sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Mhandisi nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi Mbunge Naibu Waziri wa Maji; Mhandisi Anthony Damian Sanga, Katibu Mkuu; Mhandisi Nadhifa Sadiki Kemikimba, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wataalam na Watumishi wote wa Wizara ya Maji; pamoja na Watumishi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru familia yangu kwa upendo, ushirikiano na faraja pia bila kumsahau mama yangu mzazi Fatma Omary Masanga, mama Ntilie ambaye umenizaa mimi mtoto leo kijana wako nipo hapa katika Bunge ahsante sana mama yangu Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niweze kutoa shukrani zangu kwa watangulizi wangu Mheshimiwa Aloyce Kamwelwe aliyekuwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Professa Makame Mbalawa na pia aliyekuwa Katibu Mkuu wetu

Professa Kitila Mkumbo waswahili wanasema ukimuona kobe juu ya mti amepandishwa hapandi mwenyewe ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maombi ya Fedha Kwa Mwaka 2021/2022 baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 680,388,976,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2021/2022. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 33,758,976,000 ambapo shilingi 15,273,812,000 sawa na asilimia 45.2 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo *(OC)* na shilingi 18,485,164,000 sawa na asilimia 54.8 ni kwa ajili ya kulipa mishahara *(PE)* ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni shilingi 646,630,000,000 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 346,630,000,000 sawa na asilimia 53.6 ni fedha za ndani na shilingi 300,000,000,000 sawa na asilimia 46.4 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa kwako kamati ya kudumu ya kilimo mifugo na maji na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.maji.go.tz.

## HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI MHE. JUMAA HAMIDU AWESO(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA2021/2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika**, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekitiwa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo**, **Mifugo na Maji, Mheshimiwa Daktari Christine Ishengoma (Mb),**ambayo ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2021/22.

**2. Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugona Maji** wakati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2020/21 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2021/22 yamezingatiwa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu. Natumia fursa hii kumshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya.

**3. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee ninaomba kwanza kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mama Janeth Magufuli na Familia ya Hayati Daktari John Pombe Joseph Magufuli, wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, na wananchi wote kwa ujumla kwa kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati **Daktari John Pombe Joseph Magufuli** kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021 Jijini Dar es Salaam. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. **Amina**.

**4. Mheshimiwa Spika**,vilevile, naomba kutoa pole kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kifo cha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, **Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad**. Natoa pia pole kwa Familia ya marehemu, ndugu pamoja na watanzania wote kwa msiba wa kuondokewa na aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa **Balozi Mhandisi John WilliamHerbert Kijazi.** Aidha, ninatoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, Familia za marehemu, Ndugu na Watanzania wote kwa misiba ya kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, **Mheshimiwa Martha Umbula** na aliyekuwa Mbunge wa Muhambwe, **Mheshimiwa Atashasta Nditiye**. Naomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na moyo wa uvumilivu wafiwa na azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. **Amina**.

**5. Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Chama cha Mapinduzi (CCM)

kwa ushindi mkubwa kilioupata katika uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika mwezi Oktoba 2020. Aidha, ninampongeza kwa dhati **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwa kuapishwa kwake kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ninampongeza **Mheshimiwa Daktari Philip Isdor Mpango** kwa kuteuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge kwa kishindo kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwaondoehofu watanzania kwamba hatujaachwa yatima kwa kuondokewa na **BABA** bali tuna **MAMA akisaidiana na Makamu wa Rais** ambaoniwalezi madhubuti, wapenda haki, wapenda maendeleo na wapenda wananchi wao na hasa kinamama wanaoguswa moja kwa moja na Wizara yangu. Nina imani kubwa kwamba chini ya uongozi wao sekta ya maji ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa itasimamiwa kikamilifu na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**6. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa,** Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, kwa kuteuliwa tena kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu kwa Muhula wa Pili ni ishara kwamba utumishi wake ni wa kutukuka.

**7. Mheshimiwa Spika**,ninaomba nikupongeze sana wewe binafsi kwa kuchaguliwa tena na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mheshimiwa Daktari Tulia Ackson (Mb)** kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Naibu Spika.Nawapongeza pia, Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwenu kuwa Wabunge wa Bunge la **12** la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**8. Mheshimiwa Spika**,vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzaniakwa kuniamini na kunipa ridhaa ya kuwa Waziri wa Maji, Wizara inayomgusa kila mwananchi. Sina njia ya kurudisha imani hiyo kubwa isipokuwa kuwatumikia wananchi wa Tanzania kwa uadilifu, haki na bila upendeleo. Ninaahidi kufanya hivyo kwa

uwezo wangu wote kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.Aidha, nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa Hotuba yake hapa Bungeni tarehe 22 Aprili 2021 ambayo pamoja na mambo mengine imebainisha muelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya maji kwa kipindi cha mwaka 2021-2025. Maelekezo yake nimeyapokea na mimi pamoja na viongozi wenzangu ndani ya Wizara tutahakikisha kuwa malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi yanafikiwa.

9. **Mheshimiwa Spika**,nitumie fursa hii, kuwapongeza **Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca WinfriedMahundi (Mb)** kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Maji, **Mhandisi Anthony Damian Sanga** kuwa Katibu Mkuu na **Mhandisi Nadhifa Sadiki Kemikimba** kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yangu. Kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo ni dhahiri kuwa wameonekana kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yao katika Sekta ya Maji.

10. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa**(Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa bungeni ambayo inatoa dira ya utekelezaji wa kazi za Serikali na kulikuwa na hoja za Wizara yangu. Hotuba hiyo, imeonesha mwelekeo wa uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 - 2025. Nawapongeza pia, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na wabunge waliochangia hoja hizo.

11. **Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, napenda sasa kutoa maelezo ya hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ambayo imejikita katika maeneo yafuatayo:-Hali ya Sekta ya Maji Nchini; Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21; Mafanikio yaliyopatikana; Changamoto na Hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo; Mpango kwa mwaka 2021/22; Shukrani na Maombi ya fedha kwa mwaka 2021/22.

# 1. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI

**12. Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa maelezo kuhusu hali ya Sekta ya Maji nchini kwa kuzingatia hali ya rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; na upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini.

## 1.1. Hali ya Rasilimali za Maji

**13. MheshimiwaSpika**, tafiti zilizofanywa na Wizara mwaka 2019 zimeonesha kuwa rasilimali za maji zinazoweza kupatikana kwa mwaka kwa matumizi mbalimbali nchini ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126. Kati ya hizo, mita za ujazo bilioni 105 ni maji juu ya ardhi na mita za ujazo bilioni 21 ni maji chini ya ardhi. Kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu milioni 55.9 katika mwaka 2019, kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni wastani wa mita za ujazo 2,250. Kiasi hicho ni zaidi ya wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.

**14. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Oktoba 2020, mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini yalikadiriwa kuwa ni takribani mita za ujazo **bilioni 60** kwa mwaka. Mahitaji hayo ya maji yanatarajiwa kuongezeka hadi kufikia wastani wa mita za ujazo **bilioni 90** kwa mwaka ifikapo mwaka 2035. Hali hiyo inaonesha kuwa ni lazima juhudi za makusudi zichukuliwe katika kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za maji, kuendelea kuhamasisha matumizi yenye ufanisi, teknolojia zinazotumia maji kidogopamoja na kuvuna maji ya mvua ili kuongeza upatikanaji wa maji katika kipindi cha kiangazi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

**15. MheshimiwaSpika**, vilevile, wastani wa kiwango cha mvua nchini kwa mwaka wa kihaidrolojia (Novemba 2019 – Oktoba 2020) kilikuwa **milimita 1,470** ambacho ni juu ya wastani wa muda mrefu wa milimita 921 kwa mwaka. Hali hiyo imesababisha kiasi cha maji katika mito, mabwawa na maziwa kuendelea kuimarika katika maeneo mbalimbali nchini.

### 1.2. Hali ya Huduma za Ubora wa Maji

**16. Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa ubora wa maji ni mojawapo ya mambo muhimu katika kutimiza malengo ya kitaifa na kimataifa katika kulinda vyanzo vya maji na viumbe hai waishio ndani ya maji pamoja na ulinzi wa afya ya binadamu.Katika kutimiza hilo Wizara kupitia maabara zake 16 za ubora wa maji nchini pamoja na Kituo cha Utafiti wa Kuondoa Madini ya *Fluoride*-Ngurdoto imeendelea kuhakiki ubora na usalama wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji mijini na vijijini kwa lengo la kutoa maamuzi juu ya matumizi kwa kuzingatia viwango vya ubora wa maji kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**17. Mheshimiwa Spika**, hali ya ubora wa maji katika vyanzo vya maji kwa maeneo mengi nchini inaonesha kuimarika. Hiki ni kiashiria kwamba afya ya ikolojia katika vyanzo hivi inaendelea kuimarika na maji yake yanaweza kutumika baada ya kuchakatwa kulingana na matumizi yaliyokusudiwa. Aidha, Wizara imeweza kuainisha viashiria vya ubora wa maji juu na chini ya ardhi ambavyo ni changamoto chache katika baadhi ya maeneo nchini. Kwa upande wa maji juu ya ardhi changamoto kubwa ni uwepo wa kiwango kikubwa cha *Nitrogen*, *Phosphorous*, tope (*turbidity*) pamoja na vimelea vya vijidudu vinavyosababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji. Kwa upande wa maji chini ya ardhi changamoto ni uwepo wa kiwango kikubwa cha chumvichumvi, tindikali (*acidity*), *Nitrate*, madini ya *Fluoride*, Chuma, *Manganese* na *Chloride*.

**18. Mheshimiwa Spika**, mifumo yetu ya usambazaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani imeendelea kusambaza maji yanayokidhi viwango vya ubora wa maji vya kitaifa licha ya kuwepo kwa changamoto kwenye baadhi ya maeneo. Changamoto hizo ni pamoja na uwepo wa madini ya *fluoride* kwenye ukanda unaopitiwa na Bonde la Ufa katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida na Shinyanga; na madini ya chumvichumvi kwenye maeneo ya Pwani na Ukanda wa Kati katika mikoa ya Dodoma na Singida. Katika kukabiliana na changamoto za ubora wa maji

yanayosambazwa, Wizara imeendela kuwekeza katika uimarishaji wa miundombinu ya kusafisha na kutibu maji ikiwa ni pamoja na kuweka mitambo inayotumia teknolojia za kisasa zenye uwezo wa kupunguza madini na chumvichumvi kufikia viwango vinavyokubalika kwa matumizi ya binadamu.

### 1.3. Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya MajiVijijini

**19. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini. Lengo ni kuhakikisha kuwa huduma ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi inafikia zaidi ya **asilimia85** ifikapo mwaka 2025. Hadi kufikia Machi, 2021 hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imefikia wastani wa **asilimia 72.3** kutoka wastani wa **asilimia 70.1** mweziMachi,2020. Kiwango hicho kinatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi mipya, ukarabati na upanuzi wa miradi **355**.

### 1.4. Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

**20. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya maji mijini hufanyika kupitia Programu ndogo ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Mijini. Kutokana na utekelezaji wa miradi ya maji, hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi imeendelea kuimarika na wakazi wengi zaidi wameendelea kupata huduma za maji. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi katika maeneo ya mijini imeongezeka kutoka **asilimia 84** mwezi Machi, 2020 hadi **asilimia 86** mwezi Machi, 2021.

**21. Mheshimiwa Spika**, hali ya huduma ya uondoshaji majitaka imefikia **asilimia13** mwezi Machi 2021. Mtandao wa majitaka umeongezeka kutoka **kilomita 844** za mwaka 2019/20 hadi **kilomita954.8** mwezi Machi 2021 na maunganisho kutoka **49,864** hadi **53,008**. Hadi sasa, miundombinu ya uondoshaji wa majitaka imejengwa katika miji 11 ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tabora, Moshi, Tanga, Songea na Iringa. Vilevile, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya uondoaji majitaka katika

miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Musoma na Bukoba. Aidha, katika miji mingine huduma ya uondoaji wa majitaka inatolewa kwa kutumia magari ya majitaka na kutiririshwa kwenye mabwawa au maeneo yaliyotengwa na Halmashauri husika.

## 2. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2020/21

### 2.1. Hali ya Upatikanaji wa Fedha

**22. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Fungu 49 – Wizara ya Maji iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 733,284,075,000**;kati ya fedha hizo **Shilingi 28,275,145,000** zilikuwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 705,008,930,000**zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2021, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 396,771,027,717.02**sawa na **asilimia 54.1** ya bajeti. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 376,421,602,120.50**nifedha za maendeleo sawa na **asilimia 53.4** ya bajeti ya maendeleo. Kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida, jumla ya **Shilingi 20,349,425,596.52**zilipokelewa sawa na **asilimia 72** ya bajeti ya fedha za Matumizi ya Kawaida.

### 2.2. Miradi na Programu Mbalimbali Zilizotekelezwa katika Mwaka 2020/21

**23. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekelezamiradi na programu mbalimbali za maji nchini kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Aidha, Serikali kwa Kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza Mradi wa Kusaidia Sekta ya Maji Awamu ya Pili ( *Second Water Sector Support Project – WSSP II*) unaogharimu takribani **Shilingibilioni 537.073** kwa lengo la kuimarisha uwezo wa upangaji na usimamizi wa rasilimali za maji; kuboresha upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo yanayohudumiwa na DAWASA; na kujenga uwezo kwa watekelezaji. Hali ya utekelezaji wa miradi na programu hizo katika mwaka 2020/21na mafanikio yaliyopatikana katika maeneo ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji;huduma za ubora wa maji; huduma za usambazaji maji vijijini; huduma za usambazaji

majisafi na usafi wa mazingira mijini;nautekelezaji wa kazi mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Wizara na masuala mtambuka ni kama ifuatavyo:-

### 3.2.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

**24. Mheshimwa Spika**, rasilimali za maji nchini zinasimamiwa na kuendelezwa kupitia Bodi za Maji za Mabonde **tisa** ambazo zimepewa majukumu ya kufanya tathmini na ufuatiliaji wa rasilimali hizo; kuhifadhi na kuthibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji; kugawa maji kwa sekta mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji na kiasi cha maji kilichopo; na kuendeleza rasilimali za maji.

**(i). Tathmini na Ufuatiliaji wa Rasilimali za Maji (a) Mwenendo wa Rasilimali za Maji**

**25. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu kwa sasa ina vituo **1,175**vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji vilivyojengwa katika maeneo mbalimbali nchini kwenye mabonde ya Pangani vituo 162, Ziwa Tanganyika 59, Ziwa Nyasa 85, Wami/Ruvu 227, Ruvuma na Pwani ya Kusini 93, Ziwa Rukwa 99, Ziwa Victoria 118, Rufiji 226 na Bonde la Kati vituo 106. Hadi mwezi Machi 2021, jumla ya vituo **159** kati ya **180** vilivyopangwa vimekarabatiwa katika Mabonde ya Ziwa Tanganyika vituo **7**, Wami-Ruvu **21**, Ziwa Nyasa **16**, Ziwa Rukwa **17**, Pangani **17**, Rufiji **35**, Ruvuma **27**, Ziwa Victoria **9** na Bonde la Kati vituo **10**.

**(b) Ugawaji wa Rasilimali za Maji na Udhibiti wa Migogoro**

**26. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde ina jukumu kubwa la kuhakikisha maji yanagawiwa kwa sekta zote za kijamii, kiuchumi na mazingira kwa haki, usawa na uwazi ili sekta ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kulingana na mahitaji kwa kuzingatia rasilimali zilizopo. Hadi mwezi Machi 2021, jumla ya vibali vipya **1,096**vya matumizi ya maji vimetolewa na kufikisha jumla ya vibali **11,311** vilivyotolewa.Uwepo wa vibali hivyo unasaidia katika uratibu na kuwa na takwimu sahihi za matumizi ya maji. Niwahimize wananchi wote kwa ujumla wanaotaka

kuchukua maji kutoka katika vyanzo mbalimbali wafahamu kuwa wanao wajibu wa kisheria wa kuomba vibali vya matumizi ya maji hayo kutoka katika Bodi za Maji za Mabonde.

**27. Mheshimiwa Spika**, udhibiti na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya maji umeendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini kupitia Bodi za Maji za Mabonde kwa kushirikiana na Jumuiya za Watumiaji Maji. Katika mwaka 2020/21 jumla ya migogoro **22** ya matumizi ya maji ilijitokeza katika Mabonde ya Pangani **minne (4)**, Wami/Ruvu **10**, Ziwa Nyasa **miwili**, na Ziwa Tanganyika **6** ambapo migogoro **16** imetatuliwa (Pangani **mitatu**, Nyasa **mmoja**, Wami - Ruvu **6** na Ziwa Tanganyika **6**) na migogoro **6** (Pangani **mmoja**, Wami – Ruvu **minne** na Nyasa **mmoja**) inaendelea kutafutiwa ufumbuzi. Aidha, elimu kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 imeendelea kutolewa kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kuepusha migogoro katika matumiziya rasilimali za maji.

### (c) Udhibiti wa Uchimbaji Holela wa Visima

**28. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uchimbaji holela wa visima, Wizara imeendelea kuratibu na kusajili kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima pamoja na kutoa leseni na vibali vya uchimbaji kwa makampuni yanayokidhi vigezo. Hadi mwezi Machi 2021,jumla ya leseni **25** za uchimbaji na leseni **3** za utafiti zimehuishwa na vibali **465** vya kuchimba visima vya maji katika maeneo mbalimbali nchini vimetolewa.

### (d) Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji

**29. Mheshimiwa Spika**, uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji unahusisha utambuzi wa vyanzo, uwekaji wa mipaka na kutangaza maeneo/vyanzo hivyo katika Gazeti la Serikali kama maeneo tengefu. Ili kuimarisha usimamizi, Wizara imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuunda Jumuiya za Watumia Maji na kuanzisha majukwaa ya watumia maji kwa lengo la kuwashirikisha wananchi katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009.

**30. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2021, vyanzo vya maji **25** kati ya **45** vilivyopangwa vimewekewa mipaka kama hatua ya awali ya uhifadhi katika mabonde ya Ruvuma chanzo **kimoja**, Rufiji **4**, Pangani **12**, Ziwa Rukwa **2**, Ziwa Nyasa **2**, Wami/Ruvu **2**na bonde la Kati vyanzo viwili **2**. Vyanzo vya maji **27** viko katika mchakato wa kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kama maeneo tengefu. Hadi sasa Wizara imetambua vyanzo vya maji **1,213**, kuweka mipaka vyanzo **133** na kuvitangaza vyanzo **18** kwenye Gazeti la Serikali ili vilindwe kisheria.

**31. Mheshimiwa Spika**, utunzaji wa vyanzo vya maji na usimamizi endelevu wa matumizi ya maji ni jukumu la kila mmoja wetu. Hata hivyo, katika muundo wa kitaasisi, Wizara huziunda na kuzitumia jumuiya za watumia maji ambazo huwa na jukumu la kushirikisha jamii katika maeneo ya vyanzo ili kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa na maji yanatumika kwa njia sahihi. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, jumuiya **9** za watumia maji zimeanzishwa katika mabonde ya Ruvuma **2**, Ziwa Tanganyika **3**, Ziwa Rukwa **1**, Ziwa Nyasa **2** na Ziwa Victoria **1** na kufanya jumla ya Jumuiya za Watumia Maji zilizoundwa mpaka sasa kufikia **139.** Aidha, kamati **3** za vidakio vya maji (*Catchment Water Committees*) zimeanzishwa katika Mabonde ya Ziwa Victoria **1**, Wami/Ruvu **1** na Ziwa Rukwa **1** na hivyo jumla ya Kamati za Vidakio vya Maji zilizoundwa kufikia **8;** Rufiji **2**, Pangani **2**, Ziwa Victoria **2**, Wami Ruvu **1** na Ziwa Rukwa kidakio **kimoja**.

### (e) Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji

**32. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji unaotokana na kemikali za kuchakata madini na mali ghafi za viwandani, Wizara imeendelea na ukaguzi wa mara kwa mara katika viwanda na migodi. Kwa Viwanda na migodi ambavyo majitaka yake yanakidhi viwango vinavyokubalika, vibali vya kutiririsha majitaka kwenye mazingira vimeendelea kutolewa. Hadi mwezi Machi 2021, vibali **8** vya kumwaga majitaka vimetolewa ambapo Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria imetoa vibali **3** na Bonde la

Ziwa Tanganyika vibali **5**. Idadi hiyo inafikisha jumla ya **vibali 167** vilivyotolewa hadi sasa katika mabonde yote.

**(f) Mradi wa Kunusuru Vyanzo vya Maji kupitia Mpango Endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhikatika Mabonde Madogo ya Mito ya Zigi na Ruvu**.

**33. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Kunusuru Vyanzo vya Maji kupitia Mpango Endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Mabonde Madogo ya mto Zigi na Ruvu unatekelezwa katika Milima ya Uluguru na Usambara Mashariki ambayo ni vyanzo muhimu vya maji katika mito hiyo. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na unalenga kunusuru vyanzo vya maji kwa kuimarisha uwezo wa jamii katika kuanzisha shughuli mbadala za kiuchumi na kuhamasisha utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Hadi mwezi Machi 2021, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya matumizi bora ya ardhi; kuanzisha mfuko wa kusaidia usimamizi wa matumizi bora ya ardhi; kuanzisha mashamba darasa matatu ya kilimo; ununuzi wa mizinga ya nyuki; ujenzi wa majiko sanifu na banifu; ujenzi wa tanki la kuvunia maji ya mvua lenye ujazo wa lita 8,000 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji wa mbogamboga; na uhamasishaji wa ufugaji bora wa kuku na ng'ombe wa maziwa.

**(ii).Uendelezaji wa Rasilimali za Maji (a) Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

**34. Mheshimiwa Spika**, Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji ni hitaji la kisera na kisheria linalolenga kupanga, kusimamia, kutunza na kuendeleza rasilimali za maji kwa kushirikisha wadau mbalimbali katika ngazi zote. Hadi mwezi Machi 2021, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mipango kwa Mabonde **7**ambayo ni Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, Mto Rufiji, Bonde la Kati na Bonde la Wami/Ruvu. Aidha, maandalizi ya Mpango katika Bonde la Ziwa Victoria yanaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2021 na kwa Bonde la Pangani Wizara inaendelea kufatuta fedha

kwa ajili ya maandalizi ya mpango huo. **(b) Utafutaji wa Vyanzo Vipya vya Maji**

**35. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha wananchi waishio mijini na vijijini wanapata huduma endelevu ya maji, Wizara imeendelea na utafutaji wa vyanzo vipya vya maji katika maeneo mbalimbali nchini ili kuvihifadhi na kuviendeleza viweze kutoa huduma. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, jumla ya vyanzo vipya **253** vya maji juu ya ardhi vikihusisha mito, vijito, chemichemi, mabwawa na ardhi oevu vimebainishwa katika Mabonde ya Rufiji vyanzo **197** na Pangani **56**. Aidha, Wizara imefanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika vijiji **79** vilivyo katika Mabonde ya Ziwa Victoria vijiji **19**, Ziwa Nyasa **1**, Ziwa Rukwa **1**, Ruvuma **7**, Pangani **33**, Ziwa Tanganyika **4** na Bonde la Kati vijiji **14** na kubaini maeneo **618** yanayofaa kuchimba visima.

**(c) Ujenzi wa Mabwawa ya Kimkakati na Mabwawa ya Kuvuna Maji ya Mvua**

**36. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na mpango wa ujenzi wa miradi ya kimkakati ya mabwawa ya Farkwa (Dodoma), Lugoda/Ndembera (Iringa), Songwe (Songwe), Kidunda (Morogoro) na Bwawa la Dongo (Manyara). Usanifu wa Mabwawa hayo umekamilika na sehemu ya fidia ya kiasi cha **Shilingi bilioni 18.5** kwa wananchiwatakaopisha ujenzi wa mabwawa ya Farkwa na Kidunda imelipwa. Kwa upande wa Bwawa la Kidunda, visima vya maji vimechimbwa katika maeneo ambayo wananchi waliopisha ujenzi wa bwawa hilo wamehamishiwa.

**37. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mipango ya kujenga na kukarabati mabwawa ili kukidhi mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali nchini. Kwa mwaka 2020/21, Wizara imekamilisha ukarabati wa bwawa la Mwadila lililopo Wilaya ya Maswa mkoa wa Simiyu; usanifu kwa ajili ya ukarabati wa mabwawa **matatu (3)** ya Itobo (Nzega), Engukument (Monduli) na Horohoro (Mkinga); na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa **mawili (2)**katika maeneo ya Muko na Chiwanda Wilaya ya Momba. Vilevile,

usanifu wa Malambo (*Charco dams*) **sita (6)** umekamilika katika mwambao wa barabara kuu ya Dodoma-Babati ikihusisha Wilaya za Bahi malambo **mawili (2)** na Chemba **manne (4)**.

**38. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti ubora wa ujenzi wa mabwawa ya maji Wizara imeanza kusajili wataalam wanaohusika na ujenzi wa mabwawa kwa lengo la kuhakikisha miundombinu hiyo inajengwa katika viwango stahiki ili kuepusha hasara ya mali na maisha ambayo inaweza kupatikana iwapo miundombinu hiyo itajengwa chini ya viwango stahiki. Hadi mwezi Machi 2021, Wizara imesajili jumla ya wataalam wa mabwawa **28** kwa ajili ya ujenzi na ukaguzi ili kudhibiti ubora wa miundombinu ya mabwawa inayojengwa nchini.

**(d) Uanzishwaji wa Majukwaa ya Wadau wa Maji**

**39. Mheshimiwa Spika**, ushirikishwaji wa wadau kwenye usimamizi wa rasilimali za maji ni muhimu katika kuhakikisha matumizi bora na endelevu ya rasilimali za maji. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, Wizara imeendesha jukwaa **moja** (**1**) la Kitaifa; majukwaa **tisa** (**9**) katika mabonde yote nchini na kuanzisha jumla ya majukwaa **16** katika ngazi ya vidaka maji. Uanzishwaji wa majukwaa hayo umefanikisha utoaji wa ushauri mbalimbalina umeongeza mwamko wa wadau kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

**(iii). Usimamizi wa Rasilimali za Majishirikishi**

**40. Mheshimiwa Spika**, Tanzania ina vyanzo vya majishirikishi 14 ambavyo ni Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa, Natron, Chala na Jipe pamoja na Mito ya Kagera, Mara, Malagarasi, Momba, Mwiruzi, Umba, Ruvuma na Songwe. Idadi hiyo inaifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zenye vyanzo vingi vya maji vinavyovuka mipaka ya nchi Barani Afrika. Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika vyanzo vya majishirikishi unahusisha ushirikiano na nchi wanachama ambazo ni Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Uganda, Malawi, Msumbiji

na Zambia. Nchi nyingine tunazoshirikiana nazo ni Angola, Botswana, Ethiopia, Misri, Namibia, Sudan, Sudan Kusini, Zimbabwe na Eritrea.

**41. Mheshimiwa Spika**, ushirikiano katika usimamizi wa rasilimali za majishirikishi unafanyika kupitia Taasisi za Kikanda na Kimataifa pamoja na Mikataba mbalimbali. Tanzania ni mwanachama wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (*African Ministers' Council on Water-AMCOW*); Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*Zambezi Watercourse Commission ZAMCOM*); Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative- NBI*); Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe (*Joint Songwe River Basin Commission*); Mamlaka ya Usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Authority – LTA*); Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*); Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria pamoja na Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Ruvuma. Aidha, Tanzania imesaini na kuridhia makubaliano mbalimbali ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za majishirikishi. Lengo ni kulinda maslahi ya Taifa na kutumia fursa zilizopo kwa manufaa ya nchi yetu. Katika mwaka 2020/21, Serikali imeendelea kushirikiana na nchi washirika katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za majishirikishi kama ifuatavyo:-

**(a) Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative - NBI*)**

**42. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Mpito ya Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative - NBI*) ni ushirikiano baina ya nchi 11 za Bonde la Mto Nile ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Misri, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Sudan, Tanzania, Uganda na Eritrea ambayo ni mtazamaji (*observer)*. Kupitia Taasisi hiyo, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa makubaliano ya nchi wanachama. Hadi mwezi Machi 2021, usanifu wa vituo **nane (8)** vya kisasa vya kukusanya takwimu za mtiririko wa maji katika mito mikubwa ya Mara, Kagera, Simiyu na Rusumo iliyopo katika Bonde la Ziwa Victoria kupitia Mradi wa *Nile Basin Regional Hydromet System* umekamilika.

**43. Mheshimiwa Spika**, vilevile kwa upande wa mradi wa kuboresha Usimamizi wa Pamoja wa Rasilimali za Maji Juu na Chini ya Ardhi unaotekelezwa katika *aquifer* ya Kagera ulizinduliwa mwezi Septemba 2020 na utatumika kuimarisha usimamizi katika maeneo mengine nchini.Aidha, uandaaji wa Mipango ya pamoja ya Usimamizi wa maeneo oevu (*Wetlands Management Plans*) katika eneo oevu la Sango Bay (Uganda) na Minziro (Wilaya ya Misenyi - Tanzania) kupitia Programu ya Uhifadhi wa Bioanuai na Matumizi Endelevu ya Rasilimali za Ardhioevu zenye Umuhimu wa Kimataifa katika Bonde la Mto Nile umekamilika na Kamati ya usimamizi wa maeneo husika imeundwa.

**(b) Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe**

**44. Mheshimiwa Spika**,Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe kwa niaba ya Serikali za Malawi na Tanzania inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe (*Songwe River Basin Development Program*). Programu hiyo inakusudia kuongeza uwezo wa kukabiliana na mafuriko ya mara kwa mara na mabadiliko ya tabianchi kupitia ujenzi wa mabwawa ambayo pia yatatumika kwa ajili ya kuzalisha umeme wa megawati 180, kilimo cha umwagiliaji, usambazaji maji na uvuvi. Mradi huo unatekelezwa katika kipindi cha miaka minne kutoka 2019 hadi 2023**.** Hadi kufikia Machi, 2021 kazi zilizofanyika ni pamoja na kuwatambua wakulima waliomo ndani ya maeneo yenye uharibifu mkubwa wa mazingira katika Bonde hasa katika Wilaya ya Ileje (Tanzania) na Karonga (Malawi) na katika eneo la umwagiliaji lenye hekta 6,200 katika Wilaya za Kyela, Tanzania na Karonga, Malawi pamoja na uimarishaji wa Taasisi kwa kuajiri wataalam washauri katika maeneo ya manunuzi, mazingira na mafuriko.

**(c) Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC***

**45. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imeendelea kushirikiana na Jumuia ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ambapo kupitia Taasisi yake ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji chini ya Ardhi (*SADC Groundwater Management Institute - GMI*) imekamilisha utekelezaji wa mradi wa uchimbaji wa **visima**

**vitano (5**) vya kufuatilia mwenendo wa maji ardhini katika eneo la Kimbiji-Kigamboni. Lengo la visima hivyo ni kupata taarifa za mwenendo wa maji chini ya ardhi ambazo zitasaidia usimamizi madhubuti pamoja na uzalishaji wa maji chini ya ardhi. Aidha, Tanzania imeshiriki katika kuandaa taftishi ya maeneo yenye ukame ili kutafuta maji chini ya ardhi kwa nchi wanachama wa SADC kwa lengo la kuweka mikakati ya usalama wa maji katika maeneo hayo.

### (d) Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (AMCOW)

**46. Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni mwanachama wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (*African Ministers' Council on Water - AMCOW*) lenye jukumu la kushughulikia masuala ya maji katika nchi za Afrika. Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Tanzania imeshiriki katika Mkutano wa Pili wa Kamati ya Wataalamu wa Kanda ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 7 na 8 Septemba, 2020; Mkutano wa 20 wa Baraza la Mfuko wa Usimamizi wa Maji wa Afrika tarehe 4 Desemba, 2020; na Mkutano wa 12 wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika. Mkutano wa Baraza la Mawaziri ulipitisha Mwongozo wa Sera ya Afrika kuhusu Usafi wa Mazingira (*African Sanitation Policy Guidelines*). Mwongozo huo unazisaidia nchi za Afrika ikiwemo Tanzania kufikia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 hususan lengo linalohusu Usalama wa Maji na Usafi wa Mazingira.

### (e)Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria

**47. Mheshimiwa Spika**, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria inatekeleza Programu na miradi mbalimbali ikiwemo Programu ya pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria inayogharimu takribani **Shilingibilioni 83.7**kwakushirikianana Serikali ya Ujerumani; na Mradi wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria kwa ushirikiano na Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) kwa gharama ya takriban **Shilingi bilioni 11.675**.Hadi kufikia mwezi Machi 2021, upembuzi yakinifu wa mradi wa kupanua mtandao wa

majitaka katika Jiji la Mwanza kupitia Programu ya pamoja ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria umekamlika.

**48. Mheshimiwa Spika**, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, Wizara imeshiriki katika Maazimisho ya **tisa** (9) ya siku ya Bonde la Mto Mara yaliyofanyika tarehe 15 Septemba 2020 wilayani Butiama Mkoani Mara. Siku ya Bonde la Mto Mara hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuhamasisha na kuelimisha wananchi waishio kandokando ya Bonde la Mto Mara juu ya utunzaji na uhifadhi wa Bonde hilo. Katika mwaka 2020/21 utoaji wa elimu na uhamasishaji upandaji miti umefanyika kwa makundi na Taasisi **16**;upandaji miti rafiki ya maji**1,300**; na uwekaji wa mipaka katika maeneo ya Mto Mara. Aidha, kupitia Mradi wa *the Sustainable Water Partnership (SWP)* uliokamilika mwaka 2020, Wizara imeandaa Mwongozo wa Ugawaji Maji katika Bonde la Mto Mara. Mwongozo huu utasaidia kuandaa Mipango ya Ugawaji Maji katika Mabonde mengine.

**(iv). Kujenga Uwezo wa Taasisi Zinazosimamia Rasilimali za Maji**

**49. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaendelea kuzijengea uwezo Taasisi zinazosimamia rasilimali za maji kwa kuimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu za mwenendo wa maji katika mabonde yote tisa nchini, utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji, ununuzi wa vitendea kazi na kujenga uwezo kwa wataalam. Hadi mwezi Machi 2021, Wizara imeendelea na ujenzi wa ofisi kwa Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu, ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari 23, pikipiki 100 na vifaa vya ofisi katika ngazi ya Wizara, Bodi za Maji za Mabonde na Jumuiya za Watumia Maji. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Morocco na Shirika la *Atomic Energy*, imeanzisha Maabara ya Teknolojia ya *Isotope* inayosaidia kufanya utafiti wa mwenendo wa rasilimali za maji, kubaini vyanzo vya uchafuzi na kuanisha maeneo ambayo yanavilisha maji chini ya ardhi.

**(v).Kituo Mahiri cha Rasilimali za Maji**

**50. Mheshimiwa Spika**,Wizara imeanzisha Kituo Mahiri cha Rasilimali za Maji (*Water Resources Centre of Excellence - WRCoE*). Kituo hichoni kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali na kujenga uwezo kwa wataalam wa Wizara, sekta zingine zinazohusiana na maji, Bodi ya Maji ya Taifa na Bodi za Maji za Mabonde katika masuala ya Usimamizi na Uendelezaji Shirikishi wa Rasilimali za Maji. Takribani **Shilingi bilioni 5.604**zinatumika kutekeleza kazi za uanzishwaji wa Kituo kwa muda wa miaka minne ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo. Aidha, kupitia Kituo hicho, mafunzo yamefanyika kwa watalaam **217** katika maeneo ya Matumizi ya vifaa vya kutafiti na kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi na usimamizi wa kanzidata ya maji chini ya ardhi (washiriki **76**); matumizi ya teknolojia ya *GIS* katika usimamizi wa rasilimali za maji (washiriki **56**); mafunzo juu ya uandaaji wa miradi kupitia Mifuko ya Mazingira ya Dunia yaani GCF na GEF (washiriki **54**); na mafunzo kuhusu namna ya kutumia mbinu za kisayansi za kukabiliana na mafuriko (washiriki **31**).

**3.2.2 Huduma za Ubora wa Maji**

**51. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora na usalama wa maji katika vyanzo na mitandao ya kusambaza maji kwa lengo la kulinda afya ya jamii na ikolojia. Katika mwaka 2020/21, Wizara ilipanga kukusanya sampuli 10,000 kwa ajili ya kuhakiki ubora wa maji ili kubaini mwenendo wa ubora wake katika vyanzo na kwa ajili ya matumizi ya majumbani, viwandani, umwagiliaji, ujenzi na utafiti. Kwa upande wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira Wizara ilipanga kukusanya na kuhakiki sampuli 1,500. Maelezo ya kina kuhusu matokeo ya uchunguzi wa hali ya ubora wa maji ni yafuatayo:-

**(i). Ubora wa Maji Katika Vyanzo**

**52. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo kwa kukusanya na

kuzifanyia uchunguzi wa kimaabara sampuli **478** kutoka katika vyanzo **62** vya maji vya kimkakati kwa ajili ya afya ya ikolojia. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha kuwa ubora wa maji wa vyanzo hivyo ni wa kuridhisha katika kulinda Ikolojia na vinaweza kuendelea kutumika au kuendelezwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

### (ii). Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani

**53. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji yanayosambazwa na Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs), Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Taasisi binafsi pamoja na vyanzo vya maji vinavyomilikiwa na watu binafsi katika kulinda afya ya jamii. Hadi mwezi Machi 2021, jumla ya sampuli za maji **2,756**zimekusanywa na kuhakikiwa ubora wake kwa kulinganishwa na viwango vya ubora wa maji ya kunywa vya kitaifa. Matokeo ya uhakiki yalionesha **asilimia 83** sawa na sampuli **2,275** zilikidhi viwango vinavyokubalika. Aidha, baadhi ya sampuli hazikukidhi viwango vya ubora wa maji kutokana na kuwa na viwango vikubwa vya madini ya chuma, *Manganese* na chumvichumvi katika mikoa ya Mtwara na Lindi; pamoja na kiwango kikubwa cha madini ya *Fluoride*katika mikoa yaArusha, Manyara na Singida. Katika kukabiliana na changamoto hizo ushauri wa kitaalam ikiwa ni pamoja na kusafisha na kutibu maji ulitolewa kwa wasambazaji wa maji mijini na vijijini.

**54. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha maji yanayomfikia mtumiaji yanaendelea kuwa na ubora unaotakiwa, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ili ziweze kuandaa Mipango ya Usalama wa Maji inayohusisha Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Resilent Water Safety Plans –CR WSPs*) kwa kuzingatia Mwongozo uliotolewa.Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Songea, Dar es Salaam na KASHWASA ziko katika hatua za mwisho za kukamilisha mipango hiyo. Vilevile, Wizara imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Kusafisha na Kutibu Maji unaotumika na wadau wote wanaojihusisha na usambazaji wa maji ya kunywa

hususan Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira na Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs). Mwongozo huo unaelekeza namnaya matumizi sahihi ya madawa ya kusafisha na kutibu maji ili kutimiza lengo la kusambaza majisafi na salama.

### (iii). Ubora wa Maji kwa Matumizi Mengine

**55. Mheshimiwa Spika**, maji yanayotumika katika shughuli za kiuchumi yanatakiwa kukidhi viwango vinavyokubalika kwa matumizi husika. Ili kutimiza lengo hilo, Wizara imeendelea kuhakiki ubora wa maji yanayotumika kwa shughuli za kiuchumi ambazo ni viwandani, ujenzi, umwagiliaji na tafiti mbalimbali. Hadi mwezi Machi, 2021 jumla ya sampuli **310** zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli **210**za maji zilichunguzwa kwa ajili ya matumizi ya viwandani, sampuli **10** kwa ajili ya ujenzi, sampuli **24** kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji na sampuli **66** kwa ajili ya utafiti. Matokeo yalionesha maji kukidhi viwango kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**56. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kutoa wito kwa wadau wa shughuli za viwanda, ujenzi, umwagiliaji na utafiti kuendelea kutumia maabara za ubora wa maji za Wizara kwa ajili ya kupima ubora wa maji kwa matumizi yaliyokusudiwa.

### (iv). Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa Kwenye Mazingira

**57. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kufuatilia na kuhakiki ubora wa majitaka ambapo hadi mwezi Machi 2021, jumla ya sampuli **346**zilikusanywa kutoka kwenye mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka. Kati ya hizo,sampuli **126** ni kutoka kwenye mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka ya Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Tanga, Mbeya, Iringa, Arusha, Mwanza, Dar es salaam na Morogoro; na sampuli **220**za majitaka kutoka viwanda vya nguo, rangi na kusindika vyakula. Matokeo yalionesha asilimia **81.4** ya sampuli za majitaka zilikidhi viwango vya kurudishwa kwenye

mazingira. Aidha, Mamlaka za Maji pamoja na viwanda ambavyo majitaka yake hayakukidhi viwango ushauri wa kitaalam ulitolewa ili kuongeza ufanisi wa mifumo ya kusafisha na kutibu majitaka.

**(v). Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji**

**58. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara imeendelea kuhakiki ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji ya kunywa kabla ya manunuzi kufanyika. Hadi mwezi Machi 2021, jumla ya sampuli **29** za madawa ya kusafisha na kutibu maji kutoka Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira pamoja na Taasisi mbalimbali zilichunguzwa ubora na ufanisi wake. Sampuli hizo ni za madawa ya kusafisha maji aina ya *Aluminium Sulphate* (Shabu) sampuli ***11***, *Polymerblend**3**, Polymer**1**, Poly Aluminium Chloride **1**, Poly aluminium Sulfate **1***, *Algal floc**2**,Sodium Carbonate 1* na *Polydad Mac 03* sampuli **moja**. Vilevile, sampuli **9** za dawa aina ya*Calcium Hypochlorite* kwa ajili ya kutibu maji zilihakikiwa ubora wake. Matokeo ya uchunguzi yalionesha madawa hayo yanakidhi viwango vinavyokubalika kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji.

**(vi). Uondoaji wa Madini ya *Fluoride* katika Maji.**

**59. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya *Fluoride*kwenye maji ya kunywa na kupikia katika mikoa iliyoathirika zaidi na madini hayo (*fluoride belt*). Katika kutekeleza Mkakati huo, mitambo **25**ya kuondoa madini ya *fluoride*imesambazwa na kunufaisha wananchi wapatao **200**pamoja na kufuatilia ufanisi wa mitambo **221** inayotumiwa katika ngazi ya kaya na mitambo **10** ngazi ya jamii katika mikoa ya Arusha na Manyara. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na matumizi ya teknolojia ya kuondoa madini hayo kupitia vyombo vya habari na makongamano mbalimbali ikiwemo maonesho ya Nanenane, Wiki ya Maji na Maonesho ya Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### (vii). Maabara za Maji Kupata Ithibati

**60. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa maabara, Wizara imeendelea kuziwezesha maabara za ubora wa maji ili kupata ithibati (*accreditation*). Hadi mwezi Machi 2021,maabara **sita (6)** za Dar es Salaam, Singida, Shinyanga, Musoma, Bukoba na Kigoma zimepata ithibati na kuongeza idadi ya maabara za ubora wa maji zenye ithibati kutoka moja ya Mwanza hadi kufikia **Saba (7)**.Vilevile, Wizara imeendelea kuziwezesha maabara zote 16 kutekeleza matakwa ya Mwongozo mpya wa Kimataifa wa Uendeshaji uchunguzi wa kimaabara (*ISO 17025:2017*) kwa lengo la kukidhi vigezo vya utoaji wa takwimu sahihi za uchunguzi wa kimaabara.

### 3.2.3 Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini

**61. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilipanga kutekeleza jumla ya miradi **1,169**.Utekelezaji huo ulihusishakukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea, ujenzi wa miradi mipya, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji.Vilevile**,** Serikali ilipangakukarabati na kujenga mabwawa **19** nakufanyausanifu wa miradi **390**.

**62. Mheshimiwa Spika**,hadi kufikia mwezi Machi 2021, utekelezaji wa jumla ya miradi **355 (Kiambatisho Na. 1)** yenye jumla ya vituo vya kuchotea maji **6,687** umekamilika na kuanza kutoahuduma ya majisafi na salama kwa wananchi **1,984,575**. Utekelezaji wa miradi hiyo umegjarimu kiasi cha **Shilingi 154,659,469,079.00**. Aidha, utekelezaji wa miradi**814**iliyobakiunaendelea na upo katika hatua mbalimbali. Vilevile,Wizara kupitiaRUWASA imefanya usanifu wa miradi **196** kati ya miradi **390** na kuchimba visima **155** katika vijiji **148**;kufanya usanifu wa mabwawa matatu(Msanga na Pofu – Ikulu ya Chamwino na Sengenya ya Nanyumbu);kuendelea na ujenzi wa mabwawa **manne** ya Nsekwa (Mlele), Ikozi (Sumbawanga), Chole (Kisarawe),

Mwakijembe (Mkinga);na kukamilisha ukarabati wa bwawa la Vikonje lililopo Ikulu ya Chamwino.

**63. Mheshimiwa Spika**,kwa kutambua changamoto za upatikanaji na uendelevu wa huduma za maji nchini hasa kwa wananchi wa vijijini, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji kupitia programu mbili ambazo ni:-

**(i). Programu ya Malipo kwa Matokeo (*Payment by Results - PbR*)**

**64. Mheshimiwa Spika**,Serikali kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*DFID*) inatekeleza Programu ya Malipo kwa Matokeo (*PbR*) kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 5.334** zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa programu. Aidha, jumla ya miradi **311** imekamilika kwa kufanyiwa ukarabati na upanuzi na hivyo kurudisha huduma kwenye vituo **3,871** vya kuchotea maji katika vijiji **874**.

**(ii).Programu kwa Matokeo (*Program for Results -PforR*)**

**64. Mheshimiwa Spika**,Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inatekeleza Programu kwa Matokeo (*Program for Results - PforR*)ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini inayotekelezwa kwa kipindi cha miaka sita (20192024) katika Wilaya **86** kwenye Mikoa **17.** Kupitia makubaliano yaliyofikiwa kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ukarabati, upanuzi wa mtandao pamoja na ujenzi wa miradi mipya itakayoibuliwa ni takribani **Shilingi bilioni 817.285**.Hadi kufikia mwezi Machi 2021, miradi **148**yenye jumla ya vituo vya kuchotea maji **2,725**imejengwa na kukamilika ambapo wananchi wapatao **843,790** wanapata huduma ya majisafi na salama katika vijiji **343**.

**(iii). Matumizi ya Teknolojia ya Nishati Jadidifu (*Renewable Energy*)**

**66. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia Ufadhili wa *Global Partnership on Output-Based Aid* (GPOBA) inaendelea na maandalizi ya kutekeleza mradi wa Kubadili Miradi ya Maji inayotumia Teknolojia ya Nishati ya Dizeli kwenda Nishati Jua *(Accelerating Solar Pumping via Innovative Financing Project)*. Gharama za mradi ni takribani **Shilingi bilioni 19.848**ambapo utekelezaji wa mradi utaanza katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Mtwara na Taborana wananchi wapatao **840,000** katikavijiji **280** watanufaika. Lengo kuu la kutekeleza mradi huo ni kutatua changamoto za gharama kubwa za uendeshaji wa miradi ya maji vijijini hususan miradi inayotumia nishati ya mafuta ya dizeli ambayo ni ghali.

**67. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi 2021, taratibu za kuwapata Wakandarasi zimekamilika ambapo utekelezaji utaanza mwezi Mei, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2021 kwa miradi **77** katika mikoa ya Dodoma na Singida. Aidha, taratibu za manunuzi ya Wakandarasi kwa mikoa ya Shinyanga, Tabora na Mtwara zinaendelea.

**(iv). Utekelezaji wa Miradi yenye Changamoto za Muda Mrefu**

**68. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini inakuwa bora na endelevu, Serikali imekuwa ikifanya maboresho ya kimuundo na kisheria. Hapo awali, hali ya utoaji huduma ya majina usafi wa mazingira hususan vijijini na kwenye Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo haikuwa ya kuridhishakutokana na changamoto za usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji. Hali hiyo kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na mfumo uliokuwepo, ambapo usimamizi na utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Maji ulikuwa kwenye Wizara mbili tofauti ambazo ni Wizara ya Maji na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (ORTAMISEMI). Hali hiyo husababisha mlolongo mrefu katika kuchukua hatua kunapotokea ukiukwaji wa taratibu za kiutumishi au kiutendaji. Kufuatia changamoto hizo za

kimfumo, tarehe 10/05/2018 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya maamuzi ya kisera na kuelekeza kuhamishwa kwa majukumu ya utoaji wa huduma za maji kutoka ORTAMISEMI kwenda Wizara ya Maji.

**69. Mheshimiwa Spika**, kufuatia maamuzi hayo, Serikali ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) unaohusika katika ujenzi wa miradi na usimamizi wa huduma ya maji vijijini. Kuanzishwa kwa Wakala huo kumeenda sambamba na kurithi miradi yote ya maji ikiwemo ya vijiji 10 iliyokuwa inatekelezwa chini ya Halmashauri za Wilaya. Baadhi ya miradi ya maji iliyorithiwa imekuwa na changamoto ya kutokukamilika kwa wakati na mingine kukamilika bila kutoa maji. Jumla ya miradi **177** ilibainika kuwa na changamoto hizo ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2021, miradi **85** imepatiwa ufumbuzi na kugharimu jumla ya **Shilingi 66,923,173,686.28** na tayari imeanza kutoa huduma ya maji. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na miradi ya maji ya Ntomoko – Dodoma, Nyamtukuza – Geita, Mibono – Tabora, Rugeye – Mwanza, Malinyi – Morogoro, Muze *group* – Rukwa, Kinesi – Mara na Imalabupina-Ichwankima – Geita (**Kiambatisho Na. 2**). Ukwamuaji wa Miradi hiyo unaendelea kwa kutumia Timu Maalam za Wataalam na tumezipa jina maarufu kama "***Water Rescue Team***".

### (v).Uimarishaji wa Vyombovya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii

**70. Mheshimiwa Spika**, kwa utaratibu wa awali, miradi ya maji vijijini inapokamilika ilikuwa ikikabidhiwa kwa wananchi ambao huunda Jumuiya (*Community Owned Water Supply Organisations COWSOs*)kwa ajili ya kuiendesha. Muundo wa Jumuiya hizo haukuzingatia utaalam kwenye nafasi zake za usimamizi. Hali hiyo ilisababisha kukosekana kwa uendelevu wa miradi ya maji vijijini kwa kuwa wajumbe wengi wa jumuiya hizo hawakuwa na utaalam kwenye nafasi walizopewa. Kupitia Sheria **Na. 5** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, muundo wa jumuiya hizo kwa sasa umeboreshwa na kuwa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji ngazi ya Jamii (*Community Based Water Supply*

*Organisations – CBWSOs*) kwa kuweka hitaji la kuwa na watalaam wa ufundi na usimamizi wa fedha. Aidha, RUWASA imeendelea kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi kuendesha miradi ya maji vijijini kwa utaratibu maalum watakaoingia na Vyombohusika chini ya usimamizi wa RUWASA ambapo hadi sasa miradi **83** inaendeshwa na Sekta Binafsi.

**71. Mheshimiwa Spika**,Wizara imeendelea kutekeleza Kanuni za Usajili na Uendeshaji wa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii *(The Water Supply and Sanitation Registration and Operations of Community Based Water Supply Organisations Regulations, 2019)*. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii vipatavyo **2,155**vimeundwa na kuhuishwa katika mikoa 25 ya Tanzania bara.Aidha, kuna jumla ya Vyombo**1,109** ambayo vimeunganishwa na kufanya jumla ya Vyombo vyote vinavyofanya kazi kwa kutumia Sheria mpya Na.5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 kufikia **3,264**.

### 3.2.4 Huduma za Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini

**72. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza miradi**177** ya maji inayolenga kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji midogo na Miradi ya Kitaifa. Hadi mwezi Machi 2021,utekelezaji wa miradi miradi **67**kwa gharama ya Shilingi **759,211,390,669.00** umekamilika **(Kiambatisho Na.3)**na utekelezaji wa miradi **110** upo katika hatua mbalimbali. Utekelezaji wa miradi hiyo unahusisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na usafi wa Mazingira, pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa kuzipatia mafunzo, vitendea kazi na kujenga ofisi.Utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maji katika maeneo ya mijini ni kama ifuatavyo:-

**(i). Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha**

**73. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Jiji la Arusha unaogharimu takribani **Shilingi bilioni 520**ambapo AfDB inatoa takribani **Shilingi bilioni 492.612**na Serikali takriban **Shilingi bilioni 53.59**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu **56**; ujenzi wa matanki **10**; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji; upanuzi na ukarabati wa mitandao ya majisafi na majitaka; ujenzi wa mabwawa mapya **18** ya majitaka; ujenzi wa ofisi ya Mamlaka; ununuzi wa vitendea kazi; na kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi.

**74. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2021, kazi zilizokamilika ni pamoja na uchimbaji wa visima **41**; ujenzi wa mabwawa mapya ya kutibu majitaka**18**; na upanuzi na ukarabati wa miundombinu na mifumo ya majisafi na majitaka maeneo ya *Central Business District* (*CBD)*. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa ofisi kuu na za kanda za Mamlaka; ujenzi wa mitambo ya kutibu na kusafisha maji; upanuzi wa mtandao wa majisafi; upanuzi wa mtandao wa majitaka nje ya CBD; naujenzi wa vyoo vya mfano. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 62** na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2021.

**75. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **milioni 40** hadi lita **milioni 200** kwa siku, muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi kutoka saa 12 za sasa hadi saa 24 kwa siku pamoja na kuongeza huduma ya uondoshaji wa majitaka kutoka **asilimia 7.6** za sasa hadi **asilimia 30.**

**(ii).Miradi ya Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dodoma**

**76. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma kwa

kutekeleza miradi mbalimbali. Utekelezaji wa miradi upo katika mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu.

**a) Mpango wa Muda Mfupi**

**77. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa kutoa maji katika visima vya Ihumwa kwenda tanki la Njedengwa ambao unagharimu **Shilingi bilioni 2.4**. Ujenzi wa mradi unahusisha ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 11.6; ufungaji wa pampu; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji yenye urefu wa kilomita 4.2. Hadi mwezi Machi 2021, utekelezaji wa mradi umefikia wastani wa **asilimia 30** na unatarajia kukamilika mwezi Mei, 2021.

**78. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea na ujenzi wa tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita **milioni 2.5** katika eneo la Chamwino. Ujenzi huo umelenga kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika maeneo ya Chamwino. Tanki hilo linatarajiwa kuanza kutumika mwezi Mei 2021.

**79. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Wizara imeendelea kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi na uchimbaji wa visima katika maeneo oevu ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dodoma. Hadi mwezi Machi 2021, visima **nane** (**8**) vimechimbwa na visima **vitatu** vya zamani vimekarabatiwa. Kazi ya ufungaji wa miundombinu inaendelea na inatarajia kukamilika mwezi Juni 2021 ili kuongeza muda wa upatikanaji wa maji kwa wakaazi wa Dodoma.

**b) Mpango wa Muda Mrefu**

**80. Mheshimiwa Spika**, mahitaji ya maji katika Jijila Dodoma kwa sasa yanakadiriwa kuwa ni **mita za ujazo 103,608.76** kwa siku ambapo uzalishaji wa sasa wa visima vya Mzakwe vilivyopo Makutopora *wellfield* ni **mita za ujazo 55,000** kwa siku. Uwezo wa uzalishaji kwa eneo lote lenye uwezekano wa kuchimbwa visima ni **mita za ujazo 72,000** kwa siku. Kufuatia hali hiyo, Serikali imeanza kuchukua hatua za muda mrefu zinazolenga kuondoa adha ya upatikanaji wa huduma ya

maji kwa kuanza maandalizi ya mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria.

**81. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2021, upembuzi wa awali umekamilika na taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu *(Feasibility Studies)* na usanifu wa kina *(Detailed Design)*zinaendelea. Aidha, taarifa ya upembuzi wa awali imeonesha matokeo chanya na kwa asilimia kubwa, wazo la mradi limekidhi vigezo vya kihandisi, kimazingira na kiuchumi. Vilevile, taarifa hizo zinaonesha kuwa maeneo yatakayonufaika na bomba kuu la mradi huo ni pamoja na baadhi ya maeneo ya mikoa ya Singida na Dodoma.

**(iii). Kuboresha Huduma ya Majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya Maeneo ya Mkoa wa Pwani**

**82. Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na maeneo ya Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze na Bagamoyo. Miradi inayotekelezwa ni kama ifuatavyo:**(a) Mradi wa Maji wa Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera**

**83. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa uchimbaji wa visima virefu vya maji maeneo yaKimbiji na Mpera ambapo kwa upande wa Kimbiji ni visima **12** na Mpera visima **8.** Gharama za mradi ni **Shilingi bilioni 18** na vinatarajiwa kuzalisha maji lita **milioni 260** kwa siku. Hadi mwezi Machi 2021, uchimbaji wa visima **14** umekamilika ambapo kati ya hivyo, visima **11** ni vya Kimbiji na **3** ni vya Mpera. Kati ya visima vilivyokamilika, visima **4** vyaKimbiji na **kimoja**chaMpera vimekamilka kwa kiwango cha kufaa kuwekewa miundombinu ya kusambaza maji. Ukamilishaji wa visima vilivyobaki unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2021.

**84. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa usambazaji wa maji, ujenzi wa miradi umeanza kutoka katika visima vya Kimbiji ambapo utekelezaji wake umegawanywa katika vipande

vinne. Kipande cha kwanza kinahusu ujenzi wa miundombinu ya kutoa maji kwenye visima kwenda kwenye pampu kubwa ambapo mkandarasi yupo katika hatua ya *mobilization*, kipande cha pili kinahusu ujenzi wa kituo cha kusukuma maji pamoja na bomba la kutoa maji kwenda kwenye tanki la kuhifadhia lenye ujazo wa **lita milioni 15** eneo la Kisarawe II ambapo utekelezaji umefikia **asilimia 35**, na maandalizi ya utekelezaji wa kipande cha tatu na nne vinavyohusu miundombinu ya usambazaji maji yanaendelea.

### (b)Mradi wa Maji wa Chalinze

**85. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India inaendelea kutekeleza awamu ya tatu ya mradi wa maji Chalinze kwa gharama ya takriban **Shilingi bilioni 41.3**. Mradi wa Chalinze awamu ya tatu umelenga kunufaisha vijiji **68** ambapo vijiji **19** viko kaskazini na **49** viko kusini mwa mto Wami. Mradi ulikusudia kufanya kazi zifuatazo; upanuzi wa mtambo kwa kuongeza uzalishaji kutoka mita za ujazo **500** hadi **900** kwa saa; ujenzi wa mabomba makuu ya kusafirisha maji (*transmission mains*) kutoka mtamboni kuelekea maeneo ya wateja kilomita **124.379;** ujenzi wa mfumo wa mabomba ya kusambaza maji wenye **kilomita 1,022.8**; ujenzi wa vituo **9** vya kusukuma maji *(booster stations*); ujenzi wa tenki kubwa lenye mita zaujazo **2,000** eneo la Mazizi; na ujenzi wa matenki mengine **18** yenye kuanzia mita za ujazo**50**hadi**1,000;**na ujenzi wa vitekeo maji (*kiosks*) **351** kwenye vijiji na vitongoji mbalimbali vilivyopo eneo la mradi. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, utekelezaji wa mradi umefikia wastani wa **asilimia 87.5** na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2021.

### (c) Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi

**86. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji majisafi katika Mkoa wa Dar es Salaam unaogharimu takriban **Shilingi bilioni 200.818**kwa fedha kutoka Benki ya Dunia. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 130.765**ni kwa ajili ya ujenzi wa matanki na kupanua mtandao wa kusambaza maji wenye urefu wa **kilomita 1,440** na kuunganisha wateja wapya

**64,000**ambapo mkandarasi ameajiriwa na yupo katika eneo la mradi. Vilevile, **Dola za Marekani milioni 20** ni kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kupunguza upotevu wa maji ambao upo kwenye hatua za kuajiri wataalam washauri wa kusimamia mradi; na **Dola za marekani milioni 10** ni kwa ajili ya ununuzi wa dira za maji **50,000** na taratibu za kumpata mzabuni zinaendelea. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, mradi wa maji kutoka matenki ya Chuo Kikuu hadi Bagamoyo umefikia **asilimia 22**. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa kwa miezi 36 na kukamilika mwezi Desemba 2022.

**(iv). Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Kigoma**

**87. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Kigoma unaendelea ambapo kazi zilizokamilika ni pamoja na ufungaji wa pampu **tisa** (**9**); ujenzi wa matanki **sita** (**6**); ujenzi wa vituo 55 vya kuchotea maji; ukarabati wa matanki **matatu** (**3**);ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 22 kutoka kwenye chanzo hadi kwenye matanki ya kuhifadhia maji; ulazaji wa mabomba ya mtandao wa usambazaji maji yenye urefu wa kilomita 32; ulazaji wa bomba za chumazenye urefu wa kilomita 8.3; ununuzi wa vipuli mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo; na ujenzi wa bwawa la majitaka. Aidha, ujenzi wa choteo (*Intake*) umeanza mwezi Aprili 2021 na mkataba ni wa miezi 12. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita **milioni 9.5** hadi lita **milioni 42** kwa siku na utawezeshawananchi wapatao **384,500** kupata huduma ya majisafi na salama.

**(v).Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Lindi**

**88. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mji wa Lindi utekelezaji wa mradi ulihusisha uchimbaji wa visima 10na ufungaji wa pampu katika visima; ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 9.8 kutoka kwenye visima kwenda kwenye mtambo wa kutibu maji wa Ng'apa; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji eneo la Ng'apa; ujenzi wa matanki **mawili** (**2**) ya

kuhifadhia maji lita **milioni 5;** ulazaji wa mabomba ya mtandao wa usambazaji maji yenye urefu wa kilomita 27; ufungaji wa mfumo wa uendeshaji visima; kujenga bwawa la majitaka katika eneo la Mitwero; kununua gari la majitaka; na kufanya majaribio ya msukumo wa maji (*Pressuretest*) katika bomba kuu lenye urefu wa kilomita 3.6. Mradi huo umeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni **3.6** hadi lita milioni **15** kwa siku na kuwezeshawananchi wapatao **91,968** kupata huduma ya majisafi na salama.

**(vi). Mradi wa Kuboresha Huduma yaMajisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Shinyanga**

**89. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(French Development Agency-AFD)* inaendelea na upembuzi yakinifu wa mradi wa usambazaji majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Shinyanga ambao unagharimu takriban **Shilingi bilioni 1.674**. Kazi hiyo inatekelezwa na Mtaalam Mshauri na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2021.

**(vii). Mradi wa Maji wa Isimani – Kilolo**

**90. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa maji wa Isimani – Kilolo kwa gharama ya Shilingi bilioni 9.2 na unahusisha kupeleka maji katika vijiji 29 vya Wilaya za Kilolo (vijiji 5) na Wilaya ya Iringa (vijiji 24). Mradi huo umesanifiwa kuhudumia wananchi wapatao 80,000 ifikapo mwaka 2038. Hadi mwezi Machi 2021, wastani wa utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 37** na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2021.

**(viii). Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Morogoro**

**91. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(French Development Agency-AFD)* inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Morogoro ambao utagharimu **Euro milioni 70**. Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya uandaaji wa

Mpango Kabambe wa Rasilimali za maji wa Mji wa Morogoro pamoja na kazi ya kuboresha bwawa la Mindu. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, mkataba kwa ajili ya kuwapata wataalamu washauri umeandaliwa na kupelekwa AFD kwa ajili ya kibali cha kusaini mkataba. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2025 na utaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 35 hadi lita **milioni 89** kwa siku.

**(ix). Mradi wa Mugango- Kiabakari- Butiama**

**92. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia *(Saudi Fund for Development – SFD)* imeanza kutekeleza mradi wa maji utakaohudumia maeneo ya Mugango, Kiabakari na Butiama kwa gharama ya takriban **Shilingi bilioni 56.976**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa choteo la maji katika Ziwa Victoria; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji; ujenzi wa tanki kubwa la maji safi eneo la Mugango pamoja na mantaki **matano** (**5**) katika maeneo ya Kong, Kiabakari, Butiama hill na Bumangi; ulazaji wa bomba kuu kutoka Mugango kwenda Kiabakari hadi Butiama lenye urefu wa **kilomita 48**; ulazajiwamabombayamtandao wa kusambaza maji wenye urefu**kilomita 140**; ujenzi wa ofisi na nyumba za wasimamizi wa mitambo; ukarabati wa matanki **mawili** (**2**) katika maeneo ya Kyatungwe na Bisarye; ujenzi wa vioski**40** vya maji na ununuzi wa dira za maji **2,000**.

**93. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi ulianza mwezi Desemba 2020 hadi sasa Mkandarasi ameanza utekelezaji wa mradi kwa ujenzi wa nyumba ya wafanyakazi katika eneo la Mugango; upimaji wa njia kuu ya bomba; upimaji na uandaaji wa eneo la mtambo wa kusafisha maji; upimaji na uandaaji wa maeneo ya matanki; na uletaji wa vifaa vya ujenzi eneo la mradi. Utekelezaji wa mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2022 na utanufaisha zaidi ya wananchi **100,000** waliopo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita **12** kutoka bomba kuu.

**(x). Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi katika MjiwaOrkesumet**

**94. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji katika Mji wa Orkesumet unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu (BADEA) na Mfuko wa Nchi zinazozalisha Mafuta kwa Maendeleo ya Kimataifa *(OPEC Fund for International Development – OFID)*. Utekelezaji wa mradi huo umegawanyika katika vipande viwili ambapo kipande cha kwanza kinagharimu **Shilingi bilioni 12.99** na kipande cha pili **Shilingi bilioni 25.12**. Hadi kufikia mwezi Machi 2021, utekelezaji wa kipande cha kwanza kinachohusisha ujenzi wa chanzo cha maji na mtambo wa kutibu na kusafisha maji umefikia **asilimia 88.7**.

**95. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa kipande cha pili unahusisha ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 35**; vituo **vitatu** (**3**) vya kusukuma maji; matanki **tisa** (**9**) yenye ujazo kuanzia lita 50,000 hadi lita 1,600,000; mtandao wa usambazaji maji wenye urefu wa kilomita 64; vituo **10** vya kuchotea maji; birika **10** za kunyweshea mifugo, ujenzi wa ofisi; ununuzi na ufungaji wa pampu na *crane;* na kupeleka umeme kwenye chanzo. Utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 96.7** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021 na utanufaisha wakazi wapatao **52,000** pamoja na mifugo yao.

**(xi). Mradi wa Maji Tabora, Igunga na Nzega**

**96. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim-India imetekeleza mradi wa upanuzi wa mtandao wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na vijiji 102 vilivyopo kilometa 12 pembezoni mwa bomba kuu kwa gharama ya takriban **Shilingi bilioni 617**. Mradi huounauwezo wa kuhudumia zaidi ya wakazi **milioni 1.2** wa maeneo mbalimbali ya mradi ambao mahitaji yao ya maji yanafikia kiasi cha mita za ujazo **54,145** kwa siku.

**97. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mradi ulihusisha kuongeza uzalishaji maji katika kituo cha Ihelele kwa kufunga pampu

mpya **mbili** (**2**); ulazaji wa bomba kuulenye ukubwa kati ya milimita 350 na milimita 1,100 kutoka Kijiji cha Solwa hadi mji wa Nzega, kutoka mji wa Nzega hadi Tabora mjini na kutoka mji wa Nzega hadi Igunga mjini lenye umbali wa Kilomita 281.3; ujenzi wa matanki 29ya kuhifadhia maji, yenye ujazo wa kuanzia lita laki moja hadi lita milioni tisa katika maeneo mbalimbali ya mradi; ulazaji wa mabomba ya usambazaji katika Miji na Vijiji jumla ya **kilomita 1,200**; ujenzi wa vituo **724** vya kuchotea maji; ujenzi wa Ofisi za Mamlaka za Maji KASHWASA na Mamlaka za Maji za miji ya Tabora, Nzega na Igunga; na ujenzi wa nyumba **21** za waendesha mitambo katika maeneo mbalimbali ya mradi ikiwemo eneo la chanzo cha maji cha Ihelele na katika miji ya Nzega, Igunga na Tabora.

**98. Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji wa mradi huo umekamilika na ulizinduliwa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Daktari. John Pombe Magufuli tarehe 30 Januari, 2021. Wananchi katika Miji ya Tabora, Igunga, Nzega, Uyui na vijiji **102** vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu wanapata huduma ya majisafi na salama.

**(xii). Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria Kwenda Miji ya Tinde na Shelui**

**99. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim-India inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji ya Tinde na Shelui.Mradi huounatekelezwa kwa gharama ya takriban **Shilingi bilioni 24.752**.Usanifu wa mradi huo umekamilika na utiaji saini wa Mkataba wa ujenzi ulifanyika tarehe **25 Februari 2021**.

**100.Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji katika mji wa Tyeme kata ya Shelui; kulaza bomba kuu kutoka Kijiji cha Chembeli hadi Tinde lenye urefu wa kilomita 20.93 na bomba la kupeleka maji kwenye tanki la Didia lenye urefu wa kilomita

1.5; kujenga matanki matatu ya kuhifadhia maji yenye mita za ujazo 250, 300 na 1,150 katika maeneo mbalimbali ya mradi; kulaza bomba kuu kutoka kwenye bomba kuu linalokwenda Igunga katika Kijiji cha Ipumbulya hadi Mgeta, Shelui lenye urefu wa kilomita 70.5; ukarabati wa matanki manne ya kuhifadhia maji katika maeneo ya Didia, Shelui na Tyeme; na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 12.

**(xiii).Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe**

**101.Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe unatekelezwa katika miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji **38** vilivyomo kandokando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*, *OFID*, *SAUDI Fund* na *Kuwait Fund.* Mradi utakapokamilika utazalisha maji lita **milioni103.7**kwa siku na utawanufaisha wananchi wapatao **438,930**katika Wilaya za Same **246,790**, Mwanga **177,090**na Korogwe **15,050.**

**102.Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2021, ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji wa maji unaojumuisha kitekeo cha maji, bomba kuu la kusafirisha maji, mtambo wa kusafisha maji na matanki ya kuhifadhi maji umefikia asilimia **64**; ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika Mji wa Mwanga umefikia asilimia **60** na katika mji wa Same umefikia asilimia **87**.

**103.Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 25 Desemba, 2020 Wizara ilisitisha mikataba kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huo baada ya kuonekana wakisuasua katika ukamilishaji wa mradi. Wizara imeamua kwamba sehemu ya utekelezaji wa mradi inayohusu miundombinu ya usambazaji itafanyika kwa utaratibu wa *Force Account*kutumia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) ili kukamilisha kwa haraka kazi hizo. Aidha, kwa kazi nyinginetaratibu za manunuzi ya kumpata mkandarasi atakayekamilisha mradi unaendelea. Mradi huo unatarajiwa

kukamilika mwezi Desemba 2021 na utaondoa kero ya maji ya muda mrefu kwa wananchi wa maeneo husika.

**(xiv). Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28**

**104.Mheshimiwa Spika**, Serikali imepata mkopo wa **Dola za Marekani milioni 500** kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim India kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara na mji mmoja visiwani Zanzibar. Hadi mwezi Machi 2021,taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi zimekamilikana wakandarasi watakuwa maeneo ya miradi mwishoni mwa mwezi Mei 2021.

**(xv). Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu**

**105.Mheshimiwa Spika**, mradi wa kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Simiyu unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya KfW na Mfuko wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund - GCF*) na Serikali ya Ujerumani. Lengo la mradi huo ni kuboresha afya na kuongeza uzalishaji mali ili kuinua hali ya maisha ya wananchi walioathirika na mabadiliko ya tabianchi kwa kuimarisha huduma za maji. Katika awamu ya kwanza mradi utatekelezwa katika Wilaya za Busega, Bariadi na Itilima kwa gharama ya takribani **Shilingi bilioni 477.09**. Kulingana na mkataba wa makubaliano ya utoaji fedha GCF watachangia takriban **Shilingi bilioni 286.53**, Serikali ya Ujerumani itachangia **Shilingi bilioni 72.819**, Serikali ya Tanzania **Shilingi bilioni 113.55**na nguvu ya wananchi **Shilingi bilioni 4.185**.

**106.Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huo utachukua maji kutoka Ziwa Victoria na kuyapeleka katika Miji Mikuu ya Wilaya za Busega, Bariadi na Itilima na vijiji zaidi ya 200 vilivyoko pembezoni mwa bomba kuu umbali wa kilomita 12 kila upande; ukarabati na ujenzi wa mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji na mifugo; uimarishaji wa huduma za usafi wa mazingira kwa kujenga mabwawa ya majitaka na vyoo vya

mfano katika mashule na vituo vya afya; na kujenga uwezo wa watumishi wa sekta ya maji kwa Wilaya husika, Mkoa pamoja na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ili kutimiza malengo ya mradi kwa ufanisi.

**107.Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2021, uthamini wa ardhi na mali zilizopo kwenye maeneo ambayo bomba kuu la maji litapita umekamilika. Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mtaalam Mshauri atakayejenga uwezo wa Wataalam na Mtaalam Mshauri atakayefanya mapitio ya usanifu na kusimamia ujenzi wa mradi zinaendelea. Ujenzi wa mradi unatarajia kuanza mwezi Desemba, 2021.

**(xvi). Miradi ya Usafi wa Mazingira**

**108.Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kujenga miundombinu ya majitaka katika maeneo mbalimbali mijini ili kuboresha huduma ya uondoshaji majitaka. Ujenzi wa miundombinu hiyo unaendelea katika miji ya Arusha, Tanga na Mwanza. Aidha, katika Miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Bukoba na Musoma usanifu wa miundombinu ya majitaka unaendelea na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**109.Mheshimiwa Spika**, kwa miji inayotoa huduma ya uondoshaji wa majitaka kwa kutumia magari maalum ujenzi wa mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka umekamilika katika Miji ya Kahama, Misungwi, Lindi, Magu, Kigoma, Nansio na Lamadi. Aidha, Serikali inaendelea kuboresha huduma kwa kujenga na kupanua mifumo pamoja na ununuzi wa magari ya uondoshaji majitaka kwa lengo la kufikisha wastani wa**asilimia 30** ifikapo mwaka 2025.

**(xvii). Miradi ya Maji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa**

**110.Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya kandokando ya maziwa makuu wanapata huduma ya maji safi, salama na ya kutosheleza, Serikali imeanza kutekeleza miradi ya kutoa maji kwenye maziwa hayo. Miradi hiyo ni mradi wa maji wa Ziwa

Victoria, Mradi wa Maji wa Ziwa Tanganyika na Mradi wa Maji wa Ziwa Nyasa. Utekelezaji wa miradi hiyo utasimamiwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

**(d)Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria**

**111.Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria ambapo hadi mwezi Machi 2021, usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni umekamilika. Mradi huo utagharimu **Shilingi bilioni 750.697** na unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka 2021/ 22.Mradi utakapokamilika unatarajiwa kuhudumia wananchi wapatao **2,854,292** walipo katika vijiji **300** vya Halmashauri za Wilaya za Geita, Chato, Nyangh'wale na Mbogwe katika Mkoa wa Geita; Sengerema, Magu, Misungwi, Buchosa na Manispaa ya Ilemela katika Mkoa wa Mwanza; Bukoba Mjini, Bukoba Vijijini, Muleba, Biharamulo na Misenyi (Mkoa wa Kagera); Rorya, Musoma Vijijini na Bunda (Mkoa wa Mara); na Busega mkoani Simiyu. Utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2021/22. **(e) Mradi wa Maji wa Ziwa Tanganyika 112.Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2021, usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa maji wa Ziwa Tanganyika umekamilika. Mradi huo utagharimu **Shilingi bilioni 117.412** na utahusu ujenzi wa skimu **32**. Utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2021/22 na unatarajiwa kuwanufaisha wakazi wapatao **616,000** wa vijiji **73** vya Halmashauri za Uvinza, Nkasi, Kalambo, Mpimbwe na Tanganyika.

**(f) Mradi wa Maji wa Ziwa Nyasa**

**113.Mheshimiwa Spika**, usanifu wa kina wa mradi wa maji wa Ziwa Nyasa unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021. Mradi huo utatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kwenye Mkoa wa Ruvuma na Halmashauri ya Ludewa ilipo katika Mkoa wa Njombe. Mradi unatarajiwa kuhudumia wananchi wapatao **30,000** wa vijiji **13** vya Wilaya

ya Ludewa na wananchi wapatao **120,000** wa vijiji**27** vya Wilaya ya Nyasa.

### 3.2.5 Taasisi zilizo Chini ya Wizara

#### (i). Mfuko wa Taifa wa Maji

**114.Mheshimiwa Spika**, Serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Maji kupitia Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na.12 ya mwaka 2009. Kwa sasa Mfuko unatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019. Majukumu ya Mfuko ni kutafuta vyanzo vya fedha, kutoa fedha kwa watekelezaji kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na kufuatilia matumizi ya fedha hizo.

**115.Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 vyanzo vya mapato ya Mfuko ni pamoja na fedha zitakazoidhinishwa na Bunge, misaada pamoja na fedha nyingine zitakazolipwa kwenye Mfuko kwa mujibu wa Sheria nyingine. Katikamwaka 2020/21 Mfuko wa Taifa wa Maji ulitengewa **Shilingi 175,912,837,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji. Hadi mwezi Machi 2021, jumla ya **Shilingi 131,742,995,737.13** sawa na **asilimia 74.9** zimepokelewa kutoka Hazina na kutumika kutekelezamiradi ya maji nchini.

#### (ii). Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

**116.Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira, Serikali kupitia Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019, ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Lengo la kuanzishwa kwa Wakala huo ni kuongeza ufanisi katika ujenzi na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini ikiwa ni pamoja na jukumu la kuchimba visima na kujenga mabwawa. Pamoja na majukumu hayo, RUWASA pia imepewa jukumu la kudhibiti utoaji wa huduma ya maji vijijini kwa kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (*Community Based*

*Water Supply Organisation – CBWSOs*).Kwa sasa, RUWASA inafanya kazi kwenye Mikoa 25 isipokuwa Mkoa wa Dar es Salaam ambao unahudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

**117.Mheshimiwa Spika**, RUWASA imeendelea na ujenzi wa miradi ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na kusimamia utoaji wa huduma hiyo kupitia Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) ikiwa ni pamoja na kuvijengea uwezo vyombo hivyo ili viweze kutoa huduma bora na endelevu. Vilevile, RUWASA imeendelea kuimarisha utendaji kazi wake na kujenga uwezo kwa kununua vitendeakazi, kujenga Ofisi na kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuwezakutekeleza na kusimamia miradi kwaufanisi zaidi.

**(iii).Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira**

**118.Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019. Mamlaka hizo, zimepewa jukumu la kutoa huduma za majisafi na salama pamoja na usafi wa mazingira katika maeneo ya mijini. Katika mwaka 2020/21 maunganisho ya wateja kwa huduma ya majisafi katika Mamlaka za miji mikuu ya mikoa yameongezeka kutoka wateja **869,275** mwezi Machi 2020 hadi kufikia **942,995** mwezi Machi, 2021.

**119.Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zimekuwa zikiendelea na jitihada mbalimbali ili kuimarisha huduma ya uondoshaji majitaka katika maeneo ya mijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miundombinu ya majitaka. Kutokana na jitihada hizo, idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa majitaka imeongezeka kutoka wateja **50,685** mwezi Machi, 2020 hadi kufikia wateja **52,661**mwezi Machi 2021.

**120.Mheshimiwa Spika**,huduma ya uondoshaji wa majitaka pia hutolewa kwa kutumia magari maalum ya kuondoa majitaka. Hadi mwezi Machi 2021 huduma hiyo inatolewa katika Mamlaka za Sumbawanga, Bukoba, Musoma, Geita,

Kigoma na Sengerema ambapo kumejengwa mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka. Aidha, katika mwaka 2020/21 ujenzi wa mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka umekamilika katika miji ya Kahama, Lindi, Misungwi, Magu na Lamadi.

### (iv). Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA)

**121.Mheshimiwa Spika**, EWURA imepewa majukumu ya kudhibiti utoaji wa huduma za nishati na maji. Kwa upande wa sekta ya nishati, EWURA inadhibiti huduma za umeme, mafuta na gesi asilia na huduma hizo zinasimamiwa na Wizara ya Nishati. Kwa upande wa sekta ya maji, EWURA inadhibiti masuala ya ubora wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira zinazosimamiwa na Wizara ya Maji. Katika kutekeleza majukumu yake ya udhibiti, EWURA inatoa leseni kwa watoa huduma; kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma; kutathmini na kuidhinisha bei za huduma; pamoja na kutoa miongozo mbalimbali na kutatua migogoro baina ya watoa huduma na wateja wao.

**122.Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, kwa upande wa sekta ya maji EWURA imeendelea kudhibiti huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini.Kazi zilizofanyika ni pamoja naukaguziwa miundombinu inayotoa huduma ya majisafi na uondoshaji wa majitaka katika mamlaka za maji **78**; uhakiki wa ubora wa majisafi katika mamlaka **64**; na uhakiki wa ubora wa majitaka yanayotoka katika mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka katika mamlaka **12**.

**123.Mheshimiwa Spika**, vilevile EWURA ilifanya ukaguzi kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira za Dodoma eneo la huduma la Chamwino katika kuhakikisha kuwa mamlaka hiyo inatibu maji kabla ya kusambaza kwa wateja na Mamlaka ya Maji Tanga katika kuhakikisha wananchi wanapata ankara zilizo sahihi kulingana na matumizi yao ya maji. Aidha, Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira za Gairo, KASHWASA, Nzega, Igunga na Tabora zilifanyiwa ukaguzi maalum.

Kutokana na matokeo ya kaguzi hizo, EWURA ilitoa maelekezo na ushauri ikiwa ni pamoja na taratibu bora za uendeshaji, matengenezo, ukarabati, matumizi ya teknolojia bora na uboreshaji wa miundombinu ili kuboresha utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwenye mamlaka husika.

**124.Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti bei za maji, EWURA ilifanya tathmini na ukaguzi wa bei, tozo na mfumo wa utoaji wa ankara za maji kwa mamlaka za maji **20** nchini na kuchukua hatua za kiutendaji na kisheria kwa mamlaka za maji zilizokiuka taratibu. Mamlaka hizo ni Bunda, Musoma, MugangoKiabakari, Sengerema, Mbeya, Vwawa-Mlowo, Songea, Njombe, Makambako, Tanga, Kigoma, Shinyanga, Kahama, Bukoba, Geita, Ngara, Arusha, Moshi, Kibaigwa na Iringa. EWURA pia ilitoa maelekezo kwa mamlaka za maji nchini kuhakikisha kuwa zinawashirikisha wateja wakati wa usomaji wa dira (mita za maji) kwa kutumia mfumo wa kieletroniki ambapo wateja watakuwa wanapata ujumbe mfupi kwenye simu kuwajulisha kuwa dira zao zimesomwa na kiasi cha matumizi ya maji kwa mwezi husika. Aidha, EWURA imeendelea kutoa elimu kwa wadau wake kuhusu masuala mbalimbali ya kiudhibiti ikiwa ni pamoja na taratibu za kupanga bei za maji.

**125.Mheshimiwa Spika**, aidha, EWURA imeendelea kuzijengea uwezo mamlaka za maji nchini kuhusu kuandaa mpango wa ufuatiliaji wa ubora wa maji. Vilevile, mamlaka za maji 25 zilipatiwa mafunzo ya kuandaa mpango wa biashara ili kuweza kuongeza mapato. EWURA pia ina jukumu la kuandaa taarifa za utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kila mwaka. Taarifa hizo husaidia kuchochea ushindani wa Mamlaka za Maji nchini katika kuboresha huduma.

### (v). Chuo cha Maji

**126.Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Maji ni Taasisi yenye jukumu la kuandaa wataalam wa Sekta za maji na umwagiliaji. Majukumu mengine yanayotekelezwa na chuo ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na kufanya tafiti mbalimbali

kwa ajili ya maendeleo ya Sekta. Chuo kinatoa mafunzo katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada. Katika ngazi ya Astashahada na Stashahada mafunzo yanayotolewa ni Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Engineering*); Uhandisi wa Umwagiliaji (*Irrigation Engineering*); Haidrojiolojia na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Water Well Drilling*); Haidrolojia na Hali ya Hewa (*Hydrology and Meteorology*); pamoja na Teknolojia ya Maabara na Ubora wa Maji (*Water Quality Laboratory Technology*). Katika ngazi ya Shahada, mafunzo yanayotolewa ni katika fani ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation*). Vilevile, Chuo kinaendesha kozi mbalimbaliza muda mfupi katika sekta za maji na umwagiliaji.

**127.Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, wanafunzi **801**wa Astashahada na Stashahada wamedahiliwa.Udahili huo umeongezeka kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi **450** waliodahiliwa katika mwaka 2019/ 20. Vilevile, wanafunzi **218** wa Shahada ya kwanza ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji walidahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi **206**katika mwaka 2019/20. Kwa sasa, chuo kina jumla ya wanafunzi **2,093** ambapo wanafunzi **1,403** ni wa Astashahada na Stashahada na wanafunzi **690** ni wa Shahada ya kwanza. Aidha, katika mahafali ya Januari 2021, jumla ya wanafunzi **529** walihitimu mafunzo yao ambapowanafunzi **153** ni waShahada, **355** wa Stashahada na wahitimu **21** walikuwa wa ngazi ya Astashahada.

**128.Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha taaluma bora inatolewa, Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake katika ngazi za Shahada ya kwanza, Uzamili na Uzamivu. Hadi mwezi Machi 2021,watumishi **11** wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*); Mtumishi **mmoja** (**1**)ni Shahada ya pili (*Masters*) na watumishi **watatu** (**3**) ni Shahada ya kwanza. Vilevile, kupitia fedha za ndani, Chuo kinajenga zahanati mpya ambayo ujenzi wake umefikia asilimia **70**. Aidha, chuo kimenunua vifaa vya maabara za *Hydraulics* na *Hydrogeology*.

### 3.2.6 Masuala Mtambuka

**(i). Sera ya Taifa ya Maji**

**129.Mheshimiwa Spika**,Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 imetekelezwa kwa zaidi ya miaka 18 sasa. Katika kipindi hicho, kumekuwepo na mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na kimfumo katika Sekta ya Maji. Haya yote yanahitaji mabadiliko ya kisera ili uwekwe mfumo endelevu wa usimamizi wa rasilimali za maji na utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira wakati nchi yetu inaelekea kuwa ya uchumi shindani. Kwa kuzingatia hayo, katika mwaka 2020/21, Wizara yangu imeanza mchakato wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002.

**(ii).Sheria**

**130.Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake, sekta ya maji inaongozwa na Sheria ambazo zimegawanyika katika maeneo muhimu matatu ya rasilimali za maji; utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira; na udhibiti wa utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira.

**131.Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009inasimamia rasilimali za maji zilizo juu na chini ya ardhi ikiwemo mito, maziwa na mabwawa, na kuzuia uchafuzi wa maji katika vyanzo. Malengo na madhumuni ya Sheria hii ni kuhakikisha rasilimali za maji hapa nchini zinatunzwa, zinatumiwa, zinaendelezwa, zinaboreshwa, zinasimamiwa na kudhibitiwa kwa ajili ya manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

**132.Mheshimiwa Spika**,katika mwaka 2020/21 Wizara imekamilisha kutayarisha rasimu ya mapendekezo ya kuirekebisha Sheria Na. 11/2009 kwa lengo la kuimarisha mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji. Mapendekezo hayo yapo katika hatua za mwisho za kuridhiwa na Serikali kabla ya kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu. Aidha, Wizara ilikamilisha kutayarisha Oda ya kutangaza mabonde madogo (*catchments*) katika Bonde la Ziwa Victoria na Notisi ya

kutangaza eneo la hifadhi ya eneo oevu la chemichemi ya Kitwiri lililopo katika Bonde la Rufiji kuwa chanzo cha maji kinacholindwa kisheria.

**133.Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 inasimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira katika miji na vijiji katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Malengo na madhumuni ya sheria hii ni kuhakikisha kuwa kila mtu anapata huduma ya maji na usafi wa mazingira ya uhakika na endelevu.Katika utekelezaji wa Sheria hiyo,kwa mwaka 2020/21 Wizara imekamilisha kuandaa notisi ya kuanzisha mamlaka moja ya maji na notisi za kuongeza maeneo ya huduma ya mamlaka za maji tatu kama zifuatavyo:-

(i). *The Water Supply and Sanitation (Busega Urban Water Supply and Sanitation Authority)(Establishment) Notice, 2020.*

*(ii). The Water Supply and Sanitation (Kahama Shinyanga Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area) Notice, 2020.*

*(iii). The Water Supply and Sanitation (Sengerema Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of the Service Area) Notice, 2020; na*

*(iv). The Water Supply and Sanitation (Bukoba Urban Water Supply and Sanitation Authority)(Extension of the Service Area) Notice, 2020.*

**(iii). Ujenzi wa Majengo Katika Wizara**

**134.MheshimiwaSpika**, Wizara imeendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi kwa Bodi za Maji za Mabonde na Maabara za Maji. Hadi mwezi Machi, 2021, ujenzi wa majengo ya ofisi za Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu-Morogoro pamoja na Ofisi ya Jumuiya ya Watumia Maji ya Kilosa umefikia **asilimia 70**, Ofisi ndogo za Bonde la Wami/Ruvu Dodoma **(95)**, Ruvuma na Pwani ya Kusini-Lindi **(97)**, Ziwa NyasaNjombe na ukarabati wa ofisi ndogo za Bonde la Ziwa

Nyasa – Songea **(55),** Ziwa Rukwa - Mbeya na Sumbawanga **(80),** Rufiji - Iringa **(60)** na Ofisi za Jumuiya za Watumia Maji za Kimani na Mkoji **(85)**;na Bonde la Kati - Singida ujenzi wake umefikia **asilimia 99**. Kwa upande wa Maabara za Maji, ujenzi wa Maabara ya Maji Mtwara umefikia **asilimia 95,** Morogoro **70**, Sumbawanga **85**, Mbeya **50** na ukarabati wa Maabara ya Songea umefikia asilimia **56**. Aidha,kwa upande wa jengo la ofisi ya Wizara katika Mji wa Serikali, usanifu wa jengo na maandalizi ya michoro umekamilika na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea.

**(iv). Mapambano Dhidi ya Rushwa**

**135.Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu (*National Anti-Corruption Strategy and Action Plan - NACSAP III*) kwa lengo la kupambana na vitendo vya rushwa kwenye maeneo yote ya kazi. Vilevile, Wizara iliunda Kamati ya Uongozi na Usimamizi pamoja na Kamati ya Uadilifu kwa ajili ya kusimamia mapambano dhidi ya rushwa ngazi ya Wizara naTaasisi zake. Hadi mwezi Machi, 2021 jumla ya watumishi **2,182** walipatiwa elimu juu ya mapambano dhidi ya rushwa na uadilifu. Aidha, jumla ya watumishi **14** walichukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu na kisheria kutokana na makosa ya rushwa na uadilifu. Juhudi za mapambano dhidi ya rushwa zinaendelea sambamba na kuhakikisha kuwa wananchi wanatambua haki na wajibu wao katika kupokea huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara kupitia Mkataba wa huduma kwa mteja.

**(v).UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza**

**136.Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Mwongozo wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa kutoa elimu kuhusu magonjwa hayo kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Hadi mwezi Machi, 2021, mafunzo kwa watumishi kuhusu kujikinga na magonjwa hayo yametolewa kwa watumishi **2,182**.Aidha,posho kwa ajili ya kununua lishe bora na usafiri kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI imeendelea kutolewa.

### (vi). Rasilimali Watu Katika Sekta ya Maji

**137.Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha sekta ya maji inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija hususan baada ya mabadiliko ya kimuundo na kimfumo, Serikali iliajiri watumishi **472** kwenye sekta ya maji na kufanya idadi ya watumishi kufikia **8,729**. Hata hivyo, katika sekta ya maji bado kuna upungufu wa takriban watumishi **1,547** ili kukidhi ikama ya watumishi. Wizara inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais-UTUMISHI kwa ajili ya kupata kibali cha kuajiri wataalam wa kutosha katika sekta ya maji ili kukabiliana na upungufu uliopo. Vilevile, Wizara itaendelea kuzihimiza Taasisi zake zenye upungufu kutenga fedha kwa ajili ya kuajiri watumishi.

**138.Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbalimbali. Hadi mwezi Machi, 2021, jumla ya watumishi **558** wamepata mafunzo na kati yao watumishi**28** walipata mafunzo ya muda mrefu na watumishi **530** walipata mafunzo ya muda mfupi. Wizara imeendelea kutoa miongozo mbalimbali na kuhimiza matumizi ya sheria na nyaraka katika kushughulikia masuala ya watumishi kwenye Taasisi zake.

## 3. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

**139.Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya maji ni pamoja na:-

(i). Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kutoka asilimia 70.1 vijijini na 84 mijini mwaka 2019/20 hadi **asilimia 72.3** vijijini na **86** mijijni;

(ii). Kuongezeka kwa idadi ya maabara za ubora wa maji zenye ithibati kutoka moja (1) ya Mwanza hadi kufikia **Saba (7)**;

(iii). Kuzinduliwa kwa miradi mikubwa ya maji ya Tabora – Igunga - Nzega pamoja na Isaka – Kagongwa baadaya kazi kubwa ya utekelezaji wake kukamilika;

(iv). Kukamilika kwa utekelezaji wa kihistoria wa miradi 422 ya maji ambapo kati ya hiyo ya vijijini ni miradi 355 na mijini miradi 67;

(v). Kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji na kupungua kwa gharama za ujenzi kutokana na kutumia utaratibu wa *force account*; na

(vi). Kuanza kutoa huduma ya maji kwa miradi 85 iliyokuwa na changamoto baada ya kupata ufumbuzi.

## 4. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

**140.Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/21 Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa vyanzo vya maji,upatikanaji mdogo wa fedha za kutekeleza miradi ya maji, utendaji usioridhisha wa wakandarasi, mwamko mdogo wa wananchi kulipia huduma ya maji na upungufu wa Wataalam wa Sekta ya Maji. Maelezo ya kina kuhusu changamoto na hatua zinazochukuliwa kukabiliana nazoni kama ifuatavyo:-

### (i). Uharibifu wa Vyanzo vya Maji

**141.Mheshimiwa Spika**, Wizara imekabiliwa na changamoto ya uharibifu na uvamizi wa vyanzo vya maji ikiwemo mito, maziwa, mabwawa, chemichemi na ardhi oevu. Hii inatokana na ongezeko la watu linaloenda sambamba na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii ili kukidhi mahitaji ya kila siku ya mwanadamu. Shughuli hizo zinahusisha kilimo, ufugaji na uanzishaji wa makazi katika maeneo ya vyanzo vya maji. Mbali na kuongezeka kwa shughuli hizo za kibinadamu, uharibifu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na uelewa mdogo wa jamii juu ya utunzaji wa mazingira na

madhara yatokanayo na uharibifu wa vyanzo vya maji, uhaba wa miundominu ya umwagiliaji na kunyweshea mifugo na uelewa mdogo juu ya sheria ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Aidha, Wizara ya Maji katika kulinda na kusimamia vyanzo vya maji nchini inashirikiana na Wizara za kisekta.

**142. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde imeendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano (*Communication Strategy*) kwa kutoa elimu juu ya sheria ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji na kuhamasisha jamii katika utunzaji wa vyanzo vya maji. Elimu imekuwa ikitolewa kupitia vipindi vya Television na Radio, Warsha, Semina, Makongamano, Majukwaa ya wadau wa maji na maonesho mbalimbali. Aidha, Wizara imeendelea kuweka mipaka katika vyanzo vya maji vilivyo katika hatari ya kuharibiwa au kuvamiwa na kutangaza baadhi ya maeneo ya vyanzo vya maji kwenye Gazeti la Serikali kama maeneo tengefu. Vilevile, Wizara imeendelea na uanzishaji wa Kamati za Vidakio (*Catchment Water Committees*) na Jumuiya za Watumia Maji katika maeneo mbalimbali ya vyanzo vya maji nchini ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali hiyo.

**(ii).Mahitaji Makubwa ya Kutekeleza Miradi ya Maji**

**143.Mheshimiwa Spika**, mahitaji ya fedha katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji ikiwemo ujenzi wa mabwawa ya Kidunda, Farkwa, Songwe na Ndembera/Lugoda na miradi ya kutoa maji kwenye mito mikubwa na maziwa ni makubwa kulinganisha na fedha zinazopatikana. Hali hiyo, imesababisha kuchelewa kuanza kutekelezwa kwa miradi hiyo. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kukidhi mahitaji ya miradi ya maji kulingana na mipango.

**(iii). Utendaji Usioridhisha wa Wakandarasi**

**144.Mheshimiwa Spika**, baadhi ya Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji wamekuwa hawatekelezi

majukumu yao kwa kadri ya matakwa ya mikataba. Hali hiyo imesababisha baadhi ya miradi kusuasua hivyo kutokukamilika kwa muda uliopangwa. Miradi hiyo ni pamoja na, Same-MwangaKorogwe, Usafi wa mazingira Musoma, Majisafi na usafi wa mazingira Kigoma, Majisafi na usafi wa mazingira Lindi na mradi wa majisafi Chalinze Awamu ya tatu. Serikali imeendelea kukabiliana na changamoto hiyo ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kuvunja mikataba iliyoingiwa kati ya Wizara na Watoa huduma hao na wakati mwingine kuamua kutumia utaratibu wa *Force Account* katika utekelezaji wa miradi ili kukwamua miradi hiyo.Vilevile, Serikali itahakikisha uhakiki na upekuzi wa kina (*due diligence*) wa wakandarasi na wataalam washauri unafanyika ili kujiridhisha kuhusu uwezo wao wa kitaalam na kifedha na hivyo kupata watoa huduma wenye uwezo unaostahiki.

**(iv). Mwamko mdogo wa Wananchi kulipia Huduma za Maji**

**145.Mheshimiwa Spika**, Sera ya Maji ya mwaka 2002 imeeleza umuhimu wa jamii kuchangia gharama ya uendeshaji na matengezo ya miradi ya maji vijijini kwa kulipia huduma hiyo. Hata hivyo, mwitikio wa jamii katika kulipia huduma ya maji vijijini ni mdogo hivyo kusababisha miradi mingi kushindwa kujiendesha na kuwa endelevu. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeendelea kuwajengea uelewa wananchi na kuwahamasisha kulipia huduma ya maji ili kumudu gharamaza uendeshaji na matengezo ya miradi ya maji vijijini. Aidha, katika kuimarisha ushiriki wa jamii katika miradi ya maji, Vyombo vya Utoaji Huduma za Maji ngazi za Jamii (*CBWSOs*) vimeundwa na kujengewa uwezo ili kusimamia kikamilifu utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini.

**(v).Upungufu wa Wataalam katika Sekta ya Maji.**

**146.Mheshimiwa Spika**, sekta ya maji inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wataalam wa kada mbalimbali wanaohitajika katika utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji. Kwa sasa sekta ya maji ina watumishi **8,729** ambapo mahitaji halisi ni watumishi **10,276** na hivyo kuwa na upungufu wa

watumishi **1,547**. Katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi, Wizara inaendelea kuomba vibali vya ajira kutoka Ofisi ya RaisUTUMISHI kwa ajili ya kupata wataalam wa kutosha na wenye sifa katika Sekta nzima ya Maji.Vilevile, Wizara itaendelea kuzihimiza Taasisi zake zenye upungufu kutenga fedha kwa ajili ya kuajiri watumishi.

## 5. MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2021/22

**147.Mheshimiwa Spika**,napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mpango wa Utekezaji wa miradi ya maji kwa mwaka 2021/22 umeshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge katika kuibua miradi ya kipaumbele**.** Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano na OR-TAMISEMI katika kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi ya maji katika Halmashauri za Wilaya nchini. Nimatumaini yangu kwamba utaratibu huu utawezesha kufikia malengo ya sekta ya maji kwa haraka na uhalisia**.** Mpango na Bajeti umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2016 – 2030, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Sera mbalimbali za Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 – 2025) na Maagizo na ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais na Viongozi wengine wa Kitaifa; pamoja na maoni ya waheshimiwa Wabunge kama nilivyotangulia kusema.

**148. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Serikali imepanga kuendelea kuweka msisitizo katika usimamizi wa watendaji, uvunaji wa maji ya mvua hususan kwenye maeneo kame, usimamizi wa Vyombo vya Utoaji Huduma za Maji Vijijini (CBWOs), kutumia Chuo cha Maji kikamilifu na kuimarisha kitengo cha uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa. Aidha, mipango imejikita katika maeneoyausimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma za ubora wa maji; huduma za usambazaji maji na usafi wa mazingira vijijini; huduma za usambazaji majisafi na usafi wa mazingira mijini; na utekelezaji wa kazi mbalimbali katika Taasisi zilizo chini ya Wizara na masuala mtambuka kama ifuatavyo:-

### 5.1. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za maji

**149.Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa takwimu za hali ya rasilimali za maji, kusimamia utoaji wa vibali vya matumizi ya maji ili kupunguza migogoro, kuratibu uchimbaji wa visima vya maji nchini, uvunaji wa maji ya mvua hususan kwenye maeneo kame, kutangaza vyanzo **28** kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji, kubaini vyanzo vipya kwa lengo la kuvitunza, kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali na kuimarisha ushirikiano na nchi wanachama katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji shirikishi.

### 5.2. Usimamizi wa Huduma ya Ubora wa Maji

**150.Mheshimiwa Spika**,kwa upande wa huduma ya ubora wa maji, Wizara itaendelea kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo na mifumo ya usambazaji kwa kukusanya na kuchunguza sampuli **15,000** za maji, kutoa elimu juu ya viwango vya ubora wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali, kuhakiki ubora wa madawa ya kutibu maji, kutengeneza na kusambaza mitambo **800** ya kuondoa madini ya *fluoride* inayotumika ngazi ya kaya, kuimarisha uhakiki na ufuatilia ubora wa majitaka kwa kupima na kuhakiki takribani sampuli **2,000** za majitaka pamoja na kuendelea kuimarisha maabara za maji.

### 5.3. Miradi ya Majisafi na usafi wa Mazingira

**151.Mheshimiwa Spika**,katika mwaka 2021/22, Serikali imepanga kutekeleza jumla ya miradi **1,527** ya maji katika maeneo ya vijijini na miradi **114** ya mijini ikihusisha miradi mipya, miradi ya upanuzi na ukarabati wa miundombinu kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 4a** na **4b**. Aidha, Serikali imepanga kuchimba visima 516 na kujenga mabwawa 33 hususan katika maeneo kame nchini. Vilevile, Serikali imepanga kuimarisha Taasisi zinazosimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira nchini vikiwemo vyombo vya watumia maji (CBWSOs), Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na kusimamia ufuatilia wa utekelezaji wa miradi.

**152.Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali imepanga kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya maji vya maziwa makuu pamoja na mito mikubwa ya Rufiji, Ruvuma na Kiwira. Katika mwaka wa fedha 2021/22, kwa upande wa Mto Rufiji na Mto Ruvuma, Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miundombinu ya kupeleka maji katika miji iliyo karibu na mito hiyo.Aidha**,** Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa kutoa maji Mto Kiwira kupeleka katika Jiji la Mbeya. Ujenzi wa mradi utagharimu **Shilingi bilioni 75** na unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2021/22.

**153.Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali itaendelea kuboreshaji wa huduma ya usafi wa mazingira mijini kwa lengo la kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya uondoshaji majitaka kutoka **asilimia 13** hadi **asilimia 30** ifikapo Desemba, 2025

### 5.4. Taasisi za Wizara

#### (i). Mamlaka ya udhibiti wa huduma za Nishati na Maji (EWURA)

**154.Mheshimiwa Spika**, EWURAitaendelea kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake ya kiudhibiti kwa kutoa miongozo na kanuni mbalimbali kwa huduma inazozidhibiti; kukagua ubora wa miundombinu na taratibu za utoaji wa huduma; kudhibiti ubora wa huduma na bei ili watumiaji wapate huduma bora; na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kiudhibiti pamoja na haki na wajibu wao.

#### (ii). Chuo cha Maji

**155.Mheshimiwa Spika**, Chuo kitaendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuongeza wataalam wanaohitajika kwenye sekta ya maji kwa kudahili jumla ya wanafunzi **1,200;** kuboresha miundombinu katika mifumo ya majisafi, majitaka na TEHAMA; kuongeza vifaa vya kufundishia;na kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi. Aidha, ukarabati wa majengo ya

madarasa, maabara na karakana utaendelea sambamba na ujenzi wa miundombinu mipya hasa katika kampasi za Singida na Mwanza, pamoja na utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo mbalimbali nchini.

### 5.5. Masuala Mtambuka

**156.MheshimiwaSpika**, Wizara itaendelea na mapitio ya Sera ya Maji ya mwaka 2002, kuandaa kanuni na miongozo mbalimbali chini ya Sheria za Maji ili kuhakikisha kuwa sheria za maji zinatekelezwa kikamilifu, kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya 2009 kwa lengo la kuimarisha mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji. Aidha, Wizara itatafsiri sheria, kanuni na miongozo yote ya sheria za maji kuwa katika lugha ya Kiswahili.Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya Kielektroniki ili kuleta tija katika sekta,kutoa elimu na kuhamasisha watumishi wake kuendelea kupima afya zao, kusambaza vifaa kinga katika vituo vya kazi ili kudhibiti maambukizi ya *VVU.*

## 6. SHUKRANI

**157.Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa njia moja ama nyingine kufanikisha majukumu ya sekta ya maji katika kipindi cha mwaka 2020/21. Shukrani hizo ziwaendee nchi marafiki, washirika wa maendeleo, mashirika ya misaada ya kimataifa, taasisi za kiserikali, mashirika ya kidini pamoja na wadau wengine. Ninapenda kuwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika kutekeleza miradi ya maji. Kwa namna ya kipekee, ninapenda kuzishukuru nchi rafiki ambazo zimechangia katika maendeleo ya sekta ya maji nchini. Nchi hizo ni Uingereza, Ujerumani, Korea Kusini, Marekani, India, Uholanzi, Hispania, Ubelgiji, Ufaransa, Kuwait, Misri, Morocco na Saudi Arabia. Ninakiri kwamba, maendeleo hayo yanatokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika hao.

**158.Mheshimiwa Spika**, vilevile, ninapenda kuyashukuru mashirika ya maendeleo na Taasisi za kimataifa kwa misaada

ya kitaalam na fedha katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Dunia (*World Bank-WB*), Benki ya Maendeleo ya Africa (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW),* Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB)*, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development-OFID)*, Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait *(Kuwait Fund),*Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD),* Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza *(DFID),* Shirika la Maendeleo la Ujerumani*(GiZ),*Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*), *Global Environment Facility (GEF), Green Climate Fund (GCF),* Shirika la Afya Duniani *(WHO),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF),* Shirika la Maendeleo la Ubelgiji *(BTC),* Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP)* naShirika la Misaada la Marekani (*USAID).*

**159.Mheshimiwa Spika**,Mashirika na Taasisi za Kidini yameendelea kuongeza hamasa katika kuyafikia malengo tuliyojiwekea. Hivyo, ninapenda kuyashukuru mashirika na Taasisi hizo ambazo ni *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA), Norwegian Church Aid,Livingwater International, World Islamic League,* Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania,Islamic Foundation,* Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa Katoliki Tanzania na Kanisa la Kianglikana Tanzania.

**160.Mheshimiwa Spika**,vilevile,nazishukuruTaasisi zisizo za Kiserikali zinazoshiriki katika kuendeleza sekta ya maji. Taasisi hizo ni pamoja na *Association of Tanzanian Water Suppliers (ATAWAS), WaterAid, Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET),* Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya *(WAMMA),World Vision*; *Worldwide Fundfor Nature(WWF*), *Water Resources Integration Development Initiatives (WARIDI),Netherlands Volunteers Services (SNV),Plan International*, *Concern Worldwide*, *Water Mission* (T), Shirika

la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (*IUCN*) naMashirika mengine mbalimbali.

**161.Mheshimiwa Spika**,kwa namna ya pekee, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa**Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi**(Mb**)**, Naibu Waziri wa Maji; **Mhandisi Anthony Damian Sanga**, Katibu Mkuu; **Mhandisi Nadhifa Sadiki Kemikimba**, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wataalam na Watumishi wote wa Wizara ya Maji; pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu na Watumishi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha majukumu ya Wizara ya Maji yanatimizwa. Naishukuru familia yangu kwa upendo, ushirikiano na faraja katika kipindi chote na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Vilevile, natumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa jimbo la Pangani kwa kunilea, kuniamini, kunichagua kuwa mbunge wao na kuendelea kuwa nami bega kwa bega katika kutekeleza majukumu yangu.

**162.Mheshimiwa Spika**,mwisho lakini siyo kwa umuhimu ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi na watangulizi wangu katika Wizara ya Maji walionipokea na kushirikiana nami nikiwa kijana mdogo kwa kunishika mkono na kunifundisha kazi, kunishauri, kunipa miongozo na kuniimarisha kunifanya hivi nilivyo leo. Shukrani zangu ziwaendee Mheshimiwa Mhandisi **Isack Aloyce Kamwelwe**(Mb), Mheshimiwa **Profesa Makame Mnyaa Mbarawa** (Mb) na Mheshimiwa **Profesa Kitila Alexander Mkumbo** (Mb). Kwa dhati ya moyo wangu ninasema ahsante sana na mwenyezi Mungu awabariki sana.

## 7. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022

**163.Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 680,388,976,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2021/22. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 33,758,976,000** ambapo **Shilingi 15,273,812,000** sawa na **asilimia 45.2** ni kwa ajili ya kugharamia

Matumizi Mengineyo (*OC*) na **Shilingi 18,485,164,000**sawa na **asilimia 54.8** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (*PE*) ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 646,630,000,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 346,630,000,000** sawa na **asilimia 53.6** ni fedha za ndani na **Shilingi 300,000,000,000** sawa na **asilimia 46.4** ni fedha za nje.

**164.Mheshimiwa Spika**, ninaomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.maji.go.tz.

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nashangaa kwamba kuna Wabunge wamekaa na miradi yao imejaa humu kwenye hiki kitabu nawashangaa sana ama hawajasoma hiki kitabu, hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Tutaendelea sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati wa Bunge ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KUDUMU YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kunipatia nafasi ya kusoma hii taarifa, kabla sijaanza naomba taarifa yote ya kamati iweze kuingia katika Hansard pia naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(c)(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na

maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inafafanua mambo matano kama yalivyoainishwa katika taarifa mliyopewa ukurasa wa kwanza. Maoni na ushauri uliotolewa ni matokeo ya uchambuzi wa nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati, majadiliano kati ya Kamati na wadau mbalimbali na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ushauri wa Kamati. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo manne ya kipaumbele kama yalivyoainishwa katika taarifa mliyopewa ukurasa wa 3. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umetekelezwa. Aidha, baadhi ya ushauri upo katika mwendelezo wa utekelezaji katika mpango wa bajeti wa mwaka 2020/2021. Kamati inasisitiza kuongeza kasi ya utekelezaji ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yalijielekeza katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika na eneo la ukusanyaji mahuhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Machi 2021. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Fungu 49 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 733,284,075,000. Kati ya fedha hizo shilingi 28,275,145,000 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 705,008,930,000 zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 349,449,000,000.00 sawa na asilimia 49.57 ni Fedha za Ndani ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 175,912,837,000.00 ni za Mfuko wa Taifa wa Maji na shilingi 173,536,163,000.00 ni fedha zinazotokana na vyanzo vingine vya ndani. Aidha, shilingi 355,559,930,000.00 sawa na asilimia 50.43 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Aprili 2021, Wizara ilikua imepokea jumla ya shilingi 396,771,027,717.02 sawa na asilimia 54.10 ya bajeti ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi 20,349,425,596.52 sawa na asilimia 71.96 ni bajeti ya fedha za Matumizi ya Kawaida na Sh.376,421,602,120.50 sawa na asilimia 53.39 ni bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 192,167,225,844.98 ni fedha za nje, sawa na asilimia 54.04 na fedha za ndani ni shilingi 184,254,376,275.52 sawa na asilimia 45.96. Aidha, kiasi kilichotokana na Mfuko wa Maji ni shilingi 131,742,995,737.13 sawa na asilimia 74.89 na shilingi 52,511,380,538.39 ni za Mfuko wa Serikali, sawa na asilimia 30.25.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Maji ilipanga kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi 8,187,410,210.00 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Machi, 2021, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 8,283,735,610.43 sawa na asilimia 101 ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo na kuvuka lengo la ukusanyaji kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha tarehe 30 Juni. Kamati imeridhishwa na Mpango wa Wizara wa kuongeza wigo wa makusanyo ya maduhuli maradufu kwa Bajeti ya 2021/2022 ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo uliotengewa fedha kwa mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha (2020/2021). Ili kutekeleza masharti ya kanuni hiyo, Kamati ilipanga kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maji katika Mkoa wa Morogoro, Pwani, Dar es Salaam na Dodoma. Hata hivyo, ziara hiyo haikuweza kufanyika kwa ukamilifu kutokana na ziara kusitishwa, kufuatia msiba uliolikumba Taifa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kabla ya hapo, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Morogoro. Miradi iliyokaguliwa ni kama kama ilivyoanishwa katika taarifa mliyopewa, ukurasa wa 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga fedha na kuanza utekelezaji wa miradi hii yenye lengo la kuongeza upatikanaji maji kwa wakazi wa Manispaa ya Morogoro. Aidha, Kamati inasisitiza Serikali ichukue hatua za makusudi kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazotajwa kuathiri utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji, zikiwemo kukabiliana na uvamizi wa vyanzo vya maji katika Milima ya Ulugulu inayozunguka Manispaa ya Morogoro, kukabiliana na uchafuzi wa Bwawa la Mindu ambalo ni chanzo kikuu cha maji kwa Manispaa ya Morogoro. Pia Kamati inaisisitiza Serikali kutafuta vyanzo vingine vipya vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo Wizara imeendelea kusimamia kama ilivyoainishwa katika taarifa mliyopewa ukurasa wa 8. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kupitia utekelezaji uliofanywa umeweza kuwa na matokeo chanya kwa kuongezeka kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kama ilivyoainishwa katika taarifa ukurasa wa 9.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Kamati imeridhishwa na jitihada na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kutekeleza miradi ya maji sehemu mbalimbali nchini. Hata hivyo, Kamati inatoa rai kwa Wizara kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa miradi kwa kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi na hatua za kisheria kwa wakandarasi watakaoshindwa kutimiza majukumu na matakwa ya mikataba iliyopo. Ni kweli maji ni muhimu na bado wananchi wanahitaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wake. Changamoto hizo ni kama zilivyoainishwa katika taarifa mliyopewa ukurasa wa 10. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za kurekebisha kasoro hizi ili kuimarisha sekta ya maji.

Mpango wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Katika kutekeleza jukumu la Bunge la kuishauri na kuisimamia Serikali, kwa niaba ya wananchi tarehe 29 Machi 2021, Kamati ilipokea na kuchambua mpango wa bajeti wa Wizara ya Maji na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022, mpango ambao umezingatia pamoja na mambo mengine ukomo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 kazi zitakazofanyika zimejikita katika maeneo ya vipaumbele kama yalivyoainishwa katika taarifa mliyopewa ukurasa wa 12 - 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazoombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kutekeleza kazi zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Maji kupitia Fungu 49 ni kama zilizoainishwa kwenye kitabu chetu mlichopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazoombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji ya Maendeleo. Kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Maji kupitia Fungu 49 inaomba kuidhinishiwa shilingi 646,630,000,000.00. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 346,630,000,000 sawa na asilimia 53.675 ni fedha za ndani na shilingi 300,000,000,000 sawa na asilimia 46.4 ni fedha za nje. Fedha za maendeleo zinazoombwa ni za kugharamia miradi mbalimbali nchi ikiwepo miradi ya kipaumbele kama ilivyoainishwa katika taarifa mliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Maji Fungu 49 inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 15,000,000,000 kutokana na vyanzo mbalimbali kama vilivyoainishwa katika taarifa ukurasa wa 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya bajeti. Kamati imepitia, imechambua na kutathimini malengo na vipaumbele viliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti wa mwaka 2021/2022. Kamati imeridhika kwamba malengo haya ni ya msingi kwani yanalenga kuongeza upatikanaji wa maji nchini kwenye maeneo yaliyokuwa yanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mabwawa ya kimkakati kama ilivyoelekezwa katika taarifa mliyopewa ukurasa wa 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya kuboresha upatikanaji wa Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, kipekee Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua miradi ya kuimarisha upatikanaji maji katika Jiji la Dodoma. Malengo hasa ya kutembelea miradi hii katika Jiji la Dodoma ni kutokana kuwepo changamoto ya upungufu wa majisafi na salama katika Jiji la Dodoma, ambayo kwa kiasi kikubwa imetokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu lililosababishwa na Serikali kuhamia Dodoma.

Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua madhubuti inazochukua kuhakikisaha upatikanaji maji wa uhakika katika Jiji la Dodoma na kuridhishwa na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa. Miradi hii ikikamilika kwa wakati uliopangwa itachochea uzalishaji katika sekta mbalimbali na kuimarisha uchumi kwa ujumla. Hivyo, Kamati inasisitiza Wizara kuimarisha usimamizi wa utekelezaji na kukamalisha kadri ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha na mwenendo wa utengaji wa fedha za maendeleo. Pamoja na hatua na jitihada zilizofanywa na Serikali kuimarisha upatikanaji wa maji kwa wananchi, Kamati imebaini kuwa kumekuwepo na ufinyu wa bajeti inayotenga kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa Wizara ya Maji imepungua kwa kiasi cha shilingi 58,378,930,000 sawa na asilimia 8 kwa fedha za mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati imebaini pia kwamba fedha za nje zilizoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 zimepupngua kwa shilingi 59,559,930,000 sawa na asilimia 16. Kufuatia kupungua kwa fedha za nje, Kamati ilitaka kufahamu ni kwa jinsi gani Serikali imejipanga kutekeleza mipango ya maendeleo kwa kuzingatia upungufu wa fedha na hasa za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha na kusimamia Mpango Mkakati wa kuhakikisha uvunaji wa maji ya mvua unakuwa endelevu kwa matumizi ya akiba hasa wakati wa kiangazi. Nchi yetu, imebarikiwa kuwa na mvua nyingi za misimu mbalimbali katika maeneo tofauti kwa mwaka. Hata hivyo, pamoja na kuwa na mvua nyingi, maji mengi yanapotea kwa kutovunwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikizingatiwa kuwa changamoto ya upungufu wa maji nchini kubwa kwenye maeneo mengi ni wazi kuwa tunahitaji kuwa na mipango shirikishi kwa kuendelea kutunza vyanzo vya maji na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na huku tukijielekeza katika mipango ya ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua. Kamati inaishauri Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa taratibu zilizopo za uvunaji wa maji ya mvua katika majengo binafsi na ya umma zikiwepo taasisi za elimu na vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu wa kuvuna maji ya mvua umechangizwa na hotuba ya Mheshimwa Rais Samia Suluhu. Nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Taarifa hii aliitoa

wakati akilezea vipaumbele vya Serikali vya Awamu ya Sita tarehe 22 Aprili, 2021 alipokuwa akiongea na Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu ambapo alisisitiza Wizara kuandaa mipango na mikakati ya ujenzi ya mabwawa ya kuvuna maji ya mvua itakavyotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuongeza upatikanaji wa huduma za uondoaji maji taka kufikia asilimia 30 ifikapo mwaka 2025 kwa kujenga na kupanua mifumo ya uondoaji wa maji taka na mabwawa ya kutibu na kusafisha maji taka. Pamoja na mipango hiyo hii mizuri hakuna fedha za ndani zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji taka. Aidha, uchambuzi uliofanywa Kamati umebaini kwamba kiasi cha fedha za ujenzi wa miundombinu ya maji taka zinazotengwa ni fedha za nje na hujumuishwa katika miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji safi kama inavyotekelezwa katika mikoa ya Miji ya Dar e Salaam, Arusha, Dodoma, Kagera na Mara. Kufuatia hali hii, Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza mipango iliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza kasi ya kutekelekeza mipango na mikakati ya kuimarisha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma kutoka Ziwa Victoria. Kamati imeridhishwa na mipango ya kukabiliana na changamoto ya upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma. Pamoja na mikakati iliyopo, ipo haja ya kutafuta vyanzo vya uhakika ili kuweza kukidhi mahitaji ya maji yanayoongezeka kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inatokana na ukweli kwamba Jiji la Dodoma ni kitovu cha Shughuli za Serikali na kusababisha mwingiliano mkubwa wa shughuli mbalimbali na watu na hivyo kuongeza mahitaji ya maji. Kufuatia upembuzi wa awali uliofanyika na kukamilika mwezi Desemba, 2019 ulionesha uwezekano mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria kufika Dodoma. Kamati inashauri Serikali kutekeleza mipango ya muda mrefu ya kuwezesha upatikanaji wa maji wa uhakika kutoka Ziwa Victoria hadi Dodoma, pia kuendelea na utafiti wa kutafuta vyanzo vingine vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha usambazaji na upatikanaji maji vijijini, hususan katika maeneo ya wafugaji ambapo miradi ya mabomba makubwa ya maji inapita; Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuwafikishia wananchi waishio vijijini maji; na kwamba hii inachagizwa kwa sehemu kubwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba wananchi wote waishio pembezoni mwa mabomba ya miradi mikubwa wanapata huduma ya maji safi kwa kuwa wanufaika wa miradi hiyo na kuwa sehemu ya kulinda na kuhifadhi miundombinu ya miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, pamoja na nia njema na hatua zilizokwisha chukuliwa, kuanzisha na kutekeleza utaratibu mahususi wa kuwezesha upatikanaji maji kwa ajili ya wananchi na mifugo, kwa upande wa mifugo, kuongeza matawi ya kunyweshea mifugo (birika) sambamba na kuweka bei ndogo ya maji kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini, kwa kuboresha upatikanaji wa maji kwa gharama nafuu kwa ajili ya mifugo, kutasaidia pamoja na mambo mengine kuimarisha uchumi wa wafugaji pamoja na jamii za wafugaji kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa miundombinu ya maji na hivyo kuifanya miradi ya maji kuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha na kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maji; Mfuko wa Taifa wa Maji unatekeleza majukumu yake kwa kusimamiwa na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019. Kwa mujibu wa sheria hiyo, majukumu ya mfuko ni pamoja na kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya usambazaji wa maji na utunzaji wa vyanzo vya maji; kuzipatia fedha mamlaka za utekelezaji wa miradi ya maji; na kufuatilia matumizi ya fedha zinazopelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo sasa, chanzo cha fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji kimebakia kuwa kile kile, takribani shilingi 175,912,837,000/=. Hali ikiwa kwamba mahitaji ya fedha ya miradi ya maji vijijini yakiongezeka kila

siku kutokana na ongezeko la idadi ya watu na matumizi mengine ya maji. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa kiasi kinachotengwa ni kidogo na hakikidhi mahitaji halisi kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa Mfuko wa Taifa wa Maji katika kufikisha maji kwa wananchi, Kamati inaishauri Serikali kutafuta vyanzo vipya ili kuweza kutunisha Mfuko wa Maji. Kufanya hivyo kutahakikisha upatikanaji wa fedha za kutosha kukidhi miradi mbali mbali ya maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarisha Chuo cha Maji ili kiweze kuzalisha wataalam wa sekta ya maji nchini; Kamati inatambua jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali katika kutekeleza miradi na kutimiza azma ya kuwapatia wananchi maji safi na salama. Ili miradi hii iwe endelevu itahitaji matengenezo na wataalam mahususi wa kuisimamia na kuifanyia matengenezo ya mara kwa mara. Wataalam hawa hupatikana kupitia Chuo cha Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huu, ipo haja kwa Serikali kufanya uwekezaji wa kutosha kwa kukipatia Chuo cha Maji rasilimali fedha kwa ajili ya kuendesha mafunzo kwa wataalam ambao watakuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha usimamizi wa miradi iliyotekelezwa.

Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara kuongeza kasi ya kuwajengea uwezo wataalam waliopo na kuwahamasisha kujiendeleza kwenye fani za taaluma za maji. Vilevile, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi, itoe vibali vya kuajiri ili kufidia upungufu wa wataalam katika sekta ya maji, takribani watumishi 1,547.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi na Mheshimiwa Spika kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkituongoza kwa kipindi chote cha Mkutano wa Bunge la Bajeti na kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Kutokana na kazi kubwa walioifanya, natamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama walivyoorodheshwa katika taarifa, ukurasa wa 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso; na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi; Katibu Mkuu, Mhandisi Anthony Sanga; Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Nadhifa Kemikimba pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; na Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Fedha, Ndugu Michael Chikokoto, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndugu Virgil Mtui na Ndugu Rachel Nyega wakisaidiwa na Ndugu Waziri Kizingiti kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

### Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, kimeipa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwa madhumuni ya taarifa hii, taarifa ninayoiwasilisha inahusu Wizara ya Maji Fungu 49.

### Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:

(a) Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji - fungu 49, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

(b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

(c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na

(e) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** maoni na ushauri utakaotolewa ni matokeo ya uchambuzi wa nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati, majadiliano kati ya Kamati na wadau mbalimbali na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

## SEHEMU YA PILI

## UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inabainisha masuala muhimu yaliyojitokeza katika uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa kuzingatia masuala yaliyoorodheshwa katika Kipengele 1.2 cha Sehemu ya Kwanza.

### Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo manne (4) ya kipaumbele yafuatayo: -

(a) Kuimarisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, kwa kuuwezesha kuwa na wataalamu wa kutosha na vitendea kazi;

(b) Kuimarisha utengaji wa fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo;

(c) Kuongeza kasi ya ulipaji wakandarasi ili kukamilisha miradi ya maji iliyosimama kutokana na ukosefu wa fedha;

(d) Kuzingatia makubaliano na taratibu zilizopo katika utoaji misamaha ya kodi katika kutekeleza miradi ya maji, ili

kuhakikisha upatikanaji wa misamaha ya kodi kwa wakati kadiri inavyopaswa.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umetekelezwa. Aidha, baadhi ya ushauri upo katika mwendelezo wa utekekelzaji katika Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2020/2021. Kamati inasisitiza kuongeza kasi ya utekelezaji ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo ya kutekeleza ushauri wa Kamati kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi.

**Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yalijielekeza katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika na eneo la ukusanyaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Machi, 2021.

**Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Fungu 49, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **733,284,075,000**. Kati ya fedha hizo shilingi **28,275,145,000** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **705,008,930,000** zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **349,449,000,000.00** sawa na **asilimia 49.57** ni Fedha za Ndani ambapo kati ya fedha hizo, shilingi **175,912,837,000.00** ni za Mfuko wa Taifa wa Maji na shilingi **173,536,163,000.00** ni fedha zinazotokana na vyanzo vingine vya ndani. Aidha, shilingi **355,559,930,000.00** sawa na **asilimia 50.43** ni Fedha za Nje.

**Mwenendo wa utolewaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi mwezi Aprili 2021, Wizara ilikua imepokea jumla ya **Shilingi 396,771,027,717.02** sawa na

**asilimia 54.10** ya bajeti ya Maendeleo na Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi 20,349,425,596.52** sawa na **asilimia 71.96** ni bajeti ya fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi **376,421,602,120.50** sawa na **asilimia 53.39** ni bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi **192,167,225,844.98** ni fedha za nje, sawa na asilimia **54.04** na fedha za ndani ni shilingi **184,254,376,275.52** sawa na **asilimia 45.96.** Aidha kiasi kilichotokana na Mfuko wa Maji ni shilingi **131,742,995,737.13** sawa na asilimia **74.89** na shilingi **52,511,380,538.39** ni za Mfuko wa Serikali, sawa na asilimia **30.25.**

**Maoni kuhusu Mwenendo wa Utolewaji Fedha za miradi ya maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Maji Fungu 49 zilizotolewa ni **asilimia 53.4**. Kati ya kiasi kilichotolewa, fedha za nje ni asilimia **54.04** na fedha za ndani ni **asilimia 45.96.** Aidha kwa fedha za ndani, Fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji zilizotolewa ni asilimia **74.89** na fedha kutoka vyanzo vingine vya Serikali zilizotolewa ni **asilimia 30.25.** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuimarisha mtiririko wa utoaji fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji. Hata hivyo Kamati haijaridhishwa na kiasi kinachotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Maji, hasa ikizingatiwa ndio chanzo mahsusi na cha uhakika cha ndani kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo Serikali imeendelea kutenga takriban kiasi kilekile cha shilingi **175,912,837,000.00** kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Maji. Na kwamba upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Mfuko huu unategemea mauzo ya mafuta ya petroli na dieseli, ambayo mauzo hayo yanategemea kuimarika kwa uchumi na uzalishaji katika matumizi ya nishati ya mafuta. Na kwamba kwa miaka mitatu mfulilizo mtiririko wa utoaji fedha za Mfuko wa Maji umekua ukiimarika. Kwa Mwaka huu, 2020/2021 hadi Mwezi April, 2021 **asilimia 74.89** tayari kimetolewa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuimarisha mtiririko wa fedha za

Mfuko wa Taifa wa Maji kwani inaonyesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kufikisha huduma ya majisafi kwa wananchi wa vijijini kwa **asilimia 85**. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutoa kiasi cha fedha za maendeleo zilizobaki kabla ya bajeti hii kumalizika Mwezi Juni 2021.

## Ukusanyaji wa maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Maji ilipanga kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi **8,187,410,210.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Machi, 2021, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **8,283,735,610.43** sawa na **asilimia 101** ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo na kuvuka lengo la ukusanyaji kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha mwezi Juni. Aidha, katika Bajeti ya Mwaka 2019/2020 Wizara iliweza kukusanya maduhuli kwa **asilimia 103.** Tafsri ya hii ni kwamba, Wizara ina wigo mpana wa kuweza kukusanya mapato mengi zaidi. Kwa muktadha huu, Kamati imeridhishwa na Mpango wa Wizara wa kuongeza wigo wa makusanyo ya maduhuli maradufu kwa Bajeti ya 2021/2022 ili kuongeza mapato ya Serikali.

## Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha (2020/2021). Ili kutekeleza masharti ya kanuni hiyo, Kamati ilipanga kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maji katika Mkoa wa Morogoro, Pwani, Dar es salaam na Dodoma. Hata hivyo, ziara hiyo haikuweza kufanyika kwa ukamilifu kutokana na ziara kusitishwa, kufuatia msiba uliolikumba Taifa, wa Mhe. Hayati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya tano, Dk. John Pombe Magufuli.

Hivyo Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya kuboresha huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Morogoro. Miradi iliyokaguliwa ni kama ifuatavyo: -

i) Miradi ya matokeo ya haraka

Mradi huu unatekelezwa ili kuongeza maji eneo la Viwandani, Kihonda na SGR- Morogoro. Thamani ya mradi ni **shilingin billion 2.8** na umepangwa kukamilika katika Mwaka wa fedha 2020/2021 na utahudumia wananchi takriban 120,000.

ii) Mradi wa muda wa kati (AFD No.C TZ 105901 W)

Mradi huu unatekelezwa kwa muda wa miaka mitano kuanzia 2020/2021. Thamani ya mradi huu ni shilingi billion 185 na utahudumia wanachi takriban 722,000. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza uzalishaji maji kwa lita million 54 kwa siku na kufanya jumla ya uzalishaji maji kufikia lita million 89 (sawa na asilimia 108 ya mahitaji ya maji kwa Manispaa ya Morogoro ifikapo 2025)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga fedha na kuanza utekelezaji wa miradi hii yenye lengo la kuongeza upatikanaji maji kwa wakazi wa Manispaa ya Morogoro. Aidha Kamati inasisitiza Wizara kuongeza uratibu na usimamizi wa utekelezaji miradi hii ili iweze kukamilika kwa muda uliopangwa kuwezesha kufikia malengo ya kuwapatia wananchi maji safi na salama. Kamati pia ina maoni kuwa ili miradi hii iweze kuwa na manufaa endelevu, Serikali ichukue hatua za makusudi kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazotajwa kuathiri utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji, zikiwemo kukabiliana na uvamizi wa vyanzo vya maji (mito na vijito) katika milima inayozunguka Morogoro, kukabiliana na uchafuzi wa Bwawa la Mindu (chanzo kikuu cha maji kwa manispaa ya Morogoro kikizalisha asilimia 75 ya maji yanayotumika sasa).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kutofanyika kwa ziara hiyo kikamilifu, Kamati ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo Wizara imeendelea kuisimamia ikiwa ni pamoja na;

a) Miradi 355 ya maji vijijini iliyomalizika mwaka 2020;
b) Miradi 67 ya maji mijini iliyomalizika mwaka 2020;

c) Miradi 85 ya maji vijijini, iliyokua imekwama kwa muda mrefu, ambayo imekarabatiwa na kuweza kutoa huduma, pamoja na

d) Miradi ya maji vijijini itakayotekelezwa katika mwaka 2021/ 2022.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kupitia utekelezaji uliofanywa umeweza kuwa na matokeo chanya kwa kuongezeka kiwango cha upatikanaji wa huduma za maji nchini kutoka: -

**i. Asilimia 70.1 vijijini** na **asilimia 84** mijini mwaka **2019/2020** hadi kufikia **asilimia 72.3 vijijini** na **asilimia 86 mijini**; Mwaka 2020/2021

ii. Kukamilika na kuzinduliwa kwa miradi mikubwa ya maji kutoka ziwa Viktoria kwenda Tabora, Igunga Nzega pamoja na Isaka – Kagongwa;

iii. Kukamilika kwa jumla ya miradi 422 ya maji ambapo ya vijijini ni 355 na mijini ni miradi 67;

iv. Kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji na kupungua kwa gharama za ujenzi kutokana na kutumia utaratibu wa *force account* na

v. Miradi 85 iliyokuwa na changamoto kutafutiwa ufumbuzi na hivyo kuanza kutoa huduma za maji kwa wananchi wa maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Kamati imeridhishwa na jitihada na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kutekeleza miradi ya maji sehemu mbalimbali nchini. Hata hivyo, Kamati inatoa rai kwa Wizara kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa miradi kwa kuwachukulia hatua za kinidhamu Watumishi na hatua za kisheria Wakandarasi watakaoshindwa kutimiza majukumu na matakwa ya mikataba iliyopo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini Serikali ikiimarisha utoaji wa fedha zilidhoidhinishwa na Bunge kwa wakati, miradi ya maji itakamilika kwa wakati na hivyo kuwezesha lengo lililowekwa na Serikali kufikiwa.

**Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

a) **Upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji, ikiwemo ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda, Farkwa na Ndembera/Lugoda**.

Miradi hii imechelewa kuanza utekelezaji wake kutokana na kuhitaji fedha nyingi kwa wakati mmoja ambapo upatikanaji wa fedha hizo umekuwa si kwa kasi iliyokusudiwa. Hali hiyo imesababisha miradi hii kuendelea kuwekwa kwenye mipango ya utekelezaji ya kila mwaka wa fedha. Katika kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutafuta fedha za kuwezesha kutekeleza miradi ya maji kutokana na umuhimu wake.

b) **Utendaji usioridhisha wa wakandarasi.**

Baadhi ya Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji wamekuwa hawatekelezi majukumu yao kwa kadri ya matakwa ya mikataba. Hali hii imesababisha miradi mingi kusuasua, hivyo kutokukamilika kwa wakati uliopangwa. Miradi hiyo ni kama vile, Mradi wa Same Mwanga-Korogwe, Maji safi na Usafi wa mazingira Musoma, Majisafi na usafi wa mazingira Kigoma, Majisafi na usafi wa mazingira Lindi na mradi wa majisafi Chalinze Awamu ya tatu.

Kamati, inaendelea kuishauri Wizara kuimarisha usimamizi wa wakandarasi, ili kutekelezwa matakwa ya mikataba kadiri ya makubaliano. Aidha, katika kuongeza kasi ya kukamilisha

utekelezaji miradi, kuendeleza utaratibu wa *Force Account* katika utekelezaji wa miradi ili kukwamua miradi iliyosalia. Vilevile, Serikali ifanye uhakiki na upekuzi wa kina (*due diligence*) wa wakandarasi na wataalm washauri ili kujiridhisha kuhusu uwezo wao wa kitaalam na kifedha na hivyo kupata watoa huduma wenye uwezo unaohitajika.

c) **Upungufu wa Wataalam katika Utekelezaji, Usimamizi na Uendeshaji wa miradi kwenye Sekta ya maji**.

Wizara na Taasisi zake ina nakisi ya **Watumishi 1,547** ili kuweza kukidhi mahitaji. Kamati inaisisitiza Wizara kuongeza kasi ya kuwajengea uwezo wataalam waliopo na kuwahamasisha kujiendeleza kwenye fani zao za kitaaluma ili kuwa na sifa kamili. Vilevile, Wizara iainishe na kuomba vibali vya ajira Ofisi ya Rais- UTUMISHI ili kuajiri wataalam wa kutosha na wenye sifa katika sekta ya maji.

d) **Mwamko mdogo wa Wananchi kuchangia Huduma ya Maji.**

Sera ya Maji ya mwaka 2002 imeeleza umuhimu wa jamii kuchangia gharama ya uendeshaji na matengezo ya miradi ya maji vijijini. Hata hivyo, kumeendelea kuwepo kwa mtazamo tofauti ambapo baadhi ya wananchi wanaona si haki kulipia maji kwa kuwa ni rasilimali ya asili. Katika kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Wizara kuongeza kasi ya kuwajengea uelewa wananchi na kuwahamasisha kushiriki kikamilifu katika uendeshaji na matengezo ya miradi ya maji vijijini. Aidha, katika kuimarisha ushiriki wa wananchi katika miradi ya maji, vyombo vya watumia maji (CBWSOs) viimarishwe kwa kuajiri Watumishi wenye taaluma stahiki ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo ili kusimamia kikamilifu utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini.

## MPANGO WA BAJETI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - FUNGU 49

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2021/ 2022 umeandaliwa kwa kuzingatia programu na miradi

mbalimbali ya maji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 yenye kulenga kuinua hali ya maisha ya wananchi na kulifanya Taifa kuimarika katika uchumi wa kipato cha kati. Dira hii inatekelezwa kupitia nyenzo mbalimbali, zikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020- 2025.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, Tanzania inashiriki kikamilifu katika kutekeleza malengo ya kimataifa, ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu *(Sustainable Development Goals - SDGs 2016 - 2030)*. Hususan lengo Namba Sita (6) kati ya malengo 17 ya Malengo Endelevu ya Maendeleo ambalo linazitaka nchi wananchama wa umoja wa Mataifa kuhakikisha kila Serikali inawapatia wananchi wake wote majisafi na usafi wa mazingira.

**Mjeshimiwa Spika,** kati ya malengo hayo, Sekta ya maji ni moja ya sekta za kipaumbele kutokana na umuhimu mkubwa wa huduma ya maji kwa ajili ya maisha ya binadamu, wanyama, mimea na mazingira. Aidha, maji ni injini ya shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi na ni nyenzo muhimu katika kutokomeza umaskini na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza jukumu la Bunge la kuishauri na kuisimamia Serikali kwa niaba ya Wananchi, tarehe 29 Machi, 2021 Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Maji na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mpango ambao umezingatia pamoja na mambo mengine Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Malengo ya Bajeti na Kazi Zilizopangwa Kutekelezwa**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/ 2022, kazi zitakazofanyika zimejikita katika maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo: -

a) Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

i) Kuendelea kutambua, kutunza, kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini;

ii) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za majishirikishi na kuimarisha Taasisi zinazosimamia rasilimali za maji nchini;

iii) Kuimarisha mfumo wa uvunaji maji ya mvua na kuanza utekelezaji wa ujenzi wa bwawa moja kwa kila Wilaya yenye mazingira yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa; na

iv) Kujenga mabwawa ya kimkakati na ya ukubwa wa kati ambayo ni Farkwa (Dodoma), Kidunda (Morogoro Vijijini), Ndembera (Iringa), Itobo (Nzega) na Enguiki (Monduli).

b) Usimamizi wa ubora wa maji

i) Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa ubora wa maji;

ii) Kufuatilia na kutathmini ubora wa maji katika vyanzo vya maji vya kimkakati 50;

iii) Utekelezaji wa mkakati wa kuondoa madini ya floridi kwenye maji; na

iv) Kuwezesha uandaaji wa Mipango ya Usalama wa maji katika Mamlaka za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira pamoja na vyombo vya watumiaji maji.

c) Usambazaji wa Majisafi Vijijini

i) Kukamilisha miradi inayoendelea na kuanza miradi mipya ya maji vijijini;

ii) Kuimarisha vyombo vya watumia maji (CBWSOs); na

iii) Kuendelea na ujenzi wa miradi katika maeneo yanayopitiwa na mabomba makubwa ya maji.

d) Usambazaji wa Majisafi na usafi wa Mazingira Mjini

i) Kuboresha huduma ya maji kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji katika Miji mikuu ya Mikoa, Miji mikuu ya Wilaya, Miji midogo na miradi ya kitaifa;

ii) Kuendelea na Utekelezaji wa miradi ya kutoa maji Ziwa Victoria;

iii) Kuanza utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na majitaka katika Jiji la Dodoma na Ikulu ya Chamwino; na

iv) Kuanza utekelezaji wa Mradi wa Maji katika Miji 28.

e) Kuimarisha Uwezo wa Kitaasisi

i) Kuendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002;

ii) Kuendelea kuajiri watumishi wenye sifa na kuwaendeleza kitaaluma;

iii) Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kujenga ofisi na ununuzi wa vitendea kazi; na

iv) Kuendelea kukiimarisha Chuo cha Maji ili kiweze kuzalisha wataalam wa sekta ya maji nchini.

## Fedha zinazoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza kazi zilizopangwa, Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Maji (Fungu 49) imetengewa jumla ya **Shilingi 33,758,976,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,972,209,000** sawa na **asilimia 47** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC), na **Shilingi 17,786,767,000** sawa na **asilimia 53** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya Watumishi.

**Fedha zinazoombwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Maji kupitia Fungu 49 inaomba kuidhinidhiwa **shilingi 646,630,000,000.00**. Kati ya fedha hizo, jumla ya **Shilingi 346,630,000,000** sawa na **asilimia 53.675** ni fedha za ndani na **Shilingi 300,000,000,000** sawa na **asilimia 46.4** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha hizo za maendeleo zinazoombwa ni za kugharamia miradi ya kipaumbele ambayo ni pamoja na:-

- Mradi wa Maji Masasi na Nachingwea;

- Mradi wa Maji katika Mji wa Same na Mwanga;

- Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Igunga, Nzega na Tabora;

- Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga;

- Mradi wa Maji wa Visima vya Mpera na Kimbiji na

- Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Farkwa (Dodoma), Lugoda/ Ndembera (Iringa), Songwe (Songwe) na Bwawa la Kidunda (Morogoro);

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Mpango wa Bajeti umezingatia miradi ya maji Vijijini na mijini, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji ujenzi na ukarabati wa mabwawa katika Wilaya mbalimbali, uboreshaji wa huduma za ubora wa maji ikiwemo kujenga uwezo wa maabara za maji, pamoja na miradi na kazi za kujenga uwezo wa Taasisi na Watumishi.

**Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Maji (Fungu 49) inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 15,000,000,000** kutokana na vyanzo vya mauzo ya nyaraka za zabuni, leseni kwa makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji, tozo mbalimbali kwa wateja wanaopata huduma ya maabara za ubora wa maji na vibali vya matumizi ya maji katika mabonde. Kati ya fedha hizo **Shilingi 750,000,000** ni ada za huduma za maabara za maji, **Shilingi 1,000** ni mauzo ya nyaraka za zabuni, **Shilingi 14,249,999,000** zinatokana na leseni kwa makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima vya maji na vibali vya matumizi ya maji katika mabonde.

**Tathimini ya Kamati kuhusu Malengo ya Bajeti na Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Maji - Fungu 49.**

**Malengo ya Bajeti**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia, imechambua na kutathimini malengo na vipaumbele viliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022. Kamati imeridhika kwamba, Malengo haya ni ya msingi kwani yanalenga kuongeza upatikanaji wa maji nchini kwenye maeneo yaliyokuwa yanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, haijaridhishwa na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mabwawa ya kimkakati. Kwa mfano; katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kiasi cha **shilingi 1,000,000,000:00** kimetengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Aidha, kwa upande wa Bwawa la Farkwa, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kiasi kilichotengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa bwawa la Farkwa ni shilingi **1,786,450,000:00.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa ujenzi wa mabwawa haya ya kimkakati unahitaji fedha nyingi, kiasi kilichotengwa hakikidhi kuendeleza utekelezaji wa miradi hii. Wasiwasi wa Kamati kutoridhishwa kunatokana na ukweli kwamba mipango ya utekelezaji wa miradi hii ni ya muda mrefu, mfano, mradi wa bwawa la Kidunda uliasisiwa miaka takribani 40 iliyopita na wananchi wanaozunguka eleo la bwawa wameshalipwa fidia. Hivyo kusuasua kwa utekelezaji wa mradi huu kunaweza kupelekea wananchi waliolipwa fidia kurejea katika eneo la mradi na hivyo kusababisha migogoro kati ya Serikali na Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kutoridhishwa na kiasi cha bajeti iliyotengwa kutekeleza miradi ya ujenzi wa mabwawa ya kimkakati, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua za makusudi ilizochukua ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya muda mrefu ambayo imekua ikilalamikiwa na Wabunge na Wananchi wa maeneo hayo. Miradi hiyo ni pamoja na Kuboresha Huduma ya Maji Katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ya Orkesumet, Mji wa Bunda, Mradi wa Maji Kyaka Bunazi, Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe. Hatua hizi zinaonesha nia njema ya Serikali ya kuwaondolea wanachi adha ya upatikanaji wa maji safi na kuboresha maisha kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** katika mipango ya kuboresha Upatikanaji wa Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, kipekee Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua miradi ya kuimarisha upatikanaji maji katika Jiji la Dodoma. Malengo hasa ya kutembelea miradi hii katika Jiji la Dodoma ni kutokana kuwepo changamoto ya upungufu wa majisafi na salama katika Jiji la Dodoma, ambayo kwa kiasi kikubwa imetokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu lililosababishwa na Serikali kuhamia Dodoma. Takwimu zinaonesha kwamba, kwa sasa mahitaji ya maji Jijini Dodoma ni lita za ujazo **103,600** kwa siku. Hivi sasa DUWASA inazalisha, kusafirisha na kusambaza wastani wa lita za ujazo **57,000,000** kwa siku. Hivyo kupelekea Jiji la Dodoma kuwa na upungufu wa maji wa lita **37,000,000** kwa siku.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia ziara hiyo, Kamati ilikagua utekelezaji wa miradi ya kuongeza upatikanaji wa Maji katika Jiji la Dododma ifuatayo: -

(a) Mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma unahusisha: -

i) Mradi wa kutoa maji katika visima vya Ihumwa kwenda tanki la Njedengwa, kwa gharama ya shilingi bilioni 2.4. Ujenzi wa mradi unahusisha ulazaji wa bomba kuu, ufungaji wa pampu; na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji na unatarajia kukamilika mwezi Mei, 2021.

ii) Mradi wa Ujenzi wa Tanki katika eneo la Chamwino, lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 2.5, mradi unaendelea na unatarajia kukamilika mwezi Mei, 2021.

iii) Mradi wa kuchimba visima 8 vipya na kukarabati visima vya zamani 7 katika maeneo mbalimbali yaliyopo pembezoni mwa Jiji la Dodoma, mradi huu unaendelea na unatarajia kukamilika mwezi Juni 2021.

(b) Pamoja na mipango ya muda mfupi ya kukabiliana na upungufu wa maji katika Jiji la Dodoma, Kamati ilielezwa Mpango wa muda mrefu ya kupata sulihisho la kudumu na kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Dodoma kwa. Kamati ilfahamishwa kwamba, Serikali imepanga kuanza kutekeleza Mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria ambapo utekelezaji wa mradi huu utanufaisha maeneo litakapopita bomba kuu ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Singida na vijiji vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu ndani ya umbali wa kilomita 12. Kwa sasa kazi iliyokwisha kufanyika ni pamoja na kuandaa andiko la awali la upembuzi yakinifu na kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua madhubuti inazochukua kuhakikisaha upatikanaji maji wa uhakika katika Jiji la Dodoma na kuridhishwa na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa. Kamati inaamini kwamba, pamoja na

kuimarisha afya za wakazi, miradi hii ikikamilika kwa wakati uliopangwa itachochea uzalishaji katika sekta mbalimbali na kuimarisha uchumi kwa ujumla. Hivyo Kamati inasisitiza Wizara kuimarisha usimamizi wa utekelezaji na kukamilishwa kadiri ilivyopangwa.

**Maombi ya fedha na mwenendo wa utengaji wa fedha za maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua na tijihada zinazofanywa na Serikali kuimarisha upatikanaji wa maji kwa wananchi, Kamati imebaini kuwa kumekuwepo na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Bajeti ya Maendeleo iliyotengwa kwa Wizara ya Maji, imepungua kwa **kiasi cha Shilingi 58,378,930,000** sawa na **asilimia 8** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati imebaini pia kwamba, Fedha za nje zilizoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendelo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ndio zimeathirika zaidi ambapo zimepungua kwa **Shilingi 55,559,930,000. 00** sawa na **asilimia 16%.** Kufuatia kupungua kwa fedha za nje, Kamati ilitaka kufahamu kwa jinsi gani Serikali imejipanga kutekeleza mipango ya maendeleo kwa kuzingatia upungufu wa fedha za nje ulioainishwa hapo juu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kupungua kwa fedha za Nje za kutekeleza miradi ya maendeleo, zipo fedha kiasi cha dola za Marekani milioni 500 ambazo ni mkopo kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim wenye lengo la kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28 ya Tanzania Bara na mji mmoja visiwani Zanzibar. Kamati inaishauri Serikali kuanza kutumia fedha hizi mapema iwezekanavyo kwani ni muda mrefu sasa Kamati imekuwa ikifahamishwa kwamba, "taratibu za ununuzi kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi zinaendelea na wanatarajiwa kupatikana mwezi Mei 2021". Ni vyema Serikali ikafahamu kuwa Kamati haijaridhishwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi huu.

## SEHEMU YA TATU

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

**Kuanzisha na kusimamia Mpango Mkakati wa kuhakikisha uvunaji wa maji ya mvua unakuwa endelevu kwa matumizi ya akiba hasa wakati wa kiangazi.**

**Mheshimiwa Spika,** Nchi yetu, imebarikiwa kuwa na mvua nyingi za misimu mbalimbali katika maeneo tofauti kwa mwaka. Hata hivyo, pamoja na kuwa na mvua nyingi, maji mengi yanapotea kwa kutovunwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya baadae.

**Mheshimiwa Spika**, mbali na jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali kwa kujenga visima vipya vya maji na kukarabati visima vya zamani ili kusaidia kupunguza tatizo la maji nchini, tatizo la maji bado ni kubwa kwenye maeneo mengi nchini. Ili kukabiliana na changamoto hii, ni wazi kuwa tunahitaji kuwa na mipango shirikishi kwa kuendelea kutunza vyanzo vya maji na kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na huku tukijielekeza katika mipango ya ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua. Vile vile, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa tatatibu zilizopo za uvunaji wa maji ya mvua katika majengo ya umma, zikiwepo taasisi za elimu na vituo vya afya.

**Mheshimiwa Spika,** ushauri huu wa kuvuna maji ya mvua umechagizwa na Hotuba ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa wakati akielezea vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita tarehe 22 Apr,2021 alipokuwa akiongea na Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu**.** Kufuatia hotuba hiyo ya Rais, Kamati inaitaka Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kuandaa mpango na mikakati ya namna ya ujenzi wa mabawa ya kuvuna maji ya mvua utakavyotekelezwa.

Mipango hiyo ni lazima iendane na utengaji wa fedha za bajeti kwa ajili ya kutekeleza kazi zitakazopangwa.

**3.2. Kutekeleza mipango ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika miji na makao makuu ya Mikoa.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imepanga kuongeza upatikanaji wa huduma ya uondoaji maji taka kufikia **asilimia 30** ifikapo 2025, kwa kujenga na kupanua mifumo ya uondoaji wa majitaka na mabwawa ya kutibu na kusafisha majitaka pamoja na kununua magari maalum ya uondoaji wa majitaka.

**Mheshimiwa Spika,** mpango huu unalenga kutekelezwa katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo, Utekelezaji wake umekuwa sio wa kuridhisha, kwani mpaka sasa wastani wa upatikanaji wa huduma hiyo ni **asilimia 15 tu**. Hali hii imetokana na ukweli kwamba, hakuna fedha za ndani zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka. Aidha, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kiasi cha fedha za ujenzi wa miundombinu ya maji taka zinazotengwa ni fedha za nje na hujumuishwa katika miradi ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi kama inavyotekelezwa katika Mikoa na Miji ya Dar es salaam, Arusha, Dodoma, Bukoba na Mara. Kufutia hali hii, Kamati inashauri Serikali ili kufikia adhima ya kuongeza huduma ya upatikanaji wa majitaka na kufikia **asilimia 30** ifikapo 2025 ni vyema Serikali ikaanza kutenga fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza mipango iliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,** kwenye miji mingine huduma ya uondoaji wa majitaka inatolewa kwa kutumia magari ya majitaka na kutiririshwa kwenye mabwawa au maeneo yaliyotengwa na Halmshauri husika. Utaratibu huu wa kuondoa majitaka kwa kutumia magari ya majitaka ni wa kizamani, umepitwa na wakati, inaigharimu Serikali fedha nyingi na inahatarisha afya za wananchi. Kamati ina taarifa kuwa ipo teknolojia mpya ambapo mtu anaweza kuchimba mashimo ya majitaka kwenye eneo la nyumba bila kulazimika kutumia magari ya majitaka kwa ajili ya kunyonya na kuyatiririsha kwenye

mabwawa yaliyotengwa. Ili kuendana na teknolojia hii mpya, Kamati inaishauri Wizara kufanya utafiti na kujiridhisha kama teknolojia hii inafaa na hivyo kutoa elimu kwa wananchi na hatimae kusimamia utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu Mamlaka za maji zimeendelea kutekeleza miradi ya miundombinu ya majitakana mara baada ya miundombinu ya barabara kuwa imeshajengwa na hivyo kuharibu barabara zilizojengwa kwa gharama kubwa wakati wa kupitisha mabomba ya majitaka. Kufuatia uharibIfu huu Kamati inazishauri Mamlaka za Maji Mijini na Mikoani kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za Serikali zinazohusika na ujenzi wa miundombinu na kupanga namna mifumo ya maji taka itakavyowekwa kabla ya ujenzi wa barabara kukamilika. Kamati inaamnini hatua hii itasaidia kuondoa gharama za kufanya matengenezo ya baraba zilizoharibika, lakini pia itapunguza foleni kwa watumiaji wa barabara kuruka mashimo yaliyosalia wakati wa ujenzi wa miundombinu ya maji taka na zaidi itaimarisha usalama wa watu na vyombo vya moto.

**Kuongeza kasi ya kutekelekeza Mipango na Mikakati ya kuimarisha upatikanaji maji katika Jiji la Dodoma kutoka Ziwa Victoria.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na Mipango ya muda mfupi ya kukabiliana na changamoto ya upungufu wa maji katika jiji la Dodoma. Pamoja na mikakati iliyopo, ipo haja ya kutafuta vyanzo vya uhakika ili kuweza kukidhi mahitaji ya maji yanayoongezeka kila siku. Hali hii inatokana na ukweli kwamba Jiji la Dodoma ni kitovu cha Shughuli za Serikali na kupelekea mwingiliano mkubwa wa shughuli na watu na hivyo kuongeza mahitaji ya maji. Kufuatia upembuzi wa awali (*Pre-Feasibility Study*) uliofanyika na kukamilika mwezi Desemba, 2019 ulionesha uwezekano mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria kufika Dodoma Kamati inashauri Serikali kutekeleza mipango ya muda mrefu ya kuwezesha upatikanaji wa maji wa uhakika kutoka ziwa Victoria hadi Dodoma.

**Kuimarisha Usambazaji na Upatikanaji maji Vijijini, hususan katika maeneo ya Wafugaji ambapo miradi ya mabomba makubwa ya maji inapita.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuwafikishia wanachi waishio vijijini maji. Na kwamba hii inachagizwa kwa sehemu kubwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba wananchi wote waishio pembezoni mwa mabomba ya miradi mikubwa wanapata huduma ya majisafi kwa kuwa wanufaika wa miradi hiyo na kuwa sehemu ya kulinda na kuhifadhi miundombinu ya miradi husika. Kamati inaishauri Serikali kuwa, pamoja na nia njema na hatua zilizokwisha chukuliwa, kuanzisha na kutekeleza utaratibu mahsusi wa kuwezesha upatikanaji maji kwa ajili ya mifugo, kwa kuongeza matawi ya kunyweshea mifugo (birika) sambamba na kuweka bei ndogo ya maji kwa ajili ya mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kwa kuboresha upatikanaji wa maji kwa gharama nafuu kwa ajili ya mifugo, kutasaidia pamoja na mambo mengine kuimarisha uchumi wa wafugaji pamoja na jamii za wafugaji kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa miundombinu ya maji na hivyo kuifanya miradi ya maji kuwa endelevu.

**Kuimarisha na Kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maji**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Maji umeanzishwa kwa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na.12 ya Mwaka 2009.Kwa sasa, Mfuko unatekeleza majukumu yake kwa kusimamiwa na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na.05 ya Mwaka 2019. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, majukumu ya Mfuko ni pamoja na kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya usambazaji maji na utunzaji wa vyanzo vya maji; kuzipatia fedha Mamlaka za Utekelezaji wa miradi ya maji; na kufuatilia matumizi ya fedha zinazopelekwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hali ilivyo sasa, chanzo cha fedha za Mfuko wa Taifa wa maji kimebakia kuwa kilekile, ili hali mahitaji ya fedha za miradi ya maji vijijini yakiongezeka kila

siku kutokana na ongezeko la idadi ya watu. Kwa mfano; Mfuko wa Taifa wa Maji kwa Bajeti za Miaka mitatu mfululizo 2019/2020 hadi 2021/2022 umekuwa ukitengewa kiasi cha Shilingi **175,912,837,000.00**. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa kiasi kinachotengwa ni kidogo na hakikidhi mahitaji halisi kwa sasa. Kwa kutambua umuhimu wa Mfuko wa Taifa wa maji katika kufikisha maji kwa wananchi, Kamati inaishauri Serikali kutafuta vyanzo vipya ili kuweza kutunisha Mfuko wa maji. Kwa kufanya hivyo kutahakikisha upatikanaji wa fedha za kutosha kukidhi miradi mbali mbali ya maji vijijini na kuifanya Serikali kufikia adhma yake ya kuwapatia wananchi maji safi na salama kufikia asilimia 85 Vijinini ifikapo Mwaka 2025, kama ilivyoainishwa kwenye mipango.

**Kuimarisha Chuo cha Maji ili kiweze kuzalisha wataalam wa sekta ya maji nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali katika kutekeleza miradi na kutimiza adhma ya kuwapatia wananchi majisafi na salama. Ili miradi hii iwe endekevu itahitaji matengenezo na wataalam mahsusi wa kuisimamia na kuifanyia matengenezo ya mara kwa mara. Wataalam hawa hupatikana kupitia Chuo cha Maji. Kwa muktadha huu, ipo haya kwa Serikali kufanya uwekezaji wa kutosha kwa kukipatia Chuo cha Maji rasilimali fedha, kwa ajili ya kuendesha mafunzo kwa wataalam ambao watakua nyenzo muhimu katika kuimarisha usimamizi wa miradi iliyokwisha tekelezwa. Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara kuongeza kasi ya kuwajengea uwezo wataalam waliopo na kuwahamasisha kujiendeleza kwenye fani za taaluma za maji. Vilevile, Serikali kupitia Ofisi ya Rais- UTUMISHI itoe vibali vya kuajiri ili kufidia upungufu wa wataalam katika sekta ya maji, takribani Watumishi **1,547**

## SEHEMU YA NNE

### HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika kwa jinsi

ambavyo mmekuwa mkituongoza kwa kipindi chote cha Mkutano wa Bunge la Bajeti na kuliwezesha Bunge letu kutimiza wajibu wake wa kuisimamia Serikali kwa niaba ya Wananchi kwa mujibu wa Katiba. Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa katika kipindi chote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Kutokana na kazi kubwa walioifanya natamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na utaratibu tuliojiwekea hapa Bungeni naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Prof Patrick Aloysi Ndakidemi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Charles John Mwijage, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mohamed Suleman Omari, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. January Yusuf Makamba, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb - Mjumbe
13. Mhe.Jackson Gideon Kiswaga, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Tumain Bryceson Magessa, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Yahya Ali Khamisi, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Christopher Olonyoike Ole Sendeka, Mb - Mjumbe

23. Mhe.Yustina Arcadius Rahhi, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb - Mjumbe
27. Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Mb - Mjumbe
28. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb - Mjumbe
29. Mhe.Khadija Hassan Aboud, Mb - Mjumbe
30. Mhe. Dkt.Ritta Enespher Kabati, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mhe. Jumma Aweso (Mb), Naibu Waziri Mhe. Mhandisi, Maryprisca Mahundi, (Mb), Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Nadhifa Kemikimba pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Kamati za Fedha Ndg. Michael Chikokoto kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega wakisaidiwa na Ndg. Waziri Kizingiti kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

DK. Christine G. Ishengoma, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**
6 MAY, 2020

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, wawasilishaji wetu wamemaliza, sasa tutaanza uchangiaji.

Tutaanza na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, atafuatiwa na Mheshimiwa David Mwakiposa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, ajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nami nianze kwanza kwa kumpongeza sana mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; pia kipekee kabisa, niendelee kumpongeza, hasa kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa Siku ya Wafanyakazi. Kwa hakika sisi ambao tumeajiri watu wawili, watatu, imetupa matumaini makubwa sana juu ya mwenendo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowaomba sana Waheshimiwa Mawaziri na watumishi wa Serikali, wafanye kazi nzuri na iliyotukuka ili ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu tunayempenda sana ya kuwawekea mafao mazuri watumishi wetu itakapofika tarehe 10, mwezi wa Tano mwakani iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, niongeze pia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, ndugu yangu, Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa hakika Wanachalinze kwa kipekee kabisa tunaendelea kumshukuru na kumpongeza kwa sababu matokeo chanya au matokeo mazuri ya miradi ya maji kwa kuondoa kero za maji Chalinze yanaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hakika nataka nikupe taarifa kwamba leo tunaposimama hapa Halmashauri au Wilaya ya Chalinze imeendelea kukushukuru wewe na kukuombea Mungu kwa sababu maji yanatoka vizuri sana katika maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu leo inajikita katika kukumbusha, siyo kulalamika kama ilivyokuwa zamani, kwa sababu mambo mazuri yameendelea kufanyika katika

eneo letu lile. Mheshimiwa Waziri, katika eneo la Halmashauri ya Chalinze ipo miradi ambayo imeanza, lakini kwa maelezo au maoni yangu, naona bado kidogo *speed* haijaniridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, upo mradi wa mabwawa makubwa ya maji kwa ajili ya kunusuru hali ya upatikanaji wa maji katika Kata ya Kibindu. Mheshimiwa Waziri, ninachokiona ni kwamba mradi ule bado umeendelea kuwa unakwenda taratibu sana. Natambua kwamba watu wa *RUWASA* ambao wako chini yako wamefanya kazi ya *feasibility study* na hata maombi ya bajeti yalishaletwa kwako. Ninachomwomba Mheshimiwa Waziri, baada ya kukupitishia mafungu haya, basi jambo hili liwe moja katika vipaumbele vya kwanza kabisa kwenda kuvitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, pamoja na hilo, ipo miradi midogo mingine inayoendelea katika maeneo mbalimbali, ukiwemo mradi ambao juzi juzi Kamati inayoongozwa na ndugu yangu, Mheshimiwa Humphrey Polepole, ilikuja kuona Kata ya Ubena pale, mradi ambao uko katika Kijiji cha Tukamisasa na unaoenda katika maeneo ya Makao Makuu ya Kata ya Ubena, nao bado unaendelea kusuasua. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, uiangalie miradi midogo kama hii ambayo inakwenda kutatua kero za watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo natambua pia katika mafungu ya Mheshimiwa Waziri, yako mafungu kwa ajili ya kurekebisha malambo yetu ambayo yanaendelea kujaa michanga katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Chalinze. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri hili nalo liwe kipaumbele kwako ili wananchi wa Chalinze kama walivyo maeneo mengine, waendelee kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Waziri ameeleza juu ya msaada mzuri na muhimu sana unaotoka katika Serikali ya India ambao wametenga zaidi ya shilingi bilioni 13 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maji nchini. Hata hivyo namkumbusha Mheshimiwa Waziri, katika Awamu ya Pili ya Mradi wa Maji wa *CHALIWASA,* unaotoka Wami

kwenda Chalinze, iko *component* ya ujenzi wa matanki makubwa ya maji ambayo mpaka leo bado yameendelea kusimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipita katika maeneo kama ya Kibiki, Pera na Mazizi katika Kata ya Msata unaweza kushuhudia mwenyewe kwamba yako mahitaji makubwa ya ukamilishaji wa matanki haya. Haya ninayoyataja ni baadhi ya matanki kati ya matanki mengi ambayo yanatakiwa kujengwa katika Halmashauri ya Chalinze. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tunapokwenda kupitisha bajeti yake hii, hebu ujenzi wa matanki haya uishe mara moja kwa sababu haiwezekani kuwa kilio cha Wanachalinze kila siku ni kuwa na maji ya uhakika na wakati maji yao yanaweza kupatikana kwa ujenzi wa matanki haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo anaendelea kuangalia ustawi wa maji katika eneo la Tanzania yetu kwa kujua kabisa Tanzania inaendelea kufarijika naye mtoto wa Kitanzania anayeamua kupigania maisha ya watu kupitia eneo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, naomba nimsisitizie Mheshimiwa Waziri juu ya jambo ambalo tumekuwa tunalizungumza sana mara kwa mara. Serikali ilibuni Mradi wa Maji wa Bwawa la Kidunda, bwawa ambalo kwa namna moja au nyingine linaunganisha Mkoa wa Morogoro na Halmashauri ya Chalinze kwa maana ya Mkoa wa Pwani. Ujenzi wa bwawa hili ndiyo utatuzi wa maji katika eneo la Pwani, Dar es Salaam na mikoa ya jirani kama ambavyo mradi utakuwa umeelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, anajua mradi huu utakapokamilika mradi wetu wa maji wa Ruvu Chini na Ruvu Juu, hautakuwa na ukakasi wa kwamba ipo siku maji yatakauka, kwa sababu mradi huu wa maji utakapokamilika unatarajiwa kuchukua maji yasiyopungua lita milioni 200 kama sikosei. Ukamilishaji wake maana yake utasaidia, hata kama pakitokea kiangazi cha namna gani, maana yake maji yakikauka katika Ruvu yatakuwa yanafunguliwa na

kupelekwa Ruvu na wananchi wa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani wataendelea kufaidika na huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nmwomba sana Mheshimiwa Waziri, wanapokaa na kubuni miradi ya maji hasa kwa maeneo yenye watu wengi kama Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam, hili ni eneo muhimu sana, na pia ukiangalia Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa miradi midogo na mizuri ambayo anaendelea kuisimamia. Pia naomba, kwa wajomba zangu na shemeji zangu kule Same, ule mradi wao ni muhimu sana. Nimeona jinsi ambavyo ulivurugika kwa mara ya kwanza. Mimi sio *engineer* lakini ukiusoma mradi ule, unajua tokea kwenye *design* ya mradi ule kulikuwa na matatizo. Sasa naamini kabisa, katika kipindi cha miaka sita Mheshimiwa Waziri alichokaa katika Wizara hiyo, ameweza sasa siyo tu kuwa mwanasiasa, pia amekuwa *engineer* wa maji kwa maana ya kwamba sasa hata tukizungumza *gravitational force* kwa ajili ya kupitisha maji tunamaanisha kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia kila la heri ndugu yangu, Mheshimiwa Waziri, nawombea sana katika utekelezaji wa majukumu yake na mwisho nimtie moyo kabisa, asiwe na wasiwasi, ndugu zake tupo, tutaendelea kumwombea Mungu na kumsimamia kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Juliana Shinza ajiandae.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa ya kuzungumza katika sekta yetu hii muhimu sana ya maji. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wake pamoja na wataalam wengine, hususan wa pale kwetu

Mufindi na katika Mkoa wetu wa Iringa kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, kwa hotuba yake aliyoitoa alipokuja hapa Bungeni. Kwenye ukurasa wa 29 alizungumzia vizuri sana sekta ya maji. Moja ya changamoto alizozizungumza ni usimamizi thabiti kwa lengo la kufikia malengo yaliyowekwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza, lakini pili, napenda kushauri kwenye baadhi ya maeneo. Pale kwangu nikiri kabisa Mheshimiwa Waziri ameanza kwa *speed* kubwa na nzuri sana. Unaona miradi kichefu chefu ambayo ilikuwa kero kwa muda mrefu, inaanza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza mchango wangu kwenye eneo langu la Mufundi Kusini, Jimbo ambalo limejitolea kutunza vyanzo vya maji kwa kupanda miti mingi ili Watanzania kwa ujumla waendelee kunufaika na mvua na hatimaye maji tuendelee kuyapata kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na mradi wa Sawala. Nakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri, umekwenda pale; huu ni mradi wa muda mrefu sana na kuna miradi kama mitatu ambayo imeanzishwa kwa muda mrefu lakini bado haijakamilika japo *speed* yake kwa sasa inaridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina maombi mawili; moja, napenda kupata *commitment* yako Mheshimiwa Waziri, utusaidie ili ikamilike haraka iwezekanavyo, ikiwezekana mwaka huu hii miradi iishe. Pili, mradi huu ulikuwa katika vijiji vine; una Vijiji vya Lufuna, Sawala, Mtwango na Kibao. Katika Kata hiyo kuna Kijiji kinaitwa Mpanga na Kitilu, haufiki. Namwomba Mheshimiwa Waziri kupitia atusaidie mradi huu ufike maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunao Mradi wa Kimilinzowo, nao huu ni sehemu ya miradi kichefuchefu; kwa miaka mingi huko nyuma tangu ulipoanzishwa haukukamilika.

Nimeona kasi yako na wataalam, na nimemwona Meneja wa Maji wa Mkoa na Meneja wa *RUWASA* wa Wilaya wanavyohangaika. Mheshimiwa Waziri toa *timeframe,* mwaka huu mradi huu ukamilike tumalize kabisa hii kazi. Pia na vijiji Jirani kama Ihawaga vipate maji, Kinegembasi kipate maji, Nyigo napo unasuasua; tusaidie Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu, tuna mradi wa Nyororo. Bahati nzuri miradi hii yote Waziri wetu sio mgeni, amefika. Huu mradi wa Nyororo ni mradi ambao unagusa watu wengi kama miradi mingine nilivyoizungumzia, na uko barabarani pale. Changamoto ya mradi huu pia katika Kata yenye vijiji vinne unazungumzia kijiji kimoja. Moja, haujakamilika; naomba pia miradi hii mitatu hebu ikamilike basi. Hii *story* ya kuzungumziwa mradi umeanza, umeanza, iishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, tulizungumza hapa kwenye simu, akazungumza na Katibu Mkuu wake wa Wizara ya Maji, akazungumza na wataalam, wamekwenda *site,* Meneja wake wa Mkoa na Wilaya wamekwenda kwenye vijiji vingine ambavyo viko katika Kata hiyo; wamekwenda Njojo, wamekwenda Ving'ulo na Nyororo shuleni kufanya *design* ili iwe *extended* katika Kata nzima. Nakupongeza sana, lakini wakaenda mpaka na jirani ya Maduma na vijiji vyake vya Honga Maganga, Maduma na Ihanganatwa. Lengo ni kwamba Kata hizi mbili zinufaike na mradi huu. Naomba sana, hebu ukamilike basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia mradi maarufu kwenye Jimbo letu wa *IMAI*. Huu ni mradi unaogusa Kata tatu za Ihowanza, Malangali na Idunda. Ni mradi wa muda mrefu sana. Changamoto ni moja tu; miundombinu imechakaa. Nashukuru kuona kwamba katika mwaka huu wa fedha mmezungumza kwamba mtatutengea fedha kwa ajili ya kuufanyia marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, mradi huu, moja, angalau na wenyewe ukikamilika vijiji zaidi ya kumi

vitanufaika. Pili, kama mkianza kuufanyia matengenezo ya miundombinu iliyochakaa, naomba sana Mheshimiwa Waziri aende ukaguse mpaka Kata ya Mbala Maziwa ambako changamoto ya maji ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo ningependa kukugusia miradi mipya. Hapa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoiitikia kwenda kusaidia kuanzisha miradi mipya mitatu katika Jimbo letu la Mufindi Kusini Mungu akubariki sana. Wanamufindi Kusini wanamshukuru kwa jinsi alivyoanza *design* katika Kata ya Igowole mradi wa kupampu maji ambao utagusa Vijiji vya Ibatu, Nzivi, Igowole mpaka Kisasa. Nimwombe sana, kwanza ni hatua ya kwanza kumaliza jambo linguine, ikianza itimie ndani ya muda mfupi ili wananchi waweze kupata maji katika jimbo letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri, nimeona ameweka Mradi wa *Gravity* hapa wa Mgogoro ambao unakwenda mpaka Kata ya Kihohela. Nimshukuru sana kwa sababu eneo hili ndiyo kila siku naongea na Waziri wetu wa Ujenzi hapa, ni eneo ambalo kuna viwanda vingi, barabara ni mbovu, maji ni changamoto, lakini Mheshimiwa Waziri wa Maji, umekuwa msikivu, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ombi langu, Vijiji vingine kama Kitasengwa sijaviona, nimwombe aende Kitasengwa, Lole, Lugema mpaka Mabaoni pamoja na Makungu ili wote wanufaike. La pili, Mheshimiwa Waziri anapokwenda kwenye Kata ile ya Kihohela ambayo ni sehemu ya jirani atusaidie, sijaiona Magunguri kwa sababu bado mradi wake haujakaa vizuri, Magunguri na Isaula pia inufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, lakini kabla sijamaliza, nizungumzie kidogo Mradi wa Idete, Kata ambayo ipo kama kisiwani, imeachwa kwa mara ya kwanza wanakwenda kuweka historia ya Mheshimiwa Waziri wetu, maji hayakuwahi kufika pale. Waziri amepeleka visima, nimwombe vile visima alivyopeleka pia apeleke na

mabomba ya usambazaji maji ili wananchi wa Idete waendelee kumshukuru Rais wao kwa jinsi alivyomtuma na yeye ameelewa na wasaidizi wake wameelewa, sasa wanakwenda kuwapelekea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza nina maombi madogo mawili, madogo tu na nita-*mention* kwa sababu ya muda wako, najua wachangiaji ni wengi katika sekta hii. Moja, tunayo changamoto kwenye miradi iliyokuwa imeanza kwenye Kata za Kasanga, lakini pia kuna Kata ya Mtambula na vijiji vyake, pamoja na Kata ya Mninga na Luhunga. Nimwombe sana Waziri akajaribu kutazama maeneo haya pia. Namwomba Mheshimiwa Waziri apeleke wataalam pale wakatusaidie ku-*design* ili kero ya maji iishe. Mto Ruaha unaanzia pale, wao ndiyo wanatunza kwa nini wawe na shida ya maji? Halafu watu wengine wanufaike na maji hawa si ni Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia sasa, nipende pia kuwaombea wenzangu wa jirani kwa sababu mradi huu kwa muda mrefu umezungumzwa, mradi wa vijiji 14 ambao unagusa Kata ya Iswagi, Ihalimba na Ikongosi, namwomba sana Wazri ukakamilike mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava atafuatiliwa na Mheshimiwa Juliana Shonza na Mheshimiwa Edward Olelekaita ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti ya Wizara ya Maji. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujalia uzima na ametuwezesha kuendelea kuwepo ndani humu na kuendelea kuwatumikia watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nimpongeze sana ndugu yangu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso

kwa kuwa Waziri wa Maji, lakini pia kwa kazi kubwa wanayoifanya yeye na wataalam wake wote kwenye Wizara ya Maji. Wanafanya kazi kubwa sana, nami ni muumini wa kumpongeza mtu anapofanya vizuri. Wanafanaya kazi kubwa na nzuri, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bajeti hii ya mwaka huu, nitumie nafasi hii kutoa ushauri kwenye baadhi ya maeneo machache. Pamoja na kazi nzuri wanayoifanya kwenye Wizara ya Maji na Taasisi zao zote, tumeanzisha *RUWASA, RUWASA* inafanya kazi nzuri na ni moja ya chombo ambacho kinakwenda kuwakomboa sana watu wetu hasa sisi watu wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maboresho machache ninayoshauri tuyafanye kwa upande wa *RUWASA* ili iendelee kufanya kazi zake vizuri. Eneo la kwanza Mheshimiwa Waziri, nilisema mwaka jana na leo narudia tena. Tuiimarishieni *RUWASA* kwa kuweka Bodi za Manunuzi, hata kama hatuwezi kwenye Wilaya lakini basi tuwe na Bodi za Manunuzi za *RUWASA* kwenye mikoa yote. Haiwezekani *RUWASA* Mkoa wa Tanga kwa mfano, manunuzi wakitaka kufanya mpaka tutegemee Bodi ya Manunuzi ya TANGA - *UWASA,* ambayo ina majukumu yake, ina mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tunachelewa na miradi yetu inachelewa kutekelezwa kwa sababu ya kutokuwa na Bodi za Manunuzi. Kila mkoa kwenye Ofisi za *RUWASA* tupate Bodi ya Manunuzi, kuwe na Mtaalam wa Manunuzi ili manunuzi yafanywe na *RUWASA* wenyewe tusitegemee Mamlaka nyingine hizi za maji. Huo ni ushauri wangu kwenye eneo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili Mheshimiwa Waziri, sehemu kubwa ya kazi za maji tunafanya kwa kutumia *force account*, tunatumia wale watu wetu tunaita *local*-fundi. Hao mafundi wanaofanya kazi ni mafundi wa chini kabisa ambao hawana mitaji mikubwa na hata miradi wanayopewa ni miradi midogo, tuziboreshe na Ofisi za

*RUWASA* kwenye ngazi ya Wilaya. Waweke Wahasibu pale, haiwezekani fundi wa mradi wa milioni 15 anayelipwa *labour charge,* aki-*raise* kabarua kake ka kuomba alipwe milioni tatu atoke Lushoto, atoke Mlalo aende Tanga Mjini kwenda kufuata malipo yake ya fedha, haiwezekani. Nawaomba tuziboreshe hizi Ofisi za Wilaya, kuwe na Wahasibu na Wataalam pale ili waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Bodi za Watumia Maji, kama tumeweza kwenye Serikali kuajiri wataalam wa kilimo karibu kwenye kila kata, tunashindwaje kuwa na Mtaalam wa Maji kwenye kila kata ambaye ameajiriwa na Serikali. Sehemu kubwa tunatumia mafundi wale *local* ambao tunao wanashirikiana na wananchi wenyewe. Naiomba Wizara wafikirie kuajiri watu wa kwenda kufanya kazi za maji kwenye kata zetu, tuwe na Mtaalam wa Wizara, tuwe na Mtaalam wa Serikali aliyeajiriwa na anayelipwa ili kuwa na ufanisi mzuri wa kutekeleza majukumu yao kwenye yale maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ninalotaka kushauri kwa ujumla ni kwenye eneo la Sera ya Maji. Maisha yanabadilika na yanakwenda kasi sana, maendeleo yetu yanakwenda kwa *speed* kubwa, Sera yetu ya Maji inatwambia kufikisha maji mita 400, nadhani tunapoelekea tunapaswa tuangalie kufikisha maji kwenye nyumba za Watanzania. Miji yetu inakuwa kwa kasi, vijiji vinakuwa kwa kasi, kuna haja ya kuingalia vizuri Sera hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huo wa jumla, niende hasa kwenye mambo ambayo yanawagusa Wanakorogwe. Tunao mradi wa Mwanga – Same – Korogwe, mradi huu umechelewa sana na Mheshimiw;a Waziri ni shahidi. Nimpongeze kwa hatua alizochukua za kuvunja mkataba wa Mkandarasi na kutafuta namna nyingine ya kufanya ile kazi. Pamoja na hilo lakini bado *speed* ya kazi ile siyo nzuri sana na hairidhishi. Ninachotaka tu Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha atuhakikishie kwamba ni kweli huu muda aliotuambia kwamba mradi utakamilika ni kweli utakamalika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi kukamilika kwake ndiyo kuwapa maji wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini hasa Kata za Mkomazi na Mkumbara ambao ndiyo wapo mwishoni mwa mradi huu. Mradi huu umechelewa kwa muda mrefu, tulitamani sisi tupate maji kutoka hata kwenye Mto Pangani au Mto Ruvu ambao unapita pale Mkomazi, lakini kila tukijaribu kutoa hayo mawazo tunaambiwa haiwezekani kwa sababu kutakuwa na *double allocation of resources*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watuambie kama huu mradi bado sana na kama hakuna uhakika na muda huu, waturuhusu na watutafutie fedha tuchukue maji kutoka kwenye mito tuliyokuwa nayo, ipo mito mingi na maji mengi ya kutosha, tupeleke maji kwa watu wa Mkomazi na watu wa Mkumbara kuliko kusubiri mradi huu mpaka muda ambao haujaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumzia Miradi ya Miji 28 na moja kati ya maeneo ambayo Waziri amesema yanakwenda kunufaika na mradi huu ni eneo la Mji wa Korogwe ambalo ni Jimbo la Korogwe Mjini. Mheshimiwa Waziri anajua kwa sababu tulifanya ziara naye, chanzo cha maji cha mradi huu kupeleka maji Korogwe Mjini na kupeleka Handeni, kupeleka na Muheza na Pangani kinatoka pale Korogwe, kwenye Kata ya Mswaha eneo ambalo vijiji vyake vyote havijapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomwomba Mheshimiwa Waziri atuhakikishie watu wa Korogwe, tulishaomba kuwa sehemu ya mradi huo, sasa wanapochukua maji kuwapelekea Korogwe Mjini, Muheza na Handeni, hivi vijiji hivi wasivisahau. Kama Mheshimiwa Waziri anavyosema kwamba anapowadhuru wengine asitupite, basi wasiwapite wale wananchi. Tumesema muda mrefu lakini hatujajua kama walitukubalia, walituingiza kwenye mpango au hawajatuingiza. Kwa kuwa tunabmatumaini mradi unakwenda kutekelezwa sasa, tunaomba Waziri atupe ahadi na uhakika wa Serikali kuwa wananchi hawa watanufaika na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna bwawa ambalo nimeshawahi kumwambia Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara, Bwawa la Mayuyu ambalo linapatikana kwenye kule Kata ya Kerenge. Bwawa hili lilikuwa likitoa huduma ya maji kwa wananchi wetu, liliharibiwa na mafuriko, wakatuahidi kwamba wanatafuta fedha na kuna wakati wakasema wamepata fedha kutoka kwa wenzetu wa Misri, lakini mpaka leo bado kupo kimya. Namwomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kwenye majumuisho atuambie tu ili tujue lini wananchi wa Kerenge na watu wa Mayuyu wanakwenda kupata ile huduma ya bwawa ili kurudisha huduma ya maji na kuendeleza shughuli za kiuchumi kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema nimeangalia bajeti ya Waziri vizuri na nimeisoma nimeona kwenye ukurasa 219 mpaka 220 ametenga fedha kwa ajili ya Vijiji vya Wilaya ya Korogwe kupata maji. Tunayo miradi ya kutosha pale, tunayo miradi mingi, lakini sehemu kubwa fedha hizi ni fedha za kuanzia na ni fedha ambazo hazitoshelezi na *ceiling* tuliyopewa ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara ya Maji, lakini pia Serikali, ipo haja ya kuangalia namna ya kuongeza bajeti ya maji ili miradi hii iweze kukamilika. Tunamwomba Waziri atusaidie hilo ili wananchi wetu waweze kupata huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge mnapochangia nirudie tena, mnapochangia mnakuwa mnazungumza na kiti, ukiongea moja kwa moja na Serikali tunarudi kule kule nyuma, kwa hiyo nawakumbusha.

Mheshimiwa Juliana Shonza, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Subira Mgalu, ajiandae.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Maji. Kwa kuanza napenda nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anafanya katika Taifa letu, katika kuhakikisha kwamba Watanzania tunapata maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, Mheshimiwa Aweso anafanya kazi kubwa sana. Sisi kama Wabunge tutaongea masuala mengi humu Bungeni, lakini yote ni katika kushauri, haiondoi ukweli kwamba Wizara ya Maji ipo vizuri na inafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sote tunafahamu kwamba kwa miaka mingi tangu nchi yetu ipate uhuru, miradi mingi sana ya maji imeshapelekwa kwenye maeneo yetu. Kama haitoshi ni fedha nyingi sana ambazo zimepelekwa kwenye miradi ya maji na miongoni mwa Wizara ambazo zimeshapelekwa fedha nyingi ni Wizara hii ya Maji, lakini bado kilio ni kikubwa sana, unapokuja suala la maji kilio ni kikubwa sana huko kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasikitisha zaidi kwa sababu vilio hivi vinatoka kwenye maeneo yale yale ambayo tayari Serikali imeshapeleka miradi mikubwa ya maji. Ukiangalia chanzo cha haya yote ni kwa sababu hakuna usimamizi wa kutosha kule chini kwenye mikoa yetu, wilaya zetu na kata zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019, Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Maji na mojawapo ya kipengele ambacho kilikuwa ni muhimu sana kwenye hiyo sheria ni kuzipa mamlaka zile jumuiya za maji ziweze kuajiri lakini vile vile kufukuza wataalam wa maji endapo watakuwa hawajafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni jema, lakini ni lazima kwamba Serikali iweze kutia mkono wake. Serikali

pamoja na kwamba ina dhamira kubwa na nzuri ambayo inayo lakini watambue kwamba bado ina kazi ya kufanya ili kuweza kufikia malengo ambayo tumejiwekea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba Sera ya Maji ya mwaka 2002 imesema wazi kwamba jukumu la maji si la Serikali peke yake, wananchi wanajukumu kubwa la kuchangia huduma za maji. Lakini vile vile hizo fedha ambazo zinapatikana kwenye hiyo miradi ya maji lazima ziende kwenye uendeshaji, kwenye upanuzi, lakini vile vile ziende kwenye ukarabati wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri hiyo, ili sasa sheria pamoja na sera ziweze kufanya kazi, hatupaswi kuachia jumuiya za maji peke yake ndiyo ziajiri wataalam wa maji. Nasema hivi kwa sababu tumeshuhudia maeneo mengi ambapo kuna Jumuiya za maji, wataalam wengi ambao wanaajiriwa kwenye hayo maeneo ni wale ambao wengi wao hawana uzoefu wa kutosha. Lakini wengi wao hawana ujuzi wa kutosha. Kwa hiyo unakuta kwamba miradi ile pamoja na kwamba Serikali imeweka pesa nyingi, lakini ile miradi inakuwa haina *sustainability,* ndani ya muda mfupi tunaona miradi imekufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ile dhana kamili ya kuweka Sera ya Maji ili basi wananchi waweze kuona matunda ya fedha zao ambazo wanachangia kwenye miradi, inakuwa haipo. Pia sote tunafahamu kwamba, ili miradi ya maji iweze kuleta tija ni lazima kuwepo na usimamizi mzuri wa miradi ya maji. Kwa hiyo tutaongea mambo mengi sana hapa Bungeni, lakini kama hakuna usimamizi mzuri itakuwa ni sawa na kazi bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kutokana na hayo nataka nishauri masuala machache na kwa sababu najua Mheshimiwa Waziri wa Maji ni kijana ambaye ni msikivu, naamini atafanyia kazi ushauri wa Wabunge. Ushauri wangu wa kwanza; ni vema sasa Serikali ikachukua hili suala la hizi jumuiya kuweza kuajiri wataalam wa maji liwe ni suala la Serikali. Kwa maana ya kwamba Serikali iwatafute hawa

ambao ni wataalam, iwaajiri, lakini vile vile iwalipe, kwa sababu jumuiya nyingi zimeshashindwa kuwalipa na inapelekea miradi kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo zuri ni kwamba Wizara hii inayo Chuo cha Maji na kile chuo kimekuwa kinazalisha wataalam karibu kila mwaka na wale wataalam wapo tu mtaani hawana kazi. Kwa nini sasa Wizara isifikirie kwamba wawaajiri hawa watalaam angalau kwenye kila kata ili basi kila kata kuwe na usimamizi mzuri wa miradi ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Rais wetu wa Awamu ya Sita alizungumza alipokuja hapa Bungeni, alisema kwamba Serikali yake imejipanga kuweka usimamizi mkubwa wa fedha za Serikali ambazo zinatoka Serikalini kwenda kule chini kwenye miradi. Hata hivyo, swali la msingi la kujiuliza ni kwamba, hizo fedha zinapoenda kule chini je, ni nani ambaye ni mtumishi wa Serikali anayewajibika moja kwa moja? Kwa sababu hawa ambao walikuwa wanaajiriwa na hizi jumuiya hawawajibiki kwa mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawawajibiki kwa Serikali na kuna baadhi ya maeneo tumeshuhudia kabisa kwamba wamekusanya pesa na wakakimbia nazo kwa sababu hakuna sehemu wanapowajibika. Kwa hiyo nataka niombe, pamoja na kwamba Serikali italifanyia kazi hili suala, lakini kuna ulazima mkubwa sana wa Serikali watakapoajiri hawa wataalam kila kata waangalie sasa namna gani ambavyo watatekeleza ile sera ambayo tunasema kwamba ni muhimu hawa wataalam waweze kupatiwa mafunzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wapatiwe mafunzo namna gani ya kuweza kusimamia miradi ya maji, kwa sababu *good governance* ndiyo kitu pekee ambacho kinatakiwa ili miradi ya maji iweze kuleta tija. Kwa hiyo mafunzo ni suala ambalo ni la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine, tunatambua kwamba wanahitaji pia kupata uzoefu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naambiwa hapa kengele ya pili imegonga.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Aah! Mara hii imeshagonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja niweze kumalizia. Pia katika Mkoa wetu wa Songwe, naomba sana Serikali iweze kutusaidia, mkoa ule ni mpya lakini mpaka sasa hivi hatuna mradi wa kimkakati ambao tayari umeshafanyika katika Mkoa wa Songwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mradi ambao unaweza kuhudumia Miji ya Tunduma, ikahudumia Mji wa Vwava pamoja na Mji wa Mloo kwa kutoa maji Ileje, kwa hiyo napenda kumwomba sana Mheshimiwa Waziri, aweze kuliangalia vizuri suala hili la Mkoa wetu wa Songwe ili uweze kuwa na mradi mmoja wa kimkakati kuliko kuwa na miradi mingi ambayo haina tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Niwakumbushe tena Wabunge muwe mnaangalia huku mbele ili muone nikishawasha *microphone* hapa, maana yake muda wako umekwisha.

Pia nilikuwa nakumbushwa hapa mbele na Makatibu, Waheshimiwa Wabunge tuzingatie kanuni zetu. Wapo Wabunge wanajisahau hawatazami mtu anayezungumza yupo upande gani, anakatiza tu, hairuhusiwi. Kanuni ya 73, inaelezea kwamba, hairuhusiwi wewe kupita kati yangu na mtu anayezungumza. Sasa tutaanza kutaja majina, rudi ulikotoka, kwa hiyo uwe unaangalia mzungumzaji yupo wapi ili usikatishe kati kati yake.

Lingine Spika akisimama hapa wapo Wabunge huwa wanasimama ndiyo anataka aende *wash room* labda, apite

wapi, hairuhusiwi kuzunguka, ama hata kuzungumza, inabidi ukae kimya kwa kanuni zetu zilivyo. Hapa naongea nimekaa kwa hiyo ukiwa unazunguka ni sawa, lakini nikiwa nimesimama Wabunge wote mnatakiwa kuwa mmekaa mnasikiliza nataka kusema nini? Ndiyo kanuni zetu zinavyosema. Kwa hiyo, tuzingatie Kanuni Waheshimiwa Wabunge.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Edward Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na kwa wale ambao hawafahamu Mheshimiwa Naibu Spika ni Mwalimu wangu, alinifundisha *Law School of Tanzania. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze sana Waziri wa Maji; Waziri wa Maji kati ya wageni wangu niliowatambulisha leo, nilitembelewa na waliogombea na mimi, aliyegombea kupitia ACT Wazalendo Ubunge na aliyegombea kupitia CUF, wa ACT Wazalendo Ndugu Kamota amekubaliana na kasi ya Chama cha Mapinduzi na kazi anazofanya Mbunge hapa na amekubali kuungana na Chama cha Mapinduzi. Namshukuru sana kwa uungwana wake mzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiteto nilishazungumza hapa ni takribani *square* kilometa 17,000 ni majimbo mengine kama matano hivi ni jimbo kubwa sana. Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo naongelea kila wakati kwasababu, ndio *social contract* ya kwetu na wananchi ukurasa wa saba na naomba ninukuu kabisa *"Kuongeza kasi ya usambazaji maji safi na salama kwa asilimia 85 vijijini na 95 mijini"*.

Mheshimiwa Waziri, kwanza kabisa naomba bajeti ya Kiteto msiipunguze hata nukta moja, tuanzie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile, kwanza Mkoa wa Manyara *overall* ni asilimia 58 tunapata maji *below*

*national average* kwa hiyo, katika kutengeneza vipaumbele hivi tuangalie mikoa ambayo ipo nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiacha Manyara sasa, Wilaya ya Kiteto ni asilimia 52 na Mji wa Kibaya ambao ndio mji wetu kwa miaka 20 sasa, ni asilimia 44 maji na miundombinu pale mjini yamechakaa ni ya mwaka 1980. Mheshimiwa Waziri, ukitutengea milioni 100 tutaweza kufumua mifumo ya maji ile na kutengeneza vizuri sana, ili Mji wa Kibaya ambao ndio sura ya wilaya ipate maji ya kutosha. Kata kama za Njoro Mji wa Matui, Kijungu, Lengatei, Dongo hazina maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Rais mama Samia Suluhu Hassan, ukurasa wa 29... *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

**T A A R I F A**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni mdau wa Wilaya ya Kiteto nalima mashamba yangu kule, Mheshimiwa Mbunge ametaja kata ambazo zinakosa maji kwenye eneo hilo na nilikuwa namkumbusha tu kwamba asisahau Kata ya Dosidosi ambayo nimewekeza pia. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge alikuwa anaendelea kutaja kata zake. Haya unaipokea taarifa hiyo, unakumbushwa kwamba kuna kata inayohitaji.

**MHE. EDWARD O. KISAU**: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea sana sana kabisa na nimkumbushe tu kwamba Katibu wa Mbunge anatoka Dosidosi. Na napokea sana na niseme tu kwa kuwa amenikumbusha, nilipata bahati ya kutembelewa na aliyekuwa Makamu wa Rais ambaye ni Rais

wetu sasa Mama Samia Suluhu Hassan, kunitafutia kura na kituo cha kwanza kabisa ni Dosidosi. Dosidosi ni Kijiji cha kwanza tu ukitoka Kongwa na kutokana na ukame wa Jimbo la Kiteto, Mheshimiwa Rais aliahidi mabwawa Kiteto. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nakushukuru sana na ni kweli kama alivyosema naendelea kutaja kata zangu ambazo hazina maji; Kata ya Njoro, Kata ya Makame, Kata ya Lolera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema hotuba ya Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan ukurasa wa 29 naomba ninukuu. *"Aidha, kwa maeneo yasiyokuwa na vyanzo vya maji tutajielekeza katika ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua"*. Kutokana na jiografia ya Jimbo la Kiteto mabwawa, na kuna ahadi ya muda mrefu ya Serikali ya bwawa la Dongo, Kata nzima ya Dongo. Bwawa hili likijengwa vijiji sita na kata mbili zitanufaika na mradi huu na wananchi walishatenga eneo kubwa tu. Kwa hiyo, namuahidi Waziri kati ya maeneo ambayo tutakwenda ni Dongo ukaone bwawa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shida nyingine, kutokana na ukubwa wa Wilaya hii *engineer* ni mmoja tu na mafundi wako watatu, haiwezekani. Tunaomba *engineers* wawili tunaomba na mafundi sita, hatutaki wengi sana sisi sio *selfish* sana hao tu Mheshimiwa Waziri. Tukipata na magari mawili kutokana na jiografia ya jimbo hili utatusaidia sana na maji yatapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji wanaoumia sana ni wakina mama kwa hiyo, kama tutaweza kutimiza takwa hili la Chama Cha Mapinduzi tutakuwa tunawasaidia wakinamama wengi sana nchini. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa nafasi hii, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Subira Mghalu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa kuchangia katika Wizara hii ya Maji na nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, pamoja na Naibu Waziri, *Engineer* Maryprisca. Lakini pia nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa *DAWASA* kwa namna ambavyo anatuhudumia Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa shukrani, naishukuru Wizara ya Maji pamoja na Serikali kwa kukamilisha mradi wa maji wa Kisarawe, kwa kukamilisha mradi wa maji Mkuranga, lakini kwa ahadi yake ya kuanza upembuzi yakinifu ya kutoa maji ya Mto Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu wanawake wa Mkoa wa Pwani wa Wilaya hizo, watapata tija kubwa na tunaweza kuwatua ndoo kichwani. Sambamba na hilo niishukuru Wizara pamoja na *DAWASA* na pia kumshukuru sana Rais aliyepita Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa maelekezo ya mradi mpya wa kutoa maji Ruvu, Chalinze - Mboga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika mradi huu kazi inaendelea, lakini wana Chalinze pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo wameniomba pia niombe kasi ya mradi huu iongezeke. Usambazaji wa maji katika maeneo ya Bwilingu, Chalinze Mjini, Pera, Nero na uunganishaji wa wateja wanaomba kama ambavyo Mkurugenzi *Engineer* Luhemeja ametuambia inawezekana mpaka tarehe 30 Mei, 2021 mradi huu ukikamilika basi ukamilike kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni wa kawaida maombi ya wanawake, pamoja na miradi mingi ya maji lakini gharama za kuunganisha maji ni kubwa sana laki tatu. Wanawake wengi wa vijijini hawawezi kumudu kuitoa kwa wakati mmoja, wanaomba pengine ilipwe kwa *installment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, wanawake wameniomba niombe Wizara ya Maji pamoja na Taasisi zake, itoe elimu kwa namna ambavyo wanasema umetumia *unit* ngapi, mahusiano yake na ujazo wa maji. Kwasababu, yapo malalamiko ya bili kuwa kubwa na Mheshimiwa Waziri amekuwa akilisemea mara kwa mara, kupitia elimu hiyo wanaweza wanawake na watumiaji wa bili wakawa na uhakika na bili zinazowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu, wanawake pia wameniomba, utaratibu pengine wa Wizara ya Maji na Taasisi zake, zianze kutumia *prepaid meter* kwa ajili ya uhakika wa kile kitu ambacho unatumia maji hayo. Lakini sambamba na hilo, wanawake wameniomba pia na wananchi wa kawaida kwamba, inapotokea na hili hata Katibu Mkuu mama Queen Mlozi ndio amenitumia hapa. Inapotokea umehamia nyumba ambayo mtumiaji alikuwa halipi bili, bili hiyo inapewa kwa mtu aliyehamia kwa hiyo, Wizara na Taasisi zake ziweke mkazo katika kuhakikisha wanakusanya bili kwa mhusika. Lakini kumpa deni ambaye hahusiki na usipolipa maji yanakatwa hilo limelalamikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la nne pia, wananchi wa Kata ya Mpangani, Kibaha Mjini tuna mradi mkubwa wa machinjio na *DAWASA* walituahidi mradi mkubwa pale, ni miaka mitatu sasa mradi haujajengwa. Na machinjio yale halmashauri inatumia pesa nyingi zaidi ya milioni 40 kwa maji ya *ma-bulldozer* haya ukizingatia na mapato tu ya milioni 60 kwa hiyo, tunaomba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa, pamoja na hotuba ya Waziri kuainisha changamoto mbalimbali, lakini ipo changamoto ambayo hata Mheshimiwa Rais aliisisitiza, matumizi mabaya ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya upatikanaji wa maji safi na salama. Nikuombe Mheshimiwa Aweso, unawazingua wanaokuzingua, lakini kwenye hili la matumizi mabaya naomba endelea na kasi ya kuwazingua. Katika mapitio

machache tu ya taarifa ya *CAG* naomba ukawazingue watu wafuatao: - *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kwanza, katika ripoti ya *CAG* licha ya kwamba tutapata fursa ya kuijadili, lakini kwa kuwa imeainisha matumizi mabaya usichelewe hapa:-

(i) Kuna fedha zaidi za bilioni mbili na milioni 200 zimetumika kwa matumizi mengineyo, ukurasa wa 64 wa taarifa ya *CAG* ya ukaguzi maalum na amesema mchukue hatua za kisheria;

(ii) Kuna miradi ya thamani ya bilioni nne na milioni 700 haifanyi kazi, haitoi huduma, *CAG* ameomba mkachukue maamuzi;

(iii) Kuna miradi ya bilioni moja ambapo malipo yamefanyika kwa kazi ambazo hazikufanyika ni ufisadi, kawazingue Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

(iv) Kuna miradi ambayo wakandarasi wameisababishia hasara Serikali na mapungufu ya zaidi ya bilioni 10, nakuomba Mheshimiwa Waziri kashughulikie, kawazingue. Kwasababu, tunazungumza hapa namna tutakavyoongeza mfuko wa Taifa wa maji vijijini lakini tusipofanya jitihada za kutosha kwa hiki kidogo kinachotengwa, zaidi ya bilioni 680 unaziomba leo za maendeleo kwa ajili ya miradi ya maji. Tusiposhughulika na mchwa hawa kwa wakati ni wazi tunaweza tukaona kila siku hela nyingi zinatumika lakini miradi haitoi tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Aweso kasi yako nzuri, Naibu Waziri Engineer anafanya kazi vizuri. Lakini na sio wahandisi pekeyake shirikiana na Wizara ya *TAMISEMI* wameanza kazi vizuri na wao, hatua zinachukuliwa na mamlaka zingine. Pia, nimemuona Waziri wa Utumishi naye akiagiza *TAKUKURU* ipitie miradi mbalimbali. Kwa kweli, kama tusipopata muarubaini

wa kupambana na pesa zinazotumika vibaya kwenye miradi, tutaona kwamba hela nyingi zinatumika na miradi haifanikiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Mradi wa WAMI Awamu ya Tatu Chalinze tunapongeza hatua ya Serikali ya kusitisha mkataba na kumpa mkandarasi mpya kazi inaendelea. Lakini kuna maeneo kwa mfano, vitongoji vya Ludiga, Kwaruhombo, Kata ya Kibindu nao tunataka wapate maji ya bomba, maeneo ya Ubena aliyosema Mheshimiwa Mbunge na nakazia hapo hapo naomba mradi huu kama ulivyokusudiwa kwamba utakamilika mwaka huu mwishoni basi ukamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno haya nakushukuru sana kunipa nafasi naipongeza Wizara hii, nampongeza mama yetu mama Samia, nina uhakika atawatua wanawake ndoo kichwani. Na ninamtakia kila la kheri ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya ajiandae.

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru kwa kunipatia fursa hii niweze kuchangia katika sekta hii muhimu kwa wananchi wa Tanzania. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri mdogo wangu Aweso, kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye Wizara hii na nimuambie, kwa utu wake kwa wema wake Mwenyezi Mungu atakusimamia na utatenda maajabu kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kunukuu maneno ya Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan, aliyoyasema tarehe 22 April, 2021 wakati akihutubia Bunge lako Tukufu, alisema maneno yafuatayo nanukuu: "Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika miaka mitano iliyopita, tatizo la maji bado ni kubwa kwenye maeneo mengi nchini. Hali hii inachangiwa na usimamizi usioridhisha wa

miradi na vile vile, matumizi mabaya ya fedha zinazotengwa, kwa ajili ya upatikanaji wa maji safi na salama." *(Makofi)*

Mheshima Naibu Spika, naomba pia nimnukuu na nikupongeze sana Mheshimiwa Aweso kwa kutambua mchango wa watangulizi wako, Mheshimiwa Eng. Kamwele, Mheshimiwa Prof. Mbarawa. Mheshimiwa Prof. Mbarawa Waziri wa Maji wa Serikali ya Awamu ya Tano mwaka 2020 wakati akihitimisha hotuba ya Wizara yake alisema maneno yafuatayo nanukuu pia: "Tatizo ndani ya Wizara ya Maji sio upatikanaji wa fedha bali ni usimamizi wa fedha zinazopelekwa sekta ya maji." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetanguliza maneno haya ili kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, anatakiwa atengeneze kitengo chake imara cha usimamizi na ufuatiliaji wa miradi yote ya maendeleo ndani ya sekta yake husika. Hapo ndipo Taifa letu linapoteza fedha nyingi kwasababu, nimemsikia mtanguliza wangu Mheshimiwa Subira Mgalu akisema ukawazingue waliotajwa kwenye vitabu vya *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kuwazingua watu ambao wameshawaumiza watanzania faida yake ni nini! Jambo la kwanza, tunatakiwa kwanza tuimarishe usimamizi, sifa ya mradi ina mwanzo na mwisho wa utekelezaji wa mradi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika Serikali ndani ya Afrika zilizowekeza kwenye mifumo mingi ya kiteknolojia ni Taifa letu la Tanzania. Zipo *software* ambayo unaweza *uka-install* ndani ya ofisi yako popote ulipo, kwenye simu yako, ukafanya *monitoring and evaluation* ya miradi yako yote iliyopo kwenye sekta yako husika. Na hii itatuondoa kwenda kwenye *post valuation*, watanzania wanaumia wameshapelekewa fedha za kutosha hawapati matokeo chanya, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twendeni kimkakati miradi yote inayopelekewa fedha siku ya kwanza ujue inaanza

tarehe 1 mwezi Julai inamaliza tarehe 1 mwezi wa Septemba, nenda nayo kila siku na utaokoa fedha za kutosha za watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze jimboni kwangu Kondoa, sisi wana Kondoa tunabahati kubwa tuna chanzo cha maji cha Mto Moko. Chanzo cha maji cha Mto Moko umekieleza ukurasa wa 27 kwenye kitabu chako. Ulipoeleza chanzo hiki Mheshimiwa Waziri kule ambako chanzo cha maji kipo, ni vijiji viwili tu vinavyopata maji kutoka kwenye chanzo hiki cha maji. Vijiji vyote vinavyopata maji kutoka kwenye chanzo hiki cha maji vinakwenda Wilaya ya Chemba. Kwa nini mradi huu usihujumiwe na kule ambako mabomba yanapita? Wananchi wanaona maji yanakwenda Chemba lakini wao hawana maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nilishafika ofisini kwako nikakuambia, nimeona wananchi wametoboa bomba linalopeleka maji Chemba nikawauliza kwa nini wanafanya hivi? Wanasema maji yanatoka kwetu sisi hatuna maji, tunahangaika na maji tunaangalia maji yanakwenda sehemu nyingine hapana. Basi naomba Mheshimiwa Waziri nipendekeze, mnapotekeleza miradi ya maendeleo tekelezeni sera ya maji ya mwaka 2002, inayoelekeza kila Kijiji ambako miundombinu ya maji inapita, basi wao wapate maji kwanza kabla ya kule mnakowapelekea. Hii itawezesha miradi yetu na miundo mbinu yetu ya maji iweze kuwa ya kudumu kwa sababu, walinzi wa kwanza wa kudumu watakuwa ni wanavijiji ambayo mabomba yale yanapita kwenye vijiji vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 27 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri anapendekeza pia vijiji 11 vya Wilaya ya Chemba vinakwenda kupata maji kwenye bwawa la kimkakati la Kisangaji ambalo linajengwa Wilaya ya Kondoa. Kwa hiyo, vijiji 11 vipo Chemba, bwawa lipo Kondoa, hakuna Kijiji hata kimoja cha Kondoa kinachokwenda kupata maji. Wanakondoa wamekukosea nini Mheshimiwa Waziri? Naomba sana mtekeleza Sera ya Maji wapatieni maji pale

Bwala la Kisangaji lilipo vijiji vyote vilivyozunguka bwala hilo viweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba akiimarisha Kitengo cha Tathmini na Ufuatiliaji miradi yote, mfano mradi uliopo katika Kijiji cha Sauna Kisese ingekuwa ya kuendelea mpaka leo sasa miundombinu imechoka kwa sababu hatufuatilii, fedha nyingi zimewekezwa, wananchi wanakosa maji. Vijiji vya Busi, Sambwa na Pahi wana miundombinu ya maji inahitajika fedha kidogo sana lakini Wizara haifuatilii na haijui nini kinaendelea tutakuja kuwekeza fedha nyingine nyingi ambazo hazitakuwa na msaada tena maana miundombinu ile itakuwa imeshachoka na imeoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno haya nimalizie kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameanza vizuri na amesema tatizo la maji ni la kwake analibeba kwa kuwa ni mama. Nina uhakika kwa uchapakazi wa Mheshimiwa Waziri atamtendea haki mama yetu, atawatendea haki Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma anayenijalia uzima mpaka siku ya leo nimesimama katika Bunge lako Tukufu. Niwashukuru sana wana Nkansi Kaskazini kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika kipindi kigumu nachokipitia hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na suala la Mradi wa Ziwa Tanganyika. Mheshimiwa Waziri kabla sijazungumza jambo hilo na mimi nikupongeze kwa kwa uthubutu na

namna ambavyo unawajibika kwenye Wizara yako, pamoja na Naibu wako, mnafanya kazi nzuri. Hata hivyo, kazi nzuri zitaonekana kwa vitendo, tunatamani kuona maji siyo maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua mchango wa Serikali kwenye Jimbo langu la Nkasi Kaskazini katika suala zima la kupeleka maji lakini pamoja na jitihada hizo za Serikali bado kuna changamoto kubwa. Tunapozungumzia upatikanaji wa maji vijijini, Nkasi Kaskazini ni miongoni mwa majimbo ambayo yapo pembezoni na maeneo hayo Kata zote zinatoka vijijini. Serikali imetuletea kiasi cha fedha; Kata ya Kabwe kuna mradi wa maji wa bilioni 1.4, Kata ya Kilando bilioni 1.3, Kata ya Namanyere bilioni 1.7, lakini ukiangalia miradi yote hii, haiwezi kutatua changamoto ya maji hata robo ya Jimbo la Nkasi Kaskazini. Ndiyo maana tunasema kwa kuwa Mungu ametujalia kuwa na mito, maziwa na bahari kwa nini tusitumie vyanzo hivyo ambavyo ni vyanzo vya uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna jambo linaniumiza naamini na wewe Mheshimiwa Waziri linakuumiza, wakati huu ndani ya Bunge tunazungumzia mafuriko na shida ya maji, kuna shida gani? Mungu ametujaliwa mvua za kutosha, lakini wakati huo ambao tunazungumzia mvua za kutosha zina athari zake lakini tunatumiaje sisi hiyo neema ambayo Mungu ametupa ya mvua nyingi kuweza kuvuna maji tukaepukana na hizi athari ambazo zipo leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Kilando ambako ndiko chanzo cha Ziwa Tanganyika kwenye Wilaya yangu ya Nkasi ni kilometa 64 kufika Namanyere, leo tunazungumza habari ya maji miaka nenda rudi. Kuna vitu ambavyo hatuhitaji kutumia nguvu zaidi, nimezungumzia kata tatu tu juu ya miradi inayoendelea hivi sasa ambayo haiwezi kumaliza changamoto hata robo kwa nini tutumie hiyo miradi midogo midogo ambayo haiwezi kumaliza changamoto badala ya kuja na fedha ambazo tunaamini kwamba tukitumia chanzo cha Ziwa Tanganyika hatutazungumzia wanufaika Nkasi peke yake, tutazungumzia Sumbawanga

DC, Sumbawanga Mjini, Kalambo, mkoa mzima wa Katavi lakini itaunganisha na Mkoa wa Songwe. Kwa hiyo, tunazungumzia mradi wa uhakika ambao Serikali mkikaa utatusaidia. Pamoja na kwamba utatumia gharama kubwa lakini ni mradi ambao utakwenda kuwanufaika wananchi wengi na habari ya maji itakuwa historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hiyo lakini hata hivi fedha chache tunazopeleka usimamizi wake ukoje? Pamoja na kwamba kuna mambo ya ajabu yanayofanyika kwenye miradi ya maji, lakini bado kuna changamoto ya watumishi, yawezekana hata waliopo uwezo wao ni mdogo; hao waliopo ni wachache hawawezi kutatua hizo changamoto za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali, pamoja na kwamba uhaba upo wa kutosha Serikali ni moja, Wizara ya Utumishi kama kweli maji ni kipaumbele lazima itoe vibali vya kuajiri watu hawa na watu hawa wapo shida ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda kumshauri tena Mheshimiwa Waziri hata wale watumishi wachache waliopo Wizara ya Maji wanatakiwa kupewa *training.* Yawezekana kuna maeneo ambayo sisi labda tuna bahati mbaya, tunapotumia wale *local* fundi wanafanya kazi nzuri lakini wale pia wanahitaji angalau wapewe elimu ya kila wakati waweze kutusaidia. Hata hivyo, kwa nini tutumie wale kama wapo waliomaliza wapo mitaani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie miradi hiyo ya maji, pamoja na kupeleka fedha ni vizuri tukawa na utaratibu wa umaliziaji wa miradi hiyo tunayoianzisha. Tunaanzisha miradi mbalimbali tunaiacha. Tunapopeleka fedha tunataka ku-*achieve* nini? Tunataka kumaliza changamoto ya maji. Kama hilo ndio lengo kwa nini hatufiki mwisho kwenye hiyo miradi ambayo tunaianzisha? Tusifikirie kuanzisha miradi mipya wakati hii tuliyonayo bado hatujaweza kufikia hitimisho na kufikia lengo ambalo tulikusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kwa mfano ule Mradi wa Namanyere, toka mwaka jana wananchi hawapati maji. Tunaambiwa habari za *pump*, *pump* ni shilingi ngapi Mheshimiwa Waziri? Mnapokuwa mnafanya upembuzi si mnajua kwamba hapa kunahitajika *pump*? Inakuwaje mnafika mwisho mmefanya kazi mpaka asilimia 70 watu wanakaa miezi saba, miezi nane, mwaka mzima hawajapata maji kwa sababu ya *pump*, nini tunafanya? Natambua namna ambavyo unawajibika, lakini kuwajibika kama watendaji wako hawawajibiki kama wewe tutabaki kupiga *story* tu ambapo hazitatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Nkasi Kaskazini tuna kata 17; hakuna kata hata moja yenye uhakika ambayo unaweza kusema tunapata maji. Mimi leo nitakupongeza kwa sababu ya uthubutu lakini tunapata shida sana kwenye Wizara yako ya Maji na inashangaza ni kama kilometa 64 kutoa maji Ziwa Tanganyika lakini mpaka leo tunalia juu ya maji, nafikiri hili haliko sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika ugawaji angalieni utaratibu ni vigezo gani mnavitumia kwenye kugawa miradi ya maji. Kuna maeneo mengine tunapata changamoto na tunaanza kujifikiria shida itakuwa ni nini. Naomba nizungumzie katika hizohizo kata ambao zina miradi; Vijiji vya Itindi, Masolo, Lyele, Kanazi, Misunkumilo, Kolongwe, Kalila, Matine, Mkombe, Mpenge hayo maeneo yote hayana maji kabisa. Nakuomba utapokuwa unahitimisha hapa natamani na wewe ukaone yale maji yenye rangi ya njano ambayo wanakunywa wananchi wangu, uone kama kweli tunawatendea haki wananchi hawa. Ni Watanzania kama wengine na wanastahili kupata haki na ni wajibu wa Serikali kuwapelekea huduma ya maji ambayo ni safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, Mheshimiwa Cecil Mwambe ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu. Pia nimshukuru na kumpongeza Waziri wa Maji, ndugu yangu Mheshimiwa Aweso kwa hotuba nzuri na ushirikiano anaonipatia ninapompelekea hoja zinazohusu maji za Jimbo la Meatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya na kwa kuweka mkazo mkubwa katika upatikanaji wa maji hususan katika maeneo yenye uhaba mkubwa wa maji. Mheshimiwa Rais wakati akilihutubia Bunge alisisitiza zaidi katika uchimbwaji wa mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na ninaunga mkono. Ni ukweli usiopingika katika Wilaya ya Meatu yenye majimbo mawili kuna uhaba wa vyanzo vya maji. Niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikitutengea fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji lakini miradi hiyo inashindikana kutokana na ama kukosekana kwa chanzo cha maji ama maji yanayopatikana yana chumvi nyingi sana kiasi kwamba maji yale hayafai kwa matumizi ya binadamu na hata katika maabara zetu za maji yamekuwa hayakubaliki. *Solution* kubwa kwa Wilaya ya Meatu ni uchimbwaji wa mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi na Waziri ni shahidi katika Mradi wa Mji wa Mwanhuzi tumeletewa mradi wa visima kwa ajili ya kuongezea Bwawa la Mwanhuzi lakini chanzo cha maji kimekosekana imebidi tukachimbe bwawa ndani ya mto wa mchanga. Serikali imeleta fedha mpaka leo navyoongea zipo na utekelezaji wake ulitakiwa ukamilike Julai, 2021 lakini inashindikana. Zile fedha zipo toka mwezi Februari, 2021 kwa sababu utekelezaji wake umekwamisha na mvua zinazoendelea kunyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Meatu la awamu iliyopita kwa kauli moja tulikubaliana Meatu tuletewe miradi ya mabwawa ili kukabiliana na tatizo la chanzo cha maji katika Wilaya ya

Meatu yenye majimbo mawili. Serikali imekuwa ikileta fedha nyingi ili kutekeleza miradi hiyo lakini fedha hizo hazikidhi mahitaji, thamani ya fedha haipo kwa sababu imekuwa haitekelezi kwa mujibu wananchi tunavyotakiwa kutekelezewa changamoto zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee mradi mmoja wa Bwawa la Mwanjolo ambao ulitekelezwa katika awamu iliyopita na uligharibu shilingi bilioni1.8 na Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia akiwa Makamu Rais alikuja kuuzindua. Leo hii navyosema tunaambiwa kwamba haliwezi kujengwa tenki la maji lolote kwa sababu yale maji hayatoshi lakini mradi huu ulitekelezwa na watu wa Wizara ya Maji kuanzia usanifu mpaka ujengaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliwahi kutembelea wakati wa ujengaji wa mradi ule kwa macho yangu mimi ambaye siyo mtaalam niliona yale maji hayatakidhi au hayatatosheleza kusambazwa katika vijiji vinne tu vinavyoizunguka ile kata. Nimshauri Mheshimiwa Waziri afike Wilaya ya Meatu alione lile bwawa la maji. Sisi Wilaya ya Meatu tumekuwa tukionewa miradi mingi imekuwa ikiletwa inagharimu fedha nyingi lakini hainufaishi wananchi kama ilivyokusudiwa. Inauma sana bilioni 1.8 imepotea tu lakini wananchi hawajaweza kupata maji kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuishauri Serikali iendelee kutekeleza miradi itakayowezesha upatikanaji wa huduma ya maji kwa haraka ili iweze kusaidia maeneo yenye uhaba mkubwa zaidi wa maji. Miradi hii nilipendekeza vyanzo vyake iwe ni maziwa yaliyopo katika nchi yetu pamoja na mito ambayo haikauki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikubali kutumia fedha nyingi ambapo itakuwa ni mwarobaini wa kutatua matatizo ya maji hususan kwenye maeneo ambayo yanakabiliwa na uhaba wa maji. Kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Simiyu tunao mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Toka naanza Ubunge wangu 2015

mradi huu umekuwa ukizungumziwa lakini mpaka leo hakuna dalili yoyote ya kuoneshwa ni lini mradi huu utakamilika ambao unatekelezwa kwa awamu mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum wa Simiyu tarehe 30 Aprili, 2021 alisema mradi huu utakamilika ndani ya miaka minne. Hata hivyo, mradi huu ukiungalia kwenye utekelezaji wa kazi za Serikali katika awamu iliyopita haumo, kwenye mpango wa miaka mitano haumo, lakini hata kwenye mpango wa mwaka mmoja haumo. Je, mradi unaenda kutekelezwaje ndani ya miaka minne wakati hata kwenye mipango ya Serikali haujapewa kipaumbele? Mradi huu ni mkubwa utagharimu shilingi bilioni 370. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri ya mwaka jana aliahidi ungeanza kutekelezwa Julai, 2020 lakini tumekuwa tukipigwa danadana. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali lile juzi alisema utaanza kutekelezwa Agosti, 2021. Leo hii ukiangalia ni mwezi Mei, 2021 lakini hata hatua za kumpata mkandarasi wa ujenzi hazijaanzwa na wakati huu Serikali inahuisha kupitia usanifu uliofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge wa Simiyu ndio mradi uliotusababisha tukapewa kura, tuliji-*commit* kwa ajili ya mradi wa mradi wa Ziwa Victoria lakini sasa hivi sioni dalili zozote. Naomba Serikali itumie fedha za ndani ni shilingi bilioni 370 katika Awamu ya Kwanza, tunategemea fedha za nje lakini ninyi ni mashahidi fedha za nje zimekuwa zinasuasua na sasa hivi Watanzania tunajivunia kutumia fedha za mapato ya ndani. Naomba mradi wa maji ya Ziwa Victoria uanze kutengewa fedha za kutosha katika mapato ya ndani ndiyo itakuwa suluhu ya utekelezaji wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mheshimiwa Dennis Londo ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara ya Maji. Kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri kijana na machachari ambaye amedhihirisha umwamba wake katika Wizara hii ya Maji. Nadhani ukiona mpaka Mheshimiwa Rais ananukuu yale unayoyafanya maana yake unahakikisha unayasimamia kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimkushukuru kwa miradi ambayo imeainishwa kwa ajili ya wakazi wa Biharamulo. Nikushukuru kwa mradi ule wa Maziwa Mkuu, nimeona Biharamulo imetwaja; ni mradi wa shilingi bilioni karibu 750 ambayo itahudumia miji inayozunguka Ziwa Victoria na Biharamulo ipo na vijiji vyake, kwahiyo nakushukuru kwa ajili ya hilo. Pia ukurasa wa 149 nimeona miradi ambayo nimetengewa kwa ajili ya Wilaya ya Biharamulo nishukuru, itatutoa hapa tulipo na kutusogeza mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizidi kukumbushia tu nadhani nilim-*consult* kwa ajili ya ahadi ya Rais; mradi mkubwa wa kuleta maji katika Mji wa Biharamulo kutoka Ziwa Victoria. Naomba azidi kuukumbuka hata kama bajeti imebana ili shida ile ambayo imekuwepo kwa muda mrefu iweze kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze kwa nia thabiti ya kutusaidia kwa sababu nilishamuona ameniahidi baada ya bajeti mimi kama Mhandisi na yeye kama mzoefu twende pale tuangalie chanzo ambacho kinatuhudumia sasa hivi ili tuweze kuanza mwanzo mwisho ikiwezekana tupate *treatment plant* ya kuanzi sasa hivi kipindi ananiandalia mradi mkubwa. Nazidi kukushukuru kwa ajili ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani niweze kuongea mambo machache mengine yatakuwa yangu ya ufuatiliaji kwa ajili ya eneo langu ila kwa sababu ninao uzoefu mkubwa katika sekta hii kwa hiyo napenda kuongea juu ya

yale ambayo nayajua na yale ambayo nadhani tukishauri Serikali ikayabeba na wakayafanyia kazi yataweza kweli kutusaidia. Cha kwanza, niipongeze Serikali kwa uanzishaji wa *RUWASA. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ile ambayo Mheshimiwa Waziri amekuwa akiita ni kichefuchefu; mpaka anawaambiwa watu wachezee vitambi lakini sio miradi, nakumbuka iliyo mingi ni ya *BRN (Big Results Now),* ndiyo ilifeli wakati ule tukitumia wakandarasi na Halmashauri mkaona *solution* ni kuja na *RUWASA.* Kweli *RUWASA* imetusaidia kwa sababu wakati ule nakumbuka unakuta mkandarasi hajui chochote, mwingine ana *stationary* na kadhalika na miradi mingi ilikuwa ni ya viongozi hao hao waliokuwa kwenye halmalshauri zile; mainjinia na watu wengine ndio maana ilifeli. Kwa hiyo, tuhuma zile za nyuma tuziache tuku-*support* tuanzie hapa na *RUWASA* ili twende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kufuatilia utendaji wa *RUWASA,* wanafanya kazi vizuri, wote tunajua. *Development partners* wanatoa pesa kusaidia miradi ya maji vijijini, lakini *based on performance.* Nimefuatilia nimeona *DFID,* sasa hivi imetoka shilingi bilioni 23 imeenda mpaka shilingi bilioni 79. Maana yake *RUWASA* wamefanya vizuri, wame-*qualify* kwenye vigezo na fedha imeongezeka. Nimeona hata ya *World Bank* ilikuwa shilingi bilioni 118 nadhani safari hii inaenda mpaka shilingi bilioni 186, hii ni *good performance* kwa sababu wanafanya wanavyofanya, mkienda kuchujwa kwenye viegezo, inaonekana mme-*qualify* mmeenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, baada ya kuyaona haya yote na kwamba *RUWASA* inaaminiwa, ili lisiwe bomu baadaye, maana mwanzo wakandarasi waliharibu. Maana unapoongelea miradi ya maji *is purely engineering practice.* Huwezi kufanya *engineering project* bila kuwa na ma-*consultant,* na watu ambao wanahausika. Hata ukijenga nyumba yako wewe mwenyewe unaita fundi. Wewe sio mjenzi, lakini kuna kipindi

unapitia nyumba unamwambia fundi hapa ulivyopiga ripu siyo. Wewe sio *engineer* wala nini, lakini unaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba turudishe *practice* ile ya ma-*engineer.* Nimefuatilia nikaona kwamba mpango wa kuchuja wakandarasi unaendelea na ni hatua nzuri sana ambayo inafanywa na *RUWASA,* kufanya *shortlisting* ya wakandarasi mkajua kama wana vigezo *then* twende hatua ya pili ya kuwaamini wakandarasi hawa tuwarudishe kwenye miradi watusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii miradi ni mingi, hatuwezi kuifanya kwa kutumia *force account* tu. Ni lazima tu-*employ* wakandarasi. Kwanza watatengeneza ajira kwa vijana wa Kitanzania na miradi itafanyika haraka kwa sababu wananchi hawa wanachohitaji ni maji. Tukienda kwenye *process* hii ya muda mrefu, kesho na kesho kutwa tutakwama tena. Maana ni bajeti hii, mwakani utakuja na bajeti nyingine na bajeti nyingine. *RUWASA* ni mtoto mdogo ambaye mmemzaa hata miaka miwili hajafikisha, kaanza 2019. Mwezi wa Saba ndiyo anaenda mwaka wa pili. Tumwezeshe pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu utakuwa *enginee;* wote jiografia ya mazingira yetu tunaijua. Hata magari, kuna baadhi ya sehemu hawana magari bado. Kuna baadhi ya sehemu bado hawajaruhusiwa kuajiri. Ni wafanyakazi wale wale waliotoka nao Halmashauri, leo ndiyo wale wale ambao tunawategemea wafanye miradi hii. Sasa tuhakikishe kwamba kwenye bajeti hii tunawasaidia mtafute magari, vijana hawa wakafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepiga kelele sana ya *TARURA* hapa, lakini miradi haifanyiki mjini. Ni bora sasa hata *TARURA* tunawafuata wananchi kwenye sehemu ambazo wamelima wenyewe. Wote tunajua, vyanzo vya maji viko maporini, tunatoa maji kwenye mapori tunayatiririsha yanakuja kwenye vijiji au miji. Sasa kama hawana vitendeakazi hawa watu watakwama sehemu. Baadaye tutarudi hapa kuwahukumu, tutaona *RUWASA* haina maana,

tutaazimia kuivunja. Sasa tuwawezeshe. Tukishawawezesha nia hii waliyonayo ni nzuri itaweza kutusaidia.

Mheshimwia Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri *with due respect,* mimi nimekuwa na uzoefu na nimejaribu kufuatilia hususan kwenye suala la maji. Yapo makampuni ambayo yapo tayari kutusaidia kuhakikisha kwamba tunapata vifaa. Kwa sababu *almost* asilimia 60 ya miradi ya maji iko kwenye mabomba na viungio, lakini viwanda viwanda vya Kitanzania viko hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema tu-*engage private companies. Private companies* twende tukaongee nao wakubali kutoa mabomba kwa wakandarasi ambao leo tutawaleta hapa. Wakishakubali kutoa mabomba kwa wakandarasi, wakandarasi wafanye miradi ili nyie sasa mtakapoipata fedha mlipe kwenye viwanda moja kwa moja kwa niaba ya wakandarasi. Viwanda vitatoa mabomba hapa na miradi itakimbia. Maana na *best practice* najua, nawe mwenyewe unajua nimekuwa nafuatilia hayo kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kufanya hivi, kelele kubwa ni vifaa. Mabomba yakishafika *site,* hamna shida tena. Shida imekuwa kubwa kwa sababu kazi ya kuchimba mitaro na kufukia siyo *issue*. Mkandarasi anaweza akawa na fedha, lakini kazi ya kununua mabomba pale; unaenda kwenye kiwanda mtu anaambiwa shilingi bilioni 700 au shilingibilioni 800. Wakandarasi wa Kitanzania tunajua, walio wengi wamekuwa wanaandika *paper works* tu. Ukienda kwenye *reality* vile vitu havipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuwanyanyue tuwarudishe kwenye mstari wale waliokuwa wameanguka, tukubali kufanya *commitment* ya Serikali kwamba viwanda vikubali kutoa mabomba, Wizara na *RUWASA* wasimamie. Mabomba yale yakishaletwa, kateni pesa za viwanda muwalipe waweze kukopesha wengine i-*rotate* kule miradi hii itakimbia. Hakuna Mbunge hapa atakayekuja kulalamika kwa sababu kila mahali mlipopeleka mkandarasi, ataanza kufanya kazi

kwa sababu mabomba yatakuwepo, viungio vitakuwepo, kazi yake ni kuchimba mitaro na kulaza mabomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kuna jambo lingine ambalo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Ni kengele ya kwanza eh!

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kuna jambo lingine ambalo nimekuwa nalo kwa *experience* yangu. Nilichokuwa naomba, tujaribu pia kuangalia uendeshaji wa hizi taasisi tulizonazo. Nilikuwa natamani *RUWASA* iendeshwe kama inavyoendeshwa *TANROADS.* Ikiwezekana muwape *target.* Yaani *I believe in targets* kwa sababu *private companies* kwa sehemu kubwa tunafanya kazi kwa *target.* Nimekuwa *Nairobi National Water,* nimekuwa *Uganda National Water* nimeona, yaani Mamlaka ya Maji iko *responsible* kwa Bodi na wana *target.* Kwa sababu nimekuwa kwenye hii biashara kwa muda, kwa hiyo, nilikuwa nafuatilia sehemu zote. Nimekuwa Uganda na Nairobi, nimeona wanavyoendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujaribu kuwapa *target, they have to perform based on targets* kwa sababu mtu anapokuwa anafanya kazi na hana *target,* ndiyo kesho na keshokutwa unakuja kukuta uzembe mdogo mdogo wa mtu mmoja unakuletea kashfa wewe Waziri ambaye unapigana, unamletea kashfa Mkurugenzi Mkuu, lakini kwa sababu tu ya watu wachache ambao wako huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, muundo huu wa kuunda hii taasisi ni mzuri, lakini twende mbele na turudi nyuma, ni lazima iwe *performance based.* Tuifanye kama Taasisi *separate,* tusiifanye kama sehemu ya Wizara, iwe

*performance based,* Bodi ipo, iwajibishe watu wanaoleta uzembe. Kabla ya Rais kukuwajibisha wewe, hebu wewe uanze kuwawajibisha hao watu. Maana nimeona hapa ukurasa wa 29 wa hotuba ya Rais, mambo aliyoyataja kwenye upande wa maji. Usimamizi ametaja mara mbili. Nilikuwa nafuatilia hapa ukurasa wa 79. Usimamizi mbaya na huku kaja tena kwamba, ili kuimarisha usimamizi, atafanya mabadiliko moja mbili, tatu, nne kama alivyotaja hapa. Kwa hiyo, sehemu kubwa ambayo inatukwamisha, ni usimamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachoomba ili msimamizi asitafute sababu yoyote ya kukwepa, hebu tuwawezeshe. Tuwape magari na vifaa. Baada ya hapa, usimamizi ule sasa ambao unautaka wewe kupitia *RUWASA* kwenye Bodi, kupitia *RUWASA* kwenye *Management* uende ukatekelezeke huku mtu akiwa hana sababu yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine cha kumalizia, wako watu ambao wakati wa nyuma walipata shida kidogo kwenye miradi hii ya maji. Maana wakati ule miradi mingi sana ilikuwa imekwama kama ulivyosema. Miradi karibu 177 mmekuta ikiwa imekwama kabisa kabisa, lakini leo mmetekeleza *almost* miradi 85 inatoa maji. Sasa unavyoona kazi hiyo kubwa imefanyika kwa muda mfupi na miradi iliyokuwa kichefu chefu, sina budi kukupongeza. Maana nisipokupongeza wewe Mheshimiwa Waziri na *RUWASA* nitakuwa siwatendei haki. Hotuba nimeipitia, kazi mliyofanya ni kubwa. Tunaojua maji, tunajua miradi ilivyokuwa imekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake; nampongeza Naibu Waziri maana amekuwa kila anapoitwa anakubali kufika, kwangu ameshatembelea. Nampongeza pia Katibu Mkuu kwa sababu amekuwa msikivu, unapoenda kumwona yupo tayari kusaidia na Naibu Katibu Mkuu. Kwa hiyo, ni Wizara ambayo kwetu ambao tunajaribu kufanya ufuatiliaji, mmekuwa tayari kutusikiliza na kutuhudumia. Kwa hiyo, haya

ambayo yanafanyika hapa na *especially* kazi ngumu ya kukwamua miradi iliyokuwa imekwama, mnastahili sifa ya pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge tuwaunge mkono kwenye bajeti hii tuweze kuipitisha sasa ili yale ambayo wananchi wanayategemea hasa kwenye maji, maana kilio cha Watanzania ni maji; maji ni uhai na bila maji, uhai wetu hautastawi; na tusipopata maji huko tunakoelekea majimboni mnajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Londo na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa namna ya pekee kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi hii kwenye Wizara ya Maji kama ambavyo hoja iko mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Naamini imetokea hii kwa sababu ya umahiri wa wasaidizi wake akiwemo Naibu Katibu Mkuu, mama yetu tulimwona hapa mchana na kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kwenye utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na nichukue pia nafasi hii kumpongeza Meneja wa *MANAWASA* Masasi, Ndugu David pamoja na Meneja wa Wilaya wa *RUWASA* Masasi Eng. Juma kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa sababu ni wasaidizi wake na tunapokuwa na shida wakati fulani tunakwenda kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niyaseme machache kwa maana sasa ya kutaka kuboresha kwenye

bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Nimesikia hapa unatajwa mradi wa maji wa Ruvuma. Sina uhakika sana kama Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe umefika pale, lakini mradi huu ni ukombozi mkubwa sana hasa zaidi kwa sisi wakazi wa Mtwara kwa maana ya Mkoa, Wilaya ya Masasi na hasa Jimbo la Ndanda, kwa sababu utaenda kuangazia kwenye Kata za Usikisi na Matutwe, Mpanyani pamoja na Majani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiomba kikubwa kwa Mheshimiwa Waziri, mradi huu utekelezaji wake basi uwe wa haraka kwa sababu shida ya maji anaifahamu na ukiangalia katika *statistics* katika mikoa karibu yote ya Tanzania, Mkoa wa Mtwara ndiyo uko chini kabisa kwenye upatikanaji wa miradi ya maji. Naye ni shahidi, amekuja kule mara nyingi, tumefanya kikao pamoja naye kama Wabunge wote wa Mtwara kwa ushirikiano wetu ili kuweza kusisitiza kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, naomba pia ukamilishwaji wa miradi inayoendelea kwa sababu nayo isije ikawa chechefu. Kuna mradi wa Liloya, Chikukwe utakaohudumia vijiji 26. Mpaka sasa uko pale kwenye asilimia 75 au 80. Tunaomba Mheshimiwa Waziri utakaposimama basi utueleze ukamilishaji wake utakuwa lini kwa sababu unasaidia eneo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii pia kushauri kwamba pafanyike maboresho makubwa kwenye mradi wa maji wa Ndanda kwa sababu eneo hilo limekuwa linakua kila siku na linaongezeka. Wananchi wale wanahitaji maji ya kutosha. Kwa hiyo, tuhakikishe na mradi ule nao unaboreshwa na kukamilika kwa kushirikiana na *engineer* wetu wa *RUWASA* wa Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo moja ambalo pia napenda nimshauri Mheshimiwa Waziri kwa ruhusa yako. Tunajua kwamba kuna mtandao wa umeme wa Taifa ambao unaitwa *National Grid,* lakini sidhani kama Wizara imeshawahi kufikiria kwamba tunahitaji kuwa na mtandao wa maji na wenyewe wa Kitaifa. Kwa sababu tuna Ziwa Tanganyika.

Tutakapoamua kulitumia Ziwa Tanganyika, Mto Rufiji, Mto Ruvuma, *Lake* Nyasa pamoja na *Lake Victoria* tunaweza tukaapata mtandao mzuri sana wa maji wa Kitaifa badala ya hali iliyoko sasa tunahangaika na *small water ports* ili iweze kusaidia wananchi katika eneo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naeleza hapo mwanzoni kwamba Jimbo la Ndanda limegawanyika katika mazingira mawili; upande huu wa Mashariki tatizo la maji siyo kubwa sana kama ambavyo iko upande wa Magharibi. Bahati nzuri pamoja na kwamba nimepata nafasi ya kuchangia, tumekuwa tunakaa na Waziri kila mara kujaribu kushauriana namna ya kusaidia zile Kata nilizozitaja. Nami namwomba kabisa Waziri kwa makini kabisa ahakikishe miradi hii inatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna ahadi ya visima, kusuluhisha hili jambo kwa muda mfupi, tumepata visima kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, lakini sasa tunataka tupate maji ya uhakika. Ndiyo maana unapokuja mradi wa Mto Ruvuma tunaufurahia sana kwa sababu tunaamini utakuwa ni suluhisho la kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna tatizo. Sasa hivi tunapata misaada kutoka kwa wafadhili mbalimbali kwa ajili ya visima na wakati mwingine kupata hata *network* ya usambazaji wa mabomba katika maeneo fulani. Nilikuwa hapa na marafiki zangu, mliwaona asubuhi ambao ni watu wa *Relief Partners International* kutoka Texas, Marekani na shirika lao lingine la *Thirst No More.* Kumekuwa na malalamiko kidogo kwamba mara nyingi wanapoleta vifaa Tanzania kwa ajili ya kuja kusaidia watu wenye haja ya maji, vinapofika kwenye maeneo kwa ajili ya kutaka kuvi-*clear* wanakuwa wanatozwa kodi kubwa sana kana kwamba wao wanakuja pia kufanya biashara wakati *purely* wanavileta kwa ajili ya msaada kutoka kwenye michango ya wafadhili kule kwao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hebu angalia namba ya kurekebisha hizi tozo. Badala ya kuwatoza gharama kubwa sana, pesa hiyo ingeweza kuleta hata visima vingi kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kutoa tu mfano eneo la Ndanda kama ambavyo nimesema toka mwanzo. Tumefanikiwa kupata visima vitatu kwa wafadhili hawa japokuwa wameahidi kupata vingi zaidi. Ila wanavyojaribu ku-*import* vitu hapa kwa ajili ya kusaidia; walileta *rig* hapa, wamelipa kodi karibu dola 60,000. Wanaleta vifaa kwa maana ya *pumps,* wanasema ukinunua *pump* tatu Nairobi, gharama ile ni sawa sawa na kununua *pump* moja Tanzania. Kwa hiyo, gharama zetu sisi ni kubwa zaidi kuliko ambavyo inafanyika Nairobi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wao mara nyingi wanapenda kwenda kununua Nairobi, halafu waje kutumia Tanzania kwa sababu ya ku-*save,* lakini bado wanapofika *border* kuna utaratibu unafanyika wa kujaribu kuthaminisha kwamba kwenye *SH* kodi fulani ambayo inatumika Tanzania *pump* hii thamani yake ni shilingi 700,000/=. Kwa hiyo, kodi yake itakuwa hivi. Ila kimsingi, wao hawajanunulia Tanzania, wanaingiza kutoka nchi ya jirani kwa maana ya Nairobi (tutolee mfano) lakini bado wanatakiwa walipe kodi kana kwamba wamenunua Tanzania. Kwa hiyo, kodi zinakuwa juu, wanashindwa kutimiza malengo yao na wale wanapata pesa kutoka kwa wafadhili lakini gharama za miradi zinakuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, jambo lingine kama alivyosema Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa katika suala la viunganishi, katika miradi hii ya maji ukiiangalia, sehemu kubwa ambayo inachukua gharama kubwa sana ni kwenye masuala ya viunganishi pamoja na masuala ya mabomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi mingi katika maeneo mbalimbali na nita-*cite* tena mfano wa Ndanda. Tuna mradi kwenye Kata Nanganga kwa maana ya Kijiji cha Mumburu na maeneo ya Mkwera. Kwa bahati mbaya sana mmeamua ku-*centralize* suala la manunuzi ambalo linafanywa na watu waliopo Mtwara Mjini ambao hawafahamu kabisa mazingira yaliyopo pale Ndanda, kiasi kwamba tunahamasisha wananchi wachimbe mitaro kwa

ajili ya kulaza mabomba lakini mpaka mwishoni, mitaro ile inakuja kufukiwa na maji ya mvua kwa sababu mvua zinaendelea kunyesha maeneo haya na ukiuliza kwa nini? Wanasema mtu wa manunuzi kwa sababu anakaa mbali na eneo hili na anasimamia miradi mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe Masasi tunapata mtu wa manunuzi ili kuweza ku-*fast-track* hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi wetu mwingine wa Chiwata. Kwa sababu Chiwata ni Kata ambayo iko nje kidogo pembezoni ya Jimbo la Ndanda, imejitenga na iko juu kabisa ya mlima. Tuna mradi pale wa thamani karibu shilingi milioni 400 utaanza kutekelezwa karibuni, lakini bado tunakaribia kwenda kumaliza mwaka, tumebakiza takribani mwezi mmoja na siku chache hizi zilizobakia, pesa hiyo haijaenda na mradi huo haujaanza kutekelezwa. Tunapata wasiwasi kwamba zitabakia siku chache zaidi halafu mtakuja kutuambia kifungu kile kimefungwa, tusubiri sasa mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kama kuna taratibu za manunuzi zinachelewa zipelekwe hapo mapema, hizo pesa zitoke wananchi wale waweze kupata maji kwa sababu wamekuwa wanasubiri kwa muda mrefu na eneo hili limekuwa na kiu kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri kama nilivyosema mwanzoni na sina mengi ya kusema katika Wizara yake kwa sababu tumekuwa tunawasiliana kila mara. Napongeza pia utendaji wa kazi wa watu wake akiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kwa namna wanavyotupa ushirikiano; *Engineer* wetu wa *RUWASA* wa Wilaya pamoja na *Engineer* wa *MUNAWASA* wa kule Masasi kwa ushirikiano wao. Tumekuwa tunawafanyia vikao vya mara kwa mara pamoja na Madiwani kuhakikisha tunapata suluhisho la kudumu la maji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ninaamini kaka yangu na ndugu yangu hapa Mheshimiwa Aweso atakapokuja kujumuisha, atatueleza mikakati yake mahususi kabisa kwa ajili ya Mkoa wa Mtwara, kwa ajili ya Wilaya ya Masasi, kwa ajili ya Jimbo la Ndanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Londo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland na kama muda utaturuhusu tutaenda pia kwa Mheshimiwa Nashon Bidyangunze.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya maji. Kwanza nianze tu kwa kusema kwamba naipongeza Wizara, nampongeza Waziri ndugu yetu Mheshimiwa Aweso; Naibu Waziri, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi na timu yake. Kwa kweli, wanafanya kazi kubwa nasi tunaiona. Nashukuru kwa jinsi ambayo ameweza ku-*transform* Wizara yake katika kipindi hiki kifupi. Kwa kweli, ni mwakilishi mzuri wa vijana nasi tunashukuru kwa uwakilishi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuzunguka sana katika miradi mbalimbali ya maji, sisi bado hatujakuona Jimbo la Mikumi kwa sababu hakuna mradi wa kuja kuutembelea. Hatuna mradi wa kichefuchefu wala mradi wa maji ambao unaendelea. Shida ya maji kwenye Jimbo la Mikumi ni kubwa na ninaomba niweke kwenye rekodi zako kwamba Jimbo lile linaongozwa na Mbunge ambaye anawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kuwaangalia wanyama tumewaachia *TANAPA,* kwa hiyo, sasa hivi tunaangalia shida za wananchi wetu. Wananchi wetu kule shida kubwa ambayo wanayo ni maji. Kuna miji mikubwa kama Mikumi ambayo huwa unapita ukielekea Jimboni kwako kutokea Dodoma ama kupitia Dar es Salaam. Shida

kubwa ya Mji ule ni maji. Usanifu umefanyika, lakini hakuna mradi wa maji na watu wana shida sana ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye mji wa Ruaha ambao una watu wengi sana ambao wanafanya kazi katika Kiwanda cha Sukari Kilombero, watumishi na vibarua wale kazi kubwa ambayo wanaifanya muda wao mwingi ni kutafuta maji. Mheshimiwa Waziri, huwezi kuamini kwamba muda ambao watumishi wa kiwanda kile wanatafuta maji katika Mji ule ni mwingi kuliko muda ambao wanautumia mashambani na viwandani. Hapo hatuzungumzii wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mji mkubwa wenye uzalishaji mkubwa kama huo unapokuwa na shida ya maji unashindwa kuelewa shida ikoje katika maeneo ya pembezoni kama Ruhembe, Tindiga, Mabwelebwele, Ulaya, Malolo na hata Zombo. Kwa kweli, Jimbo la Mikumi limesahaulika kama yalivyo Majimbo mengi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie Jimbo hili kwa namna ya kipekee sana kwa sababu kuna vyanzo vingi vya maji ambavyo havitumiki kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na adha ya maji ambayo inawakumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni mahusiano ya Taasisi zetu ama wakala wetu wa maji kwa mfano *MOROWASA* na *RUWASA.* Kwa kweli mahusiano yao yanatuchanganya na hatujui nani ni nani na nani anafanya lipi? Kwa mfano, katika Mji mdogo wa Mikumi wamechukua *MOROWASA* na katika maeneo yote mengine wako *RUWASA.* Yote haya tunazungumzia ni maeneo ya pembezoni ambayo *RUWASA* walikuwa wanapaswa kuwa wasimamizi wa miradi hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuelewi ni vigezo gani ambavyo Mikumi Jumuiya ya Maji imechukuliwa kwa *MOROWASA* na hasa ukizingatia kwamba ilikuwa inafanya vizuri na ilikuwa Jumuiya ya mfano katika Jumuiya zote za

maji hapa Tanzania na imekuwa ikichukua cheti cha ubora kwa miaka mitatu mfululizo. Tangu wamechukua ile jumuiya wamepeleka *MOROWASA,* Mheshimiwa Waziri anaweza akatuthibitishia hapa *performance* ya maji na shida ya maji imeongezeka maradufu. Hata hayo madogo ambayo yalikuwa yanapatikana sasahivi yanapatikana kwa mgao ambao haumithiliki.

Kwa hiyo, tunaomba wakati wanaanzisha maeneo mapya ya kuyagawa kati ya Mamkala ya Maji ya Mijini na Vijijini waangalie vilevile katika kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo hasa haya ya pembezoni. Pia hata hizi mamlaka mahusiano yake na halmashauri za miji, zinaripoti kwa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na changamoto tulikuwa tunazungumzia kuhusiana na mahusiano ya *TARURA* na halmashauri zetu, lakini changamoto hiyo bado ipo hata kwa *RUWASA.* Hatujui ni nani ambaye anapanga vipaumbele? Nani anashiriki katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi? Wananchi wanawakilishwa na nani katika Serikali za Mitaa kwenye miradi ambayo inahusiana na maji? Kwa hiyo, naomba hilo Mheshimiwa Waziri aliangaliwe kwa namna yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo chetu cha Maji cha Rwegarulila kilikuwa ni chuo maarufu sana katika miaka ya 80 na 90, lakini chuo hiki kinahitaji maboresho makubwa. Naomba kupitia Bunge lako kwamba, Mheshimiwa Waziri aangalie ni jinsi gani mitaala ya chuo hiki inaendana na changamoto zilizopo. Vile vile aangalie ni jinsi gani anaweza akashirikisha vyuo vingine vya ufundi kushirikiana na Rwegarulila katika kuzalisha wataalam wabobezi katika kusimamia, ku-*design* na ku-*implement* miradi ya maji katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza kwamba, maji ni uhai, lakini ni kwa kiasi gani kauli hii ina-*reflect* ama inaakisi uhalisia katika maeneo ya pembezoni? Kodi katika vifaa ambavyo vinahusiana na miradi ya maji bado ni kubwa.

Kwa sababu tunaamini kwamba, maji ni uhai sioni busara ya kuweka kodi kubwa katika vifaa, hasa *pump* za maji kwa sababu, *pump* za maji zinaenda kuhudumia watu. *Pump* za maji ni huduma, *pump* za maji zinaenda kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi wetu hasa katika maeneo ya vijijini. Kwenda kutoza kodi ama kufanya *pump* za maji kuwa chanzo kikubwa cha kodi ni kumuumiza mwananchi ambaye tunataka twende kumtua ndoo kichwani, hasa mwanamke wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Wizara yetu na Taasisi za Serikali zizungumze. Zione ni jinsi gani zinaenda kutekeleza ilani ya chama chetu ambayo inasema kwamba, tunaenda kumtua mama ndoo kichwani. Hatuwezi kwenda kumtua mama ndoo kichwani kama vifaa ambavyo ni muhimu katika uzalishaji na usambazaji wa maji tunaenda kuvitoza bei kubwa, hatutafikia malengo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba, kwa moto ambao Mheshimiwa Waziri anaenda nao na akishirikiana na Wizara nyingine kama Fedha na Wizara ya Maendeleo ya Jamii naamini kabisa tunaenda kutengeneza jumuiya za uhakika ambazo zinaenda kusimamia miradi ya maji katika maeneo yetu ya pembezoni, hasa vijijini. Miradi hii ambayo inatengenezwa ikawa na *ownership* ya wananchi, lakini pia ikawa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambayo tunayo ya miradi yetu ya maji huko vijijini ni kwamba, Serikali hata inapoweka fedha haiwi endelevu kwa sababu, hata jumuiya za maji kule haziwezeshwi, hazielimishwi, hazipatiwi msaada wa uwezeshaji, ili wajue majukumu yao, lakini pia wangalie miradi ambayo inawekezwa kwa fedha nyingi za Serikali kuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, atafuatiwa na Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima afya na hatimaye nimeweza kusimama kuchangia Wizara hii muhimu, Wizara ya Maji. Pia nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Aweso pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya katika nchi hii, hasa katika kuhakikisha tatizo hili la maji linaelekea kwisha, hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kuchangia katika hizi Jumuiya za Watumia Maji. Mheshimiwa Aweso bahati nzuri alikuja katika Wilaya yetu ya Mvomero, kama sitakosea mwaka 2016/2017 akiwa Naibu Waziri wa Maji. Tulikwenda Kibati, mimi nikiwa Mwenyekiti wa Halmashauri pale Mvomero, tulikuta mradi wa maji, Jumuiya ile ya Watumia Maji hawana hata senti moja na wameendelea kukusanya kila mwezi fedha kwa wananchi wale ambao wanatumia maji, lakini alikuta hawana hata shilingi 100. Bahati nzuri alichukua hatua akatoa maelekezo wakakamatwa, lakini hawajarejesha zile fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Aweso sasa hivi amekuwa Waziri kamili, tatizo bado liko palepale. Hizi Jumuiya za Watumia Maji zinahitaji mafunzo. Hawa ni wananchi wetu ambao wako vijijini, hawajui namna ya kusimamia hii miradi ya maji. Hii miradi inajengwa kwa gharama kubwa sana, lakini Wizara inashindwa kutenga hata siku tatu ama nne kwa ajili ya mafunzo ili hizi Jumuiya za Watumia Maji waelewe namna ya kusimamia hii miradi ya maji. Sasa hivi naongea na Mheshimiwa Waziri ule mradi ambao alikuja Mvomero pale Salawe, Kibati, hizi mvua zilizonyesha juzi miundombinu ya maji imeondoka na maji ya Mto wa Salawe, yaani yameondoka na mabomba ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jumuiya ile hawana maji, lakini hawana senti moja kwa ajili ya kurekebisha ile miundombinu na walikuwa kila mwezi wanakusanya zaidi ya shilingi milioni moja. Sasa Mheshimiwa Aweso atapata shida sana kila atakapoenda atakamata

watu, lakini hawa watu hawana uelewa, lazima wapewe mafunzo ili wajue wanachokifanya ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie Waziri, sisi Mvomero tuna vyanzo za uhakika vya maji, lakini ni wilaya ambayo ina shida kubwa sana ya maji. Miradi mingi ambayo iko pale kwetu bado inasuasua; tuna mradi ambao uko pale Doma, tulipata fedha za *World Bank,* huu mradi ulianza kujengwa 2008 mpaka 2010, una vituo vya kutoa maji 15, lakini mpaka leo nazungumza vituo vinavyotoa maji ni vitatu. Vituo vingine hivi havitoi maji mpaka wasikie kuna ziara ya kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013 ulipokuja mwenge pale Doma vituo vyote vilitoa maji. Mwenge ulipoondoka vituo havikutoa tena maji. Akija kiongozi mwingine yeyote yule vituo vinatoa maji. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Aweso atuangalie sana sisi Mvomero, tuna miradi mingi kama nilivyosema huu wa Doma ambayo haitoi maji, miradi hii inatoa maji pale wanapokuja viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine, *unit* moja pale Doma, wana-*charge* kwa sh.3,000 kisingizio wanasema kuna wakati wanatumia *generator* ambayo inatumia mafuta. Sasa tunashindwa kuelewa maeneo mengine sh.800 na kitu, sehemu nyingine 1,000 sehemu nyingine ndio kama hivi 3,000. Bora kuwe na bei elekezi ambayo Wizara itaitoa ili wananchi wetu wajue wanatakiwa kulipa shilingi ngapi? sh.3,000 kwa mwananchi wa kawaida na pale Doma tunajua kuna tatizo kubwa sana la tembo hakuna pale mkulima yeyote sasa hivi ambaye analima. Hali ni mbaya ya kimaisha, lakini mtu analipa *unit* moja sh.3,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri walitupa fedha kwa ajili Miradi ya Dihinda, Masimba, Vianzi, Lubungo na Kihondo. Miradi hii imekamilika japo sio kwa asilimia 100, lakini bahati nzuri inaanza kutoa maji, inasuasua kwa sababu ya hizi jumuiya. Kuna Mradi mmoja upo Dihinda kama wiki tatu zilizopita nimetoka kufanya mkutano pale, tatizo ni kwamba jumuiya ile hata kukabidhiwa mradi hawajakabidhiwa, hawajui wasimamiaje

ule mradi. Naomba sana Waziri atusaidie, lakini na miradi mingine hii kama nilivyosema bado ina changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa 2021/ 2022, nimeona katika Vijiji vya Rusungi, Mwalazi, Chenzema, Kibuko, Luwale, wametenga fedha kwa ajili ya miradi ya maji, lakini pia tutakuwa na mradi mmoja mkubwa wa kutoka Tandali kwenda Homboza ambao utakwenda mpaka Mlali. Nimpongeze sana Waziri. Pia tuna Mradi ambao nimeona Kibogoji, Pandambili na Ndole Matale; Mheshimiwa Waziri naomba sana hizi fedha zisije zikaondolewa, tupate miradi hii katika hivi vijiji ambavyo nimevisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine, nimwombe Mheshimiwa Aweso, tulikuwa na ma-*engineer* wawili wameshahamishwa wote. Mwingine amehamishwa kama wiki mbili zilizopita, pale tuna ma-*technician* watatu tu. Sasa tatizo na changamoto kama nilivyosema hapa za maji hazitaweza kwisha kama hatuna *engineer.* Nimwombe sana Mheshimiwa Aweso atupatie *engineer* pale, lakini pia atupatie na gari la uhakika kwa sababu jiografia yetu sisi ni kubwa sana, lazima awe na gari la uhakika la kuweza kufika maeneo yote kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ile miji 28 na sisi Mvomero katika Kata ya Dakawa, Wami Dakawa Sokoine, tumepata mradi. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri niombe tu pale Dakawa pana shida kubwa sana ya maji, tunategemea huu mradi utakwenda kumaliza tatizo lote la pale Dakawa.

Mheshimiwa Naibu spika kuna Kijiji kimoja cha Sokoine siku moja tuliona kwenye vyombo vya habari ng'ombe na wananchi wanatumia bwawa moja ambalo ni la wafugaji, wananchi na wenyewe wanakwenda kuchota maji pale. Kwa kweli, hali ni mbaya, hali inatisha, tunaomba sana watusaidie, japokuwa tumepata fedha za dharura kwa ajili ya kutoa maji Wami Dakawa kuyapeleka pale Sokoine, lakini bado tatizo lile litakuwepo kwa sababu, mradi ule ni mdogo, hautoshelezi Kijiji kizima cha Sokoine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine kubwa sana la maji katika Kata ya Msongozi. Kata ya Msongozi hawana chanzo chochote cha maji, wanatumia maji ya kwenye mabwawa, wanatumia maji ya kwenye mito, ndio maji yao ambayo wanapikia, ndio maji yao ambayo wanayatumia kwa ajili ya kunywa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atuangalie sana wananchi katika Kata hii ya Msongozi, kuna shida kubwa sana ya maji. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kama itakupendeza...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Van Zeeland kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana Mbunge wa Mbeya Mjini. Nataka tu nimpe Taarifa mchangiaji anayechangia sasa anavyoitaja Kata ya Msongozi ndiyo kata ambayo jina hili ninalolitumia ndio nyumbani kwa mume wangu mimi. Kwa hiyo, hakikisha maji hayo yanakwenda kwenye Kata hiyo ya Msongozi, Morogoro. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Van Zeeland, malizia mchango wako.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea Taarifa kwa mikono miwili. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge nitapambana na Mheshimiwa Aweso hadi kuhakikisha pale maji yanatoka, maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalizie mchango wangu kwa kusema, nimkaribishe sana Mheshimiwa Aweso. Baada ya Bunge hili la Bajeti kwisha Wilaya ya Mvomero iko barabarani, ni lami tupu, twende pale tukazungumze na wananchi. Matatizo ni mengi siwezi kuyaongea yote hapa matatizo ya maji, lakini kikubwa nimkaribishe Waziri Mvomero, karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Maji. Waziri wa Maji huyu ametokea kwenye nafasi ya Naibu Waziri, inaonekana Mheshimiwa Rais alimwona pale alipokuwa akitenda kazi kwenye nafasi yake ya Unaibu Waziri ndipo akaona ampandishe daraja awe Waziri kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Meneja wa *RUWASA* pale kwenye Jimbo langu la Kigoma Kusini, pale Uvinza, naye ni mpya, lakini ameanza kazi vizuri. Ameanza kwa kutembelea kata zote na kuhakikisha anaona vijiji ambavyo havina maji aweze kuona namna ambavyo anawapatia maji wananchi wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Wabunge wenzangu waliojaribu kusema namna ambavyo Wizara inaweza ikatengeneza miradi ya maji ya kitaifa. Jimbo langu liko pembezoni mwa Ziwa Tanganyika. Jimbo langu lina kata 16, lakini ni kata tatu tu ndio zina maji, lakini vijiji viko 61, vijiji ambavyo vina maji havifiki 10. Pia ni jambo la kushangaza sana kwamba, maji wananchi wanayaona, lakini uwezo wa kuyachukua hawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama ambavyo Serikali kupitia Wizara ya Maji imeweka utaratibu wa kuchukua maji katika Ziwa Viktoria na kuyafikisha katika mikoa mbalimbali na hapa Dodoma yanakuja. Kwa nini Mheshimiwa Waziri asione namna ya kubuni mpango wa kuanzisha mradi mkubwa katika eneo lile kwa kutumia maji yale ya Ziwa Tanganyika ambayo mradi ule ungeenda mpaka kwenye Wilaya ya Nkasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika jimbo letu, kama nilivyotaja, tuko karibu sana na maji, lakini iko miradi ambayo

ilipelekwa ambayo mpaka sasa haijakamilika. Kwa mfano, Lukoma; uko mradi mmoja mzuri sana wa maji ulianzishwa mwaka 2010. Mpaka leo tunavyozungumza mradi ule ulikuwa na asilimia 80, lakini mpaka sasa haujaanza. Kijiji cha Lukoma watu wanasubiri maji hawayaoni, lakini fedha ya Serikali ilikwenda kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba, miradi hii ambayo Wizara inaianzisha wakati mwingine ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anatakiwa awe na mpango madhubuti, mpango ambao utampelekea kuonesha kwamba, amefanya maamuzi magumu. Miradi ambayo ni ya pesa nyingi, lakini itakuwa na matokeo mazuri kuliko vimiradi vidogovidogo ambavyo vinakuwa na pesa kidogokidogo na mwisho wa siku miradi ile haikamiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fikiria Kata hiyo ya Lukoma ambayo ina mradi wa maji huu wa mwaka 2010 ambao mpaka sasa haujakamilika na kata ile ina vijiji saba. Hivyo vijiji vyote havina maji, ila nashukuru tu kwamba, Mgambazi ndio kijiji kimoja ambacho katika vijiji saba ambacho kina maji. Pia Mwakizega uko mradi ambao ulianzishwa mwaka 2020, lakini mpaka sasa mradi huo haujaanza. Mabomba yapo, lakini tatizo ni viunganishi kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyozungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlela pia upo mradi wa maji, kisima kilishachimbwa, lakini mradi ule wananchi wanaendelea kusubiri hawapati maji. Kandaga vile vile ndio kijiji ambacho mimi natokea, kijiji hicho kilichimbiwa visima, lakini bahati mbaya kumbe visima vile vilivyochimbwa inaonekana upembuzi yakinifu haukufanywa vizuri, vile visima havina maji, lakini fedha ya Serikali ilitumika katika eneo lile. Kwa hiyo, leo tunasubiri labda Mradi ule wa Mlela ambao tayari umeshachimbwa kisima na wataalam wale wanasema inawezekana yale maji wakayasogeza pale Kandaga ambapo ni vijiji vinafuatana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasubiri hiyo neema kama itapatikana na naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa

kweli katika eneo hili, tukiweza kumpitishia bajeti yake basi aweze kuniona, atembelee katika jimbo langu aone hiki kilio ninachokitoa kwa uhalisia kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile pana mradi pale Ilagala. Ule Mradi wa Ilagala bahati mbaya sana ni mradi ambao haukushirikisha wananchi. Walichimba kisima na bahati mbaya sana kile kisima kina maji ya chumvi wakati Ilagala kuna Mto Malagarasi, mto ambao una maji baridi. Sasa wananchi wanajiuliza, Wizara ya Maji kwa nini watuletee maji ya chumvi wakati sisi tuna maji baridi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mradi ule ni kama vile hauwezi kufanya kazi kwa sababu, wananchi hawataki kabisa yale maji. Kwa hiyo, tukienda kule Mheshimiwa Waziri nina imani atapata uchungu mkubwa kuona namna ambavyo anaweza kubadilisha ili tuweze kuwatengenezea *pump* ili wapate maji yale ya Mto Malagarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwambao mwa Ziwa Tanganyika lina kata nane, lakini katika kata zile ndio kata ambazo kwa kweli, kimsingi mvua zinaponyesha wananchi wanapata shida ya tatizo lile la kipindupindu, kwa sababu ziwa liko bondeni wananchi wanaishi juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati mwingine kutokana na mazingira yalivyo lazima walazimike kuchota maji ya ziwani ili waweze kujikimu na yale maji yanakuwa yameshachafuka kutokana na vinyesi ambavyo, maana vyoo vipo, lakini vyoo wakati mwingine vikifurika maana yake lazima choo kile kiende kule ziwani. Kwa hiyo, kuondoa tatizo la kipindupindu katika Kata za Sunuka, Sigunga, Helembe, Buhingu ni kuhakikisha kwamba tunapata miradi ya maji mikubwa ambayo inatokana na maji ya kutoka Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fikiria Sigunga ina vijiji vitatu lakini hakuna hata kijiji kimoja kina mradi wa maji. Hiyo Sunuka ambayo nimeitaja ina vijiji nane, lakini kuna kijiji kimoja tu kina ndio mradi wa maji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nirudie kumwomba Mheshimiwa Waziri, tuongozane kwenda Jimboni, ili niweze kwenda kumwonesha matatizo yaliyoko jimboni kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa uchangiaji kwa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo. Nitataja majina ya baadhi ya Wabunge ambao wataanza kuchangia mchana halafu wengine nitaendelea kuwataja kadiri uchangiaji utakapoanza; Mheshimiwa Jacqueline Kainja, Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Venant Protas. Wengine tutaendelea kuwataja kadiri tutakavyokuwa tunaendelea na uchangiaji.

Ninayo Matangazo hapa. Mojawapo ni tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi, baada ya kuahirisha Bunge hapa tunatakiwa kuelekea Ukumbi wa *White House* Makao Makuu ya Chama Cha Mapinduzi. Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa anatusubiri huko kwa ajili ya kikao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge lipo pia tangazo ambalo linatoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, katika kilele cha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu yanayoitwa MAKISATU, 2021 yatakayofanyika katika Viwanja vya Jamhuri, Jijini Dodoma, kuanzia tarehe 6 Mei mpaka tarehe 11 Mei, 2021. Waheshimiwa Wabunge wote

mnakaribishwa katika kujionea mashindano mbalimbali haya yatakayokuwepo hapo, lakini pia kujionea teknolojia mbalimbali zilizobuniwa na wabunifu mahiri wa Kitanzania. Nadhani ni muhimu sana kwenda huko ili tukawaone hata vijana wetu wale wanaoweza kuwasha taa kwa kuzungumza, nadhani watakuwepo huko. Mheshimiwa Shigongo nadhani utakuwa umehakikisha wapo eneo hilo.

Pia lipo tangazo, Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Kanda ya Ziwa wanaombwa mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, lakini pia mara baada ya futari ya Mheshimiwa Spika, kwenda *St. Gasper Hotel.* Wabunge wote kutoka Kanda ya Ziwa nadhani mnajifahamu, ndio lilivyoandikwa tangazo hapa muelekee *St. Gasper* kuonana na Mkurugenzi Mkuu wa *Bugando Medical Hospital,* Dkt. Fabian Anaklet Masaga*.*

Kwa hiyo, nadhani tangazo limeeleweka mtaenda huko, mkakutane na huyu kiongozi wa hiyo hospitali anahitaji kuwaona Wabunge wote kutoka Kanda ya Ziwa.

Sasa muda wetu umekwenda sana. matangazo mengine nitayatangaza baadaye, lakini niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, leo kuna mwaliko wa iftar ambayo imeandaliwa na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu hiyo ni ibada nataka kuamini hakuna Mbunge anayekusudia kukosa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa kumi kamili alasiri, leo.

*(Saa 7.05 Mchana, Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - WIZARA YA MAJI**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano, kuna Wabunge niliwataja kwamba tutaanza na hao Mheshimiwa Jacqueline Kainja atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Mwanyika Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara ya maji, awali ya yote nipende kuishukuru Wizara na kumshukuru Waziri wa Maji kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha kwamba wananchi tunapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kijikite moja kwa moja kwenye suala zima la kupata maji kwa njia ya uvunaji wa maji ya mvua kutengeneza mabwawa. Nasema hivyo kwa maana ya kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan ukurasa wa 29 aliweza kuongelea kuweza kulinda miundombinu ya maji na vyanzo vya maji. Lakini vile vile hakuacha mbali suala zima la kuhakikisha tutatengeneza mabwawa ya kuvunia maji hasa kwa sehemu ambazo hazina vyanzo vya maji vya kutosha zenye ukame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoka Mkoa wa Tabora Mkoa wetu hauna vyanzo vya maji vya kutosha na sehemu ambazo ziko pembezoni akinamama wanateseka sana kupata maji ya kutumia. Lakini niipongeze Wizara kwa Mradi wa Maji wa ziwa Victoria ambao mpaka hivi sasa umefika

Tabora Mjini na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba wana mpango wa kupeleka maji katika Wilaya ya Urambo, Kaliua Sikonge. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Wizara katika huu mradi wa maji wa Ziwa Victoria mradi ambao umetengewa fedha shilingi bilioni 11 kutoka maji Tabora Mjini mpaka kwenda Jimbo la Igalula Kata ya Kigwa nilikuwa ninaomba Wizara iweze kuangalia hii *National Water Fund* iweze kuwa inaongeza fedha mradi ni bilioni 11 lakini katika mradi huo wa bilioni 11 mpaka sasa hivi imetoa bilioni mbili kasoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unajaribu kuangalia kama kilometa 30 kutoka Tabora kwenda Kigwa na Mradi ni gharama kubwa za bilioni 11 unaanza kuona je, kama hawatoweza kuongeza fedha hawa *National Water Fund* je, huu mradi unaweza ukaisha kwa muda gani? Lakini vile vile niiombe Wizara iangalie kwamba kwa namna nzuri tukiweza kuwekeza kwenye uvunaji wa maji ya mvua maeneo ya pembezoni inamaana hata gharama ya kutandika mabomba ya maji ya ziwa Victoria kwenda maeneo kama Tarafa ya Kiwele, Wilaya ya Sikonge ambapo kutoka Sikonge kwenda hadi Kiwele ni kilometa 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna maeneo ya pembezoni kutoka labda Bukene Mambali kupeleka maji yale kule kama vile maeneo ya pembezoni tukiwawekea mabwawa wananchi wakaweza kuvuna maji ya mvua yale wakatoa maeneo itakuwa imewasaidia akinamama kuhakikisha kwamba tunakwenda na Sera ya kumtua mwanamke ndoo kichwani kwenye uhalisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niweze kuipongeza sekta ya maji ya Mkoa wa Tabora ambayo inafanya kazi vizuri kupitia RUWASA kwa jinsi ambavyo kuna mradi ambao ni wa Benki ya Dunia *payment for results* ambao mara ya kwanza walipewa bilioni 8.5 wakaifanyika kazi vizuri wakachimba visima vya maji lakini hivi sasa tunaona tunaletewa fedha bilioni 21 hii ni kazi nzuri sana inayofanya na sekta ya maji katika Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuangalie tunapokwenda kwenye Mkoa watu wa Tabora fedha zile tunazopeleka kwenye visima ardhi yetu ni kavu mkandarasi anakwenda pale anachimba kisima kwa gharama kisima kimoja ni milioni 25 lakini akifika chini maji hakuna. Kwa hiyo, tukiangalia namna gani nzuri katika aina mbili ya mradi huu wa Maji wa Ziwa Victoria lakini vile vile tuwekeze kwenye uvunaji wa maji ya mvua ili tuhakikishe mwanamke wa Mkoa wa Tabora tunamtua ndoo kichwani inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kuishukuru Serikali iweze kuangalia Wizara kuhakikisha mradi ambao umeshatengea fedha wa Bukene maji kwenda ya bilioni sita na mradi wa Nsimbo wa bilioni nne tuhakikishe basi hizi fedha zinakwenda kwa wakati, ili akina mama hao wa Nsimbo kwa Jimbo la Manonga na akinamama hawa wa Jimbo la Bukene na kata zote za mbali Kamangaranga na kwingine kote huko waweze kupata nafuu ya upatikanaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Mwanyika atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mheshimiwa Joseph Musukuma ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Maji. Nianze kwa kumpongeza Waziri na watendaji wote ndani ya Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha Watanzania wanapata maji. Naelewa kwamba ni kazi ngumu na tunaelewa kwamba ina changamoto nyingi lakini niseme tu kwamba kazi hii wamepewa ni lazima wafanye kwasababu iko ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwamba wananchi wa Tanzania wa vijijini kwa asilimia 82 watapata maji na asilimia 95 watapata maji ifikapo mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo maneno ndani ya Ilani watu wa Njombe bado yanatutatiza Mji ya Njombe Wabunge wengi hapa wamelalamika na wanalalamika kwamba hawana maji ni tatizo kubwa lakini wengi wanalalamika kwa vile wana uhaba wa maji, lakini Njombe ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna maji ya kutosha, tuna maji mengi, tuna mito inapita kati kati ya mji wetu wa Njombe upande wa huku kula Agafilo upande huku kuna mto mwingine wa Ruhuji lakini tuna visima ukichimba tu unapata maj. Pia tuna maji ya chemichemi lakini cha kushangaza ni kwamba bado mji wa Njombe tatizo kubwa kero kubwa kuliko zote ni maji, hatuna maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Njombe wanapata maji kwa kiwango cha asilimia kama 60 tu na wakati wa kiangazi inakuwa mbaya zaidi, sasa niseme ni aibu lakini ni aibu ambayo lazima tuishughulikie. Kumekuwa na miradi midogo midogo ambayo Serikali imekuwa ikiitekeleza kwa ajili ya kutoa tatizo hili na Rais alipotembelea Njombe Marehemu Mungu Amrehemu mara mbili alipouliza shida yenu hapa ni nini wananchi wa Njombe walisema ni maji mwaka 2015 akigomea alisema shida yenu nini watu wakasema ni maji alipokuja tena kuomba kura akawauliza watu wakamwambia hatujapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Prof. Mbarawa alikuwa pale aliitwa na akasema kwamba atahakikisha ndani ya miaka miwili maji yanapatikana ni miaka mitano sasa wananchi wa Njombe mjini hawana maji tunaongelea mjini. Jimbo la Njombe Mjini lina kata 13 kata 10 ni za vijijini na Kata tatu ni za mjini naongelea kata za mjini hazina maji sijaenda hata vijijini bado, tatizo ni kubwa tunafahamu kabisa kuna mradi mkubwa ambao umekuwa ukiongelewa lakini sisi wana Njombe tunapata wasiwasi bado hata na mradi huu mkubwa ambao tunasema wa miji 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sababu kubwa ni kwa vile tulikuwa ndani ya miji 16 au 17 *scope* yake ilikuwa

inaeleweka sasa tunaongelea miji 28. Kwa hiyo, fedha zilizotengwa ni hizo hizo miji imeongezeka shida kubwa ya Njombe kwa miradi ya nyuma ilikuwa ni kwamba bado ilikuwa ni miradi ambayo haiwezi kutatua tatizo kwa kiasi kikubwa tukaambiwa huu mradi mkubwa unakuja kumaliza tatizo tunapata wasiwasi kama kweli mradi huu utamaliza tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Waziri atuhakikishie wana Njombe kwamba maeneo yote yaliyokuwa kwenye *scope* yatapata maji, maeneo ya Magoda yatapata maji, maeneo ya Lunyanyu yatapata maji Chuo Kikuu cha *Lutheran* kitapata maji, maeneo ya Ngalange yatapata maji na maeneo ya Msete yatapata maji, mji wa Njombe ni katika miji inayokuwa haraka sana katika Tanzania ukuaji wake ni karibu asilimia 3.5 ni kidogo juu ya *average* kwakweli na kuna eneo la Nundu linakuwa kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri hata kama *scope* imebadilika watu wa Njombe wawaangalie kwa tofauti kwasababu ni mji mpya ni Mkoa mpya, Mikoa mingi iliyoongezwa ina miradi mingi ya maji, hapa Njombe hatujawahi kupata mradi mkubwa hata mmoja wa Serikali, na ndio maana Rais alisema wazi Njombe tutahakikisha maji yanapatikana na Mheshimiwa Prof. Mbarawa ni shahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine tuna mradi mwingine mkubwa ambao umekuwa ukiendeshwa kwa takribani miaka mitano sasa miaka sita unaitwa EGOGWI ninashukuru kwamba mradi huo umeonekana katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri lakini bado ni kwa kiwango kidogo sana cha fedha, mradi huo ni kama wa bilioni nne wakati Mheshimiwa Rais Mama Samia anapita katika maeneo ya Njombe kuomba kura alisimamishwa eneo ambalo mradi unapita na akaahidi kwamba maji yatapatikana katika eneo hili. Nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba kwakweli ahadi ya Mheshimiwa Rais ambaye wakati huo alikuwa ni mgombea ilikuwa ni kwamba maji lazima yatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nipende kusisitiza mradi ule ni moja ya miradi ambayo hadi leo haijakamilika kwasababu ninaamini ni uzembe wa watendaji waliopita ndani ya Mamlaka ya maji wakati ule ilikuwa chini ya halmashauri kwakweli tunauhakika kabisa na tunaomba tunapokwenda mbele wataalam wafanye stadi za kutosha za maeneo kujua kama kuna maji ya kutosha na wahakikishe wanatumia hata wananchi wa kawaida kuwaeleza kwamba jamani pamoja na stadi zetu eneo hili lina maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam kwenye Mradi wa *EGOGWI* waliambiwa kwamba chanzo hicho mnachotaka kuweka vijiji zaidi ya nane hakitoshi lakini walibisha matokeo yake *pipe* zimewekwa maji hayatoshi *scope* imebidi ianze kuandaliwa upya, ninadhani ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kwakweli Mheshimiwa Waziri tunawashukuru sana Watendaji ambao wako *RUWASA* kwa sasa maana yake wameweza kuja na mradi mpya ku-*scope* upya hilo eneo na kuja na mradi mpya ambao unatupa moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini watendaji waliopita nadhani ni vizuri kauli ya Rais ianzie hapo kuhakikisha mnashughulika nao maana yake wapo na wapo kwingine na huko watafanya hivyo watafanya hivyo watatengeneza miradi isiyotoa maji na fedha za Serikali zinatumika, ni vizuri tukachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuongelea mradi mwingine mdogo wa mji wa Njombe eneo la Kibena, tunaishukuru Serikali ilitumia fedha za kutosha kwa kiasi fulani kuleta maji katika mji wa Kibena Kata ya Ramadhani. Lakini kilichotokea ni kwamba ndani ya mradi huo mdogo maji yameweza kuja kwa maana Serikali imeweza kuongeza *Capacity* ya *pumps* imejenga *Intech* mpya imeongeza mabomba ukubwa wake kutoka inchi tatu mpaka inchi tisa, sasa kuna maji ya kutosha na hospitali yetu ya Wilaya ya Njombe ya Wilaya inapata maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushangaza na cha kusikitisha ni kwamba eneo lile lina wananchi wengi waliounganishwa ni wananchi kama 3,000 bado kuna uhitaji wa watu wengine 3,500. Hapa niliuliza swali la msingi nikaomba kwenye swali la nyongeza kwamba tunaomba eneo la Kibena ile *project* ambayo maji ni mengi yanaonekana yanamwagika iongezewe fedha kidogo basi ili *distribution line* iweze kuenea na watu wapate maji kuliko wao wapo mjini wanaangalia maji kwa macho na maji yanamwagika kwenye matenki sababu tu *project* ya kwanza ilikuwa ni ndogo haikukamilika, nakuomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hilo kwa jicho la huruma kwa wananchi wa Njombe eneo la Kibena ili angalau tupate fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijaona fedha zimetengwa katika bajeti hii labda kama nimeshindwa kusoma maeneo yote, lakini sijaona eneo lolote ambalo Kibena *Project* ya kuongezea ili wananchi waweze kupata maji ya kutosha, wananchi 3,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa hii nafsi na niombe kwa kumalizia kwa kusema tuna matumaini makubwa sana na Mheshimiwa Waziri na wana Njombe wanamatumaini makubwa sana na Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii wanachapa kazi lakini tutawapima kwa matokeo wana Njombe watawapima kwa matokeo niwatie moyo kwamba bado tunategemea kwamba mtafanya kazi nzuri na mtakamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Mimi dakika zangu

sijui kumi, saba, tano nitaongea kitu kimoja tu, nitaongea kitu kimoja ambacho ni kikubwa sana fedha za miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kuanzia Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne, ya Tano hadi hii awamu ya sita, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inajitahidi sana kupeleka fedha za miradi ya maji kwenye Mikoa kwenye Wilaya kwenye kata hadi kwenye vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee kitu ambacho naomba Serikali inisikilize vizuri Waziri unisikilize vizuri, miaka ya 1970, 1971,1972 na 1973 nilikuwa msichana mdogo ambaye nilikuwa Sekondari nina akili timamu kuanzia mwaka 1970 hii ilikuwa ni Awamu ya Kwanza, nakumbuka wakati pale kijijini kwetu,ninatokea Same Kata ya Kihurio Kijiji cha Uzambara miaka hiyo ya 1970 hadi 1974 nakumbuka Serikali ilileta mradi wa maji kwenye Kata yangu ya Kihurio, Kijiji cha Uzambara. Mradi ule Mheshimiwa Waziri ulikaa kwa muda mrefu sana kwanini? Serikali ya Chama cha Mapinduzi inapeleka fedha za mradi nyingi sana kwenye Mikoa, Wilaya na Kata lakini wakishapeleka ile miradi wanaachia uangalizi wa ile miradi wananchi ndio waangalie ile miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka ni vema nifanye *comparison* mwaka 1970, 1971, 1972 hadi 1980 mradi ulioletwa kwenye Kata yangu ya Kihurio, mradi ulikuwa unaangaliwa na kijana mmoja akiitwa Ally Mabomba, kijana huyo ameajiriwa na Serikali ndiye kila saa 12 asubuhi mnaona maji yanatoka amekwenda kufungua maji kwenye chanzo huko, huko kwenye tenki maji yanapotokea saa 12 jioni Ally Mabomba anakwenda kuyafunga yale maji siku nzima Ally Mabomba anazunguka na Baiskeli kuangalia mradi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameajiriwa na Serikali anazunguka siku nzima na baiskeli yake Kijiji kwa Kijiji kitongoji kwa kitongoji anaangalia mradi wake wa maji mahali kuna kasoro anarekebisha yeye. Sasa tuangalie sasa hivi miradi yetu inakwendaje? Serikali inapeleka fedha nyingi sana za

miradi nyingi sana, miradi ile inawekwa vizuri inajengewa matenki, wanafanya kila kitu miradi ile ikishaisha kunaundwa kamati ya maji sijui huko kwenye Kata zetu na vijiji vyetu wale ndio wanaoangalia ile miradi kule kwenye Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mbunge hiki ni kipindi cha tano na tangu nimekuwa Mbunge kumekuwa na miradi kuanzia bendera, mradi wa kihurio, Mradi wa Ndungu, mradi wa Mahore, mradi wa Kalemau miradi hii inaletwa na Serikali mtakaa miezi sita, saba mradi umeharibika wanaanza kupelekana mahakamani fedha zimeliwa wanaanza kusumbuana huyu ndiye amekula, ile Kamati inayoangalia ule mradi sio, ni kamati wananchi wameichagua wenyewe na ninaona kama Mbunge lakini hakuna mtu mwenye taaluma hata kidogo ya miradi. Sasa nimeomba nizungumzie hili na Waziri unisikilize vizuri tuleteeni fedha za miradi ya maji huko kwenye Majimbo yetu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ile mkishaiweka vizuri fanyeni kila mahali penye mradi kuwe na mtaalam anayeangalia mradi ule. Ama sivyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi mtaendelea kutumia pesa nyingi sana kupeleka miradi ile lakini kwa sababu uangalizi wa ile miradi siyo, inakuwa hamjali tena, mkisha-*install* mradi wa 20 milioni, kama sasa hivi kuna mradi mkubwa unakuja huko umetokea Same, Mwanga, Korogwe umechukua mabilioni ya pesa mradi ule utakapoingia kwa wananchi naziona pesa ni nyingi sana, mimi kwa sababu nimekaa muda mrefu kwenye Majimbo miradi mingi inakufa sana kwa sababu Serikali hawarudi kuangalia ile miradi. Tunafanya sherehe, mradi tumeanza, tunachinja kuku na ng'ombe baada ya hapo hatuwaoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta tunatengeneza Kamati ya Maji sijui wanakusanya hela wanaiba huko huko, wanagombana huko huko hata koki wanashindwa kutengeneza. Mheshimiwa Waziri mtakuwa mnatuletea pesa ambazo hazitoi matokeo mazuri. Sisi tunawashukuru sana mnapotuletea pesa na mnapoanzisha hii miradi kwenye kata zetu ahsanteni sana lakini rudini muiangalie ile miradi, kila mradi uwekeeni mtu kama yule kaka aliyekuwa anaitwa Ally

Mabomba, nimekaa naye kuanzia 70 mpaka 78. Marehemu mama yangu alivuta maji kutoka pale ambapo jumuiya yote tunachota maji akaweka uani yale maji nimeyachota kwa miaka nane sasa hivi hakuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilisimama hapa kuiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ahsanteni sana mnatuletea miradi mingi sana lakini mkishaiweka ile miradi wekeni wataalamu wa kuiangalia. Nilikuwa na moja tu la kuzungumza, nashukuru kama Serikali imenisikiliza lakini naomba hili tuliangalie na Waheshimiwa Wabunge huko mliko kwenye Majimbo yenu mhakikishe Serikali ikiweka miradi inaleta wataalam kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Protas, Mheshimiwa Grace Tendega ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mungu ambaye ametuumba na ametupa kibali muda huu tuko katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku hii ya leo. Naomba nimpongeze sana Waziri wa Wizara hii ya Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya, tunajua mnahangaika sana kutuletea pesa na kuhakikisha kila mtu anapata manufaa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jimbo langu mimi kusema ukweli kuna miradi Serikali imeleta pesa mbalimbali, lakini miradi yote haiendi, wananchi hawana maji. Miradi ipo lakini imechukua muda mrefu takriban miaka miwili, mitatu mpaka miaka minne mitano miradi ile haiendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi mmoja wa Mtakuja - Songambele ambao mpaka sasa hivi uko asilimia 70 lakini mkandarasi anadai shilingi milioni 112 mpaka leo

hajapata pesa zake mradi umesimama. Naomba nishukuru Serikali tanki na vile vituo 11 vimekwisha lakini hakuna mabomba wala *pump* ya kusukuma maji katika maeneo yale ili maji yaweze kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi wa Stalike – Igongwa, mkandarasi anadai shilingi milioni 68 mradi umefika 80% leo miezi mitatu mkandarasi hajalipwa pesa zake. Kuna mradi Katisunga, huu mpaka leo ulikuwa una takriban shilingi milioni 138, mkandarasi mpaka leo hajalipwa pesa zake miezi sita mradi umesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi ambayo Serikali imeleta pesa lakini tumeshindwa kumalizia takriban miaka minne, mitano, wananchi bado wanaiangalia miradi ile tunasema matanki yamekwisha lakini wananchi bado hawajanufaika na miradi ile. Najua kuna kazi kubwa inayofanyika lakini tunaomba mliangalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mkurugenzi wa *DAWASA* wa Dar es Salaam, Mkurugenzi huyu tunamuona *site,* anatoka ofisini anaenda kusimamia miradi. Sasa Wakurugenzi na ma-*engineer* wengine wanashindwa nini kwenda *site?* Kwa usimamizi huu wa Mkurugenzi wa Dar es Salaam matokeo yake Dar es Salaam sasa hivi shida ya maji kila siku inapungua. Wahandisi wengine wanafanya nini maofisini? Kazi yao ni kwenda kuhakikisha wananchi wanapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Nsimbo kuna Kata ya Ugala wana Mto Ugala uko pale pale kijijini wananchi wale wanaliwa kila siku na mamba, tunashindwa kuchukua maji pale kutoka pale kwenye mto kuwawekea hapa gati ili waweze kupata maji? Tunajua mnafanya kazi nzuri lakini kuna upungufu mkubwa sana ndani ya maeneo yetu, ma-*engineer* hawatoki tunaomba watoke wakafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna mradi ambao sasa hivi nimepewa hela wa Kijiji cha Matandarani lakini unachukua Kitongoji cha Magula ambako kuna wananchi

wengi sana pale. Mradi wa Magula unaenda mpaka kwenye Kata ya Ibindi lakini pesa zimeletwa toka mwaka jana mpaka sasa hivi mradi huu uko asilimia 10. Mpaka sasa hivi mmetuletea takriban shilingi milioni 100 na kitu lakini umesimama. Kabla sijaingia hapa nimemuuliza Mhandisi wangu kule mradi unaendaje anasema bado ndiyo kwanza tunaanza kujenga tanki, tutafika kweli? Ukiona tuna mradi huu na ule lakini haiendi wananchi wanapata shida. Mfano, Kata yangu ya Litapunga ina vijiji 10, Kijiji cha Litapunga hawajui maji hata bomba hawajawahi kuona. Najua Waziri anafanya kazi nzuri sana lakini tunaomba miradi hii iende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Katumba yenye vijiji 16 wametuletea kama shilingi milioni 200 lakini mradi umesimama, uko vilevile. Mheshimiwa Waziri anatembea sana katika miradi na shughuli mbalimbali tunamuona anahangaika lakini watendaji wake wamelala. Waziri anahangaika lakini watendaji wake wamelala usingizi. Kama wangekuwa wameamka kufuatilia miradi wala haya mambo yasingetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi tuna Ziwa Tanganyika. Suluhisho la maji ndani ya Mkoa wetu wa Katavi ni maji kutolewa Ziwa Tanganyika na kusambazwa kwa sababu hatuna vyanzo vingi vya kuweza kutosheleza maji ya wana Katavi zaidi ya maji kutoka katika ziwa hili. Naomba sana, najua kuna mikakati mingi na mambo mengi najua Mpanda kuna programu ile lakini naomba katika ile programu ambayo mmetuweka maji yatoke Ziwa Tanganyika ili yaweze kusaidia Mkoa mzima wa Katavi. Maji yakitoka kule haya matatizo ndani ya Mkoa wetu wa Katavi tutakuwa hatuna shida tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana na naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega, Mheshimiwa Justin Nyamoga ajiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe mmoja wa wachangiaji katika mjadala huu wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja kwa sababu tangu asubuhi Mheshimiwa Waziri amewasilisha bajeti yake ya Wizara ya Maji na nimepitia *alhamdulilahi* Jimbo langu la Igalula nimeona vijiji vingi. Namshukuru sana Naibu Waziri na Waziri wake, kweli Jimbo la Igalula tunakwenda kwenye mapinduzi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita kupitia Bunge lako hili Tukufu katika maswali ya nyongeza niliuliza Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria unaotekelezwa kwenye Jimbo langu la Igalula katika Kata za Goweko, Igalula, Nsololo na Kigwa. Nikasema mradi ule utekelezaji wake umesimama na nikaiomba Serikali iweze kunipatia fedha kwa sababu umesimama kutokana na kutokuwa na fedha. Kwa Serikali Sikivu ya Chama cha Mapinduzi niliweza kuletewa shilingi bilioni moja ili mradi ule uanze utekelezaji wake wa kupeleka maji katika Jimbo langu la Igalula.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna changamoto katika mradi huu. Nimshukuru Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tabora ameweza kuuzungumzia. Mradi wa Ziwa Victoria katika Mkoa wetu wa Tabora Jimbo la Igalula halikuwepo katika mpango. Wakati kampeni tulivyokuwa tunanadi sera alipokuja Hayati Dkt. John Pombe Magufuli tulimuomba Jimbo la Igalula liingizwe katika mpango wa kupelekewa maji ya Ziwa Victoria naye alipokea na akatoa maagizo na ule mradi ukawekwa katika mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi ule ni mkubwa sana, unakwenda takriban vijiji 16 vilivyoko katika maeneo hayo na una vituo 100 lakini tangu tumeubariki mradi ule mpaka saa hizi na malengo ya kukamilika mradi kufikia mwezi Desemba, 2021 sasa hivi tuko mwezi wa tano nikuambie kupitia Bunge hili mradi ule umekamilika kwa asilimia 10. Tumekuwa tukifanya ziara mbalimbali kuuliza kwa nini mpaka saa hizi tunakwenda taratibu na wananchi wana hamu na

shauku ya kupata maji kutoka Ziwa Victoria, wanasema tatizo ni fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda kwa Mheshimiwa Waziri mara nyingi sana, mradi ule ni wa kiasi cha shilingi bilioni 11 mmetupelekea shilingi milioni 900 ya kwanza mkatuongezea shilingi bilioni moja na kwenye bajeti hii nimeona mmeweka shilingi bilioni 1.4 kwa maana kwamba huu mradi utakwenda kukamilika baada ya miaka mitatu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri hebu aliangalie Jimbo la Igalula kwa sababu tangu tumeumbwa hatujawahi kufungua maji yanayotokana kwenye koki. Kwa hiyo, wananchi wa Jimbo la Igalula, kupitia kata hizo nne watafurahi sana huu mradi ukikamilika kama ulivyopangwa Desemba, 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu nina changamoto kubwa sana ya maji na mlifanya juhudi za makusudi kututolea maji ya Ziwa Victoria kuyaleta Tabora, ni umbali mkubwa sana lakini mlitambua kuwa ardhi na eneo letu la Mkoa wa Tabora upatikanaji wa maji ya kuchimba kwa kutumia visima ni mgumu sana. Nimwombe Mheshimiwa Waziri katika kuibua vyanzo vya upatikanaji wa maji hebu tubuni mbinu mbadala kwa haya maeneo ambayo yamekuwa yana changamoto ya uchimbaji wa visima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu mimi naishukuru Serikali imechimba visima vingi lakini vinafanya kazi kwa miezi miwili, mitatu ni kwa sababu ardhi yetu ina miamba haina maji. Vilevile mmekuwa mnapoteza fedha nyingi, mkandarasi mnampa tenda ya kuchimba visima anawaambia eneo hili lina maji akienda kuchimba anasema maji yalikimbia yakahamia upande mwingine sasa fedha inapotea, haileti tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali tubuni vyanzo vingine, kwetu tuna majaluba mengi sana, kuna mikondo mingi ya maji yamekuwa yanaleta mafuriko kwa nini tusiyavune haya maji tukatengeneza mabwawa

makubwa. Tukiweka bwawa pale katika Kata yetu ya Kizengi ninyi wenyewe mashahidi wakati wa masika kabla hatujatengeneza barabara ya Chaya - Nyaua ilikuwa kila mwaka barabara inakatika eneo la Kizengi kwa sababu ya maji mengi lakini tungebuni pale yale maji yasiende barabarani yakategwa yangeweza kusaidia hata katika shuhuli za kilimo siyo tu matumizi ya binadamu. Katika eneo letu hasa Mkoa wa Tabora Jimbo la Igalula naomba Wizara ibuni vyanzo vingine vya upatikanaji wa maji maana yapo kwa sababu kila msimu mvua inanyesha na maji yanakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mradi katika Kata yangu ya Tura alishawahi kuja Waziri wa wakati huo Mheshimiwa Prof. Mbalawa Machi, 2019. Alivyokwenda kwenye Kata ya Tura alikuta kuna bwawa ambalo liliachwa na mkoloni ambalo linatumiwa na *Railway Station* akasema hiki ni chanzo kizuri pale pale akatoa shilingi milioni 300 ili wananchi waanze kutumia maji katika Kijiji kile cha Tura. Wakaahidi baada ya miezi mitatu maji yataanza kutumika katika Kijiji cha Tura leo mwezi wa 18 maji wananchi wa Tura wanayasikia kwenye redio tu, hawajawahi kutumia maji yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi tumeenda kufanya ziara pale tukimuuliza mkandarasi anakuambia tulipewa shilingi milioni 300 mradi wa shilingi milioni 800, kwa hiyo tunasubiri shilingi milioni 500 zingine ili tuweze kuukamilisha. Sasa tunakuwa tunamlaumu mtaalamu, *engineer* tunaanza kumpigia kelele lakini ukija kuangalia tatizo lingine huku fedha Serikalini hazijatoka. Niiombe Serikali ule mradi ni mzuri sana, ni bwawa kubwa sana lina maji mengi tukiutengeneza vizuri hata wananchi wangu wa Vijiji vya Kalangasi, Malema, Kizengi, Maguliati na Migongwa wanaweza kupata maji kwa sababu ni chanzo kikubwa ambacho waasisi wetu walituachia. Katika bajeti hii nashukuru vijiji vyangu vingi umeniwekea fedha lakini kwenye hii miradi inayoendelea hasa ya Ziwa Victoria na ule mradi wa Tura, naomba aniongezee fedha ili niweze kukimbia na wananchi waweze kuona matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri amenipa visima sita katika Kata za Mmale, Mwaokoyesengi, Migongwa, Mbulumbulu na Misole. Kwa hivi visima amasema atanipa shilingi milioni 156 huyu mkandarasi anayekuja wamlipe baada ya kutumia maji ndani ya miezi sita asije akaniachia mashimo halafu akaondoka na fedha zikaondoka. Anapokuja kuchimba visima katika haya maeneo ambayo umeniainishia tuone tija ya wananchi wetu ya upatikanaji wa maji kwa sababu tunajua kabisa upatikanaji wa maji kule ni tatizo asije akachukua hizi fedha kwa sababu wamezileta akadhani ni gombania goli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Waziri yeye ni mkali asimamie haya, wamekuwa wakichimba wanaacha visima havitoi maji na ushahidi upo. Kila siku mnatenga hela za ukarabati wakati visima havitoi maji na penyewe mpaangalie, haiwezi kuwa kila siku tunakarabati kisima halafu hakitoi maji wawaambie visima vinavyotoa maji viko wapi? Katika Jimbo langu la Igalula labda bomba moja au mawili ndiyo yanayotoa maji lakini kwenye takwimu za Waziri unaweza kukuta zaidi ya mambo 40 lakini hayatoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai maana binadamu kila siku lazima atumie maji, akila chakula atatumia maji, ni lazima tuliangalie hii sekta katika kipaumbele chake. Nakuomba Mheshimiwa Waziri mradi wangu wa Ziwa Victoria wananchi wa Igalula, Kata za Kigwa, Goweko, Nsololo na mimi nimekuwa nikikuambia kila mara mzee nisaidie na kweli nisaidie nipelekee maji kwenye vile vituo 100 ambavyo umeviandika kwenye bajeti hii wananchi wanasubiri maji kwa hamu ili akina mama wapumzike kuamka alfajiri na kwenda kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi niunge mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Nyamoga na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENGEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Kwanza nianze kwa kusema, bila maji kunakuwa hakuna uhai tena. Nitachangia kwa kuanzia na gharama ya kuunganisha maji. Tunasema tunakwenda kumtua mama ndoo kichwani, lakini gharama za kuunganisha maji zimekuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasikia Waheshimiwa Wabunge wengine wakizungumza hapa, hii inamfanya mtu anataka kuunganisha maji, anatamani apate maji safi na salama, lakini anashindwa kuunganisha maji yafike nyumbani kwake kwa sababu ya kutotimiza takwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia katika Wizara yake namna ambavyo wanaweza kupunguza gharama kwa kuwafanya hawa wanaotaka huduma ya maji angalau waunganishiwe kwanza iangaliwe jinsi wanavyofidia bili zao ili waweze kupata maji. Kwa maana wengi wanataka maji lakini wanashindwa kwa sababu ya gharama ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, vifaa vya kuunganisha maji ni gharama kubwa sana. Kwa hiyo, mwone mtakavyoona vifaa hivi viweze kuwa na gharama ndogo ili watu wengi waunganishe maji na tupunguze hii adha ya akina mama wengi kukosa maji kwa sababu ya gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kwamba kumekuwa na mabambikizo ya bili za maji. Wakati mwingine maji yanakuwa hayatoki, lakini unakuta bili inakuja kubwa sasa kuna maeneo mengine ambayo tunaishi unakuta angalau wanatoa taarifa hata *message* kwamba msoma mita amekuja, amesoma unaweza *uka-compare* na mita ukaona. Basi hii ienee maeneo mengi ili wananchi wengi waache kulalamika kwa sababu kumekuwa na mabambikizo makubwa ya bili za maji wakati mwingine sivyo zinavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tufanye kama wanavyofanya *TANESCO,* pia tuwe na *prepaid meters*. Zile *meter* zinasaidia. Katika Mkoa wa Iringa zipo kwa baadhi, mijini, lakini tunapenda angalau ziwepo, maana mtu atatumia maji kulingana na anavyohitaji maji na hatakuwa na malalamiko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, upotevu wa maji. Wamezungumza wenzangu hapa, wakati tunakua sisi wengine umri umekwenda kidogo. Wakati tunakua kulikuwa na watu ambao wanatazama haya maji yanavyotoka na kuangalia bomba linafunguliwaje, wanafunga na kama bomba limetoboka wana-*repair*, lakini sasa hivi hakuna hicho kitu. Unaweza ukapita mara tano mpaka mara sita wiki nzima maji yanamwangika tu, hakuna anayetoa taarifa, hakuna anayepita kuangalia haya maji. Inaumiza kwa sababu maji yanapotea na tunapoteza fedha nyingi. Kwa hiyo, mwangalie jinsi ambavyo mnaweza mkaweka utaratibu wa maji haya yasipote ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alisema atabeba ajenda ya maji kuhakikisha wanawake na Watanzania tunapata maji safi na salama. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri, kwani katika Mkoa wa Iringa nimeona kuna miradi 34. Nashukuru sana kwa sababu kwa miaka mitano tulikuwa tunapiga kelele maji yamekwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea Kalenga. Nimekuta kuna miradi ambayo itabeba Kata ambazo tulikuwa tunazipigia kelele. Kuna hii Nyamlenge *Construction* nimeiona, Isupilo, Tanangozi na nyingine za Isimani na Iringa nzima, tunashukuru hiyo miradi. Tunaomba pesa zinazotengwa, basi na zitoke ziende zikafanye kazi hiyo, maji yapatikane. Tutarudi mwakani tutaulizana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri akasimamie ili pesa hizi zitoke na maji yakapatikane. Wamezungumza wengine pia, lakini pesa pia

zikitoka tuhakikishe wale wanaosimamia maji vijijini, hawana mafunzo yoyote wanayoyapata. Hakuna mafunzo wanayoyapata wale wasimamizi wa maji ndiyo maana unakuta miradi mingi inaanzishwa na inakufa. Kwa mfano, Maafisa Elimu huwa wanakwenda mpaka vijijini, tuache mijini. Mganga wa Wilaya anakwenda kuzungukia wilaya yake. Kwa nini tusiwe na watu wa maji wazungukie hivyo hivyo ili wahakikishe maji yanapatikana kila sehemu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uangalie utaratibu utakaofaa kuhakikisha hawa wanaoendesha maji huku, vikundi vile vipate kwanza mafunzo ya kuona jinsi ambavyo maji yatatoka vizuri na pia wale wasimamazi waende kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *CAG* imezungumzia jinsi ambavyo Wizara hii imepata changamoto kubwa na nivitu gani ambavyo vimesababisha hiyo? Wamesema miradi mingi haikukamilika kwa wakati kwa sababu hiyo, imeongeza gharama ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waziri ahakikishe jeshi lake au kundi lake linakamilisha miradi kwa wakati ili tusiingize pesa nyingine zaidi katika miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hakuna ubora. Unakuta kuna maeneo wamechimba visima, lakini havitoi maji kwa sababu hakuna chanzo cha kudumu cha maji. Sasa tunajiuliza, hawa ni ma-*engineer* gani wanaokwenda pale kuchimba kisima tupoteze pesa baada ya mwezi mmoja hakuna maji? Hii haikubaliki, lazima usimamizi madhubuti uwepo kwa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha kwa wakandarasi. Wanafanya kazi, lakini pesa haitolewe kwa wakati. Ofisi ya Rais, TAMISEMI ikiwa na Wizara ya Maji, mhakikishe mnatoa pesa kwa wakati ili wale wakandarasi waweze kuendeleza shughuli za utoaji na kukarabati miundombinu yote ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, najua muda umekwenda lakini mengine nitaleta kwa mahandishi ili niweze kutoa ushauri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro na Mheshimiwa Stella Fiyao, ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Maji. Kwanza nianze kwa kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara nzima kwa ujumla. Natambua hivi karibuni ulitembelea mradi wa maji wa Kilolo, Isimani mradi ambao unaendelea na uko asilimia zaidi ya 30 na ninaamini utakamilika. Pia ninaendelea kushukuru kwa sababu ya ukamilishaji wa mradi wa maji ya Ilula ambao ulikamilika kipindi kile kilichopita na nimeshautaja huo mradi huko siku za nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikija kwenye kuchangia, kwanza nianze kwa kutoa ushauri mdogo. Kuna baadhi ya mashirika ambayo yanatoa huduma za maji, lakini siyo kupitia mfumo wa Serikali. Kama pale Iringa, nafahamu kuna shirika linaitwa Waridi na wamefanya kazi nzuri tu, lakini pia sehemu nyingine nchini yapo mashirika kama hayo. Mimi nashauri kuwe na mfumo wa uratibu ili tujue, kwa sababu wakati mwingine ile miradi wakishaijenga wanaondoka. Wakiondoka kwa sababu haikuwa kwenye mfumo wa Idara za Maji, unakuta wakati mwingine nayo inakufa kama wengine walivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu, tungefanya tathmini ya miradi ambayo imefadhiliwa na watu wengine nje ya mfumo wa Serikali, lakini inafanya vizuri ili iweze kuingizwa kwenye mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikijikita kwenye eneo la Kilolo yenyewe, jambo la kwanza nakuomba kupitia kiti chako, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie ule mradi wa

maji wa Ilula ambao nimeutaja, kwamba ulijengwa na maji yamefika pale, lakini usambazaji bado haujafanyika. Kwa hiyo, watu wanaweza kwanza kwenda kuchota kwenye tanki, inakuwa ni kitu kile kile. Mimi natamani sana kungepatikana fedha ili usambazaji ule ufanyike kupitia mifumo ya maji ile na kuondoa kabisa upotevu wa maji ambao kama tukitumia mifumo ile ya zamani sana, maji yale yatapotea na hayatawafikia walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuongezea, ule mradi unasimamiwa na *IRUWASA* na sasa *RUWASA* wana Kata za pembezoni ambazo zinaweza kunufaika. Napendekeza kuwe na mazungumzo kati ya *IRUWASA* na *RUWASA* ili Kata kama ya Uhambingeto ambayo iko pale karibu iweze kuchukua maji kutoka kwenye ule mradi. Hili nimeshalifikisha kwa viongozi wa *IRUWASA* na *RUWASA* Mkoa na nina hakika ukiwekwa msisitizo, basi litafanyika kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo miradi mingine ambayo inaendelea ambayo ningependa kuitaja. Kuna mradi mdogo wa maji wa kule Kata ya Kimala. Huu mradi ulianzishwa na wananchi wenyewe kwa nguvu zao na unaendelea vizuri na haya maeneo ya milimani, ndiyo ile mnaanza kusema wakati mwingine Iringa kuna udumavu. Ni kuchota maji, kwa sababu ni milima, watu wanaposhuka na kupanda na wamebeba madumu, yanawakandamiza, kwa hiyo, wanashindwa kurefuka. Kama utafiti ukifanyika,0 utaona kwamba uchotaji maji kwenye milima unasababisha watu wafikiriwe kuwa wadumavu au wafupi. Ni aghalabu kukuta watu watu warefu kwenye maeneo hayo kwa sababu ya uchotaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata kama ya Kimala, hiyo inatatizo ya maji na wameanzisha wananchi wenyewe ule mradi. Ili utunusuru tuweze kurefuka, tunakusihi Mheshimwa Waziri, tafadhali ule mradi wa maji uweze kukamilishwa pale Kata ya Kimala. utahudumia...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba Mkoa wa Iringa na baadhi ya Mikoa mingine inajulikana kwa udumavu ambao unatokana na mambo ya lishe. Sasa akiongea kama Mbunge, akasema ni udumavu wa kubeba maji tu, atakuwa anapotosha hata na ile elimu ya kutoa kule chini ili watu wetu waweze kuendana lishe bora watake, kuachana na udumavu. Inawezekana waliokuwa na udumavu wa juu, yaani baada ya kubeba, ni shingo tu, lakini hudumavu wa Iringa ni wa ukosefu wa lishe bora kwa wananchi wetu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti ukifanyika utadhibitisha kama kuchota maji na kubeba, kunaweza kusababisha mtu kuwa mfupi au kurefuka. Kwa hiyo, siipokei kwa sababu utafiti bado haujafanyika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin ngoja niliweke vizuri. Mtu mfupi haimaanishi ana udumavu, lazima tuwe tumeelewa vizuri. Ufupi hauna uhusiano na udumavu, kwa sababu hata mtu anaweza kuwa ni mrefu na akawa na udumavu. Kwa hiyo, tutofautishe jamani, hayo ni mambo ya kisayansi. Udumavu ni ukosefu wa chakula katika umri fulani hivi; chakula bora, ama lishe bora. Mimi mwenyewe nimeshabeba ndoo Mheshimiwa usiwe na wasiwasi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Justin Nyamoga, malizia mchango wako.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba niendelee kuchangia. Kwa hiyo, kuna

hiyo Kata ya Kimala, lakini pia kuna Kata ya Ukwega, Vijiji vya Mkalanga, Makungu, Uinome, Lukani, vyote hivyo bado havijafikiwa na vina miradi midogo midogo ya maji ambayo ningependa ikamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi ambayo inahitaji kukarabatiwa. Hii ni ile miradi unayokuta ina ukarabati, na nimeiona kwenye bajeti, nashukuru; mradi kama pale Kitoo, Mradi wa Ihimbo, Magana Ilindi na Mradi wa Kipaduka. Hiyo ni miradi ambayo ipo; na miradi ya kule mingi, kwa sababu vyanzo vinapatikana, kwa hiyo, siyo miradi mikubwa kwa sababu ni chanzo, halafu maji yake yanatumia *gravity,* ambapo kwa kawaida ukarabati wake siyo wa gharama. Kwa hiyo, napenda miradi yote ile iliyopo kwenye Jimbo la Kilolo iweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna mradi mkubwa. Ule mji wa Kilolo unakua na ninajua kwamba Mji wa Kilolo hauko kwenye miji 28. Miji hii ambayo wilaya zinaanzishwa ikiwa ni vijiji, inapokua kwa kasi halafu hatuweki miundombinu ya maji, kawaida baadaye tunapata shida ya maji. Kuna pendekezo limeletwa na *IRUWASA* la Mradi wa Mto Mtitu na limeshapokelewa kwenye Wizara yako; naomba mradi ule kwa sababu ni mkubwa na utakidhi mahitaji siyo ya Jimbo la Kilolo tu, unaenda pia kwa baadhi ya maeneo ya Jimbo la Kalenga na unafika hata katika Jimbo la Iringa mjini. Nasihi ule mradi uweze kuangaliwa kwenye Mfuko wa Maji ili uweze kufanya kazi katika maeneo hayo na wale watu waweze kutua akina mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba suala zima la kumtua mama ndoo kichwani ni la muhimu sana kwenye Jimbo la Kilolo kama nilivyosema. Nimesema kwa kuzingatia sana suala la maeneo yenye miinuko la milima na maji yanakuwa chini, ndiyo maana nilizungumzia kuhusu kupanda na kushuka kila siku; na nimeshangaa Mheshimiwa Naibu Spika, kama nawe ulibeba ndoo na ukaweza kuwa na kimo hicho, lakini kwetu sisi haifikii hivyo mara nyingi. Nami nasema utafiti ukifanyika, tumebeba sana maji, ndiyo maana tunakuwa hivi. Kwa kuwa sasa tuna

Waziri makini, nina hakika wananchi wa Kilolo hasa wale wa maeneo ya milimani wataungana nami kwamba baada ya kuacha kubeba maji na baada ya hili tatizo kwisha, tutakuwa nasi tunapata nafuu kidogo au ahueni hata ya kurefuka ili tuweze kuwa kama Watanzania wengine. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja ili hii bajeti iweze kupita na wananchi wa Kilolo waweze kupata maji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Hayo mengine, naona Mheshimiwa Neema itabidi atoe elimu kuhusu lishe, lakini kimo cha mtu kina uhusiano na chakula, lakini siyo sana. Ni kwa sehemu ndogo. Mimi acha ndoo tu, nimebeba mtungi na hauanguki. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi juu ya hilo. *(Makofi)*

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, atafuatiwa na Stela Fiyao na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ngara ninakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji. Kwa namna ya kipekee kabisa ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, kaka yangu Juma Aweso; napenda kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Maryprisca; napenda kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, *Eng.* Sanga kwa utendaji wao mkuu uliotukuka wa Wizara ya Maji. Kwa kweli tunawashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, napenda kuwashukuru viongozi hawa kwa kuridhia kuidhinisha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga Mradi wa Maji wa Ngara Mjini ambao pia utafikisha maji kwenye Kijiji cha Mkididili, Buhororo, Kumuyange, pamoja na Nyamiaga. Ninawashukuru sana kwa kuidhinisha hiyo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, napenda kuwashukuru Serikali ya Uingereza, Balozi wa Uingereza

pamoja na mtu anaitwa *Eng.* Lukas Kwezi, kwanza kwa kubuni mradi wa nyumba ni choo, lakini kwa kubuni mradi wa *RBF (Result-Based Financing)*. Kwa Jimbo la Ngara peke yake kupitia ubunifu wa hii miradi na ruzuku walizotupatia kama Taifa, tumepata takribani shilingi milioni 604 kwenye awamu iliyopita ya mgawanyo wa fedha za *RBF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwomba ndugu yangu *Eng*. Lukas Kwezi aendelee kuwa na ubunifu huu na kwa vile mradi huu unakaribia kufika mwisho, basi aweze kubuni mradi mwingine wa miaka mitano ili katika kipindi changu cha miaka mitano cha kuongoza Jimbo la Ngara niendelee kupata mgao kama huu kila mwaka ili niweze kuondokana na changamoto za maji zilizoko kwenye Jimbo la Ngara. Napenda pia kushukuru, nimeona ukurasa wa 154 orodha ya miradi iliyotengewa fedha na Wizara ya Maji kwa ajili ya Jimbo la Ngara, kwa kweli ninashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielekeze mchango wangu kwenye upande wa usimamizi endelevu wa rasilimali za maji. Waheshimiwa Wabunge waliotangulia hapo nyuma kabla yangu, wameeleza changamoto nyingi zilizopo kwenye usimamizi wa miradi ya maji. Nami naomba hapa Wizara ya Maji mnisikilize vizuri, nina uzoefu kwenye kutengeneza hizo *CBUWSO* ambazo ndiyo Kamati za Maji na kuzisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimuundo wa hizi *CBWSO* kuna tatizo la *social setup*. Maeneo mengine ni ngumu kutenganisha uongozi wa Kamati ya Maji pamoja na Uongozi wa Serikali ya Kijiji. Maeneo mengine utakuta Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina wa Kamati ya Maji wana undugu na Serikali ya Kijiji. Hivyo, hata kwenye uwajibikaji wao inakuwa ni ngumu. Hata mimi Mbunge siwezi kukubali Kamati ya Maji iwajibishwe wakati Kamati hiyo hiyo ukitaka kuiwajibisha ni kama vile unawajibisha wapigakura wangu walionichagua kwenye kile kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaomba Wizara ya Maji waje na *model* nyingine ya kusimamia miradi

ya maji vijijini inayoitwa *Franchise Model.* Sina Kiswahili cha jina hilo, lakini *Franchise Model* ni utaratibu wa kusimamia miradi ya maji kwa kuwapa mikataba watu binafsi au kampuni ziweze kuendesha ile miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hii nchi kuna *double standard* kama mjini kuna Watanzania na vijijini kuna Watanzania, halafu mjini zimepewa kusimamia maji kama *DUWASA* na *DAWASA,* halafu vijijini tumeachiwa sisi wananchi wenyewe tusimamie miradi yetu ya maji. Haya mambo hayakubaliki kwa sababu kama wanatuachia sisi wananchi hatuna mafunzo, hatuna wataalam, tunawezaje kusimamia miradi hii ya maji ambayo ni uwekezaji mkubwa, fedha ya Serikali inaingia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara ya Maji waruhusu *RUWASA* iweze kuwapa mikataba makampuni binafsi ama watu binafsi wenye uwezo wa kuendesha hii miradi ya maji. Ni rahisi kumwajibisha mtu binafsi, *pump* ikikataa kufanya kazi, bomba likikatika ama *tape* ikavunjika ni rahisi kwenda kumwajibisha mtu binafsi ama kampuni binafsi kuliko kuwawajibisha wananchi ambao ndio wasimamizi wa hiyo miradi ya maji. Hilo naomba lieleweke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielekeze mchango wangu pia kwenye kitu kinaitwa Mfuko wa Maji wa Taifa yaani *National Water Fund*. Maji unayoyaona tunayoyatumia yana sehemu mbili, ukishachukuwa maji ukayatumia, asilimia kubwa ya maji yanayotumika yanageuka kuwa maji taka yaani *waste water.* Maji taka haya ni yale tunayotumia vyooni, ni yale tunayotumia bafuni na asilimia 80 ya maji yote unayopeleka nyumbani yanabadilika na kuwa maji taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Taifa wa maji una jina ambalo haliakisi mnyororo mzima wa maji. Jina lake ni *National Water Fund,* nawaomba sana Wizara Maji mwende mkabadilishe hili jina kutoka *National Water Fund* kwenda kuwa *National Water Fund and Sanitation* yaani Mfuko wa

Maji wa Taifa na Usafi wa Mazingira. Hapo tutakuwa tumeakisi ile sehemu ya pili ya matumizi ya maji ambayo maji mengi yanaenda kubalika na kuwa maji taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji taka uwa tunayahifadhi vyooni hasa yale tunayoyatumia vyooni na tunayahifadhi kwenye *septic tank,* maji mengine ambayo ni maji taka ni yale yanayotoka jikoni. Tunavyoyahifadhi haya maji kwenye *septic tank* zile *septic tank* zina tumika na baadaye zinajaa. Ukienda ukachukua sampuli ya maji taka kwenye *septic tank* vyooni ukiyapima unakutana na virusi zaidi ya laki moja, unakutana na *protozoa* zaidi ya elfu 10, unakutana na *virus protozoa* pamoja na bakteria, wadudu wengi wako kwenye yale maji taka, ndio maana kuna umuhimu wa kuwekeza fedha kwenye usimamizi endelevu wa maji taka ili...*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashusha nondo na najua watanitafuta ili niwaongezee nondo. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kupiga makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee, yale maji taka yale kwenye maeneo ya mijini ambako kuna mifumo ya *sewerage* yaani ya sewer *system,* vyoo vile vinaunganishwa kwenye ile mifumo na yale maji yanaenda kutibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo ya miji inayokuwa hasa kwenye Jimbo langu la Ngara, Mji wa Rulenge na Mji wa Ngara Mjini hata hapa Dodoma, maji haya yapo kwenye *septic tank* yanahitaji kuchukuliwa na magari yanayokwenda kufyonza yale maji na kwenda kuyapeleka kwenye mifumo ya kuyatakasa ili maji hayo yanapotolewa kwenye ile mifumo yawe *pathogens free* yaani yasiwe na hao wadudu niliowataja na maji hayo hata tukuyaruhusu yakarudi ardhini yanakuwa hayawezi kuchafua maji yaliyoko chini ya ardhi yaani *underground water.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana naishauri Wizara ya Maji kubadilisha jina la Mfuko kutoka kuwa kwenye

Mfuko wa Maji wa Taifa kuwa kwenye Mfuko wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Taifa na matumizi ya fedha iliyoko kwenye huo Mfuko yaweze kuwekezwa kwenye kusimamia hayo maji taka ili tuweze kuondoa magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikia milipuko mjini ujue ni hayo maji taka yaliyosambaa. Ukisikia magonjwa kama kipindupindu na mengine ya kuhara ujue ni haya maji yameachiliwa, yametapakaa mijini yanaleta magonjwa kwa wananchi. Ndio maana siku ya leo nachukua fursa hii kuwaomba Wizara ya Maji na kuwashauri kabisa kwa namna ya kipekee, mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Maji na Usafi wa Mazingira, nimeshaanza kuuita hivyo, ziende kwenye maji safi na ziende kwenye kusimamia maji taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba Wizara ya Maji iwekeze kwenye mifumo ya kisasa ya kutibu maji taka inaitwa *Faecal Sludge Treatment System,* haina Kiswahili sijawahi kukisikia, lakini kuna mfumo mwingine unaitwa *Decentralized Waste Water Treatment System (DEWATS)*. Hii nayo

**NAIBU SPIKA:** Hiyo Mheshimiwa...

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, hii nayo haina Kiswahili chake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba hiyo ungekuwa umemwona Mheshimiwa Maige kabla angekupa tafsiri hiyo. *(Makofi)*

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia na kwenye kamusi sijaona, naomba unisamehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuchangia kwamba, Wizara ya Maji iwekeze kwenye kujenga hiyo mifumo ili katika sehemu nyingi katika nchi hii ambapo *septic tank* zinajaa, wananchi waweze kwenda kunyonya vyoo vyao na wapeleke maji taka hayo yaende kutibiwa kwenye hiyo mifumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba Wizara itakapoanza kutekeleza haya mawazo yangu, Jimbo langu la Ngara liwe la kwanza kupewa *allocation* kwa sababu hizi nondo nimezileta mimi na Wizara itakapoanza kufanyia kazi mchango wangu sisi jimbo la Ngara tuweze kupewa kipaumbele. *(Makofi)*

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruhoro kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka kumpa taarifa mzungumzaji hilo neno alilosema tiritimenti, kwa lugha ile ya kwetu ni *treatment.* Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, malizia sekunde thelathini.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mchango wake, sijui nini hiyo aliyoitoa nimeikataa, kwa sababu mimi ningemuambia ataje *Faecal Sludge Treatment System* asingeliweza kutaja, kwa hiyo naikataa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa, naomba mawazo yangu mawili hayo Wizara ya Maji iweze kuyachukua na iende ikayafanyie kazi hasa hili la kubadilisha jina la Mfuko wa Maji wa Taifa

**NAIBU SPIKA***:* Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** lakini vilevile na kwenye mifumo ya usimamizi endelevu wa miradi ya maji yaani Kamati za Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Fiyao atafutiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na Mheshimiwa Martha Maliki ajiandae.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fiyao sekunde chache upande wa Wabunge wa CCM, kwa sababu kuna nafasi mbili kuna Wabunge ambao waliandikwa hapa lakini nadhani bado wako kwenye uchaguzi huko na kwa sababu wale viongozi wanaotakiwa kuleta majina hawako hapa majina Wabunge wawili ambao wako tayari kuchangia leo walete majina yao halafu wakishakamilika mimi nitafunga hapa. Naona Mheshimiwa Husein ameshanyosha, bado mmoja.

**MBUGE FULANI:** Mheshimwa Naibu Spika, huku.

**NAIBU SPIKA:** Huku wapi sasa? Waheshimiwa ngoja hiyo nafasi moja nyie andikeni halafu atakayewahi atapata. Mheshimiwa Fiyao, endelea.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji, Mkoa wa Songwe pia umekuwa ni miongoni mwa mikoa ambayo imekumbwa na changamoto kubwa sana ya maji. Mkoa wa Songwe ni mkoa wenye kata 94 lakini kati ya kata zote hizo hakuna kata ambayo ina uhakika wa kupata maji. Hivyo changamoto hiyo imepelekea wananchi wa Mkoa wa Songwe kutumia muda wao mwingi sana kuhakikisha wanapambana kutatua changamoto ya maji kwenye maeneo yao.

Mheshimia Naibu Spika, naamini kabisa changamoto hii ya maji ikiweza kutatuliwa itaweza kuepusha migogoro mingi ya ndoa ambayo inatokea pasipo sababu za msingi. Pia changamoto hii ikitatuliwa endapo tutaweza kuondoa migogoro ya ndani ya ndoa tutaepusha pia changamoto

kubwa ya watoto wa mitaani ambao ni zao kubwa la migogoro ya ndoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba utekelezaji wa miradi ya maji umekuwa na changamoto kubwa sana na utekelezaji huu bajeti yake imekuwa ikitekelezwa kwa kiwango kisichoridhisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika,katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, fedha ambazo zilikuwa zimetengwa katika utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika miradi ya maji ni bilioni 913.83, lakini fedha ambayo ilikuwa imetolewa ilikuwa ni bilioni 230.99 tu. Jambo hilo lilisababisha utekelezaji wa miradi ya maji kutekelezwa kwa asilimia 25 tu na kutotekelezwa kwa asilimia 75, jambo ambalo pia linawakwamisha sana wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ilitengewa bilioni 623.6, lakini fedha ambazo zilikuwa zimetolewa zilikuwa ni bilioni 135.19, ambapo miradi iliweza kutekelezwa kwa asilimia 22 tu, hivyo tuliweza kufeli kwa asilimia 78, miradi ya maendeleo ya maji haikuweza kutekelezwa kwa asilimia 78 jambo ambalo tulifeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2018/2019, bajeti iliweza kutekelezwa kwa asilimia 15 tu na kwa mwaka 2019/2020, bajeti iliweza kutekelezwa kwa asilimia 61, lakini kwa mwaka 2021 bajeti iliweza kutekelezwa kwa asilimia 40. Jambo hili linatupelekea kukwama sana kwa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hiyo ya bajeti ndogo, kumekuwa na changamoto kubwa pia ambayo inapelekea kufeli sana hasa kwenye visima ambavyo tunachimba. Changamoto hiyo inasababishwa na upungufu wa wataalam wa kufanya tafiti kwenye maeneo yetu ili kujua ni wapi maji yanaweza kupatikana; kuna maeneo tumechimba visima maji hayajapatikana kabisa, hivyo ikapelekea kuonekana kama fedha tunatupa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti ya *CAG,* inaonyesha wazi kabisa kwamba kati ya visima 10,485 visima vilivyochimbwa visima 490 havikuweza kuwa na maji. Pia *CAG* alibaini wazi kwamba, kati ya fedha bilioni 768 zilizopelekwa kwa ajili ya uchimbaji wa visima ambazo pia baada ya visima hivyo kuchimbwa, visima hivyo havikuweza kuwa na maji, maana yake tukapelekea kuonekana kwamba tumetupa karibu ya kiasi cha Shilingi bilioni 764.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizi zinasababishwa na kutokuwa na watafiti wa kutosha katika maeneo yetu. Hivyo naishauri Serikali, tuna sababu kubwa ya kuwa na wataalam wengi wa kufanya tafiti kabla ya kuchimba visima vya maji ili Serikali tusiweze kuingia hasara. Tukifanya hivyo naamini tutaweza kufanikiwa katika suala zima la maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa ambayo pia imebainishwa na *CAG,* suala zima la madai ya Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira *(RUWASA),* imebaini kuwa karibu kiasi cha bilioni 12 wanaidai Serikali. Ili tuweze kufanikiwa katika miradi ya maji, tulipe haya madeni ambayo tunadaiwa na *RUWASA* ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kwa moyo kabisa. Tukifanya hivi naamini tutaweza kupunguza changamoto kubwa ya maji ambayo imekuwa ikiwakabili wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote naomba nizungumze wazi, nimesema hapo awali wananchi wa Mkoa wa Songwe ni wahanga wakubwa wa suala zima la maji safi na salama. Jambo hili limekuwa likipelekea wananchi wetu kuugua *typhoid* mara kwa mara kwa sababu maji wanayoyapata sio safi na salama, lakini bado hawapati maji ya kutosha maana yake hayohayo yasiyo na salama bado sio ya kutosha kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atuambie ni lini atatekeleza mradi wa maji kutoka Ileje ili uweze kuwakomboa wananchi wa Mkoa wa Songwe, waweze kuondokana na

changamoto kubwa ambayo imekuwa ikiwakabili katika kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Maliki na Mheshimiwa Hussein Amar ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amebeba dhana hii ya mahitaji ya maji kwa Watanzania na kwenye hotuba yake akaeleza kinagaubaga kwamba ataenda kusimama kuhakikisha Watanzania wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama niliwahi kusema hapa sio mzuri sana wa kusifiasifia, lakini huwa nasifia kwa sababu. Sasa naomba sana nimsifie Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo anapambana na wale wazinguaji, hongera sana. Pia Naibu Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya wakati amekuja kwenye ziara yake pale Hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Hai tulikuwa na watu wanaotuzingua sana kwenye zile Bodi za Maji walikuwa na utaratibu wao wamejiwekea, wanalazimisha wananchi kununua vifaa kwenye maduka yao, lakini alivyokuja pale alitoa tamko la Serikali na leo wananchi wa Hai wanafurahia, wananunua vifaa kwa bei ya soko na sehemu wanayoitaka, nipongeze sana kwa hilo. Nipongeze ziara ya Naibu Waziri pia ilinisaidia sana tukapata maji kule Rundugai. Sio hivyo tu nafahamu kwamba chanzo chetu ambacho kilikuwa kimesimama muda mrefu pale Kikapu Chini na chenyewe kimetengewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana pamoja na hayo mazuri machache ambayo wameyafanya ndani ya Jimbo la Hai, lakini bado tunayo changamoto kubwa ya maji. Wakati wa kampeni, Mheshimwa Hayati Dkt. Pombe John

Pombe Magufuli, aliwaambia watu wa Hai wakati anaomba kura, mmenifunga kwa kipindi cha muda mrefu, naomba nileteeni Saashisha na Madiwani wake mnifungue niwaletee maji. Sauti hiyo bado ipo kwenye mwangwi wa masikio ya watu wa Hai, pale Jimbo la Hai tunashida ya maji sana nadhani na sisi tunapaswa kuingizwa kwenye maajabu ya dunia, kwa sababu tunavyo vyanzo vya maji vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlima Kilimanjaro unatiririsha maji mazuri ya kunywa lakini tunalia kwamba Jimbo la Hai hatuna maji. Chini wataalam watatuambia tuna maji ya kutosha, lakini hatuna maji, hususani kata za tambarare, kuanzia Kata ya KIA, Muungano, Bondeni, Boma Ng'ombe, Weruweru, Rundugai, mpaka Mnadani hakuna maji; nazungumza hakuna maji kabisa na Mheshimiwa Waziri anajua. Tunafahamu kulikuwa na jitihada mradi mkubwa wa Serikali wa kupeleka maji Arusha, nikawaomba jamani huwezi kupeleka maji Arusha ukaacha watu wa Hai hawana maji, kuna visima 18 vinachimbwa ndani ya Wilaya ya Hai, lakini vinapeleka maji Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapenda sana ndugu zetu wa Arusha, lakini nashukuru nilizungumza na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Arusha akaniahidi kwamba vyanzo vile vya maji vitapitisha maji pale Hai. Hili ni jambo la sera ya maji kwamba maji yanapogundulika yanaanzia basi wale wanufaika wapate maji. Niiombe sana Serikali pamoja na kwamba najua ni gharama kubwa kuyaleta maji pale lakini chanzo hiki kitumike watu wa Bomba Ngombe na KIA waweze kupata maji, maana hii ndio changamoto kubwa tuliyonayo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho lingine ambalo tunaweza kutumia tuna chanzo cha hakika na kimeshafanyiwa upembuzi yakinifu, thamani yake ni bilioni 3.5. Hii Serikali ya mama Samia Suluhu ina hela, tunaomba watusaidie pale fedha za kutosha. Nafahamu jitihada ambazo wamefanya wametutengea milioni 500, milioni 500 kwenye bilioni tatu bado ni ndogo. Niombe sana kama inawezekana kwa *level* ya Wizara tafuteni mkandarasi,

chanzo hiki kianze kujengwa, tuna shida kubwa ya maji na kwetu kukosa maji wakati tunaona Mlima Kilimanjaro pale na tunaona vyanzo kibao vya maji kwa kweli ni aibu niombe sana Mheshimiwa Waziri atusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tunazo Bodi za Maji pale. Bahati nzuri baada ya ziara ya Naibu Waziri tulifanya vizuri sana, tukarekebisha zile bodi. Niombe zile bodi zinaweza kulelewa vizuri na zikafanya vizuri sana. Kihistoria tumeanza nazo tangu tukiwa watoto. Kwa hiyo niombe Waziri asiziguse sasa hivi kwa sababu zimeanza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine niombe, wakati Mamlaka ya Maji Wilaya ya Hai haijaanzishwa tulikuwa na mali zetu na hapa nilizungumza na Waziri, naomba nirudie tena kusema, tuna mali zetu zilipelekwa Mamlaka ya Maji Moshi Mjini, pesa taslimu milioni 357 na ushee, lakini kulikuwa na madeni ya milioni 300 ambayo waliambiwa wakakusanye, kulikuwa na magari sita, kontena ambalo lilikuwa na vifaa vya watu wa Hai vyenye thamani ya bilioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine niombe, wakati Mamlaka ya Maji Wilaya ya Hai haijaanzishwa, tulikuwa na mali zetu. Na hapa Waziri nilizungumza na wewe, naomba nirudie tena kusema; tuna mali zetu ambazo zilipelekwa Mamlaka ya Maji Moshi Mjini; pesa taslimu milioni 357 na ushehe. Kulikuwa na madeni ya milioni 300 ambayo waliambiwa wakakusanye; kulikuwa na magari sita; kulikuwa na kontena ambalo lilikuwa na vifaa vya watu wa Hai vyenye thamani ya bilioni 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali itujereshee vitu vyetu, hizi ni hela za watu wa Hai na Siha ambazo waliweka ili ziweze kuwahudumia kwenye eneo la maji. Na nina wasiwasi na hizi fedha kama kweli bado zipo, kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha hapa utuambie hizi fedha zetu tutazipata lini. Kwako siwezi kushika shilingi kwasababu wewe na Naibu Waziri mmetusaidia sana watu wa Hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninataka nichangie; hivi karibuni tumepata mafuriko makubwa ndani ya Jimbo la Hai. Mafuriko haya yamesababisha maafa makubwa; tumepoteza ndugu zetu watatu, na nyumba karibu 1,500 watu wamekosa sehemu ya kuishi, kwa hiyo, sasa hivi kule tuna njaa haswa. Tunashukuru Serikali imetupelekea chakula lakini bado wananchi tathmini ya mazao yao na vitu vingine vilivyoharibika havijaguswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye eneo la maji tuna vyanzo ambavyo vimeharibika na hakuna maji kabisa. Mto wa Nau ambao ni chanzo cha maji hakuna maji kwasababu kimeharibiwa na mvua; Mto wa Semira chanzo kile cha maji kimekufa; Mto Alonzo chanzo cha maji kimekufa; Makoa chanzo hiki kimekufa; pale Kalali tuna chanzo chetu cha maji na chenyewe kimekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana wananchi wanalia, shule za sekondari pale Msufini hakuna maji, pale Kalali hakuna maji, shule nyingine za *Machame Girls* na shule kubwa hizi zote hakuna maji kwasababu vyanzo vile vya maji vimeharibika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na miundombinu hapa katikati ukiachilia kule kwenye vyanzo vya maji na vyenyewe vimeharibila kwasababu ya mvua hizi. Kwa hiyo, niombe sana Serikali iingilie kati iturejeshee maji. Ukanda huu wa juu hakuna maji, kule chini hakuna maji, lakini kama nilivyosema vyanzo vya maji ni vingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni shauri, ni kwa faida ya nchi si kwa Jimbo la Hai tu. Hapa tuna mahitaji ya maji lakini vifaa vya kusababisha tupate maji ni ghali mno; tuone namna ya ku-*regulate* bei za hivi vitu kwa kupitia ruzuku, watu watuletee vifaa vya kuchimba kisima na mitambo hii ili tuondoe tatizo hili kwa *level* ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Martha Mariki, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Amar, Mheshimiwa Jerry Silaa ajiandae.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni ya leo katika Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini kipekee sana, ninampongeza sana Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wetu wa Maji na dada yangu, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, kwa jinsi wanavyoendelea kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mpanda ni mji ambao upo katika Makao Makuu ya Mkoa wetu wa Katavi. Mji huu wa Mpanda una fursa nyingi sana zikiwemo fursa za kilimo, kiutalii na kimadini. Lakini Mji wetu huu wa Mpanda una changamoto sana ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naiomba sana Serikali kwanza kwa kuipongeza kwa jinsi ambavyo wameonesha jitihada zao katika kuhakikisha Mji huu wa Mpanda unakwenda kupata maji ya uhakika ili kuweza kuwakomboa wananchi wake. Naishukuru sana Serikali kwa kutuletea Mradi wa Ikorongo Na. 01, lakini wakaona haitoshi, Mradi wa Ikorongo Na. 01 ulivyokuwa hautoshelezi kwa maji wakatuletea Ikorongo Na. 02. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali kupitia Waziri wa Maji, ije ifanye ziara katika Mkoa wetu wa Katavi ili iweze kuangalia, je, hizi pesa Serikali ilizozitenga na kupeleka fedha hizi katika Mkoa wetu wa Katavi, je, *value for money* ipo katika miradi hii ya maji? Maana kumekuwa kuna ubabaifu, wanafunga mabomba maeneo mengine maji hayatoki, lakini baadhi ya mabomba yamekuwa yako chini ya kiwango yanapasuka na hivyo kupoteza fedha nyingi sana za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe sana kaka yangu, Mheshimiwa Jumaa Aweso, aje katika Mkoa wetu wa Katavi kuhakikisha kwamba anafanya ziara ili aweze kwenda kushughulika na wale wote wanaokwenda kucheza na pesa za Serikali. Hususan tukiangalia kabisa maji ni uhai na wananchi wa Mkoa wa Katavi wengi wanahitaji maji ili tuweze kufikia ile azma ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; niiombe sana Serikali kwa kuwa imeleta miradi mbalimbali ya maji katika Mkoa wetu wa Katavi na maji hayo yameonekana hayatoshi, niwaombe sana Serikali kipo chanzo cha uhakika sana cha Ziwa Tanganyika. Na kutoka Mji wetu wa Mpanda mpaka lilipo Ziwa Tanganyika ni sawa na kilometa 120. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo niiombe sana Serikali kutoa maji katika chanzo cha uhakika ambacho ni Ziwa Tanganyika ili kwenda kumkomboa mama kwa kumtua ndoo kichwani. Mama zetu wamekuwa wakipata taabu sana katika Mkoa wetu wa Katavi kuhangaika kutafuta maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo sasa jamani ni wakati wa kumuaminisha mama wa Mkoa wa Katavi na wa Tanzania kwa ujumla kwamba Serikali yetu Sikivu inayoongozwa na mama yetu Samia Suluhu, kwamba yukotayari kuwatua ndoo kichwani akinamama wa Mkoa wetu wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Jumaa Aweso, akinamama wa Mkoa wa Katavi wanalalamika sana wenyewe ndio wamekuwa wahanga wakubwa wa kubambikiziwa *bills* zinazotokana na maji. Niwaombe sana Wizara ya Maji ikiwezekana kwa nini tusitumie utaratibu kama wa luku; kama luku, mtu anakwenda ananunua *units* zake anatumia umeme na anakuwa habugudhiwi na mtu ni kwa nini tusifanye utaratibu huu katika suala la maji? Mtu anunue *units* zake za maji atumie maji, zinapokwisha zikate ili kuondokana na usumbufu wa watu kubambikiziwa bili kubwa za maji ambayo

hawajayatumia. Maana kumekuwa kuna maeneo mengine unakuta maji hayajatoka hata miezi miwili lakini bado bili za maji zinakuja, sasa bili hizi zinatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri akashughulike sana na watendaji kwani watendaji wamekuwa wakikwamisha sana Wizara hii ya Maji. Kaka yetu, Mheshimiwa Jumaa Aweso, amekuwa akijitahidi sana na Wizara hii ni ngumu kwa kweli, Wabunge wote tunafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Jumaa Aweso akashughulike na watendaji katika Wizara ya Maji kuanzia ngazi ya mkoa, akaangalie kule changamoto ni nini kinachokwamisha. Serikali imekuwa ikitenga pesa, inapeleka pesa lakini bado maji yamekuwa yakikwama katika maeneo mengi, wananchi wake hawapati maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana dada yangu, Mheshimiwa *Eng.* Maryprisca Mahundi na Mheshimiwa Waziri. Niwaombe sana muendelee kuchapa kazi, msife moyo, tunafahamu Wizara hii ina changamoto nyingi lakini kwa kuwa ninyi mama yetu Samia Suluhu amewaamini na amewaweka hapo, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu mzidi kutatua changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Jumaa Aweso; kwa kuwa Mji wetu wa Mpanda ambao uko katika Mkoa wa Katavi hivyo katika miji ile 28 itakayokwenda kunufaika, niwaombe sana Mji huu wa Mpanda tunahitaji maji, ni mji ambao una fursa nyingi sana za kibiashara, mji ambao unakusanya watu wengi sana wanaohitaji kufanya mambo ya kibiashara katika mji wetu. Niwaombe sana tupate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Katavi tuko chini ya miguu yenu, tunawaomba sana mtuangalie katika hiyo miji 28 jamani na sisi mtupe

kipaumbele. Mji wetu umesahaulika kwa muda mrefu, Mkoa wetu wa Katavi umekuwa nyuma kwa mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe katika suala la maji wananchi wa Mkoa wa Katavi tunawaomba sana mtuangalie katika ile miji 28 itakayonufaika na mradi kutoka India basi na sisi mtupe kipaumbele ili twende kuendelea na uzalishaji wa mazao, mambo ya kiutalii ambayo yako katika Mkoa wetu wa Katavi. Suluhisho ni kupata maji ili wananchi wale waendelee kuchapa kazi na kuongeza pato katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii, naunga mkono hoja, naomba tupitishe bajeti ya Wizara ya Maji. Ahsanteni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Amar, atafuatiwa na Mheshimiwa Jerry Silaa, Mheshimiwa Jumanne Sagini ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Lakini kwanza naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema pamoja na Wabunge wote pamoja na watumishi waliopo kwenye jengo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Waziri wa Wizara hii ya Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi pamoja na Katibu wa Wizara, *Engineer* Sanga, na watendaji wengine wote. Kwa kweli wanafanya kazi vizuri, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi nizipeleke kwa Mheshimiwa Waziri, aliwahi kufanya ziara kwenye jimbo langu akiwa Naibu Waziri na ziara ile imezaa matunda na huu mradi ambao ulikuwa umekwama takribani miaka mitano unakwenda kukamilika; hongera sana Mheshimiwa Waziri.

Kwa nini nampongeza; alivyokuja kule aliwatia pingu wale wakandarasi na kasi ikaongezeka; hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Naibu Waziri amefanya ziara hivi karibuni na kuona mradi wetu ulipofikia na akatia hamasa, na kuna fedha ilikuwa imepungua kidogo ameahidi kuipeleka ndani ya mwezi huu. Na *Inshallah* kufikia mwezi ujao mradi huu unakwenda kukamilika katika vijiji 12; hongera sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie machache sana. Mradi huu unakwenda kukamilika lakini wananchi walio wengi wa Jimbo la Nyang'hwale ambako umepita huu mradi wanahitaji sana kuvuta huduma ya maji kwenye majengo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha ajabu, gharama za uvutaji wa mabomba hayo kuingiza ndani ni kubwa. Kiwango cha chini ni kuanzia laki tatu mpaka laki nane na ni mita kama kumi tu lilipo bomba lile kuingiza ndani, mtu anachajiwa laki tatu; watu wa vijijini watapata wapi shilingi laki tatu kwa ajili ya kuvuta maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ijaribu kuangalia gharama hizi waweze kupunguza ili wananchi walio wengi waliokuwa na hamu ya kutumia maji ya Ziwa Victoria waweze kuvuta maji waweze kuyatumia ndani ili waweze kufaidika na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika mradi huu wa vijiji 12, nina kata 15 na nina uhaba mkubwa sana wa maji kwenye jimbo langu. Je, Wizara ina mpango gani sasa wa kusambaza maji kwenye Kata zifuatazo; Nyugwa, Nyijundu, Busorwa, Kaboha, Shabaka, Nyang'hwale, Nundu, Mwingilo, Hafita na Nyabulanda? Maeneo yote yale yana uhaba wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa bahati nzuri mradi huu ulikuwa na thamani ya bilioni 15, kwa usimamizi mzuri wa Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri Aweso, tumeweza

kubakiza chenji zaidi ya bilioni tatu. Kwa nini hizo bilioni tatu zisiwekewe sasa utaratibu ulio mzuri kuanza kuweka utaratibu wa kuweza kupeleka baadhi ya hizo kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nakuomba, mradi huu ili tuweze kuufaidi mradi huu vizuri ninaomba sana Meneja wa *RUWASA* awe karibu na wananchi. Kwasababu leo hii Meneja wetu wa *RUWASA* wanamtafuta wananchi ili waweze kwenda kufanyiwa tathmini ya kuvuta mabomba majumbani mwao, ile ofisi inakuwa wale watu hawapatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Meneja wa *RUWASA* – ninamsifu kwa kazi yake nzuri – awapokee wananchi wangu, awaambie gharama na ikiwezekana awape muda maalum kwamba ukilipia leo hii baada ya siku fulani maji utayapata. Lakini majibu yamekuwa hayaeleweki, bei zinakuwa ni kubwa lakini hawapewi muda maalum wa kwamba utakapolipa ni muda gani utapata maji; naomba hili lichukuliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata asubuhi niliuliza kwenye swali la nyongeza, nilitoa ushauri kwamba kwa nini Wizara isiweke mfumo kama wa *TANESCO* kufunga mita za kutumia luku ili kupunguza hii sintofahamu na kutengeneza mazingira ya rushwa. Nitatoa mfano; leo hii Dar es Salaam, kila wanapopita wasomaji wa mita lazima kila mwezi nitume mtu wa kwenda kurekebisha. Unaambiwa 180,000 lakini akienda mtu kule kurekebisha anaambiwa kuna makosa ya kiuandishi tunapunguza gharama unalipa kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Dar es Salaam tufanye mfano ina watumiaji wa maji labda 1,000, wasomaji wa mita wako watano, kwa nini wasifanye haya makosa? Lakini mtakapotumia huu mfumo ambao ni wa kufunga mita ambazo mtu anatumia kutokana na mahitaji yake, akiwa na shilingi 1,000 anunue 1,000 akiwa na 10,000 anunue 10,000 na akiwa hana inakata kuliko haya masuala ya kila mwisho wa mwezi wanapita wasomaji wa mita, wanakuwa

wanachoka. Anakwenda chini ya mti anatafakari tu hii nyumba tuiandikie ngapi anaandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hili linafanyika na ni mhanga mmoja wapo. Huwa ninalipa bili ya shilingi 50,000 mpaka 60,000 lakini unakuta inaandikwa mpaka shilingi 200,000, ukituma mtu anakwenda kurekebishiwa; hii ni sehemu yangu moja, je ni watu wangapi ambao wanapata shida kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii inajenga mazingira ya rushwa pia. Mtakapofunga hizi mita haya mazingira yaliyopo hayatakuwepo, hata zile foleni za watu kwenda pale kwenye Wizara ya Maji kurekebisha bili zao hazitakuwepo. Chukueni mfano huo upande wa *TANESCO,* leo hakuna foleni kwenye masuala ya ulipaji, mtu ananunua luku kulingana na uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba myachukue haya mawazo yangu myafanyie kazi, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jerry Silaa, atafuatiwa na Mheshimiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini, Mheshimiwa Nicodemas Maganga ajiandae.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu, kwanza kipekee kuipongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso; Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi na watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, *Eng.* Sanga na mwanamama machachari Naibu Katibu Mkuu, *Eng.* Nadhifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuseme kwenye Wizara hii kazi kubwa imefanyika. Serikali imefanya kazi kubwa ya kufanya utambazaji wa maji kwenye nchi yetu. Na wote

mmesikia kwenye hotuba kwamba malengo ya kusambaza maji vijijini kwa asilimia 85 kufikia 2025 mpaka kufikia mwezi Machi tayari asilimia 72.3 maji yamesambazwa. Lakini malengo ya kusambaza maji mijini tumefikia asilimia 84; tunaipongeza sana Wizara ya Maji kwa kazi kubwa waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niipongeze Serikali, zaidi ya shilingi bilioni 200 zimewekezwa katika kazi ya kusambaza maji safi na salama kwenye Mkoa wa Dar es Salaam. Lakini iko miradi mingi mikubwa; upo ule mradi wa Arusha, zaidi ya shilingi bilioni 520; upo Mradi mkubwa wa Tabora – Igunga – Nzega, zaidi ya bilioni 600; lakini iko miradi ile ya miji 28 ya zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 500, kazi kubwa sana imefanyika kwenye sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye wanufaikaji wa miradi hii na Jimbo la Ukonga ni wanufaikaji. Sisi kwa miaka yote tulikuwa tukipata maji toka Ruvu chini, maji ambayo yalikuwa mpaka yapite katikati ya Jiji la Dar es Salaam yapandishe Mlima wa Magereza – pale Magereza kulikuwa na mashine ya maji – yaje mpaka Gongo la Mboto – pale Gongo la Mboto kulikuwa na mashine ya maji, na mtafahamu Jimbo la Ukonga lina asili ya Milima ya Pugu mpaka Milima ya Kisarawe kwa kaka yangu, Mheshimiwa Selemani Jafo. Na kwa kipindi kirefu tokea miaka tisini hatukuwahi kupata maji safi na salama ya bomba. Katika uwekezaji huu wa Serikali, Mradi wa Maji wa Ruvu Juu na Ruvu Chini imeboreshwa na uzalishaji umeongezeka kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini maji haya yalipofika Kibamba ukabuniwa mradi mwingine ukatoa maji Kibamba mpaka Kisarawe na Kisarawe imejengwa njia ya maji mpaka Pugu limejengwa tanki kubwa la lita milioni mbili na tayari mradi ule umezinduliwa, na hivi ninavyozungumza Jimbo la Ukonga linapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani kwa niaba ya wananchi wa Ukonga, Mheshimiwa Waziri alifika, alikuja na Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais kuzindua

mradi ule; tunawashukuru sana. Na *DAWASA* kupitia Mhandisi Cyprian Lwemeja, wanafanya kazi kubwa ya kuendelea kusambaza maji yale kwa uwezo wao wa ndani. Tayari kazi ya *transmission* imekamilika na hivi wmaeshapata fedha wanaanza kazi ya *distribution.* Sisi tunaamini katika malengo ya 2025 tutakuwa wa kwanza kuyafikia kabla ya wakati na maji yatasambaa kwenye Jimbo la Ukonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mpaka kufikia mwezi huu Aprili, fedha za maendeleo zilizopokelewa ni asilimia 54.1. Katika fedha zilizopangwa za Mwaka wa Fedha 2020/2021 mpaka kufikia mwezi huu wa Aprili ni asilimia 54.1 tu ndiyo zimepokelewa na Wizara. Imebaki miezi miwili, siamini kwamba kufikia mwisho wa bajeti hii Wizara ya Maji itakuwa imepata fedha zote za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Wizara hii isipopata fedha maana yake maombi yote uliyoyasikia hapa Waheshimiwa Wabunge wakiyaomba, miradi yote ambayo umeisikia inaendelea kwenye majimbo yote ndani ya Bunge hili haitakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wenzetu wa Wizara ya Maji ni waombaji kama sisi tunavyoomba, inapokuja hapa bajeti kuu ya Serikali naomba tusimame tuseme Wizara hii ipatiwe fedha za kutosha. Pia isipatiwe tu fedha kwa maana ya kuzitenga kwenye bajeti lakini na fedha zenyewe zipelekwe tena kwa wakati ili miradi ya kuwasambazia maji Watanzania iweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie pia ama kuongezea pale alipochangia Mheshimiwa Anne Kilango Malechela, miradi ya maji hasa vijijini ukiondoa hii ya mijini ambayo inasimamiwa na Mamlaka ni kweli inagharimu fedha nyingi. Niungane na mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango, Wizara ya Maji, *RUWASA*, Menejimenti ya *RUWASA* na *DG* yupo hapa nadhani anasikia, Clement anafanya kazi nzuri kujenga taasisi hii mpya na changa iliyoanzishwa muda mfupi uliopita, mjitahidi mtengeneze mfumo utakaofanya wale akina Ali

Mabomba waliokuwa Same waweze kupatikana kusimamia miradi hii nchi nzima. Itakuwa ni kichekesho kutengeneza miradi ya thamani kubwa ya mabilioni ya shilingi lakini kuiacha kwenye mikono ya watu ambao hawana utaalamu, lakini hawana usimamizi wa kitaalamu chini ya taasisi yetu hii ya *RUWASA.*Ni vyema tukajipange na hili litawezekana kama Wizara hii itakuwa na fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kusisitiza *RUWASA* kutengeneza utaratibu wa kuwa na wataalam wa kutosha kusimamia miradi lakini nitaendelea kuliomba Bunge lako na tutakutana tena hapa kwenye bajeti kuu ya Serikali kuendelea kuitaka na kuishauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya maji ili utendaji huu uliotukuka tunaouona wa Waziri wetu Mheshimiwa Jumaa Aweso uweze kwenda kwa vitendo akiwa na fedha za kulipa makandarasi wanaofanya kazi kule chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jumanne Sagini atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii ambayo kwa kweli ni kama ya nyota ya jaha baada ya wale wawili uliowataja kutoonekana hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuungana na Wabunge waliopita kuipongeza Wizara ya Maji na Serikali kwa ujumla kwa namna wanavyofanya kazi. Mheshimiwa Aweso na Naibu wako mnaitendea haki Wizara hii. Nami niwaombee kwa Mungu muendelee kuwa na afya njema mchape kazi ili hatimaye malengo ya upatikanaji wa maji wa asilimia 90 mjini na asilimia 80 vijijini yaweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maji, nami niungane na wajumbe

waliokwishachangia Wizara hii inahitaji fedha za kutosha. Nimekaa TAMISEMI tulikuwa na uhusiano wa karibu na Wizara ya Maji, wakati mwingine twaweza kuwalaumu lakini wanajitahidi kufanya kazi, maana wao lazima wapate *consultant* awaonyeshe kwamba hapa pana maji halafu wapate *contractor* achimbe, changamoto huja pale ambapo *consultant* ameonyesha pana maji hapa halafu *contractor* anakuja kaambiwa chimba mita 90, anachimba mita 90 hapati maji. Nadhani ndiyo maana Wabunge wanalalamika kwamba yanakuwa ni mashimo wananchi hawapati maji na imekuwa ni vilio vya muda mrefu tangu kwenye vile visima kumi vilivyofadhiliwa na *World Bank* miaka kadhaa iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni kubwa ni utaalamu na wataalamu wa sekta hii ya maji. Mimi nataka niamini kwamba wataalamu wale hawatoshi na Serikali ifanye uamuzi wa makusudi hasa kwenye kipindi hiki ambacho wanatumia mfumo wa *force account* kuwa na wataalamu wa kutosha kutimiza majukumu ya Wizara hii, vinginevyo itakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona pale Butiama sina hakika kama wataalamu wanazidi wawili wale ambao ni *water engineers* (wahandisi wa maji), lakini wana wale mafundi michundo *(technicians)*, ambao ndiyo wengi lakini hawana uwezo wa kutelekeza miradi hii kwa utaratibu wa *force account* kwa sababu panahitajika na uzoefu wa namna fulani. Kwa hiyo, wakati tunazungumzia utekelekezaji huu bila kumwezesha nguvu kazi ya wataalamu itakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la ujumla ambalo nataka niliseme ni mfumo tu wa kuwaunganishia wananchi maji. Mimi hapa naomba nikiri kwamba *Engineer* Cyprian Luhemeja wa Dar es Salaam amefanya ubunifu mzuri sana ndiyo maana Dar es Salaam inafanya vizuri. Niliwahi kumuuliza kwa nini kasi ya upelekekaji wa maji kwa wananchi imekuwa kubwa, anasema yeye anatumia mapato yake ya ndani kununua vitendea kazi na kusambaza maji mpaka kwa

walaji. Kwa hiyo, gharama zile zinakuja kufidiwa baadaye kwenye *bill* za watumiaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huku wilayani wananchi wanatakiwa walipie vifaa, vifaa vyenyewe mara nyingi vinakuwa vya bei kubwa, wale wataalamu ndiyo wakanunue zaidi ya laki tatu, nne, tano, mwananchi wa kawaida kijijini kuzipata kwa mara moja inaweza ikawa ni changamoto. Kwa hiyo, tunapofika kwenye usambazaji Waziri atusaidie wajenge uwezo wa taasisi zao ziweze kugharamia vifaa hivi halafu wananchi wakatwe kidogo kidogo wanapolipia *bill* hizi za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye Mkoa wa Mara. Mkoa huu una wilaya zake kama nne zinazungukwa na Ziwa Victoria; Wilaya za Bunda, Musoma, Rorya na kwa kiasi fulani Butiama. Hata hivyo, ukiondoa Musoma Manispaa wilaya nyingine zote zilizobaki zina changamoto kubwa ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Butiama pale kwa Baba wa Taifa, Ikulu pale hawana maji ya uhakika. Ni bahati mbaya wakati fulani viongozi wa Wizara walikwenda hadi wakafanya sherehe ya kusaini mikataba ya utekelezaji wa mradi wa maji ya Mgango, Kyabakari, Butiama na vijiji vile zaidi ya 19 vitakavyonufaika lakini haukutekelezwa wananchi walibaki kushangaa. Namshukuru Mungu mwaka huu kwa kasi ya aina yake wame-*sign* na mkandarasi na vifaa tumeanza kuviona *site,* kwenye hili tunawapongeza sana Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu sisi watu wa Butiama ni vizuri mradi huu utekelezwe kwa kasi ya aina yako Mheshimiwa Waziri. Mimi naomba baada au kabla Bunge halijaisha twende tuone ile kasi kama inalingana na mpango kazi wa utekelezaji wa mradi ule kwa sababu bado wananchi wana mashaka, je, itakuwa kweli? Sasa kweli tupite kule yale mambo unayofanya maeneo mengine Mheshimiwa ufike pale ukohoe ili watu tuwe na imani kwamba kweli mradi ule utatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaomba mradi ule utekeleze kwa kasi kuna kata zinazoambaa na Mto Mara na Ziwa Victoria hasa pale Nyabange hawana maji ya uhakika. Ukienda Butiama hawana maji wakati wanaulinda Mto Mara. Mmesea vizuri kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri kwamba kila mwaka tunaadhimisha Mto Mara na sherehe hizo hufanyika Butiama lakini vijiji hivi vinavyokulindia Bonde la Mto Mara havina maji. Hizi kata zote nne za Bwiregi, Namimange, Buswahili, Silolisimba, zinapakana na Mto Mara lakini hawana maji kabisa, haieleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunafarijika kama Taifa kwamba maji ya Ziwa Victoria sasa yanaelekea kuja Dodoma maana tayari yapo Igunga na Tabora Mjini wanasema pameshapata ni zaidi ya kilometa 500 lakini wale wanaopakana na Ziwa Victoria *zero* kilometa hawana maji. Hatuna roho mbaya, lakini haipendezi kwa watu wanaokulindia chanzo hiki kukosa maji kwa muda wote huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi mingine ikiwemo mikubwa hii ya kitaifa na hata ile ya visima, ni ushauri wetu taasisi zenye watu wengi kama shule tuhakikishe angalau tunapoweka miradi hii iwe karibu na hizi shule. Haipendezi shule ina watoto 1,000 au 2000 hawana chanzo cha maji kwenye maeneo ya shule na wakati huo tunaambiwa kuna magonjwa mengi yanayosababishwa na utumiaji wa maji yasiyofaa. Tuna shule nyingi za sekondari, shule za msingi wilaya ya Butiama na wilaya zingine lakini hazina maji.

Ni ombi langu wakati tunatekeleza miradi hii ambayo tunashukuru Mkoa wa Mara na Wilaya ya Butiama imepata vijiji kadhaa tukumbuke kuliko na taasisi za elimu hizi ziweze kupata maji mfano vituo vya afya, zahanati na hospitali ziweze kupata maji ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneo hayo, naomba niunge mkono hoja na niwatakie utekelezaji mwema wa bajeti hii. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa tena nafasi nzuri ya pekee niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, napenda nimshukuru Waziri, Mheshimiwa Jumaa Aweso, nilifanya naye ziara kwenye Jimbo langu siku saba zilizopita kutokana na swali ambalo nililiuliza hapa siku hiyo alikuwepo Naibu Waziri wa Maji dada yangu Mheshimiwa Maryprisca Mahundi. Nina furaha kubwa kwa niaba ya wananchi wangu wa Mbogwe, kwanza baada ya kumuona Waziri wa Maji anafika kwa wakati muafaka na akanipa ahadi nyingi ikiwemo gari kwa ajili ya wananchi wa Mbogwe kwa maana ya Meneja wa Maji wa Mbogwe. Cha kusema kikubwa mimi niwaombe tu Wabuge wenzangu leo nisingependa hata nione mtu hata mmoja anashikilia shilingi maana huyu Waziri ni mwaminifu sijawahi kuona Waziri mwaminifu namna hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Rais wetu, Mama yetu kwa ziara zile anazoendelea nazo huko nje. Sisi kama Wabunge tunampa *support* asilimia mia moja. Tukio lililotupata mwaka huu lilikuwa kubwa sana na mataifa yalitegemea kuona sisi tunaanguka lakini kwa uwezo na nguvu za Mungu mpaka sasa hivi tunajadili bajeti na mipango yetu kama watu wenye akili timamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, nitumie nafasi hii kushauri, Katiba inasema mimi ni mtunga sheria lakini vilevile nimshauri wa Serikali. Pamoja na pongezi zote kwako Mheshimiwa Waziri nikutie moyo, kuna watu wengi kweli unaenda unawaelimisha pengine walikuwa hawajui majukumu yao, ikiwemo watendaji wako wale wa chini kwenye halmashauri huko wilayani, kuwapa maelekezo mazuri ili kusudi wawe karibu na wananchi na wananchi kiukweli wanaimani kubwa sana na awamu hii. Kwa hiyo, kwa vile umeniahidi mimi vitu vingi na mimi nikuahidi tu, kwanza miradi ile mikubwa ikianza kukamilika pale kwenye Jimbo

langu nitaandika jina lako Jumaa Aweso ukumbukwe hata kama siku umekufa kwamba palikuwa na Waziri Awamu ya Sita alikuwa anaitwa Jumaa Aweso. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine sasa hivi mimi naishi hapa Dodoma kwa nguvu za wananchi wa Mbogwe. Nipende tu kumsaidia Mbunge wa hapa Dodoma haipendezi sana tupo Makao Makuu halafu tunakuwa hatuna maji, nyumba zetu tunajenga tunaweka ma-*simtank,* kwa kuwa wewe ni Waziri wa nchi nzima ukimaliza basi kwenye majimbo yetu yale ya Kanda ya Ziwa ufanye juu chini kama unavyofanya ili na Dodoma hapa tupate maji hayo ya mradi mkubwa wa Ziwa Victoria. Maana maji yetu kule ni mazuri halafu huku tunatumia maji yenye chumvi. Sura yangu mimi nilikuwa mzuri sana sikuwa na sura ya hivi, ninarudi nyumbani tena nikiwa na sura nyingine. Kwa maana hiyo nikuombe ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde tusaidiane tu kuwa tunamkumbusha Waziri wetu ili na hapa tuweze kuupata huo mradi mkubwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi kwa vile natoka Geita, sasa tuna wilaya tano, mwenzangu amezungumza pale, ni vyema wilaya zetu ambazo zipo karibu na Ziwa Viktoria zipewe huo mradi wa maji mkubwa ili kusudi wananchi wa kule waweze kufaidika na maji yao ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwaombe tu hata Wabunge wenzangu, nina imani kuna Wabunge wengine baada ya kuchaguliwa hawarudi majimboni kutazama shida za wananchi, tusije tukapata tena kazi ngumu 2025 kukawa na jimbo halina maji tena tukaanza tena kampeni zile za kutumia nguvu sana. Maana wananchi tuliwaahidi kwamba watakuwa na maisha mazuri, tutawapa huduma za maji pamoja na mambo mengine lukuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe Wabunge wenzangu tuwe tunamkumbusha Mheshimiwa Jumaa Oweso ni mtu mzuri sana na atatusaidia tu na nina imani naye maana nimeona kwa vitendo, kuna bilioni karibia

50 mradi mmoja ambao ulikuwa unaenda Katoro, alimpongeza hadharani *Engineer* mmoja jina nimeshalisahau, kuna dogo mmoja hivi ni *Engineer* pale Geita alisema ameokoa bilioni karibia arobaini kitu. Kwa maana hiyo, wewe *brother* ni muaminifu na ungekuwa na tamaa kama watu wengine siwezi kuwataja hapa, wanaomtumikia shetani ina maana hizo ungepiga kimya tu na wala hakuna mtu angekusumbua, kama ni kesi ina maana ingeendelea mbele kwa mbele. *Brother* wewe ni muaminifu endelea kuwa na imani hiyo na Mungu atakusaidia mambo mengi na siku zako zitakuwa nyingi sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nikupongeze wewe mimi leo nina miezi sita hapa Bungeni, nilikuwa kiukweli sijui kabisa kuongea mbele ya watu wakubwa kama nyie hivi, wakiwemo Mawaziri ambao nilikuwa nawaona tu kwenye *screen* wakina Prof. Palamagamba Kabudi lakini sasa hivi kwa vile tunaonana vizuri sana. Niwaombe Mawaziri muige mfano kwake huyu Waziri Jumaa Aweso kwenye Wizara zenu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana toka tuanze kuchangia bajeti hapa kila mtu aliyeleta bajeti yake tunaipitisha, ni vyema sasa unapoipokea ile bajeti yako uwe na kumbukumbu kwamba nilipitishiwa bilioni 60 zimefanya kazi hivi hivi. Mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge tupate siku moja kuja kuwahoji hawa Mawaziri kwamba tulipitisha bajeti mwaka 2020 zilienda wapi? Kwa mawazo hayo tutaenda vizuri na wananchi wetu waliopo kijijini kuliko tu kila kitu tutasema ndiyo, ndiyo halafu vitu vyenyewe vinakuwa havifanyiki huko majimboni na vijijini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, wale watumishi wa Mungu mmenielewa lakini wale wenye roho mbaya na dhamira mbaya *message sent* mjipange. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nimekusikia.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru kwa michango mbalimbali ambayo mmeitoa baada ya hoja kuwasilishwa hapa. Kama mnavyojua Wizara hii ya Maji itaendelea kuchangiwa kesho na nafikiri inahitimishwa siku ya Jumatatu labda kama wachangiaji watakuwa wameisha. Wabunge ambao walikuwa wana udhuru hawajaweza kuchangia leo ni Mheshimiwa Joseph Musukuma na Mheshimiwa Miraji Mtaturu, watapata nafasi zao kesho.

Kuna Mbunge alisimama hapa akitaka mwongozo lakini kabla sijamruhusu kusema hilo jambo analotaka kulizungumzia labda nisisitize jambo moja ama mawili. Mheshimiwa Waziri wa Maji Wabunge wamesisitiza sana hapa kuhusu ankara za maji. Wakati tunasuburi mbadilishe mfumo wa kulipa pengine kabla mtu hajatumia ili kuondokana na huko kunakoitwa kubambikizwa bili nadhani mtengeneze utaratibu wa kutoa elimu kwa umma. Kwa nini elimu ni muhimu? Ni kwa sababu yale maji yanayotiririka mtu anaweza kuwa amefungua maji lakini anaosha glasi moja, anatumia lita mbili. Sasa mpaka aje amalize glasi sita hizo ni lita nyingi, kwa hiyo, akija kuletewa *bill* atasema mimi niliosha glasi sita tu. Vivyo hivyo, mtu anafua nguo, anasuuza lakini anasuuza maji yakiwa yanaendelea kumwagika, lakini akielewa vizuri atafahamu. Sisi ambao tumetoka zile sehemu za kubeba maji kichwani huwezi kutumia ndoo nzima kusuuza shati moja.

Kwa hiyo, lazima Wizara kipindi hiki wakati mnasubiri kubadili mfumo mjielekeze pia kwenye elimu kwa sababu mna mpango wa kumtua mama ndoo kichwani sawa, lakini asitolewe ndoo kichwani halafu *bill* ikawa kubwa maji akawa anafungiwa kila wakati tena tukarudi pale pale. Kwa hiyo, ile huduma ya maji atakuwa haipati sawasawa kwa sababu atakuwa anadaiwa *bill* kubwa.

Pia Mheshimiwa Waziri jambo lingine lilosisitizwa hapa ni kuhusu miradi. Umetusomea bajeti nzuri sana, ina miradi mingi sana kila mahali lakini ukiangalia Wabunge hapa

wengine wanataja kata, mtu anataja kata tisa, mwingine anataja hadi vijiji kwamba vijiji vitatu vina miradi lakini vijiji kumi havina. Maana yake miradi iliyopo kwenye hivi vijiji ni midogo midogo haiwezi kuvuka kijiji kimoja ama haiwezi kuvuka kata moja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hapa wamechangia tunakoelekea, kwa sasa hivi inabidi twende hivyo kidogo kidogo, lakini Wizara lazima ijipange kwa ajili ya miradi mikubwa ambayo itakuwa na gharama kubwa lakini inatoa huduma sehemu kubwa zaidi. Kwa mfano, huu mradi unaotajwa wa Ziwa Victoria ni wazi unapita kwenye mikoa mingi. Unatumia fedha nyingi lakini eneo ambalo unatoa huduma pia ni kubwa kwa hivyo unapunguza gharama zile za uendeshaji wa hiyo miradi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninyi kama Wizara haya ni mambo ya muda mrefu. Kwa mfano, umetaja Nyasa, nilikuwa nafuatilia humu, Ziwa Nyasa lina maji mengi, hakuna sababu ya Ziwa Nyasa kutoa huduma kwa Jimbo la Nyasa halafu akasimama Mbunge hapa pengine wa Nyasa akaelezea namna ambavyo Nyasa imefaidika na Ziwa Nyasa wakati Ziwa Nyasa lingeweza kutoa huduma kwa mikoa yote iliyokaribu na hilo ziwa. Mtatumia gharama kubwa za uwekezaji lakini mtatoa huduma sehemu kubwa. *(Makofi)*

Nimeona humu pia umetaja mradi wa Mto Kiwira na mimi nikushukuru, lakini sasa mradi kama ule ni kati ya hiyo tunayoiita miradi mikubwa. Hapa umesikia mradi wa Ileje, umesikia Momba maji hayapo, Mbozi na Tunduma. Ile miradi mikubwa mfano ukiwekeza fedha nyingi Ziwa Tanganyika watatoa huduma Mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe. *(Makofi)*

Pia huu mradi wa Mto Kiwira vivyo hivyo, utatoa maji wilaya nyingi za Mkoa wa Mbeya na hivyo hivyo huko Ileje kunakotajwa, pengine hata huo mradi unaweza ukawa ni mdogo kuliko huo Mradi wa Kiwira. Kwa hiyo, mkiwekeza fedha nyingi kwenye mradi mkubwa hayo maji yatatumika sehemu kubwa pamoja na kwamba itatuchukua muda lakini

huo ndiyo uwe mwelekeo. Kwa sababu hata haya tunayolalamika kwamba kuna vijiji wanahitaji huduma mtakuwa na wafanyakazi wengi sana kuliko mkiwa na miradi mikubwa ambayo inapeleka hizo huduma kila mahali. Nadhani hilo nalo mlitazame ili pamoja na kwamba gharama zitakuwa kubwa lakini huko tuendako lazima tufike mahali ambapo tutakuwa na hiyo miradi mikubwa inayotoa huduma eneo kubwa kuliko kutoa sehemu ndogo ndogo.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo la wageni ambao wapo hapa jioni hii. Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni watumishi wa Hospitali ya Bugando kutoka Nyamagana Jijini Mwanza wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Dkt. Fabiani Massanga. Karibuni sana, naona amekuja peke yake. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni wa Mheshimiwa Charles Kajege ambao ni rafiki zake na huyu ni Ndugu Mohamed Mussa na Ndugu Othman Wadi kutoka Zanzibar, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ufafanuzi wa jambo moja, kuna wakati Wabunge wanakuwa wameona orodha zinazotoka kwenye vyama zinazoletwa hapa mbele halafu Mbunge anakuwa anahesabu wale Wabunge walioitwa hapa kuchangia anaanza kulalamika kwamba nilikuwa namba moja mbona nimeitwa wa watatu, mbona sijaitwa bado. Mtagundua ndiyo maana Wabunge wakisimama huwa wanaanza kwanza kwa kushukuru kwa kupewa fursa ya kuzungumza; ni mpaka ukiitwa ndiyo zamu yako inakuwa imefika, siyo orodha ile iliyoletwa hapa kwa sababu inaweza ikaletwa hapa orodha watu wakawa wanaudhuru, ana mgonjwa, ana safari anaenda jimboni kwake kuna mafuriko, lazima huyo apewe fursa wewe unaweza ukapewa fursa hata ya kuchangia kesho. *(Makofi)*

Kwa hiyo, yale mamlaka mliyotupa Waheshimiwa Wabunge tunayatumia kadri tuwezavyo kuwapa nyinyi huduma ile mnayostahili. Kwa hiyo, msione mahali labda umechelewa kuchangia unalalamika mbona nilikuwa

watatu, maana hapa kuna vyama vingi pia unaweza kuwa ulikuwa watatu kwenye orodha ya chama chako lakini wapo pia Wabunge wa vyama Vingine lazima waingie hapo. Kwa hiyo, hakuna nia mbaya Waheshimiwa Wabunge tuelewane katika hilo na usishike sana ile namba yako mpaka utakapoitwa ndiyo maana huwa tunaita mengi ili mtu ajiandae kwamba na yeye yupo.

Waheshimiwa Wabunge, leo kuna Iftari ambayo imeandaliwa na Mheshimiwa Spika wetu. Niliwakumbusha asubuhi niwakumbushe tena, tukitoka hapa baada ya kuahirisha shughuli za Bunge tutaelekea lile eneo la maegesho kwa ajili ya ibada hiyo ya Iftari.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.07 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 7 Mei, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*